

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 24 Mei, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Madadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. CECILIA D. PARESSO - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. ASIA P. MINJA - KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, sasa aulize swali lake.

Na. 219

### Hitaji la Bararaba kwa Wananchi wa Kavuu

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Halmashauri ya Kavuu ni mpya na mapato yake yako chini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa inawapatia wananchi mawasiliano ya barabara japo kwa kiwango cha changarawe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Jimbo la Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa barabara za changarawe katika Halmashauri mpya ya Mpingwe ni kilomita 37.7, sawa na asilimia 19 ikilinganishwa na kilomita 202.5 kwa Wilaya nzima. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Serikali imepanga kufanya matengenezo ya kilometa 42 kwa kiwango cha changarawe ambapo fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hiyo ni shilingi milioni 246.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali katika bajeti ya mwaka 2016/2017, ni kufanya matengenezo ya kilometa nyingine 49.8 kwa kiwango cha changarawe pamoja na matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya kawaida katika barabara za Halmashauri. Jumla ya shilingi milioni 324 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la msingi napenda kwanza kumshukuru ameweza kueleza kwamba kuna fedha ilitengwa kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 ambayo bajeti yake inakwisha mwezi wa Sita tarehe 30; na

hizi fedha amesema Serikali imepanga kufanya matengenezo ya kilometa 42 kwa kiwango cha changarawe ambapo fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hiyo ni shilingi milioni 246. Swali langu, je, fedha hizo zitatoka kabla ya Juni 30 mwaka huu? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamoja na kufahamu changamoto za barabara zilizoko katika Majimbo yetu hasa katika mikoa yetu hiyo ya pembezoni, tatizo siyo barabara anayoniambia ambayo imetengewa fedha ya kutoka Kibaoni kupitia Majimoto mpaka Kasansa na kwenda Inyonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la barabara nilizokuwa nikisema ni ambazo ziko chini ya Halmashauri na *concern* yangu na ya wananchi ni kwamba Halmashauri hizi mpya zikiwemo na mikoa mingine mipya ya Simiyu, Geita pamoja na Katavi kwamba hazina bado uwezo wa kuwa na hizo barabara. Swali langu la msingi hapa ni kwamba Serikali iangalie sasa namna ya kutafuta fungu la dharura kwenye barabara zilizoko ndani ya Halmashauri. Kwa mfano, kwangu, barabara ya kutoka Mamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kikwembe, naomba ufupishe tafadhali.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Kwa mfano, kule kwangu, barabara ya kutoka Mamba kwenda Kabunde, barabara ya kwenda mpaka Maimba, barabara ya kutoka Lunguya mpaka Majimoto; barabara hizi hazipo kabisa. Naomba Serikali iangalie namna ya kupata fungu la ziada kuweza kutoa hiyo kwa ajili ya kutengeneza. Naomba kupata majibu ya maswali hayo, lini fedha hizo zitatikana na ningependa zitakapokatikana tupewe taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kikwembe, tafadhali. Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI naona swali ni moja, lingine ni ombi. Naomba ombi ulijibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YARAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge anayezungumza hapa, ni Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati yetu ya TAMISEMI na Utawala Bora. Kwa hiyo, najua kwamba anajua wazi namshukuru sana, ameshiriki kwa kiwango kikubwa katika mchakato wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fedha kwamba lini zitakwenda? Hili hata jana nililisema; nikasema, miradi mingi sana kwa kipindi kilichopita ilisuasua. Jana nilifanya *reference* siyo kwa miradi ya barabara peke yake isipokuwa hata miradi ya maji na miradi mbalimbali ya elimu, miundombinu ya madarasa, yote ilikwama kwa sababu makusanyo ya fedha yalikuwa siyo mazuri. Nilisema pia kwamba kutokana na Serikali ya Awamu ya Tano ilivyojipanga, ndiyo maana tunaona kila mwezi makusanyo ya mapato yameongezeka. Sasa hivi mradi

mingi sana iliyokuwa imesimama, inaanza kutengewa fedha za kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba katika kipindi hiki Mheshimiwa Kikwembe kabla hatujamaliza, basi mafungu hayo na wenzetu wa Hazina watatuhakikishia kwamba wanapeleka fedha zinazokusudiwa ili mradi wananchi waweze kupata huduma hii ya barabara. Kwa hiyo, nakiri kweli fedha hazijafika, lakini Ofisi ya Rais (TAMISEMI) inaendelea kufanya harakati na Ofisi ya Wizara ya Fedha ilimradi fedha zile kama zimetengwa katika bajeti ya fedha mwaka huu unaomalizika, iweze kupatikana na miradi iweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Halmashauri mpya ni kweli; na kweli Jimbo lako ni Halmashauri mpya pale na siyo hilo isipokuwa ni Halmashauri mbalimbali. Ndiyo maana katika bajeti yetu ya mwaka huu mtaona tumetenga karibu shilingi bilioni 240 *plus*. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tunazifikia Halmashauri katika miundombinu ya barabara. Bajeti zile tumetenga kwa sababu sehemu nyingine kuna barabara korofi na barabara zenye vikwazo, bajeti yake nayo tumeitenga hivyo hivyo karibu shilingi bilioni 45. Lengo letu kubwa ni kuangalia jinsi gani tutafanya kwenye Halmashauri ambazo ziko katika changamoto kubwa ili tuweze kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusema kwamba hapa kuna fedha za dharura; kesho na kesho kutwa zitatoka, isipokuwa, kama Serikali, tunachukua ombi hili na lengo ni Mikoa ya Pembezoni yote, siyo Jimbo la Mheshimiwa Kikwembe peke yake bali Mikoa yote ya Pembezoni imekuwa na changamoto kubwa sana, lazima Serikali tuliangalie kwa jicho la karibu ili kuweza kutatua matatizo ya wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Tatizo la barabara hasa katika Halmashauri zetu ni kubwa sana ikiwemo hata Halmashauri ya Wilaya ya Geita na wananchi wanashindwa kwenda sehemu mbalimbali, wanashindwa kusafirisha mazao yao kwa sababu tatizo la barabara ni kubwa sana. Napenda kupata kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mnasemaje sasa kuhusu kupeleka fedha hizi ili barabara ziweze kutengenezwa kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, nakiri wazi kwamba barabara nyingi sana ziko katika hali mbaya na nakiri wazi kwamba mvua iliyonyesha sasa hivi, zile barabara ambazo zilikuwa katika hali mbaya, sasa hivi hali imekuwa ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema pale awali wakati nilipokuwa najibu swali la Mheshimiwa Pudenciana kwamba jukumu letu kubwa ni kujielekeza sisi kama Serikali. Haya makusanyo ambayo sasa hivi yanakusanyika, basi katika bajeti ya fedha ambayo mwaka huu tunaondoka nayo, ziweze kufika Majimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu ni kwamba, tunaposukuma fedha hizi, japokuwa ni kipindi kifupi kilichobakia, lakini zitasaidia hasa kukwamua barabara zenye changamoto kubwa. Nakiri wazi kwamba kweli barabara hali yake siyo nzuri na Mheshimiwa Lolesia nakiri kwamba nami nimeshafika kule Jimboni kwake kipindi naenda kuzindua mradi wa maji. Nimetembelea na nimeona barabara zile jinsi gani zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naahidi tutashirikiana ilimradi kinachopatikana siyo katika Jimbo lake peke yake isipokuwa katika maeneo mbalimbali ambayo yana changamoto kubwa, kama nilivyosema jana katika swali la msingi. Tutajitahidi ili hizi fedha ziweze kwenda na miradi iweze kutekelezeka.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

Na. 220

### **Shule za Kidato cha Tano na Sita Mkoani Lindi**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA (K.n.y. MHE. HAMIDU H. BOBALI)** aliuliza:-

Mkoa wa Lindi umekuwa na shule chache za Kidato cha Tano na cha Sita, matokeo yake vijana wanaofaulu Kidato cha Nne kuingia Kidato cha Tano hupangiwa shule za mbali:-

Je, ni kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kufanya Shule ya Sekondari Mchinga kuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi Kidato cha Kwanza hadi cha Sita?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhitaji mkubwa wa Shule za Sekondari Kidato cha Tano na Sita katika Wilaya ya Lindi, tayari Halmashauri ya

Wilaya ya Lindi imependekeza Shule ya Sekondari ya Mchinga kuwa ya Kidato cha Tano na Sita. Hata hivyo shule hiyo ina upungufu ukosefu wa mabweni, matundu ya vyoo, jiko na bwalo la chakula. Halmashauri imeelekezwa kuweka vipaumbele na kutenga bajeti kwa ajili ya kurekebisha upungufu wa miundombinu ili shule hiyo iweze kupata sifa ya kusajiliwa na kuwa ya Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya upungufu huo kurekebisha na kukamilika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, itatuma wataalam kwa ajili ya kukagua vigezo vilivyozingatiwa ili shule iweze kupandishwa hadhi kuwa ya Kidato cha Tano na Sita na endapo itaridhika itatoa kibali. Aidha, Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita ni za Kitaifa na kwa mantiki hiyo, zinapokea wanafunzi waliohitimu na kufaulu Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne kutoka nchi nzima.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa shule hii ni siku nyingi sana imezungumzwa na Serikali kwamba itapandishwa hadhi kuwa shule ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita, lakini siyo kweli kwamba hii shule ina upungufu wa matundu ya vyoo, mimi shule hii naifahamu sana. Mwaka jana yamejengwa matundu 16, tatizo ni mabweni.

Swali langu la kwanza; je, Serikali ipo tayari hivi sasa kutenga bajeti ya kutosha ili shule hii ya Mchinga Sekondari waweze kujenga mabweni kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano na cha Sita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, amezungumza hapa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba shule ya Kidato cha Tano na cha Sita, mwanafunzi kutoka Lindi na maeneo mengine anaweza kupangiwa mkoa wowote, lakini shule hizi za Kidato cha Tano na cha Sita Tanzania zina matatizo mengi ya chakula na wanafunzi wanakula milo ambayo siyo kamili, wanakula maharage ya kuoza maeneo mengi. Swali langu; Serikali iko tayari hivi sasa kuhakikisha kwamba inapeleka bajeti ya kutosha ili wanafunzi wa Kidato cha Tano na cha Sita Tanzania waweze kupata milo kamili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza suala la kutenga fedha za kutosha, naomba nikiri kwamba katika mchakato wetu wa bajeti tulivyokuwa tunazungumza hapa, nilitaja miongoni mwa vipaumbele katika bajeti zetu. Vipaumbele vile viliji-reflect katika kila Halmashauri ilitenga nini. Tulikuwa na mpango mkakati mkubwa wa kuhudumia shule kongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hili nadhani mchakato wake tulishaupitisha katika suala zima la mchakato wa bajeti. Halikadhalika Mkoa wa Lindi na vipaumbele vyake vimewekwa. Lengo kubwa ni nini? Kwa sababu ilikuwa ni maelekezo na Halmashauri ya Lindi ilishatenga baadhi ya fedha kwa ajili ya ku-*facilitate* hilo jambo. Lengo kubwa ni fedha zipatikane ziweze kupelekwa ilimradi kazi ile iweze kukamilika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la kwamba shule hizi chakula chake, mgao wake hauendi vizuri; naomba niwaambie ndugu zangu, ni kwamba hili kama Serikali tumeliona na ndiyo maana kila wakati sasa hivi tunafanya rejea hata ya viwango vya posho ya kila siku ya chakula. Lengo letu ni kwamba, tufike muda tu-*realize* kwamba *unit cost* ya mwanafunzi kwa sasa ni kiasi gani, ili tunapokwenda katika mpango mpana kabisa wa kuhakikisha tunaboresha elimu Tanzania tuboreshe kwa ukubwa wake.

Naomba nikiri wazi kwamba Serikali inafanya kila liwezekanalo sasa hivi ili kutatua na kuongeza kiwango cha Walimu. Najua mpango huu mpana unapouanzisha ni lazima una changamoto yake kubwa. Sasa zile changamoto zinatupa sisi jinsi gani tutafanya tuweze kwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema katika majibu yangu ya kwanza katika lile swali lake la kwanza la nyongeza kwamba ukiangalia sasa, zile shule kongwe tunaanza kuzibadilisha, tunakwenda kuziwekea miundombinu, lakini kuangalia ni jinsi gani watoto watakapokuwa katika mazingira ya shule waweze kupata elimu bora. Sambamba na hilo upatikanaji wa elimu bora unatokana na jinsi gani mtoto anapata lishe ya kutosha pale shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inafanya utaratibu wote wa kina ili mwisho wa siku tuone elimu yetu Tanzania tunaipeleka wapi ilimradi tuweze ku-*compete* katika nchi nyingine za wenzetu za *East Africa*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tatizo la shule hasa Kidato cha Tano na cha Sita ni la Kitaifa na hii inatokana na azma ya Serikali ya kuongeza Shule za Kata ambazo zilianzia Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne. Nimeshangaa sana Naibu Waziri alipozugumzia kwamba hizi Shule za Kidato cha Tano na cha Sita ni za Kitaifa lakini hapo hapo anazungumzia habari ya Halmashauri kuendelea kujenga shule hizi. Je, anaweza akatuambia baada ya shule hizi za Kata, kuanzia Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne, Serikali imeshajenga shule ngapi za Kidato cha Tano na cha Sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwalimu Suzan Lyimo anafahamu, unapozungumzia Minaki, Tabora, Ilboru, Mzumbe zote ni Shule za Kitaifa hizo. Kwa hiyo, nilikuwa na maana kwamba huo ni msingi wa Shule za Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulielezea, kwa sababu tulikuwa na mchango mkubwa sana katika ujenzi wa shule za Kata na kila Halmashauri ilielekezwa kwa sababu watoto wengi watafaulu katika elimu ya *Form Four*, lakini idadi yetu ya shule zitakuwa ni chache kuwa-*accommodate* hao wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kila Halmashauri imeelekezwa kufanya kila liwezekanalo miongoni mwa shule zao kubainisha miongoni mwa shule nyingine ziweze kuchukua *advanced level, Form Five* na *Form Six*. Hata hivyo, haikatazi, japokuwa wamekuza; mfano Shule ya Mchinga itakapokuwa *Form Five* na *Form Six* haitakataza mtoto kutoka Wanging'ombe kwenda kule Mchinga, maana yake itakuwa ni *room* hiyo, watu kwenda maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ajenda yetu kubwa ni nini? Ni watu kupata elimu kadri iwezekanavyo. Amesema idadi ya takwimu, hata ukiangalia katika kanuni, nitampa takwimu, idadi halisi ya jinsi gani mchakato umekwenda. Sitaki kukupa jibu ambalo halitakuwa sawasawa hapa.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, sasa aulize swali lake.

Na. 221

### **Mpango wa Kujenga Zahanati Kila Kijiji na Kituo cha Afya kila Kata**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiahidi kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na Zahanati kwa kila Kijiji na Kituo cha Afya kila Kata na Hospitali kwa kila Wilaya ili kuwaondolea kero wananchi wanaosafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya na wengine kupoteza maisha wakiwa njiani:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mpango huo wa kuwa na Zahanati kwa kila Kijiji, Kituo cha Afya kwa kila Kata na Hospitali kwa kila Wilaya?



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Zahanati kwa kila kijiji, Vituo vya Afya kila Kata na Hospitali kila Wilaya, unafanyika kwa ushirikiano kati ya wananchi na Halmashauri kupitia Mpango wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD).

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya miradi hii huibuliwa na kutekelezwa na wananchi wenyewe na Halmashauri huchangia nguvu kidogo ili kukamilisha miradi hiyo. Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi, inaendelea na ujenzi wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali kila Wilaya. Ujenzi huo unafanyika chini ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi yaani MMAM, ambapo vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kwa mwaka 2016 hadi 6,935 katika mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la asilimia 31.9. Aidha, utekelezaji wa *program* hii unaendelea, ambapo katika mwaka 2016/2017 Halmashauri zimetengewa shilingi bilioni 182.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele kimetolewa katika kukamilisha miradi viporo, badala ya kuanzisha miradi mipya. Ofisi ya Rais TAMISEMI, inafanya tathmini ya utekelezaji wa MMAM ili kujua idadi ya vijiji ambavyo havina Zahanati. Kata ambazo hazina Vituo vya Afya na Wilaya ambazo hazina Hospitali. Lengo la tathmini hiyo ni kuhakikisha maeneo haya yanapewa kipaumbele na kutengewa bajeti ili kuongeza huduma za afya karibu na wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Sera ya Afya inasema, kila Kijiji kijenge Zahanati na kila Kata ijenge Kituo cha Afya; nakumbuka mwaka 2007 tulikuwa na *program* ya kujenga sekondari kwa kila Kata na kulikuwa na uhaba mkubwa sana wa watumishi; tulikuwa tunasema ni *Vodacom* ama *Voda faster* kwa sababu tu walikuwa wanamaliza *Form Six* na kwenda kufanya kazi. Je, Serikali imejipangaje ukizingatia hii ni afya kwa ajili ya watumishi watakaaoajiriwa kwa vituo ama vijiji 12,000 na kitu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Halmashauri ya Busokelo ni changa sana; tuna Hospitali moja tu, nayo hiyo Hospitali ni CDH kwa maana ya kwamba ni *Council Designated Hospital*; na tuna Kituo kimoja tu cha Afya. Je, Serikali ipo tayari sasa kushirikiana na wananchi nguvu kazi tunazozifanya ili iweze ku-*upgrade* Kituo cha Kambasegela, Kituo cha Afya Isange pamoja na Kanyerere?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sera ya afya ni kwamba kila Kijiji kiwe na Zahanati na kila Kata iwe na Kituo cha Afya. Suala la watumishi ni kweli kuna changamoto, lakini tulivyokuwa katika bajeti yetu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI), hali kadhalika wiki iliyopita tulikuwa na bajeti ya Wizara ya Afya; na Waziri wa Afya alisema wazi kuhusu mkakati wa kuajiri watumishi takriban 10,000 kwa kipindi hiki ili mradi kwenda kuziba zile *gap*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili liko katika utaratibu na naamini kwamba, wale watumishi watakapojiriwa, nimwambie Mheshimiwa Atupele kwamba, tatalipa kipaumbele Jimbo lake ili mradi ile changamoto ambayo inalikabili sasa hivi ya upungufu wa watumishi tuweze kupunguza ile kasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tunahimiza hata vyo vyetu vile vile kuongeza idadi ya watumishi, ili mwisho wa siku ile *needs assessment* tukiweza kuifanya, watu waweze kupatikana, basi katika soko, wawepo watu wa kutosha kuwapeleka katika hivi Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kushirikiana na watu wa Jimboni kwa Mheshimiwa Mbunge, kwanza namsifu sana, kwani ni miongoni wa Wabunge aliyenipa *proposal* mkononi, kwamba mimi nina *proposal* yangu ya Sekta ya Afya katika Jimbo langu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo, naomba nikiri wazi kwamba Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) itashirikiana naye, kuhakikisha kwamba changamoto zilizoko katika Jimbo hili, tuone tutazifanyaje kwa pamoja. Najua Jimbo hili hata Profesa alikuwa huko zamani. Kwa hiyo, tutashirikiana kwa pamoja kuona jinsi gani tutafanya ili mradi watu wa Jimboni kwake waweze kupata huduma ya afya hususan katika suala zima la kuongeza miundombinu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu zuri. Swali langu ni kwamba, kuna maeneo ya Wilaya ambayo hata Hospitali za Wilaya hakuna. Je, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufika maeneo kama ya Kilolo, kuja kuona anafanyaje ili kuhakikisha angalau vile Vituo vya Afya na Zahanati ambazo zimeanzishwa na wananchi, kuzipa msukumo ili angalau wapate matibabu na wao wajue kwamba ilani yao wanaitekeleza vizuri? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba niko tayari na bahati nzuri Mheshimiwa Mwamoto Jimboni kwake wanakuja hapa Ihula karibu kilometa 100. Kwa hiyo, wana changamoto kubwa na matatizo haya tunayafahamu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri wazi, Mheshimiwa Mwamoto kwamba tutajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo. Tutafika, tukiangalia tutapata jawabu kwa pamoja. Kama kuna Vituo vya Afya ambavyo vime-advance vizuri zaidi, tutaangalia jinsi gani tuvipe nguvu vile Vituo vya Afya, ili mradi wataalam kutoka Wizara ya Afya wakija kukagua, vituo vile viweze kupanda, basi viweze kutoa huduma kwa wananchi kwa hadhi ya Hospitali; kwa kadiri itakavyoonekana kama mahitaji ya kuwahamisha kutoka katika Kituo cha Afya, kwenda Hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mwamoto naomba nikiri wazi, nitafika Jimboni kwake tutabadilishana mawazo na wananchi wakE, lengo ni kuboresha huduma ya afya katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saumu.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Matatizo ya ukosefu wa Zahanati na Vituo vya Afya yapo kila sehemu. Jimbo la Pangani ni moja kati ya Majimbo ambayo yana Kituo cha Afya kimoja tu, lakini kituo chenyewe pia hakina wahudumu wa kutosha, hakina vifaa vya kutosha. Je, Serikali ina mpango gani, kuhakikisha Kituo kile cha Afya kinaboreshwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama sikosei amesema Pangani na bahati nzuri nilifika Pangani pale na kuona mahitaji, japokuwa sikwenda katika zoezi la kufanya *assessment* ya Sekta ya Afya. Bahati nzuri Mbunge wa Pangani ndugu yangu pale alikuwa kila siku ananikorofisha katika hili; na nikijua kwamba watu wa Pangani wana changamoto hii, kwa hiyo, naomba nikiri wazi kwamba, lengo letu kubwa ni kwamba, kwa watu wa Pangani siyo afya peke yake, Jimbo la

Pangani ukiangalia lina changamoto kubwa hata ya miundombinu yake ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa pamoja mimi nitakwenda na Waheshimiwa Wabunge huko, tutashirikiana kwa pamoja kubaini sasa nini tutafanya kwa pamoja? Kwa sababu jambo hili lazima tushirikiane kwa pamoja, lazima tubaini pamoja, halafu tuweke vipaumbele. Ndiyo maana jana nilimwita mtaalam wangu pale TAMISEMI aniandikie *special proposal*, lengo langu ni kwamba, mwakani inawezekana tukaja na sura nyingine hasa kutatua tatizo la afya. Nikawaambia waandike *proposal* maalum tutafanyaje kutatua tatizo la Zahanati na Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya, kama *special project ya five years* kuangalia tutafanya vipi, tuje na mtazamo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema kwamba tunatenga Halmashauri peke yake, lakini *centrally* kama Ofisi ya Rais (TAMISEMI), tunafanyaje kuhakikisha ili tunakuwa na *global program* ya kupambana kwenye suala la afya katika Tanzania yetu hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nimelichukua hilo suala, tutapanga kwa pamoja kuona ni jinsi gani tutafanya ili mradi kuboresha maisha ya wananchi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali ilianzisha mpango huu wa MMAM miaka kadhaa iliyopita na ukizingatia kwamba wanawake wajawazito na watoto ndio waathirika wakubwa; nataka kujua, nini mkakati wa Serikali katika kutoa vifaa tiba kwa akinamama wajawazito na watoto hususan katika suala zima la *misoprostol* wakati wa *PPH*? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YARAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikifahamu Mheshimiwa Mary Mwanjelwa ni Daktari, kwa hiyo, najua anaguswa sana katika hilo. Vile vile mkakati uliopo, kwanza niseme lazima sisi Watanzania tujipe faraja wenyewe, kwa sababu jana kama wale watu walikuwa wanafuatilia katika mitandao ya kijamii, walimwona Rais Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akiwa katika harakati mbalimbali za watu wanaomtunuku kwamba ameshughulikia suala kubwa sana la vifo vya akinamama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Watanzania lazima tujivunie kwa kazi kubwa aliyoifanya Rais wetu mstaafu. Harakati za sasa ni nini? Maana yake ni kujielekeza katika kila eneo katika kuboresha Sekta ya Afya. Ndiyo maana hapa nimezungumza mara kadhaa, kwamba sasa hivi tunakwenda

kuhakikisha tunatekeleza mradi mkubwa na wenzetu wa kutoka Uholanzi, kuhakikisha mradi karibuni wa shilingi bilioni zipatazo 46. Katika hili maana yake nini? Tutakwenda kufanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya Afya, hasa katika Hospitali yetu ya Kanda kuipatia vifaa tiba, lengo kubwa ni kupunguza vifo vya akinamama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati wa Serikali ni huo kwa upana, kushirikisha *the own source*, kushirikisha *income* ambazo ziko ndani ya nchi, lakini halikadhalika fursa kutoka maeneo mbalimbali. Lengo kubwa ni kwamba Tanzania iwe ni *icon* kuhakikisha tunapambana na vifo vya akinamama na watoto katika Bara la Afrika.

**SPIKA:** Tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 222

### **Mafuriko na Uharibifu wa Mazingira Mkoa wa Mara**

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Mafuriko na uharibifu wa mazingira umewafanya wahanga wa matukio haya kukosa mahitaji muhimu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mafuriko na uharibifu wa mazingira katika Mkoa wa Mara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua kadhaa za kukabiliana na tatizo la mafuriko na uharibifu wa mazingira Mkoani Mara. Hatua hizo ni kama ifutayo:-

Moja, kuelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa hifadhi ya mazingira na madhara yatoakanayo na kujenga kwenye mikondo ya maji na mabondeni ili kuepukana na athari za mafuriko na uharibifu wa vyanzo vya maji. Aidha, Kamati ya maafa ya Mkoa wa Mara, huratibu matukio ya maafa yatoakanayo

na mafuriko pale yanapojitokeza ikiwa ni sehemu mojawapo ya kupambana na athari ya mafuriko katika maeneo husika.

Pili, kubaini na kuwataka wakaazi wote wanaoishi mabondeni waliojenga katika maeneo ya mikondo ya maji, kuhama ili kuepuka athari za mafuriko sambamba na kulinda vyanzo vya maji.

Tatu, kuhimiza kampeni ya upandaji miti nchini, ambapo kila wilaya zikiwemo Wilaya za Mkoa wa Mara zinazopaswa kupanda na kutunza miti isiyopungua 1,500,000 kwa mwaka. Aidha, katika kuimarisha zoezi la upandaji miti nchini, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Upandaji Miti wa mwaka 2015 mpaka mwaka 2021, utakaotekelezwa kwa kushirikiana na taasisi za Serikali, mashirika binafsi katika maeneo yote nchini.

Nne, kusimamia na kuendeleza hifadhi ya misitu na kuwaondoa wavamizi wote katika hifadhi za misitu zilizoko Mkoani Mara. Mfano msitu wa Kinyanyali, Kalwilwi, Mrima Mkendo na Kalano, ambapo kaya sita zimeshaondolewa kutoka kwenye msitu wa Kinyang'ali. Serikali itaendelea kuhimiza wananchi Mkoani Mara na nchini kote kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kwa kutokujenga na kufanya shughuli zisizo rafiki wa mazingira katika maeneo ya mabondeni na kwenye kingo za mito ndani ya mita 60 ili kuepuka uharibifu wa mazingira na athari zitokanazo na mafuriko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sokombi, swali la nyongeza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kweli sijaridhishwa na majibu niliyopewa. Ukikaa ukiangalia, kwa mfano kule Kisorya mpaka Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama alikuja, wale watu walipewa amboni tatu tu na hawana makazi. Naomba Mheshimiwa Waziri husika anielezee kwamba atawasaidiaje wananchi wale, kwa sababu hawana sehemu za kukaa? Pia toka walivyopewa chakula na mazao yote yaliharibiwa: Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wale wananchi pia kupata chakula?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kwa nini Serikali inasubiri linapotokea janga, ndiyo wanaanza sasa kutuma wataalam wao kwenda kuwapa wananchi elimu ya mazingira? Kwa nini wasiwe wanatoa kabla? Ahsante, naomba majibu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa mujibu wa taarifa kutoka kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, kama nilivyoieleza kwamba tumekuwa tukishirikiana nao

na kuona namna majanga haya yanapojitokeza na kuweza kuwahudumia wananchi hawa waliopatwa na majanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msisitizo ambao Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba hawa wananchi sasa hawana makazi kwa muda mrefu na kwamba hawana chakula; nitafanya ziara kwenda kuona eneo analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuona namna ya kuwasaidia hawa wananchi ambao wanateseka bila chakula na bila sehemu ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijibu hili swali lake analosema kwamba Serikali inasubiri; Serikali hatusubiri, ndiyo maana muda wote, saa zote tumekuwa tukisisitiza wananchi kutokujenga mabondeni, tumekuwa tukisisitiza wananchi kutokujenga kandokando ya mito na tumesisitiza wananchi waliojenga na kuziba mifereji na kusababisha mafuriko kutokufanya hivyo. Kwa hiyo, kila siku tuko katika jambo hili katika kuhakikisha kwamba wananchi hawajengi kwenye mabonde kwenye kingo za mito wala bahari, wala maziwa ili kuepokana na maafa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, tumekuwa tukiwaondoa wananchi wanaoishi kwenye mabonde na sehemu hizo. Pia tunaweka msisitizo mkubwa wa kuhakikisha kwamba katika miradi yetu ya kimazingira, maeneo mengine ambayo yanatuama maji tunatengeneza mifereji na tunatengeneza mabwawa ya kuweza kuya-*contain* hayo maji ili sasa tuweze kuyapunguza mafuriko haya katika namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kweli kwamba Serikali inangojea tatizo litokee, Serikali iko makini na tutaendelea kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kwamba mambo haya hayajitokezi tena.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Mmasi.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa suala zima la mazingira na changamoto zake lililoukumba Mkoa wa Mara linafanana kabisa na tatizo lililotokea hivi majuzi la mafuriko, kwa Mkoa wa Kilimanjaro na kuathiri sana maeneo ya ukanda wa chini, yaani Vijiji vya Vunjo, Kahe, pamoja na Chemchem: Je, Serikali ina mpango gani, katika suala zima la uhifadhi wa mazingira kwa Mkoa wa Kilimanjaro? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijibu swali lililoulizwa kuhusu suala zima hili la mafuriko ambalo linalikumba Taifa letu. Tukubaliane katika *principle* za



kimazingira, ambapo sisi wote humu ndani ni wadau, kwamba kila mtu anatakiwa achukue jukumu hili la tunapambana katika zoezi zima la kuhakikisha kwamba mazingira yetu yako salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua uharibifu wa mazingira uliofanyika Mkoa wa Kilimanjaro. Tunajua hali ya mazingira nchini sasa hivi ilivyo, kwa hiyo, zoezi hili na mafuriko haya na maeneo yote aliyoyataja na tumekuwa tukitolea taarifa kwamba mafuriko haya hayawezi kuwa ya mara moja. Tatizo hili litakuwa ni *permanent* sasa, kutokana na uharibifu wa mazingira tulionao hapa nchini. Tuchukue jukumu wote kwa pamoja, tumeagiza, sasa hivi tumekuwa na mpango mkakati wa upandaji miti. Tunajua kabisa tukipanda miti, tutazuia kwa kiwango kikubwa mafuriko ya maji ambayo yanatokea, kwa maana kwamba ni kinga, lakini vile vile katika kurekebisha hali ya hewa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge mliunge mkono zoezi ambalo linasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais la upandaji miti, la kuhakikisha kwamba kila Wilaya inapanda miti isiyopungua 1,500,000 kwa mwaka. Nilivyotembelea Mkoa wa Kilimanjaro, nilikuta wana mkakati wa kupanda miti milioni tano kwa mwaka. Tufanyeni hili zoezi, lakini tushirikiane sana, wale watu wanaoharibu mazingira, miti inakatwa mno, hatuwezi kupona katika ukataji miti wa namna ile. Kila mwaka inafyekwa hekta laki nne, kila mwaka zinakatwa. Kwa hiyo, watu wote walioiandama misitu yetu na kuikata kiasi hicho tushirikiane kuhakikisha kwamba uharibifu huu unakomeshwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa maliza tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Vilevile jitihada nyingine za Serikali za kuleta nishati mbadala mnazisikia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina swali la nyongeza au ni ushauri kwa Wizara husika. Mafuriko mengi yanayotokea sasa hivi ni kwamba miundombinu au zile njia za maji zimejaa michanga, pamoja na mabwawa yale ambayo ni *reserves* za mafuriko nazo zimeharibika. Sasa naishauri Serikali, Wizara husika hiyo ya mazingira, pamoja na Wizara ya Maji wawe na mkakati maalum wa kudhibiti zile njia za maji wachimbe zile *drainage pattern* za mito au/na mabwawa ili ku-*conserve* au ku-*protect* mafuriko yasitokee. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa kifupi tafadhali.



**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunapokea ushauri wake mzuri na ambao tunaendelea kuufanyia kazi siku hadi siku, lakini nitoe wito kwa Wabunge wote, kushiriki siku ya usafi. Inapofika tarehe ya usafi, Waheshimiwa Wabunge wote na viongozi wote lazima tuwe kielelezo kwa wananchi kushiriki usafi huu. Tutashiriki kuzibua hiyo mitaro, kufagia na tutashiriki kuhakikisha kwamba kila eneo linakuwa safi na salama. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 223

**Marekebisho ya Sheria ya Tumbaku**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Mwaka 2013 Bunge lilirekebisha Sheria ya Ushirika wa Tumbaku ili iendane na hali ya sasa ya ushirika huo nchini:-

Je, ni marekebisho gani yanayowanufaisha wakulima moja kwa moja?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ushirika wa tumbaku kwa ujumla unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na ubadhirifu katika vyama hivyo, madeni makubwa, tozo na makato mengi na usimamizi hafifu wa Vyama vya Ushirika. Changamoto hizi ni miongoni mwa vitu vilivyochochea kuwepo kwa sheria mpya ya ushirika, Sheria Na. 6 ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya marekebisho yanayowanufaisha wanachama wa Vyama Ushirika wakiwemo wakulima wa tumbaku ni pamoja na:-

(i) Kwa kutumia sheria mpya viongozi wabadhirifu katika Vyama vya Ushirika wamechukuliwa hatua. Kwa mfano, katika maeneo yanayolima tumbaku, viongozi wabadhirifu wa Vyama vya Ushirika 26 katika Mkoa wa Ruvuma wakiwemo na Maafisa Ushirika wawili wamesimamishwa kazi na kufikishwa Mahakamani. Viongozi wa Chama Kikuu cha WETCU waliohusika na

ubadhirifu Mkoani Tabora, waliondolewa madarakani ili kupisha uchunguzi. Hatua zaidi zimechukuliwa katika Vyama vya Ushirika vya Korosho kwa viongozi watendaji na watendaji 822 kupewa hati za madai katika maana ya *surcharge*.

(ii) Kuhusu madeni, sheria ya sasa inakataza vyama kukopa zaidi ya asilimia 30 ya mali zake ili kuzuia vyama kuingia kwenye madeni makubwa yasiyolipika. Aidha, sheria ya sasa inaweka usimamizi wa karibu ambapo vyama hivi vitakuwa vikikaguliwa mara kwa mara kuzuia ubadhirifu.

(iii) Kuhusu tozo, kuanzia sasa Mkutano Mkuu utakuwa chini ya Uenyekiti huru utakaochaguliwa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu kinyume na hapo awali ambapo Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku ndiye anayekuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu. Lengo ni kulinda maslahi ya wakulima ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa tozo zote zinazoidhinishwa na Mkutano Mkuu zinakuwa na maslahi kwa wakulima wa tumbaku.

(iv) Muundo wa sasa wa Tume ya Ushirika unafanya Maafisa Ushirika wote kuwajibika moja kwa moja kwenye Tume. Hii itaongeza ufanisi na watumishi hawa wa Vyama vya Ushirika kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambalaswa, swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mlolongo wa tozo kwenye zao la tumbaku ambazo anatozwa mkulima, ilikuwepo tozo ambayo, kabla ya marekebisho ya Sheria hiyo ya 2013 kulikuwa na AMCOS, Ushirika wa Msingi, Ushirika wa Wilaya na Ushirika wa Taifa ambao ulikuwa Morogoro wakijiita APEX. Sasa sheria hii iliporekebishwa hawa watu wa APEX waliondolewa na kuondolewa kwao ina maana tozo ambayo mkulima alikuwa anakatwa ili ikafanye uendeshaji wa APEX, ilikuwa aidha irudi kwenye AMCOS au iondolewe. Je, hiyo imeondolewa au imerudi kwa mkulima? La kwanza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wote hapa tumemsika Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema baada ya Bunge hili atakwenda Tabora akaangalie matatizo yaliyomo kwenye eneo hili la tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo haya pia kuna tatizo la wanunuzi wa tumbaku. Makampuni ya kununua tumbaku hapa nchini yako matatu tu na mwaka 2015 yameanza ukiritimba wa kutokununua tumbaku yote ya wakulima. Je, Wizara inasemaje au ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tumbaku yote ya wakulima inanunuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tozo iliyokuwa inalipwa kwa APEX, nimfahamisha tu Mheshimiwa Mbunge kuwa tuko katika utaratibu wa kupitia tozo zote katika mazao yote na tutaleta taarifa hivi karibuni Bungeni, Waziri wa Fedha atawasilisha *Finance Bill* na hiyo *Finance Bill* pamoja na mambo mengi itaonesha maeneo ambayo tumependekeza kuondoa au kupunguza kodi ambazo hazina maana. Kwa hiyo, zinashughulikiwa na atapata taarifa karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ununuzi na soko la tumbaku, ni kweli kabisa kama alivyosema, tunatambua changamoto iliyopo katika soko la tumbaku kwa sababu pamoja na mambo mengine, kuna ukiritimba mkubwa kwa sababu makampuni yanayonunua ni matatu tu. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na suala la soko, ni suala la *dynamics* duniani, lakini nimhakikishie tu kwamba Wizara yangu tayari inafanya jitihada ili kuhakikisha kwamba tunapata wanunuzi wa ziada ili kuondoa ukiritimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango hii imekuwa ni pamoja na kufanya majadiliano na *The China Confederation of Industries* ili kujaribu kuwaleta wanunuzi wa tumbaku kutoka China. Nimweleze tu kwamba tumeshafikia hatua nzuri na baada ya muda siyo mrefu tuna hakika kwamba kutakuwepo na wanunuzi wa ziada kutoka China ili kuweza kuleta ushindani na hatimaye wakulima wetu waweze kupata bei nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuniruhusu nami niulize swali la nyongeza kwa niaba ya wakulima wa tumbaku. Kwa vile sheria hii ya ushirika pamoja na sheria ndogo Na. 42 iliyounda Bodi ya Tumbaku zimeendelea kuwa na upungufu mkubwa, ni lini Serikali italeta sheria hizo mbili hapa katika Bunge lako ili zifanyiwe marekebisho na kwa faida ya wakulima na zao la tumbaku nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Ushirika kufanyiwa marekebisho pamoja na ile inayounda Bodi ya Tumbaku, nimwambie kuwa Sheria ya Tumbaku ndiyo imepitishwa tu karibuni haina hata miaka mitatu, imeanza kufanya kazi tu mwaka 2015 pamoja na kwamba ilipitishwa kuanzia mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna maeneo ambayo yanahitaji marekebisho, itabidi tufuate utaratibu wa

kawaida na hatimaye sisi kama Wizara tutahakikisha kwamba inakuja Bungeni. Vivyo hivyo kwa sheria inayounda Bodi ya Tumbaku, tukipata mawazo kutoka kwa wadau mbalimbali kwamba inahitaji kufanyiwa marekebisho tutafanya utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vigumu kwa sasa kumwambia kwamba, tutaiteta kwenye Bunge hili lini kwa sababu bado kama Wizara hatujapata malalamiko makubwa au mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali ya kuweza kurekebisha.

Na. 224

### **Kodi Nyingi na Bei Hafifu kwa Wakulima wa Kahawa**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Kuna kodi zinazofikia 26 katika kilimo cha kahawa ambazo zimefanya bei wanayopata wakulima wa zao hilo kuwa kidogo sana ikilinganishwa na gharama za kulima hivyo kuwafanya baadhi ya wakulima kupeleka kahawa yao nchi jirani ambako bei yake ni nzuri na kwa kufanya hivyo nchi inakosa mapato na kudhoofisha zao hilo hapa nchini; na hata Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alilikemea jambo hilo kwenye hotuba yake ya kulifungua Bunge Jipya aliyoitoa Bungeni Novemba, 2015.

Je, ni kwa nini Serikali isiingilie kati na kufuta kodi hizo kandamizi kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kuna changamoto ya kuwepo kwa kodi nyingi siyo tu kwenye zao la kahawa, lakini pia kwa mazao mengine ya chakula na biashara hapa nchini. Kwa mfano, kwa kahawa inayozalishwa Mkoani Kagera ambayo ni aina ya Robusta inapouzwa nje kwa kupitia Vyama Vikuu au Vyama vya Msingi, vyama hivyo hutozwa kodi na tozo mbalimbali zipatazo 26, sawa na makampuni mengine binafsi. Kwa kuwa vyama hivi ni vyama vya wakulima, gharama hizi za kodi na tozo mbalimbali kwa njia moja ama nyingine huenda kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua ukubwa wa changamoto hizo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imedhamiria

kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara katika Sekta ya Kilimo kwa kupitia upya taratibu, vibali, tozo, kodi, ushuru na ada mbalimbali zinazotozwa ili kupunguza gharama za kufanya biashara. Tozo, ada na kodi zote zitakazotozwa na Bodi za Mazao na Mamlaka nyingine zitapitiwa upya na kuchambuliwa ili kutoa nafuu kwa wakulima wote ikiwa ni pamoja na wakulima wa zao la kahawa. Kodi zitakazogundulika kurudisha nyuma tasnia ya kahawa zitaondolewa mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu Mheshimiwa Naibu Waziri anasema Serikali imedhamiria na kodi zinazotozwa zitapitiwa, ina maana kazi hiyo haijaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli akiwa kwenye kampeni pale Bukoba, tulimwambia kuhusu kodi hizi na tozo nyingi sana na akasema kwamba atakapokuwa Rais akiteua Waziri wa Kilimo, Waziri wa Fedha na Waziri wa Biashara wakishindwa kuondoa kodi hizi atawatumbua. Leo yapata karibu miezi sita tangu wameteuliwa watu hawa na hakuna kodi hata moja ambayo imeondolewa. Je, hawa Mawaziri wako tayari kutumbuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rweikiza Mjumbe wa Kamati Kuu ambaye kwa nafasi yake ya Ujumbe wa Kamati Kuu naye anaweza akamtumbua Waziri yeyote. Nimhakikishie tu kwamba kwa kuwa kodi hizi zinahusisha taasisi zaidi ya moja, hivi tunavyoongea, tayari timu ya wataalam ambayo inaandaa Muswada wa Sheria ambao utaletwa hapa Bungeni ambao ndiyo unaopanga mapato na kodi zitakazofanyika katika mwaka wa fedha unaokuja, inakamilisha kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine, haya yote ambayo tumekuwa tukiyasema, hasa hili ambalo Mheshimiwa ametoka tu kulisema, sisi Waheshimiwa Mawaziri tumepigia mstari kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Rais. Jambo hili alilolisemea Mheshimiwa Rweikiza, liko ukurasa wa 17 *paragraph* ya tatu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati analizindua Bunge hapa na tuko kwenye hatua za mwisho za kulitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini tutakapokuwa tunajadiliana *Finance Bill* baada tu ya bajeti kubwa ya Serikali, mambo haya yanayohusu tozo za kero ambazo kimsingi Mheshimiwa Rais tayari alishayatolea maelekezo wakati

anatupa kazi hii, sisi tutakwenda kulikamilisha na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake wanaendelea na kazi ya kutengeneza hiyo *Finance Bill*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuongee kwa sauti za chini kidogo, maswali na majibu tunashindwa kuyasikia vizuri. Tunaendelea, Mheshimiwa Boniphance Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 225

### **Kufufua Viwanda vya Ushashi Ginnery na Kibara Ginnery**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Zao kuu la biashara katika Wilaya ya Bunda ni pamba lakini viwanda vya kusindika pamba vya *Ushashi Ginnery* na *Kibara Ginnery* vilivyokuwa vinamilikiwa na *MCU* (1984) havifanyi kazi tangu mwaka 1990:-

(a) Je, ni lini Serikali itafufua viwanda hivyo ili wakulima wa pamba wapate bei nzuri?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya kusindika pamba ili kuongeza thamani ya zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphance Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba viwanda vya kuchambua pamba vya *Ushashi* na *Kibara* havifanyi kazi tangu mwaka 1990. Viwanda hivi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge vinamilikiwa na kilichokuwa Chama Kikuu cha Ushirika cha *Musoma (MCU)* ambacho kwa sasa kipo kwenye utaratibu wa mufilisi ulianza mwaka 1997. Utaratibu wa mufilisi umechukua muda mrefu kutokana na baadhi ya wanachama wa *MCU* kukata rufaa kwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu kutaka viwanda hivi visifilisiwe na badala yake ikiwezekana viendeshwe kwa ubia kati ya sekta binafsi, wanaushirika na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya ushirika imeanza kushughulikia suala la mali za *MCU* ikiwemo viwanda hivyo ili vitafutiwe utaratibu wa kufufuliwa kwa ubia na vianze kazi ili kuwezesha ulipaji wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bunda ina *ginnery* tatu zinazofanya kazi ya kuchambua pamba inayopatikana katika wilaya hiyo. Hivyo wakulima wa Bunda wanapata huduma za uchambuzi wa pamba kupitia *ginneries* hizo. Aidha, taarifa zilizopo zinaonesha kuwa *ginneries* zilizopo katika Wilaya ya Bunda bado hazipati pamba ya kutosha na hivyo kufanya kazi chini uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahamasisha sekta binafsi na wadau wengine kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo vya kusindika pamba ili kuongeza thamani ya zao la pamba na wakulima wapate faida zaidi. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wakulima wanajengewa uwezo wa kumiliki vinu vidogo vidogo vya kuchambua pamba katika vikundi vya wakulima na Vyama vya Ushirika. Kwa kuwa tayari Serikali inasambaza umeme vijijini kwa nguvu kubwa kinachofuata sasa ni kujenga mazingira ya kuwawezesha wakulima kumiliki viwanda vya kusindika mazao yao ikiwepo pamba. Hii ndiyo nia na namna ya bora ya kuleta mapinduzi ya viwanda nchini katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inawashauri wamiliki wa vinu vikubwa vya kuchambua pamba wafikirie kuwekeza kwenye hatua zinazofuata za mnyonyoro wa thamani kama kusokota nyuzi katika maana ya *spinning*, kufuma vitambaa, *weaving* na kutengeneza nguo (*textile*).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, ni ukweli usiopingika kwamba zao la pamba bei yake ni ndogo mno ukilinganisha na uzalishaji wake. Ni lini Serikali itafanya mikakati ya dhati ya kupandisha bei ya pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi viwanda vidogo vidogo ambavyo kwa swali la msingi wamevitaja kwamba vitaanzishwa kwenye Wilaya ya Bunda hasa jimbo langu la Bunda ni lini vitaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ikilinganishwa na nchi nyingine pamba yetu haipati bei nzuri. Hii inasababishwa pamoja na mambo mengine na ukweli kwamba wakulima wetu wengi wanauza pamba ikiwa ghafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wakulima katika vikundi vyao wanajengewa uwezo wa kumiliki viwanda vidogo vidogo ili waweze kuchambua pamba kwa sababu faida kubwa kwenye pamba ipo katika hatua nyingine za mnyororo kama kuchambua ambayo wakulima wetu hawashiriki. Hiyo kazi imefanywa na watu



wachache. Kwa hiyo, tunataka tuwajengee uwezo waweze wenyewe kumiliki viwanda vidogo vidogo kama vya alizeti ili waweze kufaidika na mazao mengine yanayotokana na pamba kama mafuta pamoja na *cotton seed*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile bei ya pamba inashuka kutokana na ukweli kwamba wakulima wetu wanakuwa na gharama kubwa za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kununua pembejeo kwa bei ambayo ni ghali. Ndiyo maana Serikali imechukua maamuzi ya kuangalia namna ya kupunguza tozo na kodi mbalimbali zinazotowwa kwenye pembejeo ili kuondoa gharama kubwa za uzalishaji na hivyo baadaye wakulima wetu waweze kupata bei nzuri wakati wanapouza pamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, viwanda kama nilivyosema, mkakati wa kujenga viwanda vidogo, nafikiri mlishasikia bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwamba katika Awamu hii ya Tano tunataka kujenga uchumi wa viwanda na hasa viwanda vile vinavyotumia malighafi inayopatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba pamba kama tungekuwa na viwanda vya kutengeneza nguo, kusingekuwa na haja hata ya kuhangaika ya kuuza pamba yetu nje. Kwa hiyo, ni kweli kabisa kwamba kuna mkakati mkubwa sasa wa kuhakikisha kwamba tunarudi kuwa na viwanda vya kutengeneza nguo ili pamba iweze kupata bei nzuri zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia sana kuhusu kuwawezesha wakulima ili waweze kujenga viwanda, lakini pia amekiri kwamba pembejeo ni bei ghali sana kwa wakulima wetu. Sasa nikijaribu kuangalia bajeti iliyopita juzi tu kwa Wizara hii, bajeti ya mbolea imeshuka shilingi bilioni *plus*, imekwenda mpaka *around* shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *gap* hiyo ya kushuka kwa bajeti ya mbolea kutaenda kuondoa ukali wa bei kwenye mbolea na kutawasaidia vipi wakulima kuondokana na kuzalisha katika hali ngumu sana na kuendelea kuwa maskini? Vinginevyo tutakuwa tunaendelea kupiga porojo tu hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa ufupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na ukweli kwamba katika bajeti kulikuwa na changamoto kuhusiana na fedha za pembejeo, lakini nimhakikishie



Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara kwa sasa inaandaa utaratibu mpya wa kutoa ruzuku katika pembejeo ambao utaruhusu wakulima wengi zaidi kuliko ilivyo sasa kuweza kunufaika na ruzuku na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu wa sasa, wote mmesikia malalamiko kwamba pamoja na kwamba Serikali ilitoa fedha nyingi, kwa mfano, katika mwaka wa fedha unaokwisha Serikali ilitoa shilingi bilioni 78 kwa ajili ya ruzuku, lakini mnafahamu utaratibu unaotumika sasa unaowafanya wachache wanufaike na mara nyingi ruzuku ile haiendi kwa wananchi. Sasa Serikali inakuja na utaratibu ambao inawezekana kwamba mbolea zote zikawa na ruzuku na zikapatikana nchini kama tunavyosema, kama bidhaa nyingine na siyo kwa wakulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na changamoto iliyopo, haitaathiri nia ya Serikali na uwezo wa Serikali kuweza kuwapatia wananchi pembejeo kwa bei nafuu.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Josephine Thabita Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 226

### **Hitaji la Viwanda vya Kusindika Mazao - Geita**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Vijana wengi wa Mkoa wa Geita hawana ajira kutokana na ukosefu wa viwanda na hasa ikizingatiwa kuwa sehemu kubwa ya uchumi wetu unategemea kilimo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda vya kusindika mazao katika Mkoa wa Geita?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI,** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Thabita Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa viwanda katika kuchangia ukuaji wa nchi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia mkakati unganishi wa maendeleo ya viwanda (*Integrated industrial Development Strategy*), lengo ni kuhamasisha wananchi na wadau kuwekeza katika kuanzisha viwanda. Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vidogo,

viwanda vya kati na viwanda vikubwa vyenye lengo la kuzalisha bidhaa zinazotokana na rasilimali zinazopatikana hapa nchini zikiwemo zile za kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini zitakazounganisha nchi nzima pamoja na Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati huo pia unazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa na Miji kutenga maeneo ya uwekezaji katika viwanda hadi ngazi ya Kata ambayo itatumika kuanzisha Mitaa ya Viwanda kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika maeneo husika. Wizara itakuwa na jukumu la kuwaelimisha, kuwahamasisha na kuwajengea uwezo wananchi ili waweze kuanzisha viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara inamfuatilia mwekezaji ambaye ni bingwa wa kutengeneza *juice* akichukua kati ya namba tano mpaka saba duniani ili ajenge kiwanda mkoani Geita. Ujenzi wa kiwanda hicho utaenda sambamba na uwekezaji katika kilimo cha kisasa ambapo makubaliano yatafikiwa kwa kuwa na *nuclear farm* na wakulima wanaomzunguka kuweza kupatiwa huduma (*outgrowers*). (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) itaendelea kushirikiana na wadau Mkoani Geita kuibua miradi kupitia *program* ya Wilaya Moja, Bidhaa Moja, (*One District One Product-ODOP*) kwa lengo la kuanzisha na kukuza viwanda katika ngazi ya Wilaya na hivyo kuleta ajira kwa vijana vijijini. Hatua hiyo itasaidia kupunguza wimbi kubwa la sasa lililopo la vijana kukimbilia Mijini sambamba na kuongeza pato binafsi na pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane katika kuhamasisha na kuvutia sekta binafsi kuwekeza na kutumia fursa zilizopo katika Mkoa wa Geita. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chagula, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru sana Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kututia moyo wananchi wa Mkoa wa Geita. Nina swali moja tu la kumuuliza. Kwa kuwa vijana wetu wangependa sana kujijajiri au kuajiriwa, lakini hawana ujuzi; je, Serikali iko tayari kuwapa ujuzi? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote. Katika kila Mkoa kuna Ofisi ya *SIDO*. Mojawapo ya kazi ya *SIDO* ambayo analipwa pesa na

Serikali ni kutoa elimu ya ujasiriamali kwa watu wote. Semina na mafunzo yale yanatolewa bila gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Chagula, awasiliane na Meneja wa Geita, aandae vijana wake waende wapate elimu hiyo, halafu kuanzia hapo tuone watajiendeleza namna gani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kabisa naomba nikubaliane na sekta ambayo inaongozwa na Waziri mwenye dhamana ya Viwanda na Biashara kupitia *SIDO* ili kutengeneza ujuzi na kuajiri vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo kinachoshughulikia Kazi, Vijana na Ajira katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali imetenga fedha ambazo zitatumika kwa makusudi mazima kuongeza ujuzi kwa vijana mbalimbali walioko katika nchi ya Tanzania na ili kuwafanya vijana hao; kwanza, waweze kujajiri wao wenyewe, lakini vilevile waweze kuajiriwa katika viwanda vilivyopo na vitakavyoanzishwa katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, shilingi bilioni 15 zilizotengwa zinaweza kutoa msaada mkubwa sana wa kuongeza ujuzi kwa vijana wa Tanzania na kukabiliana na tatizo hili la ukosefu wa ajira. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa John Peter Kadutu Mbunge wa Ulyankulu, sasa aulize swali lake.

Na. 227

### **Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Ulyankulu.**

**MHE. JOHN P. KADUTU** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Ulyankulu kwa muda mrefu wamekuwa wakipata tabu ya usafiri kutokana na barabara zake kuwa mbovu kwa muda wote:-

(a) Je, ni lini barabara ya kutoka Tabora hadi Ulyankulu itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuondoa kero hiyo?

(b) Je, ni lini barabara ya kutoka Ulyankulu hadi mpakani mwa Kahama itaimarishwa zaidi hata kwa kiwango cha moramu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja?

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Tabora – Ulyankulu yenye urefu wa kilometa 79 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS). Kwa sasa kipaumbele ni kuunganisha Mkoa wa Tabora na Mikoa ya Mwanza, Kigoma, Singida na Katavi kwa barabara za lami. Hatua hii ikikamilika Serikali itaanza kujenga barabara za mikoa kwa kiwango cha lami kwa vipaumbele kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Ulyankulu – Kashihi - Nyandeka hadi Kahama yenye urefu wa kilometa 344 ni sehemu ya barabara ya mkoa kutoka Mpanda – Ugala – Lumbe – Kaliua - Ulyankulu hadi Kahama yenye urefu wa kilometa 428 ambayo ipo katika mpango wa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utakapokamilika, barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji na fedha. Ujenzi huo utajumuisha madaraja yaliyopo katika barabara hii. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kadutu, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yenye kukatisha tamaa, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mpango wa kujenga kwa lami inaonekana haupo kwa sasa na kwa kuwa barabara hizi mbili zinatengenezwa vipande vipande kila wakati na kuleta usumbufu kwa wananchi wetu: Je, sasa Serikali iko tayari kujenga kwa kiwango cha changarawe barabara nzima badala ya vipande vipande? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kadutu kwa uamuzi huo ambao naweza kuuita wa kihistoria wa kurudi nyuma. Ila namwomba sana Mheshimiwa Kadutu, tunapojenga vipande vipande, hatimaye tutakamilisha.

Nami siamini kama wananchi wa Ulyankulu watapenda barabara hii ibakie katika kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa namna anavyotusumbua ofisini, maana yake nimeambiwa na Waziri wangu jinsi alivyokuwa anapoteza muda wake pale Dar es Salaam kwa ajili ya kufuatilia ujenzi wa barabara hii. Namhakikishia kile ambacho tulimwambia ofisini tutakitekeleza. Atupe fursa ya kujenga vipande vipande hadi itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hii barabara ipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 na namhakikishia katika kipindi hicho tutatekeleza ahadi hiyo ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoahidiwa. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kwandikwa.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara hii inaunganisha Mikoa ya Katavi - Tabora na Mkoa wa Shinyanga ikianza Mpanda – Ugala – Kaliua - Ulyankulu katika Jimbo langu la Ushetu na hadi Kahama Mjini; na kwa kuwa ipo katika mpango na kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imetengewa fedha kwa ajili ya *feasibility study* na *detailed design*; na kwa kuwa barabara hii katika hatua za awali...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa fupisha swali lako tafadhali.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Kwa kuwa inasimamiwa na Meneja wa TANROAD, Mkoa wa Katavi; je, kwa nini Mameneja wa Mikoa mingine hawahusiki katika usimamizi na utaratibu huu ukatumika katika hatua za ujenzi wa lami? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani ni maswali yaliyoulizwa kiaina hapo, kwa hiyo, chagua moja ujibu. Mheshimwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Kwandikwa tukutane ofisini tulijadili kwa undani ili majibu ambayo tutampa yawe na uhakika na yatakayotekelezeka. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgeni Jadi.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Tanga daraja la Wami ni jembamba mno, magari mawili hayawezi yakapishana kwa

wakati mmoja; hata juzi tu gari la maiti liliwahi kutumbukia: Je, Serikali ina mpango gani wa kulipanua daraja hilo? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Mbunge atakumbuka, tulipokuwa tunaongelea bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kati ya miradi tuliyoongelea ni upanuzi wa daraja la Wami. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia, kwa kuwa mmetupa fedha, tutatekeleza kile ambacho kipo katika bajeti yetu.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 228

### **Mkakati wa Kudhibiti Bandari Bubu Nchini**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Wapo baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ambao wamekuwa wakitumia bandari 'bubu' ili kukwepa kodi na kusababisha Serikali kukosa mapato:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti wafanyabiashara hao wanaotumia bandari bubu?

(b) Je, ni wafanyabiashara wangapi waliokamatwa katika bandari bubu na kufikishwa Mahakamani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu(a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa wafanyabiashara wasio waaminifu, wanaotumia bandari zisizo rasmi, yaani bandari bubu kupitisha biashara za magendo, madawa ya kulevya, maliasili, uhamiaji haramu, uvuvi haramu na matumizi ya vyombo vya majini visivyo salama ili kukwepa kodi na pia kuhatarisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulipatia ufumbuzi suala hili, Serikali imeanzisha utaratibu wa kufanya vikao vya Wakuu wa Mikoa ya Mwambao wa Bahari ya Hindi na Zanzibar, Kamati za Ulinzi na Usalama na kushirikisha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Taasisi zinazoshughulikia usafiri majini ambayo ni Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*), Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (*ZMA*), Shirika la Bandari Zanzibar (*ZPC*) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, vikao hufanyika kila robo mwaka. Lengo la vikao hivyo ni kutambua na kurasimisha bandari bubu ambazo kulingana na vigezo vya wingi wa biashara inayopita katika bandari hizo na umuhimu wa bandari hizo kijamii, zinastahili kuendelea kuwepo na kusimamiwa na Halmashauri za maeneo husika. Bandari ambazo hazikidhi vigezo hivyo zinatakiwa kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari bubu zilizoamuliwa kurasimishwa katika mwambao wa Bahari ya Hindi kwa upande wa Tanzania Bara ni hizi zifuatazo:-

Mkoa wa Dar es Salaam ni Mbwani, Pwani ni Mlingotini, Kisiju na Nyamisati. Kwa Mkoa wa Tanga ni Jasini, Kigombe, Kipumbwi, Mkwaja na Pangani. Kwa Mkoa wa Mtwara ni Kilambo na kwa Mkoa wa Lindi ni Rushungi na Kilwa Kivinje.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utaratibu wa kurasimisha bandari binafsi umefanyika katika Ziwa Victoria, Halmashauri ya Ilemela na Nyamagana. Bandari tisa binafsi zimetambuliwa na kurasimishwa. Utaratibu huo utaendelea pia katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wema wamekuwa wakiisaidia Serikali kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama katika maeneo yenye bandari bubu kutoa taarifa kwa vyombo vya doria kuhusu kuwepo kwa wafanyabiashara wasio waaminifu katika bandari bubu na hivyo kuwezesha kukamatwa.

Katika mwaka wa 2015 walikamatwa wafanyabiashara 81 na kuanzia mwezi Januari hadi Machi, 2016 wafanyabiashara 17 wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani. Aidha, kuna bidhaa nyingi zilikamatwa ambazo wamiliki hawakufahamika, hivyo kuzitaifisha moja kwa moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msabaha, swali la nyongeza.



**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimwulize Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza kutokana majibu yake kuwa marefu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bandari bubu zipo mipakani; vyombo vya ulinzi na usalama huwa vinakutana na changamoto kwenye bandari hizi. Je, Serikali mnatambua kama vyombo hivi vinakutana na changamoto kubwa kudhibiti silaha na hata magendo? Mna mpango gani kuongezea vyombo vya ulinzi na usalama, stahiki zao na hata vifaa vya utendaji kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa majahazi ndiyo yanayotumika kufanya sana uhalifu, kubeba madawa ya kulevya na hata kutorosha bidhaa haramu kama pembe za ndovu: Je, Serikali mna mikakati gani kukagua majahazi na kudhibiti vyombo hivi vya majahazi ndani ya bahari na ukaguzi wa mara kwa mara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria na taratibu zinazotumika katika kulipa vyombo vya dola. Nimechukua wazo lake na tutawasiliana na Wizara mbalimbali ikiwa ni pamoja na Idara Kuu ya Utumishi pamoja na Wizara yenyewe ya Mambo ya Ndani ili tuangalie kwa pamoja uwezekano wa kuboresha kile ambacho sasa hivi kipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, limefanana na hili la kwanza ingawa limeulizwa kwa namna nyingine. Namhakikishia kwamba vyombo hivi vya ulinzi na usalama vinatekeleza wajibu wake kwa umakini sana na namhakikishia kwamba tutaendelea kudhibiti kama ambavyo sasa hivi tumekamilisha kudhibiti katika eneo hili la mwambao wa Bahari ya Hindi na tumeamua bandari hizo ambazo nimezielezea katika swali la msingi zirasimishwe na tutahusisha halmashauri husika katika kuendelea kudhibiti na kukusanya mapato.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kuongezea majibu hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vyombo vya usalama vinakabiliwa na changamoto nyingi wakati wa kukabiliana na wahalifu hawa wa magendo pamoja na uhalifu mbalimbali wa madawa ya kulevya, biashara haramu, wahamiaji haramu na kadhalika. Miongoni mwa changamoto hizo si tu



kwamba vitendea kazi ni changamoto lakini pia hali ya hewa na masafa marefu ya kuelekea kwenye kina cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatua ambazo tumechukua mpaka sasa hivi, kwanza kabisa tunajaribu kupata taarifa za kiintelijensia ili kazi ya kuweza kufanya *operation* iwe rahisi pale ambapo taarifa za uhakika tumezipa. Hii tunashirikiana vizuri sana na wananchi pamoja na jamii za maeneo husika. Lingine ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuimarisha vitendea kazi hivi hasa *speed boat* kwa kadiri hali ya bajeti itakavyokuwa inaruhusu. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa maswali, nitaleta kwenu matangazo kadhaa. Tangazo la kwanza ni la wageni waliotufikia siku ya leo.

Kuna wageni waliopo jukwaa la Spika na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni Meja Jenerali Gaudence Milanzi, ambaye ni Katibu Mkuu na pia tuna ndugu Angelina Madete, Naibu Katibu Mkuu. Karibuni sana. (Makofi)

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni pamoja na Wenyeviti wa Bodi wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara, hawa wasimame kwa pamoja, naona labda bado wako getini, siwaoni mahali. Makamishna wote, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Maafisa wengine wote kutoka Wizarani na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Karibuni sana. (Makofi)

Pia ipo familia ya Mheshimiwa Waziri ikiongozwa na ndugu Kudra Maghembe, mke wa Waziri. Karibu sana wifi yetu, shemeji yao na pia mama wa wengine humu ndani. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Kanyasu Constantine, huyu ni Mbunge Jimbo la Geita Mjini, ambao ni wanachuo wa UDOM wazaliwa wa Geita kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni 61 wa Mheshimiwa Anna Lupembe kutoka kanisa la *KKKT Cathedral* Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni 14 wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni viongozi wa Wilaya ya Kilolo kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana viongozi wetu. (Makofi)

Tunao pia wageni 22 wa Mheshimiwa Pascal Haonga, Mbunge wa Mbozi ambao ni wanafunzi kutoka vyuo vikuu mbalimbali vya hapa Dodoma

wanaotoka Jimboni kwake wakiongozwa na Dkt. Senyamanza Alexander, Mhadhiri wa *St. Johns University*, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambao ni wanahabari wanaohamasisha Watanzania kuachana na ujangili, wakiongozwa na ndugu Kunze Mswanyama, karibuni sana. Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo hapa Bungeni, kundi la kwanza ni wanafunzi 50 ambao wanatoka shule ya Seminari ya Hijra ya Mkoani Dodoma, karibuni sana. Pia tunao wanafunzi 50 wa shule ya *St. Peter Clever Primary School* kutoka Dodoma, siwaoni, nadhani labda wamechelewa mahali, lakini hao ndio wageni walitufikia siku ya leo. Karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Ninayo pia matangazo ya kazi, tangazo la kwanza ni la kikao cha Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo; Mwenyekiti anawatangazia kwamba mkutane leo tarehe 24 Mei, saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Msekwa D.

Pia tangazo lingine ni la kikao cha Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wenu anawatangazia kwamba leo baada ya kuahirishwa Bunge kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa, nadhani hizi Kamati mbili zikikutana kule zitagawana nani atabaki pale na mwingine aelekee sehemu nyingine, lakini wote wametangaziwa kukutana Msekwa.

Tangazo lingine ni tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wa makanisa ya Kiprotestanti (CCT), Waheshimiwa Wabunge ambao wako chini ya CCT wanaombwa kuhudhuria ibada katika jengo la Pius Msekwa leo siku ya Jumanne saa saba mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wanasisitizwa kuhudhuria ili kuweza kupanga mikakati na kupata viongozi. Kwa hiyo, hili ni tangazo la tatu, wote wanaelekea Pius Msekwa, nadhani wakikutana huko watagawana vyumba.

Tangazo lingine llimeletwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza akiwatangazia Mheshimiwa Margareth Sitta, Mheshimiwa Philip Mulugo, Mheshimiwa Esther Mahawe, Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Profesa Anna Tibajjuka, Mheshimiwa Doto Biteko kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe 24 saa saba ofisi ya CCM, ghorofa ya pili, chumba namba 231. Hiki chumba nadhani ni jengo la utawala.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni kumekuwa na miongozo mingi inayoombwa, kwa hiyo leo nitaisoma. Baadhi ya hiyo miongozo, mingine itasomwa kesho ama baadaye leo.

Mwongozo wa Spika kuhusu suala lililoombewa mwongozo na Mheshimiwa Ali Mohamed Keissy kuhusu swali la msingi alilouliza kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumatatu tarehe 2 Mei, 2016 katika Kikao cha Kumi cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ally Mohamed Keisy baada ya kipindi cha maswali kwisha alisimama kwa ajili ya kuomba mwongozo wa Spika akitumia kanuni ya 46(1) ya kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Kanuni ya 46(1) aliyoomba Mwongozo Mheshimiwa Ally Keissy kinasema: “Waziri aliyelizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa, isipokuwa kwamba, kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi, Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza, kabla ya muda wa kumjibu swali hilo haujafika.

Katika kujenga hoja ya mwongozo wake alieleza kuwa ametumia kanuni hiyo kwa kuwa swali lake alilouliza lilikuwa la msingi na vile vile alitaka swali hilo lijibiwe na ambaye alikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, Mbunge ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, kwa kuwa anajua mazingira ya Rukwa. Alimwona Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa hawezi kujua vizuri mazingira ya Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Nkasi. Aliendelea kusema kuwa lakini cha ajabu Mheshimiwa hakujibu swali hilo kwa ukamilifu. Maswali ya kujuliza kutokana na mwongozo huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Je, Mheshimiwa Mbunge anapouliza swali linalolenga Wizara fulani anaruhusiwa kuchagua Waziri yeyote wa kujibu swali hilo?

(ii) Je, ni kweli kuwa swali hilo la msingi alilouliza Mheshimiwa Keissy halikujibiwa inavyotakiwa?

Kwa mujibu wa kanuni ya 39(1) inayoongelea maswali na taarifa ya maswali inasema: “Waziri anaweza kuulizwa maswali kuhusu masuala yoyote ya umma au jambo lingine lolote ambalo linasimamiwa na ofisi yake....”

Swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Keisy namba 81 kwenye orodha ya shughuli za siku ya tarehe 2 Mei, lililenga Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,

hivyo Waziri anayehusika na Wizara hiyo alikuwa anawajibika kutoa majibu ya swali hilo la msingi la Mheshimiwa Keissy.

Vile vile Ibara ya 63(3)(a) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inaeleza kuwa:-

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza:-

(a) kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake.

Hivyo ni wazi kuwa Waziri anaweza kuulizwa swali lolote lile kuhusu mambo ya umma lakini kwa sharti kwamba liwe katika wajibu wake. Swali alilouliza Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, ambalo alitaka lijibiwe na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya halikuwa kwenye wajibu wake.

Aidha, kanuni ya 39(13) inaeleza kuwa swali aliloulizwa Waziri mmoja laweza kujibiwa na Waziri mwingine au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kanuni hii imetoa fursa kwa Waziri yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kujibu swali lililoulizwa kwa Wizara nyingine. Kanuni hii imetoa uwanja mpana kwa ajili ya swali kujibiwa kiufasaha endapo Waziri mwingine yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataona anapaswa kufanya hivyo, lakini haijampa nafasi Mbunge mwenye swali kuchagua Waziri wa kumjibu swali lake.

Kanuni ya 46(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inasema kuwa: "Waziri Mkuu au Waziri mwingine yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri."

Vilevile madhumuni ya kanuni hii si kwamba Mbunge muuliza swali anachagua Waziri wa kujibu swali lake la nyongeza bali ni uamuzi wa Waziri mwenyewe kama ataona kuna ulazima wa kuongeza majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri wa Wizara husika.

Kuhusu hoja kuwa swali la msingi la Mheshimiwa Ally Mohamed Keisy halikujibiwa kikamilifu, nimefuatilia Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard* na kuridhika kuwa swali hilo lilijibiwa kikamilifu na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na huo ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo mwingine pia unahusu maswali kujibiwa kikamilifu na huu ni mwongozo kuhusu suala lililoombewa mwongozo

na Mheshimiwa Devotha Minja kuhusu kutojibiwa kwa swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha kwa Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumatatu tarehe 2 Mei, katika Kikao cha Kumi cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Devotha Minja alisimama na kuomba Mwongozo wa Spika akitumia kanuni ya 68(7) pamoja na kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016.

Katika kujenga hoja ya mwongozo wake Mheshimiwa Devotha Minja alinukuu baadhi ya maneno ya kanuni ya 46(1) yanayosema kuwa; “Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa...”.

Alifafanua kuwa wakati wa kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti aliuliza swali la Msingi namba 75 ambalo lilijibiwa na Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Baada ya majibu ya swali la msingi Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha aliuliza maswali mawili ya nyongeza.

Katika maswali haya ya nyongeza swali la pili ndilo lililolalamikiwa na Mheshimiwa Devotha Minja, kwamba halikujibiwa na Mheshimiwa Waziri. Hivyo, hiyo ndiyo sababu ya kuomba Mwongozo wa Spika. Kwa mujibu wa *Hansard* swali la pili la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha aliuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ninavyoongea sasa hivi hakuna mawasiliano kwenye hii barabara, imekatika, daraja la Mto Robana limekatika, Serikali iko tayari kuji-*commit* sasa hivi kupeleka hela zikajenge yale madaraja ambayo yamebomoka?

Katika kutoa uamuzi wa kiti kuhusu Mwongozo wa Spika alioomba Mheshimiwa Devotha Minja, nimejielekeza katika hoja au swali lifuatalo:-

Je, ni kweli kuwa swali la pili la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha halikujibiwa?

Kanuni ya 46(1) iliyotumiwa na Mheshimiwa Devotha Minja kuomba mwongozo nilishainukuu wakati nikiota mwongozo wa kwanza, kwa hiyo sina haja ya kuinukuu tena. Kanuni hii aliyoitumia Mheshimiwa Devotha Minja inahusiana na maswali kujibiwa kikamilifu.

Pia kanuni ya 45(3) inafafanua bayana kuwa: “Iwapo Spika ataridhika kuwa, swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge.”

Baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge, nimeridhika kuwa swali la pili la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha halikujibiwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, hivyo naupokea Mwongozo wa Spika aliuomba Mheshimiwa Devotha Minja na naagiza kwa mujibu wa kanuni ya 45(3) kwamba Waziri husika aandae majibu ya swali hilo na atayatoa katika kikao chochote cha Mkutano huu wa Bunge unaoendelea. Huo ndiyo mwongozo wangu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge nitamalizia na mwongozo wa mwisho kwa asubuhi na huu mwongozo uliombwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu) kuhusu Kauli ya Mheshimiwa James Kinyasi Milya Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Ijumaa tarehe 20 Mei, 2016 katika Kikao cha Ishirini na Nne cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliomba Mwongozo wa Spika kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) pamoja na kanuni ya 64(1)(a) na kanuni ya 63(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Waziri aliomba mwongozo huo kutokana na madai ya Mheshimiwa James Kinyasi Milya kwamba Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama ni shemeji wa mmoja wa wabia wa kampuni ya *Sky Associates*, aliyodai ilinunua mgodi wa *Tanzanite One*, Mheshimiwa James Kinyasi Milya alitoa madai hayo wakati akichangia kwenye mjadala wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Alisema kama ifuatavyo, nanukuu:-

“Na sheria za kazi zinajulikana, bahati mbaya mama yetu Mhagama naye anatajwa humu ndani kwamba ni shemeji wa mmoja wa mbia wa hapo. Dada anayeitwa Asia Gongga ameolewa na Martin Mhagama au Yusuf Mhagama”. Mwisho wa kunukuu.

Baada ya madai hayo kutolewa Mheshimiwa Waziri aliomba Mwongozo wa Spika kwa mujibu wa kanuni ya 64(1) inayoeleza kama ifuatavyo; “Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.”

Baada ya madai hayo kutolewa Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama aliomba Mwongozo wa Spika kwa mujibu wa kanuni ya 64(1) inayoeleza kama ambavyo nimeshanukuu hapo juu. Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa Mheshimiwa Milya alisema uwongo na kwamba huyo mtu anayetajwa si shemeji yake. Aliomba Bunge limtake Mheshimiwa Milya kuthibitisha madai yake kwa ushahidi.

Kanuni ya 63(4) inatoa masharti kwamba: "Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya kanuni ya hii, atakuwa na wajibu wa kutoa au kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

Pia Kanuni ya 63(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaeleza kuwa:-

"Bila ya kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo."

Kwa kuzingatia Kanuni hiyo, namtaka Mheshimiwa James Kinyasi Millya afute kauli yake dhidi ya Mheshimiwa Jenista Mhagama au kama anao ushahidi wa kuthibitisha kauli yake autoe kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa Mheshimiwa Millya simwoni kwenye seat yake sijui kama yupo humu ndani? Mheshimiwa Millya, *Chief Whip*, sawa, Mheshimiwa Millya naambiwa hayupo, lakini Mwongozo unamtaka afute kauli yake au athibitishie. *Chief Whip* wa Kambi Rasmi ya Upinzani utausikiliza huu mwongozo, utamfikishia ujumbe atakapokuja mchana atatakiwa afute kauli yake kama hakufuta ataelekezwa nini kitafuata. Kwa hiyo, *Chief Whip* tafadhali mfikishie Mheshimiwa Millya ujumbe huu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. ASIA P. MINJA - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.



**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha  
2016/2017 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kupokea taarifa iliyowasilisha Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ikubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Niabu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana katika Bunge hili la Bajeti. Naomba pia nitumie nafasi hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, nawapongeza, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupewa ridhaa na wananchi wao kuwaongoza hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitume fursa hii pia kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuiteua kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Mwenyekiti wake, Mhandisi Atashasta Nditiye, ambayo ilijadili, ikaelekeza, ikashauri na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Sekta ya Maliasili Nchini, kabla sijaeleza hali ya maliasili hapa nchini, ningependa niseme maneno machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili zetu zinahifadhiwa na kulindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kifungu cha 27,



ambacho kinampa wajibu kila mtu kulinda maliasili za nchi. Chini ya Katiba hii, Bunge lako Tukufu limetunga Sheria za kuhifadhi, kulinda na kuendeleza maliasili za misitu na nyuki, wanyamapori, ardhi oevu na rasilimali za maji. Kazi ya Wizara yangu ni kutekeleza sheria hizi kama zilivyotungwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maliasili na Utalii inasimamia sekta ndogo za wanyamapori, misitu na nyuki, utalii na mali kale. Maeneo yaliyohifadhiwa kisheria yanajumuisha misitu ya hifadhi na mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Ndogo ya Wanyamapori, Wizara inasimamia rasilimali za wanyamapori kwenye hifadhi za Taifa 16 zenye ukubwa wa kilometa za mraba 57,365 na eneo la hifadhi ya Ngorongoro lenye ukubwa wa kilometa za mraba 8,292. Aidha, inasimamia mapori ya akiba 28 zenye kilometa za mraba 114,000 na Mapori Tengefu yenye ukubwa wa kilometa za mraba 58,565.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyohifadhiwa yanachangia uhifadhi wa bioanuai mbalimbali zilizo hatarini kutoweka kama faru, tembo, mbwamwitu, swala, twiga, simba, duma, pamoja na jamii ya ndege mbalimbali. Maeneo haya ikiwa ni pamoja na ardhi oevu ni vyanzo muhimu vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, matumizi ya kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya umeme na uzalishaji viwandani. Vile vile maeneo hayo, huchangia katika uzalishaji wa hewa safi na kuondoa hewa ukaa na hivyo, hifadhi zetu ndiyo msingi wa maisha ya binadamu na viumbe hai katika sayari dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyohifadhiwa bado yanaendelea kuongoza katika kuvutia watalii nchini ikiwa ni pamoja na kuliingizia Taifa fedha za kigeni. Pamoja na umuhimu nilioutaja, bado kuna changamoto za uharibifu wa maeneo ya hifadhi na wanyamapori kutokana na shughuli za kibinadamu na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi, ujangili, uchomaji moto, uvamizi wa mifugo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa, upungufu wa watumishi na vitendea kazi na kuingia na kuzagaa kwa silaha hususan za kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na ujangili wa mwaka 2014 - 2019 kwa kuimarisha doria, intelijensia na upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kudhibiti ujangili. Aidha, Wizara itaendelea na juhudi zinazofanywa na majirani zetu kwa kushirikiana nao na Jumuiya za Kimataifa katika kuhifadhi wanyamapori tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Ndogo ya Misitu; tathmini ya rasilimali za misitu hapa nchini ilifanywa katika mwaka 2010 mpaka 2013 na kubainisha kuwa, Tanzania ina misitu yenye ukubwa wa hekta milioni 48.1. Aidha, kuna miti

yenye mita za ujazo milioni 1,046.9 inayoweza kuvunwa kibiashara, kati ya jumla ya mita za ujazo milioni 3,322 za misitu yote iliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, maeneo ambayo uvunaji wa mazao ya misitu unawezekana kufanyika ni hekta milioni 20 peke yake, zenye asilimia 35 ya ujazo wote wa miti ambayo tunayo. Sehemu kubwa ya misitu yenye miti inayoweza kuvunwa, inapatika katika Mikoa ya Mbeya, Lindi, Ruvuma, Tabora, Katavi na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa misitu tuliyonayo unaweza kukidhi uzalishaji wa takribani tani 138,000 za asali na tani 9,200 za nta kwa mwaka. Hata hivyo, mpaka sasa uzalishaji umefikia tani 34,000 tu za asali ambayo ni sawasawa na asilimia 24.6 ya uwezo huo na tani 625 peke yake za nta. Katika kuongeza msukumo wa uzalishaji wa mazao ya nyuki na huduma za uchavuaji mimea, Wizara imeainisha maeneo ya kuanzisha hifadhi 46 za nyuki zenye ukubwa wa takribani heka 143,937. Mahitaji katika soko la ndani yanaongezeka sana katika mazao haya, sanjari na soko la dunia, ukilinganisha na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Ndogo ya Utalii imeshika nafasi ya kwanza katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni kwa kipindi cha miaka minne mfululizo, kuanzia mwaka 2012, mpaka 2015. Fedha hizo ni wastani wa dola za Kimarekani bilioni mbili kwa mwaka ambayo ni asilimia 25 ya mapato yote ya fedha za kigeni hapa nchi. Sekta pia inachangia takribani ajira 500,000 za moja kwa moja na ajira milioni moja, ambazo siyo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na miundombinu bora katika maeneo yenye vivutio ikiwemo huduma za maji, umeme na barabara. Aidha, hatuna Shirika la Ndege lenye uwezo wa kuleta watalii moja kwa moja kutoka katika nchi ambazo ni masoko ya utalii wa Tanzania. Hivyo, Wizara inaishukuru sana Serikali kwa mpango wa kununua ndege tatu katika mwaka ujao wa fedha ili kukidhi haja hii katika kipindi cha mpito, wakati Serikali ikiimarisha Shirika la ndege la Taifa. Zaidi ya hapo, hatujajenga utamaduni na miundombinu ya kuwezesha malipo ya huduma zetu kulipiwa kwa kutumia *credit cards*. Hali hii huwasumbua sana watalii na wakati mwingi kutukosesha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kukabiliana na changamoto hizo kwa kutenga rasilimali, kuimarisha ushirikiano na wadau wa sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Ndogo ya Malikale, maeneo ya malikale nchini ni zaidi ya 500 na kati ya hayo, maeneo 130 yametangazwa katika gazeti la Serikali. Kati ya hayo maeneo 14 yanasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na maeneo yaliyobaki yanasimamiwa na wamiliki binafsi, taasisi na mashirika mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2015/2016 na Malengo ya Mwaka 2016/2017; Mpango wa Bajeti wa mwaka 2016/2017, umezingatia sera na mikakati ya Serikali, malengo na kazi zilizoinishwa katika mpango mkakati wa mwaka 2016 mpaka 2021, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 na masuala yaliyojitokeza katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa kuzindua Bunge la 11, mwezi Novemba, mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2015/2016 hadi mwezi Aprili, Mwaka 2016 na Mpango wa mwaka 2016/2017, katika Wizara yangu umeainishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Idara ya Wanyamapori, katika kutekeleza Sheria na Kanuni, katika mwaka 2015/2016, Wizara imepitia baadhi ya Kanuni na inaendelea kupitia na kuandaa kanuni nne kama zilivyoainishwa katika aya ya 42 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori; katika mwaka 2015/2016, doria 109,474 zilizoongozwa na taarifa za kiintelijensia zilifanyika ndani na nje ya mapori ya akiba na mapori tengefu. Doria hizi ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa wa ujangili 1,176 na kesi 654 zimefunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, utafiti umegundua kwamba ujangili unafanywa katika ngazi tano. Ngazi ya kwanza ni baadhi ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi na watumishi wasio waaminifu. Ngazi ya pili, ni wawindaji haramu wanaojishughulisha moja kwa moja na kuua wanyama. Ngazi ya tatu, ni wasafirishaji na madalali; ngazi ya nne ni wawezeshaji kwenye nchi wanaonunua nyara ambao husambaza vitendea kazi na fedha na kiungo kati ya majangili nguli na watakatishaji wa fedha na wahalifu wanaoainishwa katika ngazi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ngazi ya mwisho, ni majangili nguli wa Kimataifa, ambao ndiyo wanaotoa fedha na kuwezesha shughuli nzima. Kazi yetu ya kupambana na majangili, sasa imesambaa kwenye ngazi zote ili kuhakikisha kwamba ujangili tunauondoa kabisa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeimarisha shughuli za intelijensia na kushirikiana na vyombo vingine vya dola na katika kufanya hivyo, tumepata mafanikio makubwa katika kuwakamata watuhumiwa wakuu sita wa ujangili akiwepo Malikia wa Pembe za Ndovu anaitwa *Queen of Ivory*, akiwepo shetani, akiwepo OG. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii, kutambua ushirikiano mkubwa ambao Wizara yangu imepata kutoka kwenye vyombo husika vya dora ikiwemo pamoja na ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai, Mkurugenzi wa Mashtaka na Tume ya Taifa ya kupambana na makosa makubwa pamoja na mhimili wa Mahakama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapori, mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori Tanzania *Tanzania Wildlife Authority* ilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Oktoba mwaka jana. Wizara yangu imekamilisha taratibu zote za kuiwezesha mamlaka hiyo kuanza kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kuanzia tarehe 1 Julai, 2016, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori itaanza kutekeleza majukumu yake rasmi katika Makao yake Makuu Mjini Morogoro. Majukumu yote ya usimamizi wa rasilimali za wanyamapori katika mapori ya akiba, mapori tengefu, ardhi oevu na maeneo ya wazi yenye wanyamapori nje ya TANAPA na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro yatasimamiwa na mamlaka hiyo. Idara ya wanyamapori itaendelea na kuratibu na kurekebu Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta Ndogo ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Mkakati wa Kuzuia Ujangili, Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara za Serikali ambao ulizinduliwa mwezi Novemba mwaka 2014. Watumishi 558 wameajiriwa na kuanzisha mfumo wa doria za ushirikiano katika mifumo ya ikolojia ya Selous-Niassa –Mikumi, Ruaha –Ruangwa, Katavi-Rukwa, Moyowosi – Kigosi, Tarangire -Manyara –Simanjiro na Ngorongoro - Serengeti. Aidha, mafunzo yametolewa na kuongeza vitendea kazi kama ilivyoainishwa katika hotuba yangu aya ya 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limeendelea na jukumu lake la msingi la usimamizi wa hifadhi za Taifa 16 kwa kuendelea doria na kutangaza utalii nje na ndani ya nchi. Ninayo furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Shirika la Hifadhi za Taifa katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro lilipata tuzo ya Kimataifa ya kuwa kivutio bora kupita vyote katika Bara la Afrika (*Africa's Leading Tourist Attraction*). Tuzo hiyo ilitolewa na Taasisi ya *World Travel Award* ya Nchini Uingereza. Tuzo hiyo itawezesha utalii wa Tanzania kutangazwa zaidi kupitia tovuti ya taasisi hiyo ambayo inatembelewa na watalii wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Shirika litakamilisha taratibu zote za kuunganisha eneo la Ghuba ya Speke kwenye Hifadhi ya Serengeti, kujenga na kukarabati miundombinu ya nyumba za watumishi, kudhibiti ujangili kwa kufanya doria na kuimarisha matumizi ya teknolojia. Aidha,

shirika litaendelea kuboresha huduma za kutangaza utalii. Vilevile, katika utekelezaji wa sera za ujirani mwema, shirika litajikita katika kuboresha miradi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwezesha vikundi 30 vya jamii vya uhifadhi katika maeneo yanayozunguka Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina furaha kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba, wiki iliyopita, shirika lilitoa madawati 16,000 kwa wilaya zote 55 ambazo zinazunguka hifadhi hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa mwaka 2015/2016, imekarabati kilometa 326 za barabara ndani ya hifadhi na nyumba mbili za askari, imenunua magari saba ya doria, imenunua magunia 22,000 ya mahindi kwa ajili ya jamii inayoishi ndani ya hifadhi na madawati 2,000 kwa ajili ya shule za msingi wilayani humo. Ninayo furaha kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba Hifadhi ya Ngorongoro itachangia madawati 10,000 kwa wilaya nyingine za Tanzania ambazo hazizunguki katika eneo la hifadhi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuvo vya Taaluma ya Wanyamapori, katika mwaka 2015/2016; Chuo cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori Mweka, kilidahili wanafunzi 578 wa ngazi za cheti, *diploma* na *degree* ya Uhifadhi ya Wanyamapori, kimenunua magari mawili na kukarabati miundombinu ya chuo na kujenga nyumba moja ya wafanyakazi katika eneo la Kwakuchinja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kituo cha Elimu kwa Jamii Likuyu-Sekamaganga kilichopo Mkoa wa Ruvuma kilitoa mafunzo ya hifadhi shirikishi kwa watumishi 91 kutoka katika Halmashauri mbalimbali. Vilevile Taasisi ya Mafunzo ya Pasiansi ilidahili wanafunzi 441, imenunua magari matano na kujenga kambi ya mafunzo ya vitendo katika eneo la *Fort Ikoma*, kule Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), taasisi imekamilisha utafiti kuhusu ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa na kubaini kirusi kinachosababisha ugonjwa huo, kirusi hicho hutunzwa kwa asilimia kubwa na wanyamapori. Aidha, utafiti umeonesha kuwa chanzo cha mlipuko wa ugonjwa huo ni pale mazingira yanapowezesha mbu kuzaana kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, taasisi itafanya sensa ya wanyamapori katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, taasisi itaendelea na majaribio ya matumizi ya ndege zisizokuwa na rubani katika kuzuia tembo waharibifu wa mazao katika mifumo ya ikolojia ya Tarangire, Manyara, Serengeti na Ngorongoro. Vilevile utafiti kuhusu uhusiano kati ya nyuki na mimea utafanyika katika kanda zote Tanzania Bara. Utafiti huo utawezesha uchoraji wa ramani kulingana na aina ya mimea,

nyuki, asali na chavua katika maeneo husika. Kazi nyingine zitakazofanyika zimeainishwa katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori; katika mwaka 2015/2016, Mfuko umegharamia kazi za uhifadhi wanyamapori, utafiti na mafunzo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ndani ya mapori ya akiba. Katika mwaka 2016/2017, Mfuko unakadiriwa kukusanya shilingi bilioni 14.6. Fedha hizo zitatumika kugharamia doria dhidi ya ujangili ndani na nje ya mapori ya akiba, hususan doria za ndege zisizokuwa na marubani, ununuzi wa vifaa vya doria (magari, risasi, sare za askari, mahema na vifaa vya mawasiliano). Aidha, Mfuko utaendelea kugharamia miradi ya maendeleo ya jamii zinazozunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Ndogo ya Misitu; katika kuimarisha uhifadhi wa misitu na kuendeleza ufugaji wa nyuki nchini, Wizara yangu imeendelea kuboresha Sera za Misitu na Nyuki za Mwaka 1998. Maboresho hayo yanazingatia mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kimazingira yanayotokea ndani na nje ya nchi yetu. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya programu mpya ya misitu na nyuki kwa kipindi cha mwaka 2016- 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998, pamoja na mambo mengine, imesisitiza ushiriki wa wananchi katika upandaji na usimamizi wa misitu binafsi. Ili kufanikisha suala hili, Wizara imeanzisha programu ya panda miti kibiashara katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Ruvuma na Morogoro. Mpaka sasa vikundi 50 vya wapandaji miti vyenye wanachama 2,351 vimeundwa. Programu hii tayari imewezesha wananchi kupanda miti katika eneo la zaidi ya hekta 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma za Misitu (TFS); Wakala unaosimamia misitu ya hifadhi ya asili (*forest reserves*) unasimamia hifadhi hizo 506 zenye ukubwa wa hekta milioni 15.5 iliyotawanyika katika maeneo mbalimbali hapa nchini; misitu 11 iliyotengwa kama hifadhi za mazingira asili (*forest nature reserves*); misitu ya hifadhi lindimaji au *catchment forests*; na hekta 115,000 za misitu ya mikoko; mashamba 18 ya kupandwa yaliyomo katika mikoa 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizotekelezwa na Wakala katika usimamizi ni pamoja na usimamizi wa rasilimali za misitu, kuimarisha misitu hiyo, uendelezaji wa vivutio vya utalii ikolojia, kuendeleza ufugaji nyuki na elimu kwa umma na usimamizi wa mashamba ya miti ya kupandwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Wakala utaendelea na doria katika maeneo ya hifadhi za misitu, maeneo ya uvunaji, usafirishaji na kudhibiti biashara ya misitu haramu, kuendeleza utalii ikolojia, kuendeleza



kusimamia manzuki 90 zilizo katika kanda na mashamba ya miti na kuzalisha asali na nyuki, kuotesha miche ya miti zaidi ya milioni 17.9 na kupanda kwenye mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania; Mfuko huu unatoa fedha katika maeneo matatu ya kipaumbele ambayo ni uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za misitu, uboreshaji wa maisha ya jamii zinazozunguka jirani na misitu kupitia shughuli kama vile ufugaji wa nyuki, ufugaji wa samaki na utafiti unaolenga kuboresha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu. Katika mwaka 2015/2016, Mfuko uligharamia miradi 217 iliyokuwa inaendelea na miradi mipya 83. Katika mwaka ujao wa fedha, Mfuko utagharamia miradi 285 inayoendelea na miradi mipya 115.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Ndogo ya Utalii; Wizara inakamilisha na kuchapisha Kanuni za ada za leseni, Kanuni za huduma za malazi, Kanuni za wakala wa utalii na Kanuni za waongoza misafara ya utalii. Katika mwaka ujao wa fedha, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999 ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika Sekta ya Utalii Duniani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaandaa mpango mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza utalii nchini na kuainisha maeneo ya uwekezaji wa hoteli za kitalii katika Ukanda wa Pwani na maeneo mengine yenye vivutio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha mazingira ya biashara ya utalii nchini, katika mwaka 2015/2016, Wizara ilitekeleza mfumo wa kompyuta wa usajili wa watoaji leseni za kufanya biashara ya utalii. Mfumo huo umerahisisha ufuatiliaji wa biashara za utalii. Katika mwaka 2015/2016, Wizara ililenga kukusanya shilingi bilioni tano nukta tisa na hadi kufikia mwisho wa Aprili mwaka huu, shilingi bilioni nne nukta sita sawa na asilimia 79 tayari zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaandaa mradi wa kuboresha utalii kusini mwa Tanzania na inatekeleza mradi unaitwa *re-grow*. Mradi huo wa thamani ya dola za Kimarekani milioni 100 utasaidia kuendeleza utalii kusini mwa Tanzania hususan katika kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kuainisha maeneo kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya utalii kwa kuzingatia vivutio vilivyopo; kufanya ukaguzi wa biashara ya utalii na kufuatilia miradi ya utalii iliyokwishapitishwa na kituo cha uwekezaji. Aidha, Wizara itaunganisha mfumo wa kompyuta wa usajili na utoaji leseni na kufanya biashara ya utalii na mfumo wa TANAPA, Ngorongoro na TAWA. Lengo ni kuimarisha udhibiti na



kuhakikisha kuwa wakala waliosajiliwa na wenye leseni ndiyo wanaofanya biashara ya utalii na kuruhusiwa kuingia katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watalii wanaoingia na kuondoka nchini; uchambuzi wa awali umebaini kwamba katika mwaka 2015, mtalii mmoja alikaa nchini kwa wastani wa siku 10 na kutumia wastani wa dola za Kimarekani 263 kwa siku kwa wale wanaokuja katika *package tours* na wastani wa Dola 137 kwa *non-package tours*. Kwa mwaka 2015, idadi ya watalii waliokuwa wameingia nchini ni milioni 1,102,000,619 na wastani wa dola bilioni 1,938,000,000 zilipatikana.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania, Bodi hii iliratibu misafara ya mawakala wa utalii na waandishi wa habari 41 kutoka Nchi za China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu mwezi Oktoba mpaka Desemba mwaka jana. Aidha, Bodi ilishiriki katika kongamano la kuvutia wawekezaji na kutangaza utalii katika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu na kuratibu safari za kupanda Mlima Kilimanjaro kwa waandishi wa habari kutoka China. Katika mwaka ujao, Bodi ya Utalii ya Tanzania itaimarisha utangazaji kwa njia za TEHAMA, mitandao ya kijamii, *portal* na *Apps* zinazopatikana katika simu za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Waendesha Biashara ya Utalii, TANAPA na Ngorongoro, itaanza mikakati ya utangazaji wa utalii katika masoko makuu ya Uingereza, Ujerumani na Marekani na kuweka matangazo ya utalii katika magazeti ya *Safari Travel Magazines* katika nchi za Uingereza, Marekani, Afrika Kusini, Ujerumani na China.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala na maendeleo ya rasilimali watu, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeajiri watumishi 1,020 na kati ya hao, watumishi 554 ni wa kada ya wanyamapori na watumishi 400 kada ya misitu. Aidha, watumishi 118 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo, watumishi 491 wamethibitishwa kazini na watumishi 30 wamebadilishwa vyeo kwa kuzingatia miundo ya utumishi wa kada hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Shukrani zangu za dhati ziende kwa wananchi, hususan wanaoishi na kuzunguka maeneo yaliyohifadhiwa katika nchi yetu, hawa nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wao katika kulinda rasilimali za maliasili na malikale umechangia maendeleo ya nchi yetu kwa kiwango hicho ambacho nimekisema. Nachukua nafasi hii kuwaomba kuendelea kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzishukuru nchi na mashirika na taasisi mbalimbali kwa ushirikiano waliutoa kwetu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Nachukua fursa hii kutaja baadhi ya nchi hizo kama ifuatavyo:-

Canada, China, *Finland*, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ujerumani, Uswisi, Jumuiya ya Nchi za Ulaya na mashirika mbalimbali likiwepo *World Bank* na mashirika mengine zaidi ya 20 ambayo yameainishwa katika hotuba ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; Meja Jenerali Gaudence Milanzi, Katibu Mkuu wa Wizara; Mhandisi Angelina Madete, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi katika Idara, Vitengo, Taasisi, Wakala na Mashirika yaliyo chini ya Wizara yangu kwa ushauri na utayari wao katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru sana kwa kuzoea na kukiri kwamba sasa tunatekeleza mambo kwa mtindo wa hapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru sana wananchi wangu wa Wilaya ya Mwanga kwa kuniamini na kunipigia kura zilionipa ushindi mnono katika Uchaguzi Mkuu wa 2015. Napenda niwahakikishie kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda nimshukuru sana mke wangu mpenzi Kudra Maghembe na watoto wetu wote kwa upendo na misaada ya kila aina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika maombi ya fedha, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya jumla ya sh. 135,797,787,000 kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017. Kati ya fedha hizo sh. 118,051,105,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 17,746,682,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumlisha sh. 59,559,676,000. Fedha za mishahara ni sh. 58,458,429,000 za matumizi mengineyo. Fedha za miradi ya Maendeleo zinajumuisha sh. 15,746,682,000 fedha za nje na sh. 2,000,000,000 zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo ni [www.mnrt.go.tz](http://www.mnrt.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika. naomba kutoa hoja (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati naona Mheshimiwa Millya amerudi tumalize jambo lake.

Mheshimiwa Millya mwongozo ulisomwa hapa kuhusu mambo ambayo ulikuwa umeongea katika kikao cha Bunge hili tarehe 20 Mei, kumhusu Mheshimiwa Mhagama, sina haja ya kurudia, lakini unapewa fursa sasa ya kufuta kauli yako kwa mujibu wa kanuni ya 63(5). Hiyo ni fursa ya kufuta, kwa hiyo nitakaa nikuruhusu ufute hiyo kauli na kama hutafuta nitakueleza nini kitaendelea. Karibu!

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwenye mawasilisho yangu wakati wa hoja ya nishati na madini nilitaja jina la Mheshimiwa Jenista Mhagama, lakini kama utaangalia vizuri Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *hansard* nilisema ametajwa na nina ushahidi wa watu wanaomtaja huko chini, upo kwenye *message* za simu. Kwa hiyo, siyo *authority* yangu, kwa hiyo ninao.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuelewa.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, unapewa siku nne kuanzia tarehe ya uamuzi huu uweze kuthibitisha ushemeji wa Mheshimiwa Waziri hapa na huyo ambaye ulikuwa umemtaja kwenye mawasilisho yako. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea lakini hapa kuna maelezo kidogo kulikuwa na swali tena lingine, liliulizwa tarehe 22 Aprili na Mheshimiwa Aida Khenani lakini takwimu zilizotolewa zilikuwa zinahusu Mkoa ambao siyo alioliulizia swali.

Sasa swali lake lilikuwa linasema hivi suala la madai ya Walimu limekuwa ni tatizo sugu hususani kwa Walimu wa shule za Msingi na Sekondari; je, Serikali imechukua hatua gani ili kumaliza tatizo hilo? Swali hilo lilijibiwa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, majibu yaliyotolewa siku hiyo na Naibu Waziri yalikuwa yanahusu Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arumeru badala ya takwimu zinazohusu Mkoa wa Rukwa anakotokea Mheshimiwa Aida Khenani. Hivyo kwa kuzingatia

matakwa ya kanuni ya 45(3), naelekeza kuwa swali hilo ambalo halijajibiwa kikamilifu, sasa liulizwe tena siku ya Ijumaa tarehe 27 Mei, 2016 na Serikali ijiipange kulijibu kwa ufasaha.

Tunaendelea Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, *Engineer* Atashasta J. Nditiye, naomba kuwasilisha hotuba hii ya Kamati, lakini naomba taarifa yote iingie kwenye Taarifa Rasmi kwa maana ya *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 69) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 7(1) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inataja majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa ni:-

- (a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii;
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hii;
- (c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hii; na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1)(2), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya Ukaguzi wa Utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kisha kuchambua Bajeti ya Wizara inazosisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 na kuchambua Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inafafanua mambo makuu matatu yafuatayo:-

(i) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

(ii) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.

(iii) Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inajielekeza katika ufafanuzi wa masuala mbalimbali kwa mtiririko ulioelezwa katika kipengele cha kwanza nukta nne cha sehemu ya kwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016, ulijikita zaidi katika makusanyo ya maduhuli ukilinganisha na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Njia zilizotumika ni pamoja na kuangalia hali halisi ya makusanyo ya maduhuli, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye Kamati na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 96.4 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato yanayotokana na Sekta ya Maliasili na Utalii. Hadi kufikia Machi, 2016, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 53.7 ambazo ni sawa na asilimia 55.4 ya lengo la mwaka. Mwenendo wa makusanyo unaonesha Wizara haitafikia lengo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 66.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 45.2 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya mishahara na shilingi bilioni 21.077 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2016, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 43.4 sawa na asilimia 65.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.7 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 32.7 kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 7.7 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 5.7 ni fedha za nje na shilingi bilioni mbili ni fedha za ndani. Hadi kufikia Machi, 2016 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilikuwa shilingi bilioni moja, fedha za nje sawa na asilimia 12.9 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na fedha za matumizi mengineyo ni asilimia 10.4, kwa miradi ya maendeleo na asilimia 89.6 kwa matumizi mengineyo. Katika miradi kumi hakuna hata mradi mmoja ulioteklezwa kwa ufanisi. Utoaji huu wa fedha za maendeleo ni hatari kwa maendeleo ya sekta hii muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla fedha iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara ni kidogo na haikutolewa kwa wakati. Udhaifu huu wa kushindwa kutoa fedha kwa wakati na kwa kiasi kilichokusudiwa kunaathiri ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Wizara hivyo kuchangia kudumaza uchumi wa nchi yetu. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, katika fedha za maendeleo hakuna hata senti ya fedha za ndani iliyotolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Fungu 69 liliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 7.7 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Machi, 2016, Wizara ilipokea shilingi bilioni moja, kwa ajili ya kutekeleza mradi namba 4646 ujulikanao kama *Participatory Forestry Management Programme REDD na CCIAP*. Fedha hizi zilitumika kutoa mafunzo kwa wananchi wa wilaya zilizoteuliwa, kutoa mafunzo kwa Wakufunzi na Wakutubi wa Chuo cha Misitu Olmotonyi, kufanya ukarabati wa nyumba saba za chuo pamoja na kununua vifaa mbalimbali vya kusaidia kuhifadhi na kuendeleza misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu kwa mwaka wa fedha unaoisha zilikuwa fedha za nje na haukuwa umetengewa fedha zozote za ndani. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na taarifa iliyowasilishwa kuhusiana na matumizi ya fedha za mradi. Kamati imeielekeza Wizara kufanya ukaguzi maalum *special audit* katika mradi ili kubaini kama kuna ubadhirifu wowote na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi huu unaonesha kuwa Serikali haiweki mkazo wa kutosha katika miradi ya maendeleo kwa kutotenga fedha za ndani na hivyo kutegemea wadau wa Maendeleo pekee kufadhili miradi. Kwa utaratibu huu si rahisi kwa Serikali kufikia malengo yake iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilipanga kutekeleza miradi kumi ya maendeleo lakini ilitenga fedha za nje kwa ajili ya mradi mmoja tu. Kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kutopatikana kwa fedha kwa wakati kunachangia kuzorotesha utekelezaji wa miradi.

(ii) Serikali kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na kutegemea fedha za nje pekee kuna athiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio kutokana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

Kufanya siku za doria 106,320 ndani na nje ya mapori ya akiba na mapori tengefu ambapo nyara mbalimbali za Serikali zilikamatwa. Jumla ya watuhumiwa 849 walikamatwa na kesi 424 zilifunguliwa dhidi yao. Aidha, kesi 189 zilitolewa uamuzi na jumla ya sh. 219,673,659 zilikusanywa kutokana na watuhumiwa kutozwa faini;

Kuunda Bodi ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania pamoja na kuteua viongozi wa kukaimu nafasi mbalimbali za Watendaji;

Kukusanya na kuainisha Takwimu za Watalii wanaoingia nchini ambapo uchambuzi wa awali unaonesha kupungua kwa idadi ya watalii kwa asilimia nane kutoka milioni moja *point* moja mwaka 2014 hadi milioni moja *point* sifuri nne nane mwaka 2015;

Kukusanya dola za Marekani 41,200 kutokana na ukaguzi wa Wakala wa Biashara za Utalii; na

Kushiriki Mkutano Mkuu wa Wanachama wa UNESCO uliofanyika Novemba, 2015 Mjini Paris, Ufaransa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto pamoja na mafanikio yaliyopatikana; bado Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Kutokutolewa kabisa kwa Fedha za Maendeleo kwa baadhi ya miradi;

(ii) Uhaba wa Watumishi wa Sekta ya Maliasili na Utalii pamoja na vitendea kazi;

(iii) Ubovu wa Miundombinu katika maeneo ya Hifadhi za Taifa;

(iv) Uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za Maliasili na Malikale; na



(v) Kuendelea kwa matukio ya ujangili yanayoangamiza idadi kubwa ya Wanyamapori na kutishia uwepo wa tembo hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na mikakati iliyowekwa na Wizara ili kukabiliana na changamoto. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

Kuendelea kuajiri watumishi wapya kulingana na ikama pamoja na kuwathibitisha watendaji wanaokaimu nafasi mbalimbali;

Kuongeza ushiriki wa wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na shughuli za utalii;

Kukuza utalii wa ndani kwa kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vya utalii; na

Kufanya mapitio ya sera na sheria ili ziendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya ushauri umezingatiwa na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuifutia Kampuni ya *Eco-Energy* ya Bagamoyo hati ya kumiliki ardhi katika eneo lililokuwa na mgogoro kati yake na Hifadhi ya Taifa ya Saadan. Kamati inasisitiza Serikali kuliacha eneo lililokuwa linagombewa kutumiwa na Hifadhi ya Saadan kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kupambana na ujangili ikiwa ni pamoja na kuimarisha doria za kiintelijensia kwa kutoa mafunzo kwa watumishi, kununua vifaa muhimu na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na wananchi wanaozunguka hifadhi zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefurahishwa na hatua ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya stahili za askari walioshiriki katika Operesheni Tokomeza. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali kuweka utaratibu wa kuwalipa fidia au kufuta machozi wananchi walioathiriwa na operesheni hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono hatua zilizochukuliwa na Serikali kuachana na mfumo wa *double entry* na kuendelea na mfumo wa zamani wa *single entry* kwa watalii wanaoingia katika hifadhi zetu. Kamati inaamini kuwa kwa kutumia mfumo wa *single entry* ukusanyaji wa mapato

yanayotokana na utalii utaongezeka na hivyo kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika pato la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali kuandaa utaratibu wa kuongeza idadi ya watalii kwa kufungua masoko mapya katika nchi za Urusi, China, Japan na Singapore. Aidha, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali kufanya zoezi la kutambua vivutio vya utalii katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Kagera, Tanga, Iringa, Singida, Katavi, Rukwa na Mwanza. Jitihada hizi zisomeke katika utambuzi tu bali vivutio hivyo viendelezwe na kutangazwa ili viweze kujulikana kwa watalii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- (i) Kuhifadhi maliasili na malikale kwa kushirikisha wadau;
- (ii) Kuendeleza na kutangaza Utalii;
- (iii) Kuboresha mifumo ya ukusanyaji maduhulii; na
- (iv) Kudumisha na kuboresha ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato; katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni nne nukta moja ikiwa ni pungufu kwa asilimia 93.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 96.4 zilizokadiriwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa mapato unatokana na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania, ambayo itasimamia mapori 28 ya akiba na mapori tengefu 49 ambayo yalikuwa chanzo kikuu cha mapato ya Wizara. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017, Makusanyo kutoka kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, yataondolewa katika makadirio ya Wizara na kupelekwa kwa Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara ya Maliasili na Utalii inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 118.051 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 17.746 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa ujumla Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, imeongezeka kwa asilimia 43.8 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/2016. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bajeti ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi bilioni saba nukta moja mwaka 2015/2016 hadi shilingi 17.7 mwaka 2016/2017. Ongezeko hili linatokana na wadau wa maendeleo

kuongeza fedha katika miradi saba ya maendeleo baada ya kuridhishwa na utekelezaji wa miradi wanayoifadhili. Aidha, Serikali imetenga fedha za Ndani kiasi cha jumla ya sh. 2,000,000,000 kwa ajili ya Miradi minne ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kama inavyofahamika, Sekta ya Maliasili na Utalii ni mhimili wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu kwani ina mchango mkubwa katika Pato la Taifa unaofikia wastani wa asilimia 17. Mchango huo ni mdogo ukilinganishwa na fursa nyingi zilizopo hasa katika Hifadhi za Taifa, wanyamapori na malikale. Endapo sekta hii itasimamiwa kikamilifu na kuendelea kupewa kipaumbele na Serikali kwa kutangaza vivutio tulivyonavyo, ni dhahiri uchumi wa Taifa utaimarika na hatimaye kupunguza kwa kiasi kikubwa kiwango cha umasikini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Eneo la Utalii; Sekta ya Maliasili na Utalii inazo fursa nyingi ambazo zikitumika kikamilifu zitachangia kukuza Pato la Taifa na kwa kuwa Serikali haijawekeza vya kutosha katika sekta hii na kusababisha kuwa na mchango mdogo katika Pato la Taifa, Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali:-

- (a) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu. Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii lakini ni nchi ya zaidi ya 130 kwa kuingiza mapato yanayotokana na utalii. Hali hii haikubaliki;
- (b) Kufanya utafiti wa kutosha ili kubainisha maeneo mapya ya utalii na kuyaendeleza ili yaweze kuvutia watalii na hivyo kuongeza pato la sekta hiyo;
- (c) Kuendeleza miundombinu kama vile barabara, huduma za jamii kama vile hoteli, vyoo na maduka ya biashara ambayo yatakutia watalii wengi kutembelea vivutio vyetu;
- (d) Kufanya mapitio ya Sera na Sheria mbalimbali katika Sekta ya Maliasili na Utalii ili kuzifanya ziende na wakati na hivyo kuipa msukumo unaostahili Sekta ya Maliasili na Utalii;

- (e) Kuendeleza rasilimali watu ili kujenga uwezo wa kuhudumia watalii kwa ufanisi. Aidha, waongoza watalii wathibitishwe ili kufikia viwango vinavyohitajika katika huduma ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona sehemu nyingi za kuhudumia watalii hasa mahoteli zikiajiri wahudumu kutoka nchi jirani wakati tunalo jeshi kubwa la vijana wasio na ajira. Vilevile Serikali iandae mazingira yatakayowezesha vijana wa Kitanzania kushiriki katika Sekta ya Utalii ili kupunguza tatizo la kutegemea wageni hata katika nafasi ambazo Watanzania wangemudu;

- (f) Kupanga madaraja ya hoteli nchini ili kuiwezesha Serikali kutoza ushuru stahiki unaotokana na huduma za hoteli; na
- (g) Mitaala ya Chuo cha Utalii ihuishwe ili iweze kutoa mafunzo yakayokidhi mahitaji ya soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyamapori, ujangili bado ni changamoto kubwa, inayoikabili Sekta ya Wanyamapori kutokana na kupungua kwa wanyama kiasi cha kusababisha baadhi ya vitalu vya uwindaji kupoteza sifa na hivyo wawekezaji kuvirejesha Serikalini. Hali hii imesababisha kupungua sana kwa Mapato yatokanayo na uwindaji. Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali:-

(a) Kuimarisha kitengo cha intelijensia cha kupambana na ujangili kwa kukipatia vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja na kutumia ndege zisizoendeshwa na Rubani kwenye hifadhi zetu. Aidha, Serikali kupitia *special force* itoe elimu ya *tracking* kwa Askari wa Wanyamapori ili kuwaongezea uwezo wa kukabiliana na ujangili; *(Makofi)*

(b) Kuhakikisha kuwa kesi za ujangili zinasikilizwa haraka na adhabu kali zinatolewa kwa watakaokutwa na hatia. Tunaipongeza Serikali kwa kuwatia mbaroni watuhumiwa wa ujangili waliotungua helikopta katika Pori la Akiba la Maswa. Ni matarajio ya Kamati kwamba, kesi hii itasikilizwa kwa haraka na kutolewa uamuzi; *(Makofi)*

(c) Kuajiri Askari wa Wanyamapori wa kutosha, kununua silaha za kisasa pamoja na magari ya doria; na

(d) Kuweka wazi takwimu za hivi karibuni za idadi ya tembo nchini ili Watanzania kwa pamoja waamue ni jinsi gani wataokoa na kulinda rasilimali hii ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu na iko hatarini kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi duniani hupata mapato makubwa kutokana na utalii katika maeneo yenye vivutio vya malikale. Hata hivyo, Serikali haijawekeza vya kutosha katika maeneo mengi yenye vivutio vya aina hii na hivyo kukosa mapato. Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali:-

(a) Kuviendeleza vivutio vya malikale na kuvitangaza ili viweze kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini kuvitembelea na hivyo kuongeza mapato.

(b) longeze watumishi wa Sekta ya Malikale katika halmashauri zenye vivutio hivyo ili kuvitangaza; na

(c) Isimamie utunzaji wa majengo ya kale yanayomilikiwa na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makumbusho ya Taifa; duniani kote hasa katika nchi zilizoendelea, makumbusho ya Taifa ni moja kati ya vivutio vikubwa vya utalii, Serikali yetu haijatoa umuhimu unaostahili kwa sekta hii na hivyo kulikosesha Taifa mapato. Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali:-

(a) Itangaze makumbusho ya Taifa sambamba na vivutio vingine vya utalii; na

(b) Ihamasishe wananchi, kutambua, kuthamini na kutembelea makumbusho ya Taifa kama hatua ya kukuza utalii wa ndani; na

(c) Iboreshe miundombinu katika makumbusho ya Taifa ili kutunza na kuhifadhi utamaduni na mila za makabila na hivyo kuvutia watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misitū; Chuo cha Misitu Olmotonyi ndiyo chuo pekee kinachozalisha wataalam wa misitu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada, Hata hivyo, Serikali inaonekana kukitelekeza kwa kutokipa mahitaji muhimu na hivyo kukifanya kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kukitengea bajeti ya kutosha ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ulianzishwa ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendelezaji wa misitu nchini. Hata hivyo, Wakala hii haijaweza kutekeleza jukumu hilo kwa ukamilifu na kusababisha misitu mingi ya Serikali kuvamiwa na kuharibiwa vibaya. Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kupitia upya Sheria iliyoanzisha Wakala ili kuipa nguvu itakayoivezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wafugaji wanaozunguka maeneo hayo. Migogoro hii imesababisha uhasama baina ya mamlaka zinazohusika na

uhifadhi na wafugaji, pamoja na upotevu wa mali na uharibifu wa mazingira. Kamati inaishauri Serikali iandae mpango wa matumizi ya ardhi utakaoinisha maeneo kwa ajili ya malisho na shughuli nyingine za kijamii ili kuwawezesha wafugaji kutumia maeneo hayo badala ya kuvamia maeneo ya hifadhi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kasi kubwa ya uharibifu wa misitu unaosababishwa na wafanyabiashara haramu wa kuni, mkaa, mbaao na nguzo. Kwa kuwa, uharibifu huo umesababisha kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji, kutishia kuenea kwa jangwa nchini na kuchangia katika mabadiliko ya tabia nchi, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti ujangili wa misitu ili kuinusuru na kuiepusha nchi yetu na madhara yatoakanayo na uharibifu wa misitu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira ya uwazi kuhusu utaratibu wa utoaji wa vibali vya uvunaji wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shoroba nyingi zimevamiwa na wananchi kwa kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa kuwa, hali hii imezungua baadhi ya Shoroba kama vile za Ngorongoro, Ziwa Manyara, Tarangire na ile ya Mikumi, Wami Mbiki, Saadan na kuathiri mienendo asilia ya wanyama, Kamati inaishauri Serikali kuzifungua na kuzilinda Shoroba hizi ili wanyamapori waendeleo kupita katika njia zao za asili. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu wa kuzibainisha, kuzifungua na kuzilinda Shoroba zote zilizofungwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijatoa kibali cha kuruhusu kuwepo kwa kituo cha kulelea wanyamapori yatima kama tembo na wengine kilichopo Selian Mkoani Arusha. Kwa kuwa kituo hicho kimeanza kutunza wanyama hao bila ya kuwa na kibali, Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kukifunga kituo hicho mpaka taratibu za kuanzisha kituo kama hicho zitakapokamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume iliyoungwa na Serikali kuchunguza athari zilizotokana na Operesheni Tokomeza Ujangili imekamilisha kazi yake na kukabidhi ripoti yake Serikalini. Kwa kuwa, waathirika wa operesheni hiyo wana hamu ya kujua hatima yao, Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali iweke hadharani ripoti ya Tume hiyo ili waathirika hao wajue hatima yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma kama vile TANAPA na Mfuko wa Taifa wa Uhifadhi wa Wanyamapori, zimekaa muda mrefu bila kuwa na Bodi na hali hiyo imeathiri utekelezaji wa majukumu ya mashirika hayo. Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kuteua Bodi za Mashirika hayo mara moja ili kuyafanya yatekeleze majukumu yake kwa ufanisi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mipaka kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi wanaoishi kuzunguka maeneo hayo limeendelea kuwa changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii na imesababisha

mahusiano mabaya kati ya Hifadhi na wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kwa kuwashirikisha wananchi kutatua migogoro hiyo ili kuendeleza mahusiano mema kati ya vijiji na mamlaka zinazosimamia maeneo yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; mwisho lakini si kwa umuhimu, nakupongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Makatibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili na Ndugu Elihaika Mtui; Msaidizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Fungu 69 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati Eng. Atashasta J.Nditiye. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.



**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA  
YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA  
WAFEDHA WA 2015/2016 PAMOJA NA  
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA  
MWAKA WA FEDHA WA 2016/2017  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**1.2 Mheshimiwa Spika**, Fasili ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inataja majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa ni :-

- (e) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
- (f) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya wizara;
- (g) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za wizara ; na
- (h) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara;

**1.3 Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98(1), (2), ya kanuni za Kudumu za Bunge imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kisha kuchambua bajeti ya wizara inazozisimamia. Naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inahusisha Mafungu mawili: **Fungu 03 Tume ya Matumizi ya Ardhi na Fungu 48 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.**

**1.4 Mheshimiwa Spika**, Kimpangilio, Taarifa hii inafafanua mambo yafuatayo:-

- i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo;
- ii) Utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa mwaka 2015/2016;
- iii) Utekelezaji wa kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017;
- iv) Utekelezaji wa kazi za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na Mpango wa kazi za Shirika kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017;
- v) Utekelezaji wa kazi za Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na Mpango wa kazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017;
- vi) Utekelezaji wa kazi za Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na Mpango wa kazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 na;
- vii) Utekelezaji wa Kazi za Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni(KDA) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Mpango wa kazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017;

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya pili inajielekeza katika kutoa ufafanuzi wa masuala mbali mbali kwa mtiririko ulioelezwa katika kipengele 1.4 cha sehemu ya kwanza kwa namna ifuatayo;

#### 2.1 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016

##### 2.2.1 Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulijikita zaidi katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Njia zilizotumika ni pamoja na kuangalia hali halisi ya makusanyo ya maduhuli, kuzingatia taarifa mbali mbali zilizowasilishwa kwenye Kamati na

majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa tarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

## 2.3 UCHAMBUZI WA TAARIFA KUHUSU UKUSANYAJI WA MADUHILI

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi **billioni 70.00** kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato yanayotokana na sekta ya ardhi. Hadi kufikia Machi, 2016, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi **bilioni 55.12** ambazo ni sawa na asilimia 78.74 ya lengo la mwaka . Kati ya makusanyo hayo, shilingi **bilioni 48.61** sawa na asilimia 88.19 ya makusanyo zinatokana na kodi ya pango la ardhi. Mwenendo wa makusanyo unaonyesha wizara itafikia lengo lake hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2015/2016 endapo mfumo wa *Land Rent Management System* utatumiwa na Halmashauri zote nchini.

### 2.3.1 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **72,356,901,000/=**. Kati ya fedha hizo shilingi **54,635,187,000/=** zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi **14,262,718,000** kwa ajili ya Mishahara na shilingi **3,458,996,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2016, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **32,686,269,342/=**. Kati ya fedha hizo, shilingi **21,012,056,233/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **10,928,931,690/=** kwa ajili ya mishahara na shilingi **3.458,996,000/** ni fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa ujumla fedha zilizopokelewa hadi Machi, 2016 ni sawa na asilimia 45.1 ya fedha zilizotengwa. Aidha uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufikia Machi, 2016 wizara ilikuwa imepokea asilimia 38.2 ya fedha za matumizi mengineyo, asilimia 76.6 fedha za mishahara na asilimia 21.5 fedha za maendeleo. Vile vile uwiano wa wa tengeo la fedha za maendeleo na fedha za matumizi ya kawaida ni asilimia 4.78 fedha za miradi ya maendeleo na asilimia 95.22 fedha za matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Udhaifu huu katika kushindwa kutoa fedha kwa wakati na kwa kiasi kilichokusudiwa unaathiri ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Wizara hali inayochangia ongezeko la migogoro ya ardhi nchini.

## 2.4 USIMIKAJI WA MFUMO WA INTERGRATED LAND INFORMATION MANAGEMENT SYSTEM

**Mheshimiwa Spika**, Katika Hotuba ya bajeti ya mwaka wa Fedha 2015/2016 Waziri alilitaarifu Bunge kwamba wizara yake ingeanza kutumia mfumo wa utunzaji wa kumbu kumbu za ardhi yaani (*Intergrated Land Information Management System*). Kuanza kutumika kwa mfumo huu kulitarajiwa kupunguza migogoro ya ardhi na kuongeza ufanisi katika kuwapatia wananchi hati za kumiliki ardhi bila usumbufu wala urasimu. Hadi wakati Kamati inakutana na Wizara kwa ajili ya kujadili bajeti yake, ilibaini kuwa usimikaji wa mfumo huu umecheleweshwa na mchakato wa manunuzi ya vifaa vitakavyotumika na ikaiagiza Wizara kuhakikisha kwamba mchakato wa manunuzi unakamilishwa haraka na vifaa vinanunuliwa kwa wakati. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kwamba mfumo huu wa *Intergrated Land Information Management System* unasimikwa haraka ili kuongeza ufanisi katika utawala wa ardhi.

## 2.5 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

**2.5.1 Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Fungu 48 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **3,458,996,000/-** kwa ajili ya mradi namba 4943 unaojulikana kama *Land Tenure Support Programme* ambao ni mradi wa umilkishaji ardhi na unatekelezwa kwa majaribio katika Wilaya za **Ulanga, Kilombero na Malinyi** Mkoani Morogoro. Mradi huu unatekelezwa chini ya Kifungu 2001-Utawala wa Ardhi (Land Administration) cha Fungu 48.

### 2.5.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati I ilibaini kuwa mradi huu ni mpya na hadi wakati wa ukaguzi ulikuwa umepokea shilingi **745,281,420/-** sawa na asilimia 21.5 ya fedha zilizotengwa ambazo ni **3,458,996,000/=**. Fedha hizi zilitumika kufanya maandalizi ya awali ya kufungua Ofisi, kununua Samani na kuajiri wafanyakazi. Aidha fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu kwa mwaka wa fedha unaoisha zilikuwa fedha za nje na haukuwa umetengewa fedha zozote za ndani. Kamati iliridhishwa na maandalizi ya awali ya mradi na tunatarajia utatekelezwa vizuri endapo fedha zote za mradi zitatolewa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea ofisi ya Wakala wa uendelezaji wa mji mpya wa Kigamboni na kujionea jinsi ofisi hiyo ilivyo tulivu kwa kuwa hakuna shughuli za kufanya. Mradi wa kuendeleza mji mpya wa Kigamboni haujatekelezwa kwa muda mrefu sasa na hakuna dalili kama

Serikali ina nia ya kuutekeleza kwa vile kwa takriban miaka minane sasa imepita hakuna kinachoendelea zaidi ya maneno matupu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kukiri kwamba imeshindwa kuuendeleza mradi huo hivyo kuvunja ofisi za Wakala na kuwapangia kazi nyingine watumishi wa wakala badala ya kuendelea kulipa pango la ofisi na mishahara pasipokuwa na tija.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitembelea miradi ya ujenzi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) iliyoko Mwongozo-Kigamboni na Kinondoni Hananasifu. Kamati ilisikitishwa kuona baadhi ya nyumba za ghorofa moja katika mradi wa Muongozo zikiwa zimejengwa chini ya kiwango. Aidha bei ya nyumba hizo ni ghali kwa sababu zinatozwa VAT na vile vile zinajumuishiwa gharama za ujenzi wa miundombinu ambayo ingejengwa na Serikali ingepunguza gharama za nyumba hizo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huu unaonesha kuwa Serikali haiweki mkazo wa kutosha katika miradi ya maendeleo na kwa hali hii si rahisi kwa Serikali kufikia malengo yake iliyojiwekea.

### **2.5.3 Maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ilipanga kutekeleza miradi mitano ya maendeleo lakini ilitenga fedha za nje kwa ajili ya mradi mmoja tu wa *Land Tenure Support Programme*. Kutokana na hali hiyo kamati ina maoni yafuatayo:-

- (iii) Kutopatikana kwa fedha kwa wakati kunachangia kuzorotesha utekelezaji wa miradi
- (iv) Kutegemea fedha za nje pekee bila kuwa kutenga fedha za ndani kunaathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- (v) Kuendelea kutoa fedha kiduchu kwa miradi ya maendeleo kunapandisha gharama za mradi na hivyo kukwamisha malipo tarajiwa.

## **2.6 MAFANIKIO**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na bajeti hiyo iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Kusimika mfumo wa MOLIS( Management of Land Information System) katika Kanda za Kaskazini, Ziwa, Nyanda za juu Kusini na Kanda ya Kati na kutoa mafunzo kwa watumishi 12 . Mfumo huu unarahisisha utunzaji wa kumbu kumbu za ardhi na hivyo kurahisisha uandaaji na utoaji wa Hati Miliki;
- Kuanzisha ofisi nane za Kanda na hivyo kupeleka huduma za ardhi karibu ya wananchi;
- Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Nyumba;
- Kusimika mfumo wa Land rent Management System( LRMS) katika Ofisi 23 za ardhi zilizopo katika Halmashauri. Mfumo huu unaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa Maduhuli na hivyo kuongeza makusanyo yatokanayo na pango la ardhi.
- Kuhakiki Mashamba 151 yaliyobainika kuwa yametelekezwa na kubatilisha milki 88 za Mashamba hayo hivyo kupunguza migogoro ya ardhi nchini.
- Kuandaa na kutoa Hati miliki za Kimila 11,778 kwa wanavijiji hivyo kuwafanya wananchi kuwa na uhakika wa umiliki wa ardhi yao na kuwaongezea hadhi ya kukopesheka (Dhamana).
- Kutolewa kwa maelekezo ya Serikali kwamba Mthamini Mkuu wa Serikali asiidhinishe uthamini wa ardhi kabla ya kuthibitisha uwepo wa fedha za kulipa fidia.
- Kuanzisha kwa Mfuko wa Fidia.
- Kuondoa uwezekano wa madhara kwa binadamu na mali zao kwa kuvunja jengo la ghorofa 16 lililokuwa katika mtaa wa Indira Ghandi.

## 2.7 CHANGAMOTO

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- 2.7.1** Kutokutolewa kabisa kwa fedha za maendeleo kwa baadhi ya miradi.
- 2.7.2** Uhaba wa watumishi wa sekta ya ardhi kwa ujumla katika ngazi zote kuanzia Wizara, Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya.

Watumishi waliopo hivi sasa ni asilimia 24 tu ya mahitaji halisi, hali ambayo inachangia ufanisi hafifu wa Wizara.

- 2.7.3** Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali. Kwa mfano migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wawekezaji na wanavijiji, Serikali na wananchi inayotokana na sababu mbali mbali ikiwemo ucheleweshwaji wa kulipa fidia n.k;
- 2.7.4** Ufinyu wa pesa zinazotengwa kila mwaka kwa kitengo cha Mabaraza ya Nyumba. Kutokana na ufinyu huu, kasi ya kufungua mabaraza katika Wilaya mbali mbali imekwama;
- 2.7.5** Upungufu wa viwanja vilivyopimwa unaosababisha kuongezeka kwa ujenzi holela mijini hasa katika miji mikubwa inayoendelea kukua kwa kasi;
- 2.7.6** Kutokuwepo kwa ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali na ardhi ya akiba (Land Bank) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kunachangia kuleta migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Serikali na kati ya wananchi na wawekezaji;
- 2.7.7** Rushwa katika vitengo mbalimbali vya Wizara;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mikakati iliyowekwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto hizo. Kamati inaamini kwamba, endapo Wizara itaisimamia mikakati iliyojiwekea kwa kushirikiana na Wizara nyingine mathalani Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kupunguza urasimu katika zoezi zima la kutoa vibali vya kuajiri endapo itapewa kwa wakati fedha inazoidhinishiwa Wizara itafanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta maendeleo kwa Taifa kwani ardhi ndio msingi wa maendeleo kwa watu wote.

## **2.8 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya Ushauri umezingatiwa na kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali kuondoa tatizo la ucheleweshwa kulipa fidia pale Serikali inapotwaa ardhi ya wananchi. Kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 wizara



imetoa mwongozo kwa mamlaka na taasisi zote unaoelekeza kwamba **“Hakuna uthamini utakaoidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali kabla Halmashauri/ mlipa fidia kuthibitisha uwepo wa fedha za kulipa fidia”**. Aidha Serikali imeanzisha mfuko wa Fidia ambao kwa mwaka huu wa fedha umetengewa shilingi billion tano kwa ajili ya kulipa fidia pale Serikali inapotwaa ardhi kwa manufaa ya umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuvunja jengo la ghorofa kumi na sita lililoko katika mtaa wa Indira Ghandi jijini Dar ES Salaam ambalo Kamati iliitaka Serikali kulivunja mara moja ili kuepusha maafa ambayo yangeweza kutokea endapo lingeporomoka. Tunaishauri Serikali kuhakikisha kwamba ujenzi wa majengo ya ghorofa unafuata kanuni na taratibu zilizowekwa ikiwa ni kujenga kulingana na kibali kinavyoolelekeza pamoja na kupata cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaridhishwa na hatua ya Serikali kuandaa utaratibu wa kuondoa utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa mashirika yote yatakayojenga nyumba ambazo kwa tafsiri itakayowekwa na Serikali zinahesabiwa kama nyumba za gharama nafuu. Aidha sambamba na hilo Serikali inakamilisha maandalizi ya Sera ya Nyumba itakayoweka miongozo mbali mbali kuhusu masuala ya nyumba. Tunaipongeza Serikali kwa kulipa umuhimu wa kipekee suala hilo na kwamba utaratibu utakapokamilika utawawezesha wananchi wa kipato cha chini na kati kumudu kununua nyumba hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imechukua hatua za kumaliza sintofahamu kati yake na wananchi wa Kigamboni kwa kuweka mazingira wezeshi ambapo mmiliki wa ardhi katika eneo la mradi wa ujenzi wa mji mpya Kigamboni atakuwa na fursa ama ya kuuza eneo lake, kukopa benki na kuliendeleza mwenyewe kulingana na Masterplan au kuingia ubia na mwekezaji na kwamba sasa mgogoro kati ya wananchi wa Kigamboni na Serikali umekwisha. Tunaipongeza Serikali kwa kukamilisha uandaaji wa Masterplan ili utekelezaji wa mradi uanze mara moja. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba yale maeneo yaliyobainishwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu basi wananchi wanalipwa fidia zao kwa wakati ili kupisha mradi. Hata hivyo Kamati inachelea kusema kasi ya utekelezaji mradi huu iko chini sana na Serikali haijaupa mradi huu uzito unaostahili kwani licha ya kutengewa bajeti finyu, fedha hizo hazikupatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza utekelezaji wa ujenzi wa mji mpya wa luguruni ambapo Kampuni ya Surbana International Consultants imekamilisha maandalizi ya Mpangokina (Masterplan).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa katika masterplan iliyoandaliwa zitakuwepo pia nyumba za gharama nafuu ambapo watu wa kipato cha chini wataapata fursa ya kununua nyumba hizo. Ni matarajio ya Kamati kwamba mradi huo utanza kutekelezwa mara moja na kwamba utakapokamilika utapunguza msongamano wa watu kati kati ya jiji kwa vile huduma muhimu zitakuwa zinapatikana katika miji ya viungani kama Luguruni.

### **3.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

#### **3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- i) Kujenga Mfumo wa ki-elektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi;
- ii) Kuboresha maabara na karakana za utafiti wa vifaa vya ujenzi;
- iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mji mpya wa Kigamboni kupitia Wakala wa Mji mpya wa Kigamboni; na
- iv) Kuandaa Mpango wa matumizi ya ardhi katika sehemu mbali mbali nchini;
- v) Kuanza kutekeleza programu ya kupima Ardhi nchi nzima;
- vi) Kupima na kumilikisha Ardhi yote ya wilaya za Ulanga, Kilombero na Malinyi;
- vii) Kuanzisha mabaraza ya ardhi 50

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na malengo yaliyowekwa na Wizara kwani yakitekelezwa kwa ukamilifu yatachangia kupunguza migogoro ya ardhi na ujenzi holela mijini. Aidha upimaji wa ardhi na utoaji wa Hati Miliki utawawezesha wananchi kuwa na uhakika wa umiliki wa ardhi na kutumia hati zao kukopa kwa ajili ya maendeleo.

#### **3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **100, 010, 000,000/** ikiwa ni ongezeko la asilimia

42.8 ikilinganishwa na mapato ya mwaka 2015/2016. Mapato haya yanatokana na tozo mbali mbali za sekta ya ardhi huku ada za ardhi (Land Rent) ikiingiza mapato zaidi ikilinganishwa na vyanzo vingine. Ongezeko la mapato linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumo wa kielektronik yaani *Land Rent Management System*.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kwamba Serikali itahakikisha mfumo wa land Rent Management System unatumiwa na Halmashauri zote nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na ada ya ardhi.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kiasi cha shilingi **61,827,711,000/=**. Kati ya fedha hizo, shilingi **41,827,711,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **20,000,000,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa ujumla bajeti ya mwaka 2016/2017 imepungua kwa asilimia 17 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/2016. Pamoja na kupungua kwa bajeti ya Wizara kwa ujumla wake, bajeti ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi bilioni **3,458,996,000/** mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni **20,000,000,000/** mwaka 2016/2017. Ongezeko hili linatokana na Wadau wa maendeleo kuongeza fedha katika Mradi wa Land Tenure Support Programme kutoka shilingi **3,458,996,000/** mwaka 2015/2016 hadi shilingi **10,000,000,000/** mwaka 2016/2017 baada ya kuridhishwa na maendeleo ya mradi. Aidha serikali imetenga shilingi **3,000,000,000/** kama fedha za ndani kwa ajili ya mradi huo. Vile vile Serikali imetenga shilingi **7,000,000,000/** kwa ajili ya miradi mingine 4 ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi cha Shilingi **20,000,000,000/=** kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kinajumuisha fedha za ndani shilingi **10,000,000,000/=** na shilingi **10,000,000,000/=** kutoka kwa wadau wa maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha juhudi za wazi katika kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati imeridhia ongezeko hilo.

## SEHEMU YA TATU

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**4.1 Mheshimiwa Spika**, ardhi ni rasilimali ya msingi na ya muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo zinafanyika juu yake. Aidha, ardhi ni rasilimali adimu ambayo hushindaniwa na watu kwa ajili ya shughuli mbalimbali hivyo kuifanya iwe na thamani kubwa. Kwa

sababu hiyo ardhi inatakiwa kumilikiwa Kiserikali na Kimila kwa Sheria, Kanuni na taratibu zinazokubalika.

- 4.2 Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kasi ya ongezeko la watu nchini, thamani na umuhimu wa ardhi, ni vyema Serikali ikasimamia Sheria zake za ardhi kwa manufaa ya maendeleo ya kila mtanzania, na kuhakikisha ardhi ya nchi yetu haiuzwi/kumilikishwa ovyo kwa wawekezaji kutoka nje.
- 4.3 Mheshimwa Spika**, kwa kuwa asilimia 80 ya wananchi wa vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, na kwa kuwa mara nyingi viongozi wa vijiji huingia mikataba mibovu na wawekezaji, ni dhahiri kwamba Serikali isipokuwa makini katika suala la kumilikisha ardhi kwa wawekezaji na kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji, wananchi wataendelea kuwa maskini na watwana katika nchi yao wenyewe.
- 4.4 Mheshimiwa Spika**, Ardhi haiongezeki hata kwa inchi moja lakini idadi ya watu na shughuli za binadamu juu ya ardhi zinaongezeka kila uchao. Tusipopanga matumizi ya ardhi yetu mapema tutaongeza migogoro.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48 kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Sekta ya ardhi inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo za migogoro ya ardhi, ujenzi holela, kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi na kwa kuwa changamoto hizo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha uchumi, nguvukazi na utaiifa, Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali:-

- a) kuipatia Tume ya Matumizi ya Ardhi fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake ili Taifa lipunguze ama liepukane kabisa na migogoro hiyo;
- b) Kuelimisha umma na watumiaji mbali mbali wa ardhi ili watambue kwa uwazi mipaka ya ardhi wanayomiliki na matumizi yake na hivyo kuepusha wananchi kuvamia ardhi wasiyoimiliki;
- c) Kuanzisha mabaraza ya ardhi katika wilaya zote nchini ili wananchi wasilazimike kwenda umbali mrefu kutafuta huduma ya mabaraza hayo;
- d) Kutekeleza kikamilifu utaratibu wa kutotwaa ardhi ya wananchi kwa matumizi ya serikali au wawekezaji bila ya Mthamini Mkuu kujiridhisha kwamba fedha za kulipa fidia zipo;

- e) Kuhakikisha kwamba wamiliki wa ardhi wanaitumia ardhi wanayomiliki kwa matumizi yaliyoidhinishwa na siyo vinginevyo. Utaratibu huu utawazuiya wamiliki wa ardhi kutumia Hati zao kukopa fedha benki kwa matumizi mengine kinyume na matumizi yaliyoainishwa katika hati za umiliki;
- f) Pale ambapo Serikali imetwaa Mashamba makubwa yaliyotelekezwa, ihakikishe kwamba kabla ya kuyagawa Mashamba hayo kwa wananchi au wawekezaji, yapangiwe matumizi ya ardhi na hati zitakazotolewa zizingatie matumizi yaliyoainishwa;
- g) Halmashauri zote zinazokopa kwa ajili ya upimaji viwanja zinarejesha fedha hizo ili ziweze kukopeshwa kwa Halmashauri zingine na hivyo kufanya zoezi la upimaji kuwa endelevu;
- h) Kusimamia na kutekeleza Sheria ya Mipango miji kwani mbali ya changamoto ya ukuaji wa kasi wa miji, kumekuwepo pia na ukaidi wa makusudi wa wananchi kutotiisheria hiyo;
- i) Kuhakikisha kwamba Mamlaka zote zinazotoa vibali vya ujenzi wa majengo yanayozidi ghorofa tano zihakikishe majengo hayo yanafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kuepusha maafa yanayoweza kutokea endapo tathmini haitafanywa;
- j) Kuharakisha kuanza utekelezaji wa ujenzi wa mji mpya wa Kigamboni ikiwa ni pamoja na kulipa fidia kwa maeneo yale yatakayojengwa miundo mbinu. Aidha Serikali iwaelimishe wananchi wanaomiliki eneo la mradi wa Kigamboni jinsi ya ama kuingia ubia na wawekezaji, ama kuuza ardhi yao kwa bei ya soko au kukopa benki benki kwa kutumia Hati za ardhi na kufanya maendelezo ya maeneo yao kwa kuzingatia Masterplan;
- k) Kusitisha utozaji wa VAT kwa nyumba za gharama nafuu zinazojengwa na Mashirika ya Umma zikiwemo zile za Shirika la Nyumba la Taifa;
- l) Kuwekeza kwenye miundombinu katika maeneo yanayojengwa na Shirika la Nyumba la taifa ili kupunguza gharama za ujenzi na kuleta nafuu kwa wapangaji na wanunuzi wa nyumba;
- m) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwezesha Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na vifaa vya ujenzi;

- n) Kuunda Bodi ya Mfuko wa Fidia haraka ili eweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
- o) Kuanzisha mchakato wa kuhamisha ajira za sekta ya ardhi kutoka Halmashauri kwenda Serikali kuu; na
- p) Kutenga fedha za ndani za kutosha na kuzipeleka kwenye miradi kwa wakati ili kutekeleza miradi kwa ufanisi;

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Atashasta Nditiye, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Kemirembe Lwota, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Fredy Atupele Mwakibete, Mb Mjumbe
4. Mhe. Devota Minja , Mb
5. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb
6. Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb
7. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb
8. Mhe. Khalifa salim Suleimani, Mb
9. Mhe. Dkt Godwin Aloyce Mollel, Mb
10. Mhe. Magdalena Hamis sakaya, Mb
11. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb
12. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb
13. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb
14. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb
15. Mhe. Risala Kabongo, Mb “
16. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb
17. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
18. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb “
19. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb
20. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb
21. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
22. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb

23. Mhe. Omari Abdallah Kigoda, Mb

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kasilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussen, Makatibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili na Ndg Elihaika Mtui, Msaidizi wa Kamati Ndg Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Eng Atashasta J.Nditiye, (Mb)

**K/MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**  
21 Mei, 2016

**NAIBU SPIKA:** Sasa tutamsikia Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

**MHE. ESTER N. MATIKO – MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Maoni haya yanatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; ningependa hotuba yangu yote iingizwe kwenye *Hansard* kwa sababu nitakwenda kusoma kwa muhtasari tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa kuendelea



kuniamini na kuiteua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii. Napenda kumwahidi yeye binafsi na Kambi nzima ya Upinzani Bungeni kwamba; nitatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu, uadilifu na weledi mkubwa ili kuboresha utendaji wa Wizara hii kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso kwa kufanya kazi bega kwa bega ili kuhakikisha hotuba hii inafanyika kwa ustadi wa hali ya juu ili kuleta tija katika sekta hii ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee zaidi napenda kuishukuru sana familia yangu kwa kunitia moyo na kunivumilia wakati wote ninapokuwa mbali nao nikiteteleza majukumu yangu ya Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama nitaacha kutumia nafasi hii adhimu kuwashukuru Wanatarime Mjini kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao na kumshinda mgombea wa CCM. Maamuzi hayo si tu kwamba yameifanya dunia kutambua mabadiliko ya kiasili ya kimtazamo na kifikra ya kwamba jamii za watu wa Tarime haiongozwi na mwanamke bali pia yameniwezesha mimi kuandika historia ya kuwa Mbunge wa Jimbo wa kwanza mwanamke kutoka koo za Wakurya. Hii ni tunu adhimu ambayo nitailinda na kuiheshimu katika uhai wangu wote kwa kuhakikisha naitumikia vema jamii yangu na nchi yangu kwa upendo wangu wote, ujasiri wangu wote na kwa uzalendo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwapongeze pia Wabunge wanawake wenzangu wote kutoka vyama vyote tulioshinda Majimbo, ni wazi kazi iliyo mbele yetu pamoja na kulitumikia Taifa kupitia Bunge hili Tukufu. Pia kudhihirishia uwezo wetu na kuwa chachu kwa wanawake wengine wengi zaidi kusaka fursa za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba wanawake tunaweza, ni suala tu la kuonesha utashi na uwezo wetu kwa jamii, kwani kati ya wagombea tisa wanawake wa CHADEMA katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 25 Oktoba 2015, tuliweza kushinda wanawake sita na mwenzetu wa CUF hivyo, sisi tumeshinda leo hii ni Wabunge wa Majimbo na tumejumuika na mwenzetu mmoja kutoka CUF, tunaweza na hata wale wanaobeza uwepo wetu humu ndani ya Bunge ikiwemo na Wabunge wa Viti Maalum, hadi kutuita majina ya kudhalilisha na yenye vimelea vya dharau, wajue hata wao kiti wanachokikalia humu ndani Bungeni kilikuwa kikikaliwa na mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara hii, ila kabla sijafanya hivyo; napenda kunukuu maneno ya Abraham Lincoln aliyesema kwamba: *"The best way to predict your future is to create it."* Yaani namna bora ya kufikia ndoto ya maisha yako, ni kuanza kuyatengeneza maisha hayo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechagua kuanza na nukuu hiyo kwa sababu Serikali zote za CCM ikiwemo hii ya Awamu ya Tano; zimekuwa zikijigamba kwamba hakuna sababu ya Watanzania kuwa maskini kwa sababu Tanzania ina rasilimali nyingi zikiwemo maliasili za nchi yetu, lakini cha ajabu ni kwamba umaskini umeendelea kuitafuna Tanzania kwa miaka yote 55 ya uhuru chini ya utawala wa CCM licha ya rasilimali lukuki tulizobarikiwa kama Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka, Serikali zote za CCM ikiwemo hii ya Hapa Kazi tu! hazikuwekeza vya kutosha katika maliasili za nchi yetu ili kuweza kuwa na mavuno endelevu ambayo yangesaidia kufikia ndoto za wananchi za kuondokana na umaskini, lakini badala yake zikageuka kuwa madalali wa maliasili zetu tena kwa wageni jambo ambalo limeendelea kuchochea kasi ya umaskini nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo wa maneno ya Abraham Lincoln, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuanza kuboresha maisha ya Watanzania sasa kwa kuwekeza vya kutosha katika maliasili na utalii wa nchi yetu ili Taifa lifikie ndoto yake ya kuwa na uchumi wa kati na kuondokana na umaskini kama Mpango wa Taifa wa Maendeleo unavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii, Hoteli za kitalii ndani ya hifadhi takribani asilimia 80 ya watalii wanaoingia nchini hulala katika hoteli mbalimbali zikiwemo za ndani ya hifadhi. Licha ya hoteli za ndani ya hifadhi kuchangia kiasi kikubwa cha mapato ya Wizara hii, hoteli hizo zimekuwa na changamoto nyingi jambo ambalo linaloathiri ufanisi wake na mapato yatoakanayo na hoteli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya hifadhi kuna hoteli za wawekezaji wazawa na zile za raia wa kigeni, lakini hoteli za wazawa zimekuwa zikikumbwa na changamoto kubwa sana. Mathalani wakati wa msimu wenye wateja wachache kwa maana ya *low season*, hoteli za wawekezaji wa kigeni hutenga vyumba yaani hufanya *block booking* kwa wageni wao katika hoteli hizo za wazawa kwa kipindi cha muda mrefu na kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, inapofika kipindi cha msimu wenye wateja wengi *the high season*, tayari unakuta hoteli hizi za wazawa zinakuwa haziwezi tena kuuza vyumba hivyo na hawawezi tena kufaidika na bei za *high season* kwa kuwa vyumba hivyo vinakuwa vimeshachukuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, changamoto nyingine ni kwamba; fedha hii inayokuwa imelipwa kwa vyumba hivi vya hoteli za wazawa ni ndogo na inakatwa kodi kubwa, lakini hoteli zile za wawekezaji wageni hupokea wageni wengi kwa kipindi hicho cha *high season* kwa bei kubwa na huwa haikatwi kodi tena. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, imekuwa ni vigumu sana makampuni madogo ya utalii kuweza kumudu soko la ushindani kwa kuwa vipaumbele vya kupata vyumba vya hoteli kwa ajili ya kulaza wageni kutolewa kwa makampuni makubwa pekee na zaidi yale ya kigeni. Hii inasababisha makampuni madogo ya ndani kushindwa kuhimili soko la ushindani na mengi hufilisika kabisa. Suala hili sio tu linaua hoteli za wazawa hapa nchini bali pia linaisababishia Serikali hasara kubwa ya kupoteza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina Tume ya Haki ya Ushindani, (*The Fair Competition Commission*) ambayo imebainisha wazi katika tovuti yake kwamba: *“The Fair Competition condition has a mandate to regulate the competitive market. It also deals with all issues of anti- competitive conduct, abuse of dominance and has provision for curtailing merges and acquisitions if outcomes are likely to create dominance in the market or lead to uncompetitive behavior”*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri rahisi kabisa ni kwamba: “Tume hiyo ina mamlaka ya kuhakikisha kunakuwepo na kiwango cha uadilifu miongoni mwa washindani katika soko. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha jambo hili linatafutwa ufumbuzi kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kunusuru makampuni haya ya wazawa ili kuweza kumudu soko la ushindani wa kibiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutumbua pia majipu katika eneo hili ambapo wawekezaji katika hoteli za hifadhi wamekuwa wakiwanyonya wawekezaji wazawa na hivyo kudumaza juhudi za Serikali na wananchi za kukuza uwekezaji wa ndani katika sekta ya utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni ya kuendesha biashara ya utalii yaani *the tala licence* Licha ya hotuba ya Rais, Dkt. John Pombe Magufuli wakati akilizindua Bunge la Kumi na Moja mwezi Novemba, 2015 kueleza nia ya kuwasaidia Watanzania wanaotaka kuwekeza hapa nchini, hakuna dalili za

utekelezaji wa azma hiyo ya Serikali jambo linatoa taswira kuwa kauli ile ilikuwa ni ya kisiasa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu kumekuwa na urasimu na tozo nyingi za kuendesha biashara hii ya utalii jambo ambalo limekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wawekezaji wa ndani na hivyo kushindwa kumudu ushindani katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzigo mkubwa umewaelemea wafanyabiashara wadogo na wengi wao wako katika hatari ya kufunga biashara hizo kwa kushindwa kupambana kwenye soko la ushindani. Kwa mfano, katika malipo ya leseni, makampuni ya nje yanalipa dola elfu tano 5000 na makampuni ya Kitanzania ni dola elfu mbili 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba hiki kiwango cha *flat rate* ya dola 200 kitazamwe upya kwa kuwa kinawaumiza wawekezaji wadogo katika sekta hiyo. Mathalani, unakuta kampuni yenye magari matano inalipa tozo sawa na kampuni yenye magari 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tatizo hilo la tozo Serikali inawataka wafanyabiashara hawa wadogo katika Sekta hii ya Utalii kuwa na uwezo wa kumiliki idadi ya magari yasiyopungua matano ili waweze kupata leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha dhahiri kuwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inataka biashara ya utalii iendeleo kuhodhiwa na watu wachache wenye fedha nyingi jambo ambalo linaondoa dhana nzima ya uchumi shirikishi ambapo kila Mtanzania anatakiwa kuwa na fursa sawa katika kujenga uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu gharama ya kumiliki gari kwa ajili ya safari za utalii mbugani ni shilingi za Kitanzania kati ya milioni 120 mpaka milioni 200. Kwa hali hiyo, ni vigumu sana kwa Mtanzania wa kawaida kuweza kumudu gharama hizo na kuweza kumiliki magari matano ili aweze kupatiwa leseni ya kufanya biashara ya usafirishaji wa watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kubadili utaratibu wa sasa wa utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara wanaosafirisha watalii kwa kuondoa sharti la umiliki wa magari matano ndipo wapewe leseni ya kufanya biashara hiyo. Tunapendekeza kiwango cha umiliki wa magari kama kigezo cha kupata leseni kipungue angalau kifikie magari mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara za fedha za tozo katika hoteli za kitalii ndani ya hifadhi iliyopatikana kutokana na Serikali kukaidi amri ya Mahakama.

Kumekuwepo na mvutano mkubwa kati ya wamiliki wa hoteli zilizopo mbugani na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kutokana na wamiliki hao kukwepa kulipa tozo zilizowekwa na mamlaka hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvutano huo ulipelekea wamiliki hao kufungua shauri Mahakamani kupinga tozo hizo. Hata hivyo, katika shauri hilo, wamiliki wa hoteli hizo walishindwa na Mahakama Kuu Kanda ya Arusha ilimtaka Waziri wa Maliasili na Utalii kutangaza katika Gazeti la Serikali tozo mpya zitakazotumika katika mahoteli hayo ndani ya hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili zianze kutumika mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na maamuzi ya Mahakama, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira wakati ikishughulikia mgogoro huo wa wamiliki wa hoteli za mbungani na mamlaka hizo ilimshauri pia Waziri wa Maliasili na Utalii kupitia Azimio la Bunge kukazia hukumu ya Mahakama na kumpa muda hadi kufikia mwishoni mwa Februari, 2015 awe ameshatoa tangazo hilo. Serikali mpaka sasa imeshindwa kukazia hukumu hiyo jambo ambalo limeikosesha Serikali mapato ya Sh. 3,076,728,545 hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba Waziri wa sasa wa Maliasili na utalii hakuwa Waziri wakati Azimio la Bunge la kuitaka Serikali kukazia hukumu hiyo linapitishwa lakini alikuwa Mbunge na analifahamu Azimio hilo. Waziri huyu wa sasa hana cha kujitetea kwa kuwa kazi yake ni kutekeleza Maazimio ya Bunge hata kama hayakupitishwa wakati yeye akiwa Serikalini kwa kuwa Serikali ni hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kutokutimiza hukumu hiyo kunaisababishia Serikali hasara kubwa sana. Kutokana na uzembe huu wa hali ya juu wa Waziri binafsi na watendaji wake, tunaitaka mamlaka yake ya uteuzi ijiridhishe kama anafaa kuendelea kuongoza Wizara hii ikiwa hadi sasa anashindwa kuokoa zaidi ya shilingi bilioni sita za Kitanzania katika tozo za hoteli za mbugani ambazo Mahakama imeshaelekeza zikusanywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu katika sekta ya utalii. Utalii wa nchi yetu unategemea sana huduma bora katika viwanja vya ndege. Hali ya viwanja vya ndege nchini bado hairidhishi. Hali hii inaathiri mapato yatokanayo na utalii kwa kuwa ubovu wa miundombinu na huduma katika viwanja hivi inasababisha vishindwe kutumika kabisa au kutumiwa na wageni wachache kutokana na hadhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani uwanja wa *Kilimanjaro International Airport* hakuna taa za kutosha za kutoa ishara nyakati za usiku na ni hatari sana kwa waongoza ndege na abiria, mashine za kupokea mizigo ziko chache sana

na wageni husubiri muda mrefu sana ili kupokea mizigo na hakuna maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya wageni na hata wale wanaopokea wageni wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni kiwanja cha ndege cha Musoma kilichojengwa kwa kiwango cha changarawe na hivyo ndege nyingi haziwezi kutua. Uwanja wa Musoma ni muhimu hasa kwa wageni wanaotembelea Mkoa wa Mara kwa shughuli za utalii wa wanyama. Ni dhahiri uwanja huo ungeboreshwa ungechangamsha zaidi shughuli za kitalii kwa kuwa ni karibu na nchi jirani ya Kenya na pia ungehamasisha wageni kutembelea kaburi la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuboresha viwanja hivi vya ndege ili kuvutia wageni wengi zaidi na hata wawekezaji wanaotamani kuleta ndege zao hapa nchini waweze kuwa na uhakika wa usalama wa ndege zao na abiria wao. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha watendaji wote ndani ya viwanja hivi wanapata elimu ya namna ya kuwahudumia wateja kwa ukarimu zaidi *(customer care and hospitality)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuathirika kwa shughuli za utalii nchini. Suala la ulinzi na usalama kwa watalii wanaoingia nchini ni la muhimu sana kwa kuwa sekta ya utalii inachangia takribani asilimia 5.1 ya uchumi wetu sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 2.97 kwa mujibu wa *World Travel and Tourism Council of Tanzania* ya 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba suala la utalii siyo suala la Muungano kama inavyoanishwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kwa kuwa inahusisha moja kwa moja masuala ya fedha na uchumi ambao kimsingi ni suala la Muungano basi haina budi kulizungumzia kwa maslahi mapana ya uchumi wa Taifa letu ikiwa ni pamoja na namna ambavyo pato la utalii linaweza kuathiriwa endapo tutakosa siasa safi na uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar kama kitovu kikuu cha utalii wa fukwe na Tanzania Bara kama kivutio kikuu cha utalii wa wanyamapori, milima na malikale hutegemeana sana kwa kuwa watalii wengi wanaoingia Tanzania Bara huelekea Zanzibar kwa ajili ya utalii wa fukwe. Halikadhalika kwa wageni wengi wanaoingia Zanzibar hutembelea vivutio vya utalii vya Tanzania Bara. Utalii huu huathirika moja kwa moja pale panapotokea misugvano ya kisiasa baina ya vyama hasa nyakati za chaguzi kama ilivyotokea Zanzibar wakati wa uchaguzi mkuu mwaka huu kutokana na ukiukwaji wa demokrasia na utawala bora. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa Serikali itazame kwa kina athari za matukio ya kisiasa katika uchumi wetu hususani katika sekta hii nyeti ya utalii. Utulivu wa nchi, usalama, demokrasia na utawala bora ni kivutio cha kwanza katika utalii. Katika Serikali zilizostaarabika siku zote uchumi ndiyo unaobeba siasa (*the economy run politics*). Kwa bahati mbaya sana hapa kwetu siasa ndizo zinazoongoza uchumi. Hii inaonyesha kwamba bado tuna dola yenye matatizo (*the problematic state*). (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika gazeti la *New York Times*, nchi kama Srilanka iliwahi kupata hadhi ya kujulikana kama nchi ya kwanza duniani kwa kivutio cha watalii. Hata hivyo, kukandamizwa kwa demokrasia na misukosuko ya kisiasa nchini Srilanka kama inavyotokea Tanzania leo ilipelekea utalii wa nchi hiyo kushuka kwa kasi ya asilimia 43 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na hivyo kuanguka kabisa kwa uchumi wa nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu hasara iliyopatikana kutokana na matukio yaliyotokea nyakati za uchaguzi na kama imeathiri idadi ya watalii wanaoingia nchini baada ya uchaguzi na hata mpaka sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kutoa zabuni katika kuuza utalii nchini nje ya nchi. Mara nyingi kumekuwa na changamoto kubwa katika utaratibu wa utoaji zabuni katika shughuli mbalimbali za Serikali. Hii inapelekea kazi nyingi kushindwa kufanyika ipasavyo, kutumia fedha nyingi kuliko kusudio au kushindwa kufikia malengo tuliyojiwekea. Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kwamba katika mwaka wa fedha 2013/2014, Bodi ya Utalii nchini ilitoa zabuni ya kufanya matangazo ya utalii kwa timu ya *Sunderland Association Football Club* na *Seattle Sounders FC* mwaka 2014. Zabuni zilizotolewa ni namba PA/036/2013-14/NC/05 kwa *Sunderland* yenye thamani ya shilingi za Kitanzania 1,252,500,000 na zabuni namba PA/036/2013-14/NC/06 kwa *Seattle Sounders* yenye thamani ya Sh.1,593,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu mbele ya Bunge lako Tukufu kwa maswali yafuatayo:-

- (i) Je, Serikali ilitumia utaratibu gani katika kutoa zabuni hiyo?
- (ii) Kulikuwa na ushindani katika utangazwaji wa zabuni hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma (*The Public Procurement Act*)?
- (iii) Je, kufanyika kwa matangazo ya utalii kwa kutumia timu hizo ilikuwa kwenye mpango wa Bodi ya Utalii na kama kutolewa kwa zabuni hiyo haikuwa kwenye mpango wa Bodi bajeti ya kugharamia zabuni hiyo ilitoka wapi? (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, viumbe hai na wanyamapori. Biashara ya nyara hapa nchini inaoongozwa na Sheria namba 5 ya Wanyamapori ya mwaka 2009, Sehemu ya Kumi, kifungu cha 80(1). Leseni ambayo inatolewa kwa mujibu wa kifungu hiki inatolewa kila mwanzo wa mwaka wa leseni. Biashara hii ya usafirishaji wa viumbe hai kwa sehemu kubwa inahusisha ngedere, nyani, vyura, mijusi, konokono, kenge, ndege, nyoka na wadudu wengine watambao.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara hii imegawanyika katika madaraja 21 kulingana na aina ya kiumbe husika. Baada ya kupatiwa leseni mhusika hutakiwa kulipia ada kwa ajili ya viumbe husika Serikalini na hulazimika kuingia mikataba ya kibiashara ndani na nje ya nchi na wageni inawalazimu kwenda katika taasisi za fedha kukopa fedha za kufanyia kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeanza kwa kutoa utangulizi huo ili kueleweka vyema na kwamba pale inapotokea Serikali imekamata viumbe au wanyama waliopo katika orodha ya leseni siyo kwamba kuna rushwa bali ni Serikali kutafuta nani hasa wa kumrushia mzigo pale ambapo mambo yanaonekana kutokwenda vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilisitisha biashara hii tarehe 17 Machi, 2016 ikiwa ni miezi miwili na nusu baada ya msimu wa biashara hiyo kuanza rasmi tarehe 1 Januari, 2016 bila ya kuwashirikisha wadau wa sekta hii na bila sababu za maana. Hii inaweza kuitwa kuwa ni hujuma kwani tayari wafanyabiashara walikamata viumbe hao kwa ajili ya kuwasafirisha nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa leseni zao, maduhuli ya Serikali ni asilimia 10 ya thamani halisi ya mauzo ya viumbe hai nje ya nchi. Takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2008-2010 maduhuli yatokanayo na biashara ya hii ya nyara ilikuwa ni sh. 408,724,551. Takwimu za maduhuli kwa sasa zitakuwa zimepanda kutokana na wadau kuongezeka katika biashara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu za Wizara zinaonesha kuwa kuna makampuni zaidi ya 214 nchini yanayojihusisha na biashara ya nyara. Tukumbuke kuwa biashara hii inaongozwa na mgao unaopangwa na wataalam mbalimbali wa Idara ya Wanyamapori kwa kuzingatia matumizi endelevu kwa kila kiumbe husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya mapato ambayo Serikali inapata bado pia kuna ajira nyingi zinazotolewa na wafanyabiashara hao kwa wananchi wanapokuwa wanaenda kukamata viumbe hao. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kuruhusu wafanyabiashara ambao tayari wana mikataba ya kusafirisha na tayari wana mzigo wa

kuwasafirisha hao viumbe nje, kwa kusitisha barua ya tarehe 19 Mei, 2016 yenye kumbukumbu namba HD.28/563/01/83 iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusitisha kwa biashara ambayo tayari wahusika wamekatia leseni na biashara ni ya kipindi kifupi ni hasara kubwa sana kwa wahusika kwani tayari mitaji iko rehani. Tukumbuke kwamba katika biashara kupata soko ni kazi ya miaka kadhaa na kupoteza soko hicho ni kitu cha dakika kadhaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa chombo wezeshi kwa wafanyabiashara badala ya kuwa chombo cha kuwafilisi wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji unaofanywa na Serikali kwa wananchi wanaoishi jirani na hifadhi. Bado kumekuwepo na tatizo sugu la migogoro kati ya misitu ya hifadhi na wananchi wanaoishi vijiji jirani na hifadhi. Wananchi hao wamekuwa wakipatwa na madhila ikiwa ni pamoja na kufyekewa mazao yao, kupigwa na askari wa hifadhi, kufukuzwa katika nyumba zao, kubakwa na kutozwa faini zisizo za kimsingi na baadhi ya askari wa hifadhi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ni wananchi wa Kijiji cha Nyamikoma, Kata ya Kyanyari (Butiama) na wale wa Hifadhi ya Kyanyari ambao wanashindwa kufanya shughuli zozote za kimaendeleo kutokana na hifadhi za misitu kuweka mipaka ndani ya makazi ya wanakijiji hao. Aidha, katika kitongoji cha Kangamburi kuna kisima cha maji salama ya kunywa ambacho sasa hivi kipo ndani ya hifadhi hiyo ya msitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizopo ni kwamba Serikali imetoa tangazo kuwa wananchi hao wanatakiwa kuwa wamehama eneo hilo mpaka tarehe 9 Juni, 2016 ambapo mazao yao bado yapo mashambani na hayajakuwa tayari kwa ajili ya kuvunwa. Jambo baya zaidi ni kuwa Serikali haijatao eneo mbadala kwa ajili ya wanakijiji hao ili waweze kuanza makazi yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, vipo vijiji vingi nchini ambavyo vimepimwa na vina hati miliki lakini bado wanavijiji wanaoishi maeneo hayo wananyanyaswa sana na watendaji wa hifadhi. Iweje, Serikali itengeneze miundombinu katika vijiji hivyo husika zikiwemo shule, miundombinu ya maji, barabara, umeme halafu iwafukuze kwa hoja kuwa vijiji hivyo vipo ndani ya hifadhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Wabunge wengi kuzungumzia migogoro hii, bado Serikali inasuasua katika kutafuta ufumbuzi wa migogoro hii. Haijaonesha nia ya dhati katika kutafuta suluhu ya kudumu. Hivyo

basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri aingilie kati suala la migogoro ya Kijiji cha Nyamikoma na kile cha Hifadhi ya Kyanyari kwa kuwa wananchi hao wameishi hapo kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe inatafuta suluhu ya kudumu kwenye migogoro kati ya wananchi wanaoishi katika vijiji jirani na hifadhi. Pia Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu askari wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma kwa kudhalilisha utu wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, operesheni tokomeza. Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali, vitendo vya ujangili vinavyofanyika nchini vimegawanyika katika makundi mawili. La kwanza, ni ujangili wa kujikimu (*subsistence poaching*). Aina hii ya ujangili inahusisha watu wenye kipato kidogo na hulenga zaidi katika kujipatia kitoweo na fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji mengine. Ujangili wa aina hii huathiri zaidi wanyama wanaoliwa na siyo tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aina ya pili ni ujangili wa biashara (*commercial poaching*). Aina hii ya ujangili inahusisha zaidi watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha na hulenga kupata nyara zenye thamani kubwa. Wanyama wanaoathiriwa zaidi na aina hii ya ujangili ni pamoja na tembo, faru, simba na chui.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kulitambua hilo tarehe 4 Oktoba, 2013 ilizindua operesheni maalum ya kupambana na ujangili huo ili kuzuia vitendo hivyo ndani na nje ya hifadhi ya Taifa, katika mapori ya akiba na mapori tengefu. Pia kuwatambua mapema majangili na kujua nyendo zao ndani na nje ya maeneo ya hifadhi kwa kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wahusika wakuu wa nyara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya operesheni hiyo kufanya kazi kwa mujibu wa hadidu rejea tajwa, ni dhahiri hadi sasa wahusika wakubwa wa ujangili wa biashara hiyo bado wapo na wanaendelea na biashara hizo. Waathirika wakubwa ambao kwa mujibu wa Kamati Maalum ya Uchunguzi ya Bunge hili hadi sasa bado hawajalipwa fidia kama ilivyoelekezwa. Je, fidia kwa waathirika zitalipwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele imelia...

**WABUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Green Miles Safaris Limited*. Katika hotuba ya Maliasili na Utalii iliyowasilishwa Bungeni na aliyekuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani mnamo Mei, 2014, alilieleza Bunge hili kuhusu uwindaji haramu usiozingatia sheria na taratibu uliokuwa ukifanywa na Kampuni ya Uwindaji ya *Green Miles Safaris Limited*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwa kina namna Kampuni hii ya *Green Miles Safaris Limited* ilivyokiuka Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009, kifungu cha 19(1), 24(2), 42,47(a),(b)(i), 56, 64(2), 65(1)(a)(i),(iv) na (v) na Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007 na hivyo kupelekea Mheshimiwa Waziri aliyekuwa wakati huo kunyang'anya leseni ya kufanya biashara ya uwindaji hapa nchini. Ushahidi wa uhalifu huo wa uvunjifu wa sheria ulitolewa na wahusika walikubaliana nao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangaa ni kwa nini Mheshimiwa Waziri sasa kwa barua yake ya tarehe 9 Mei, 2016 yenye Kumbukumbu namba *SEC.315/563/01C/7* inaonekana kuwa inaipatia tena kampuni hiyo kitalu cha uwindaji wakati tayari ilikwishapokonywa leseni kwa kuwa ilivunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa barua hiyo inaonesha kuwa, Waziri anazuia kufanya uwindaji kwa kampuni ya *Wengert Windrose Safaris Limited* kuacha shughuli zake za uwindaji katika kitalu cha *Lake Natron Game Controlled Area East Hunting*. Hoja hapa ni je, kampuni hii iliingiaje kufanya shughuli zake katika kitalu hicho? Je, Kampuni ya *Green Miles* ilikuwa inafanya wapi shughuli zake hadi kampuni nyingine ikawa inafanyia shughuli za uwindaji katika kitalu hicho? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *dinosaur* (dinosari) kutoka Tanzania. Kabla ya vita kuu ya kwanza ya dunia mabaki ya mjusi ajulikanae kama dinosari yalipatikana eneo la Tendaguru Mkoani Lindi mwenye urefu wa mita za mraba takribani 22. Mabaki ya mjusi huyo yalichukuliwa na Serikali ya Ujerumani kwenda Mjini Berlin mwaka 1918 hadi 1919 kutoka Kijiji cha Mipingo Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya *DW* ya Januari 2016 inaonyesha kuwa watalii takribani 542,000 kwa mwaka 2015 walitembelea makumbusho ya mabaki ya mifupa ya mjusi huyu mkubwa zaidi duniani ukilinganisha na idadi ya watalii 463,000 waliotembea makumbusho hayo mwaka 2014. Hii inaonyesha idadi kubwa ya watalii inaongezeka mwaka hadi mwaka. Inaonesha mpaka sasa kila mtalii anayekwenda kumwona mjusi huyo analipa kiasi cha *Euro* 20 mpaka 25. Ni dhahiri ukijumlisha watalii 542,000 mara *Euro* 20 utaona ni kiasi gani cha fedha tunachopoteza na hili suala limekuwa likiongelewa humu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hitimisho, kama nilivyosema hapo awali, ili Taifa linufaike na utalii pamoja na maliasili za nchi yetu ni lazima Serikali iwekeze vya kutosha katika Sekta hizi za Maliasili na Utalii. Nilidokeza hapo awali kwamba ni aibu kwa Taifa hili ambalo linasifiwa duniani kuwa na maliasili zenye thamani kubwa pamoja na vivutio vya utalii vilivyotia fora duniani kuendelea kuzama katika lindi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoonona kitendawili kati ya utajiri tulionao na kuongezeka kwa umaskini, ujue lipo tatizo la kimsingi linalohitaji kutatuliwa. Tatizo hilo si lingine bali ni ukosefu wa mfumo wa uongozi ambao umeshindwa kutumia fursa za kiuchumi tulizonazo kuondoa umaskini ili kuifikia ndoto ya Taifa na ndoto ya Taifa letu ni kuhakikisha tunaondokana na umaskini tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa Serikali hii inayojigamba Hapa Kazi Tu wakati nchi haina usafiri wa ndege wa uhakika. Katika hali kama hiyo ni vigumu sana kunufaika na Sekta ya Utalii kutokana na ukosefu wa usafiri wa ndege wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapata tabu kuelewa kama kweli Serikali hii ina nia ya dhati ya kupata mapato katika Sekta ya Utalii? Nasema hivi kwa sababu Serikali haiko mstari wa mbele katika kutangaza utalii wa nchi yetu kutokana na ombwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko muda wako umekwisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** *One minute.*

**NAIBU SPIKA:** Naomba umalizie sekunde moja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** *Okay.* Kutokana na ombwe hilo nchi jirani kama Kenya inatumia vivutio vya Tanzania kutangaza utalii wake. Hii ina maana kwamba kama Tanzania ingekuwa imeshatangaza vivutio vyake kwa utoshelevu na dunia ikajua kwamba mlima Kilimanjaro mathalani uko Tanzania Kenya isingeweza kuutumia mlima ule kutangaza utalii wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kufanya mzaha na maliasili ya nchi yetu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther inatoshia.

**MHE. ESTHER N. MATIKO – MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**HOTUBA YA MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII, MHE. ESTHER NICHOLAS MATIKO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI WA MWAKA 2015/16 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya kanuni za Bunge toleo la mwaka 2016)*

---

## **1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/17. Aidha, napenda kumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mb) kwa kuendelea kuniamini na kunitiua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Napenda kumwahidi yeye binafsi na Kambi nzima ya Upinzani Bungeni kwamba; nitatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu, uadilifu na weledi mkubwa ili kuboresha utendaji wa Wizara hii kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Mali Asili na Utalii Mh.Cecilia Daniel Pareso kwa kufanya kazi bega kwa bega ili kuhakikisha kuwa hotuba hii inafanyika kwa ustadi wa hali ya juu ili kuleta tija katika sekta hii ya Mali Asili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee zaidi napenda kuishukuru sana familia yangu kwa kunitia moyo na kunivumilia wakati wote ninapokuwa mbali nao nikitekeleza majukumu yangu ya kibunge.

**Mheshimiwa Spika**, aidha nitakuwa mkosefu wa fadhila kama nitaacha kutumia nafasi hii adhimu kuwashukuru wanatarime mjini kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi kuwa mbunge wao na kumshinda mgombea wa CCM. Maamuzi hayo si tu kwamba yameifanya dunia kutambua mabadiliko ya kiasili ya kimtazamo na kifikra ya kwamba jamii za watu wa Tarime haziongozwi na mwanamke bali pia yameniwezesha mimi kuandika historia ya kuwa mbunge wa jimbo wa kwanza mwanamke kutoka koo za wakurya, hii ni tunu adhimu ambayo nitailinda na kuiheshimu katika uhai wangu wote kwa kuhakikisha naitumikia vema jamii yangu na nchi yangu kwa upendo wangu wote, ujasiri wangu wote na kwa uzalendo wangu wote. Aidha, niwapongeze pia wabunge wanawake wenzangu wote kutoka vyama vyote tulioshinda majimbo, ni wazi kazi iliyombele yetu pamoja na kulitumikia taifa kupitia bunge hili tukufu pia kudhihirishia uwezo wetu na kuwa chachu kwa wanawake wengine wengi zaidi kusaka fursa za kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, Ni wazi kwamba wanawake tunaweza ni suala tu la kuonyesha utashi na uwezo wetu kwa jamii, kwani kati ya wagombea tisa wanawake wa chadema katika uchaguzi mkuu wa 25 Oktoba 2015, sita tumeshinda na leo hii ni wabunge wa majimbo tukijumuika na mwenzetu mmoja kutoka CUF, tunaweza na hata wale wanaobeza uwepo wetu humu ndani ya bunge ikiwemo na wabunge wa viti maalum, hadi kutuita majina ya kudhalilisha na yenye vimelea vya dharau wajue hata wao kiti wanachokikalia humu ndani bungeni kilikuwa kikikaliwa na mwanamke.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara hii; ila kabla sijafanya hivyo; napenda kunukuu maneno ya Abraham Lincoln aliyesema kwamba; ***"The best way to predict your Future is to create it"*** - yaani namna bora ya kufikia ndoto ya maisha yako, ni kuanza kuyatengeneza maisha hayo sasa.

**Mheshimiwa Spika**, nimechagua kuanza na nukuu hiyo kwa sababu Serikali zote za CCM ikiwemo hii ya awamu ya tano; zimekuwa zikijigamba kwamba hakuna sababu ya watanzania kuwa maskini kwa sababu Tanzania ina rasilimali nyingi zikiwemo mali asili za nchi yetu. Lakini cha ajabu ni kwamba umaskini umeendelea kuitafuna Tanzania kwa miaka yote 55 ya uhuru chini ya utawala wa CCM licha ya rasilimali lukuki tulizo barikiwa kama taifa.

**Mheshimiwa Spika**, bila shaka, Serikali zote za CCM ikiwemo hii ya hapa kazi tu, hazikuwekeza vya kutosha katika maliasili za nchi yetu ili kuweza kuwa na mavuno endelevu ambayo yangesaidia kufikia ndoto za wananchi za



kuondokana na umasikini lakini badala yake zikageuka kuwa madalali wa maliasili zetu tena kwa wageni jambo ambalo limeendelea kuchochea kasi ya umasikini nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo wa maneno ya Abraham Lincoln, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuanza kuboresha maisha ya watazania sasa kwa kuwekeza vya kutosha katika maliasili na utalii wa nchi yetu, ili taifa lifikie ndoto yake ya kuwa na uchumi wa kati na kuondokana na umasikini kama Mpango wa Taifa wa Maendeleo unavyoelekeza.

## **2. SEKTA YA UTALII**

### **2.1. HOTELI ZA KITALII NDANI YA HIFADHI**

**Mheshimiwa Spika**, takribani 80% ya watalii wanaoingia nchini hulala katika hoteli mbalimbali zikiwemo za ndani ya hifadhi. Licha ya hoteli za ndani ya hifadhi kuchangia kiasi kikubwa cha mapato ya Wizara hii, hoteli hizo zimekuwa na changamoto nyingi jambo linaloathiri ufanisi wake na mapato yatokanayo na hoteli hizi.

**Mheshimiwa Spika**, ndani ya hifadhi kuna hoteli za wawekezaji wazawa na zile za raia wa kigeni. Lakini hoteli za wazawa zimekuwa zikikumbwa na changamoto kubwa sana. Mathalani wakati wa msimu wenye wateja wachache (low season) hoteli za wawekezaji wa kigeni hutenga vyumba yaani hufanya **“block booking”** kwa wageni wao katika hoteli hizo za wazawa kwa kipindi cha muda mrefu na kwa gharama ndogo (low price), hivyo basi inapofika kipindi cha msimu wenye wateja wengi (high season) tayari unakuta hoteli hizi za wazawa zinakuwa haziwezi tena kuuza vyumba hivyo na hawawezi tena kufaidika na bei za high season kwa kuwa vyumba hivyo vinakuwa vimeshachukuliwa (blocked). Aidha; changamoto nyingine ni kwamba; fedha hii inayokuwa imelipwa kwa vyumba hivi vya hoteli za wazawa ni ndogo na inakatwa kodi kubwa, lakini Hoteli zile za wawekezaji wageni hupokea wageni wengi kwa kipindi hicho cha high season kwa bei kubwa na huwa haikatwi tena kodi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, imekuwa ni vigumu sana makampuni madogo ya utalii kuweza kumudu soko la ushindani kwa kuwa vipaumbele vya kupata vyumba vya hoteli kwa ajili ya kulaza wageni kutolewa kwa makampuni makubwa pekee na zaidi yale ya kigeni. Hii inasababisha makampuni madogo ya ndani kushindwa kuhimili soko la ushindani na mengi hufilisika kabisa. Suala hili sio tu linaua hoteli za wazawa hapa nchini bali pia linaisababishia serikali hasara kubwa ya kupoteza mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Nchi hii ina Tume ya Haki ya Ushindani (Fair Competition Commission) ambayo imebainisha wazi katika tovuti yake kwamba:

***“FCC has a mandate to regulate the competitive market. “FCC deals with all issues of anti- competitive conduct, abuse of dominance and has provision for curtailing merges and acquisitions if outcomes are likely to create dominance in the market or lead to uncompetitive behavior”***

**Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri rahisi kabisa ni kwamba tume hiyo ina mamlaka ya kuhakikisha kunakuwepo na kiwango cha uadilifu miongoni mwa washindani katika masoko. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha jambo hili linatafutiwa ufumbuzi kwa kuwa ni wajibu wa serikali kunusuru makampuni haya ya wazawa ili kuweza kumudu soko la ushindani wa kibiashara. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutumbua pia majipu katika eneo hili ambapo wawekezaji katika hoteli za hifadhini wamekuwa wakiwanyonya wawekezaji wazawa na hivyo kudumaza juhudi za Serikali na wananchi za kukuza uwekezaji wa ndani katika sekta ya utalii.

## **2.2. LESENI YA KUENDESHA BIASHARA YA UTALII (TALA LICENCE)**

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya hotuba ya Rais John Pombe Magufuli wakati akilizindua Bunge la kumi na moja mwezi Novemba , 2015 kueleza nia ya kuwasaidia Watanzania wanaotaka kuwekeza hapa nchini; hakuna dalili za utekelezaji wa azma hiyo ya Serikali jambo linatoa taswira kuwa kauli ile ilikuwa ni ya kisiasa tu.

**Mheshimiwa Spika**, nasema hivi kwa sababu kumekuwa na urasimu na tozo nyingi za kuendesha biashara hii ya Utalii jambo ambalo limekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wawekezaji wa ndani na hivyo kushindwa kumudu ushindani katika sekta hiyo. Mzigo mkubwa umewaelemea wafanyabiashara wadogo na wengi wao wako katika hatari ya kufunga biashara hizo kwa kushindwa kupambana kwenye soko la ushindani. Kwa mfano katika malipo ya leseni, makampuni ya nje yanalipa dola elfu tano (\$5000) na makampuni ya kitanzania ni dola elfu mbili (\$2000).

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba hiki kiwango cha (flat rate) ya dola 200 kitazamwe upya kwa kuwa kwa kuwa kinawaumiza wawekezaji wadogo/ wachanga katika sekta hiyo. Mathalani, unakuta kampuni yenye magari 5 inalipa tozo sawa na kampuni yenye magari 300. Huu ni uonevu wa hali juu kwa wafanya biashara hawa wadogo na ni kinyume na kauli ya Rais katika kuwasaidia wafanyabiashara wadogo. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza tozo ya dola 1000 kwa wawekezaji wadogo . Aidha, tunapendekeza pia orodha ya tozo ipuguzwe ili kubaki na tozo chache ambazo ni nafuu ili wawekezaji wadogo waweze kumudu.

**Mheshimwa Spika**, Pamoja na tatizo hilo la tozo serikali inawataka wafanya biashara hawa wadogo katika sekta hii ya utalii kuwa na uwezo wa kumiliki idadi ya magari yasiyopungua matano (5) ili waweze kupata leseni. Hii inaonyesha dhahiri kuwa Serikali hii ya CCM inataka biashara ya utalii iendele kuhodhiwa na watu wachache wenye fedha nyingi jambo ambalo linaondoa dhana nzima ya uchumi shirikishi ambapo kila mtanzania anatakiwa kuwa na fursa sawa katika kujenga uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, nasema hivi kwa sababu gharama ya kumiliki gari kwa ajili ya safari za utalii mbugani ni shilingi za kitanzania milioni 120 mpaka 200. Bei ya chini kabisa ya gari ambalo limeshatumika, kwa umbali wa kilomita 400,000 na kuendelea ni milioni 25 na kuendelea. Kwa hali hiyo, ni vigumu sana kwa mtanzania wa kawaida kuweza kumudu gharama hizo na kuweza kumiliki magari matano ili apatiwe leseni ya kufanya biashara ya usafirishaji wa watalii.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kubadili utaratibu wa sasa wa utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara wanaosafirisha watalii kwa kuondoa sharti la umiliki wa magari matano ndipo wapewe leseni ya kufanya biashara hiyo. Tunapendekeza kiwango cha umiliki wa magari kama kigezo cha kupata leseni kipunguzwe hadi kufikia magari mawili.

### 2.3. UWEKEZAJI KATIKA IDARA YA UTANGAZAJI WA VIVUTIO VYA UTALII

**Mheshimiwa Spika**, Biashara ya Utalii ni matangazo. Pamoja na vivutio vingi vya utalii tulivyo navyo, kama vivutio hivyo havitatangazwa ipasavyo, tusitegemee kupata watalii wa kutosha na kwa sababu hiyo tusitegemee pia kukusanya mapato ya kutosha katika sekta hiyo. Ili tuweze kunufaika katika sekta hii kwa kiwango kinachokusudiwa ni lazima kuwe na mpango madhubuti na bajeti ya kutosha kufanya matangazo ya vivutio vyetu vya utalii nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, imeandaa mpango gani wa utangazaji wa vivutio vya utalii na imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kugharamia matangazo hayo kwa mwaka mpya wa fedha 2016/17. Lengo la kuitaka Serikali kufanya hivyo, ni kuisaidia kuwekeza katika utangazaji wenye tija, isije ikawa inatumia fedha nyingi kwenye utangazaji halafu faida inayopatikana ni ndogo kuliko fedha iliyotumika kufanya utangazaji. Hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani hapa ni kuwa na uwiano kati ya fedha tunazotumia kwenye utangazaji na tija inayopatikana (*proportional result between input and output*).

#### **2.4. HASARA FEDHA ZA TOZO KATIKA HOTEL ZA KITALII NDANI YA HIFADHI ILIYOPATIKANA KUTOKANA NA SERIKALI KUKAIDI AMRI YA MAHAKAMA**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na mvutano mkubwa kati ya wamiliki wa hoteli zilizopo mbugani na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kutokana na wamiliki hao kukwepa kulipa tozo zilizowekwa na Mamlaka hizo.

**Mheshimiwa Spika**, mvutano huo ulipelekea wamiliki wa hoteli hizo kufungua shauri mahakamani kupinga tozo hizo. Hata hivyo; katika shauri hilo, wamiliki wa hoteli hizo walishindwa na Mahakama Kuu Kanda ya Arusha ilimtaka Waziri wa Maliasili na Utalii kutangaza katika gazeti la Serikali tozo mpya zitakazotumika katika Mahoteli yaliyo ndani ya hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili zianze kutumika mara moja.

**Mheshimiwa Spika**, Mbali na uamuzi wa Mahakama, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira wakati ikishughulikia mgogoro huo wa wamiliki wa hoteli za mbugani na mamlaka hizo ilimshauri pia waziri wa Maliasili na Utalii kupitia azimio la Bunge kukazia hukumu ya Mahakama na kumpa muda wa hadikufikia mwishoni mwa Februari, 2015 awe ameshatoa tangazo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali mpaka sasa imeshindwa kukazia hukumu hiyo jambo ambalo limeikoshesha Serikali mapato ya Shilingi 3,076,728,545.57 hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba Waziri wa sasa wa Maliasili na utalii hakuwa waziri wakati azimio la Bunge la kuitaka Serikali kukazia hukumu hiyo linapitishwa, lakini alikuwa Mbunge na analifahamu azimio hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Waziri huyu wa sasa hana cha kujitetea kwa kuwa kazi yake ni kutekeleza maazimio ya Bunge hata kama hayakupitishwa wakati wake kwa kuwa Serikali ni hiyo hiyo. Kitendo cha kutokazia hukumu hiyo na kuisababishia Serikali hasara kubwa namna hii ni uzembe wa hali ya juu wa waziri binafsi na watendaji wake na tunaitaka Mamlaka yake ya uteuzi ijiridhe kama anafaa kuendelea kuongoza wizara hii ikiwa anashindwa kuokoa zaidi shilingi bilioni 3 za tozo katika mahoteli ya mbugani ambazo mahakama imeshaelekeza zikusanywe.

### 3. MIUNDOMBINU KATIKA SEKTA YA UTALII

#### 3.1 MIUNDOMBINU NA HUDUMA KATIKA VIWANJA VYA NDEGE

**Mheshimiwa Spika**, Utalii wa nchi yetu unategemea sana huduma bora katika viwanja vya ndege. Hali ya viwanja vya ndege nchini bado hairidhishi. Hali hii inaathiri mapato yatokanayo na utalii kwa kuwa ubovu wa miundo mbinu na huduma katika viwanja hivi vinasababisha vishindwe kutumika kabisa au kutumiwa na wageni wachache kutokana na hadhi zake.

**Mheshimiwa Spika**, Mathalani uwanja wa Kilimanjaro International Airport (KIA) hakuna taa za kutosha za kutoa ishara nyakati za usiku na ni hatari sana kwa waongoza ndege na abiria, mashine za kupokea mizigo ziko chache sana na wageni husubiri muda mrefu sana ili kupokea mizigo na hakuna maeneo maalum lililojengwa kwa ajili ya kupokea wageni. Jambo hili linaleta usumbufu mkubwa kwa wageni na hata wale wanaowapokea wageni hao. Mfano mwingine ni kiwanja cha ndege cha Musoma kilichojengwa kwa kiwango cha changarawe na hivyo ndege nyingi haziwezi kutua. Uwanja wa Musoma ni muhimu hasa kwa wageni wanaotembelea Mkoa wa Mara kwa shughuli za utalii wa wanyama. Ni dhahiri uwanja huo ungeboreshwa ungechangamsha zaidi shughuli za kitalii kwa kuwa ni karibu na nchi jirani ya Kenya, na pia ungehamasisha wageni kutembelea kaburi la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto za miundo mbinu na huduma ziko takribani kwenye viwanja vyote nchini ikiwa ni pamoja na Songwe, JKNA, Dodoma, Kigoma n.k. Athari za Changamoto hizi zilijionyesha dhahiri wakati wa mgogoro kati ya Tanzania na Kenya ambapo Idadi kubwa ya wageni waliokuwa wanakuja Tanzania walionyesha kuwa hushukia uwanja wa Jomo Kenyatta.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuboresha viwanja hivi vya ndege ili kuvutia wageni wengi zaidi na hata wawekezaji wanaotamani kuleta ndege zao hapa nchini waweze kuwa na uhakika wa usalama wa ndege zao na abiria pia. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha watendaji wote ndani ya viwanja hivi wanapata elimu ya namna ya kuwahudumia wateja kwa ukarimu zaidi (customer care and hospitality).

### 3.2 NJIA YA MALIPO KATIKA VIWANJA VYA NDEGE NA HUDUMA MBALIMBALI ZA HOTELI KWA WATALII (MODE OF SERVICE PAYMENT)

**Mheshimiwa Spika**, katika viwanja vyetu vya ndege na hata mahoteli ya kitalii nchini bado malipo mbalimbali yanafanyika kwa pesa taslimu (cash payment). Takribani 9.3% ya wageni wanaoingia nchini hulipa kwa kutumia credit card na 89.8% wanafanya malipo kwa njia ya fedha taslimu kwa mujibu wa ripoti ya International Visitor's Exit Survey Report ya mwaka 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika**, nchi nyingi duniani zinatumia mfumo wa kieletroniki wa kufanya malipo mbalimbali kwa njia ya kadi yaani (credit card) . Nchi nyingi zilizoendelea hutumia mfumo huu ili kupunguza hatari za kubeba fedha nyingi ikiwa ni pamoja na kuibiwa, kupoteza n.k

**Mheshimiwa Spika**, wageni wanapokuja nchini hukutana na changamoto za kulazimika kufanya malipo kwa njia ya fedha taslimu ilhali wengi wao hawasafiri na fedha.Wageni hawa wanakumbana na usumbufu mkubwa wa kuchukua fedha katika mashine (ATM) ili waweze kufanya malipo. Hali hii imewafanya wageni wengi wanaoingia nchini kupata usumbufu mkubwa na kuona nchi yetu ni nchi iliyojaa urasimu.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kuendelea kuruhusu tabia ya kutumia mfumo wa kizamani wa kupokea fedha taslimu ilhali njia ya kadi ni salama zaidi kwa wageni wetu na hupunguza mianya ya wizi, ubadhirifu na hata rushwa basi huko ni kuendelea kuturudisha nyuma kusikoendana na matumizi sahihi ya mabadiliko ya kiteknolojia. Mfumo huu ukitumiwa vizuri utarasihisha kuongeza zaidi manunuzi (purchasing power) ya bidhaa zetu za kitanzania zinazouzwa katika mahoteli na maeneo mengine ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuanza kuwaelimisha wadau wa sekta ya utalii kujua manufaa ya matumizi ya kadi (credit card),pia kuwahamasisha kuanza kutumia mfumo huu ili kuendana na soko la utalii la kimataifa,na kuendelea na mabadiliko ya kiteknolojia duniani.

Vilevile Kambi Rasmi inaitaka serikali kuhakikisha kuwa pale mgeni anapolipia fedha za visa anapewa risiti ya kieletroniki kama ilivyo katika mfumo wa serikali unaowataka wafanya biashara wote nchini kuzitumia.

### 3. 3. KUATHIRIKA KWA SHUGHULI ZA UTALII NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, Suala la ulinzi na usalama kwa watalii wanaoingia nchini ni la muhimu sana kwa kuwa sekta ya utalii inachangia takribani 5.1 % ya uchumi wetu sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 2,975.6 kwa mujibu wa World travel and tourism Council of Tanzania 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kwamba suala la utalii **SIO** suala la Muungano kama ilivyoanishwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kwa kuwa linahusisha moja kwa moja masuala ya fedha na uchumi ambao kimsingi ni suala la Muungano basi haina budi kulizungumzia kwa maslahi mapana ya uchumi wa taifa letu. Ikiwa ni pamoja na namna pato la utalii linaweza kuathiriwa endapo tutakosa siasa safi na uongozi bora.

**Mheshimiwa Spika**, Zanzibar kama kitovu kikuu cha utalii wa fukwe na Tanzania Bara kama kivutio kikuu cha utalii wa wanyama pori, milima na malikale hutegemeana sana, kwa kuwa watalii wengi wanaoingia Tanzania Bara huelekea Zanzibar kwa ajili ya utalii wa fukwe. Halikadhalika kwa wageni wengi wanaoingia Zanzibar hutembelea vivutio vya utalii Tanzania Bara. Lakini utalii huu huathirika moja kwa moja pale panapotokea misugvano ya kiasiasa baina ya vyama hasa nyakati za chaguzi kama ilivyotokea Zanzibar wakati wa uchaguzi mkuu mwaka huu kutokana na ukiukwaji wa demokrasia na utawala bora.

**Mheshimiwa Spika**, Ni lazima sasa serikali itazame kwa kina athari za matukio ya kisiasa katika uchumi wetu hususani katika sekta hii nyeti ya utalii. Utulivu wa nchi, usalama, demokrasia na utawala bora ni kivutio cha kwanza katika Utalii. Na katika serikali zilizostaarabika siku zote uchumi ndio hubeba siasa (economy run politics). Kwa bahati mbaya sana hapa kwetu siasa ndizo zinazoongoza uchumi. Hii inaonyesha kwamba bado tuna dola yenye matatizo (Problematic State).

**Mheshimiwa Spika**, Katika gazeti la New York Times, nchi kama Srilanka iliwahi kupata hadhi ya kujulikana kama nchi ya kwanza duniani kwa kivutio cha watalii. Lakini kukandamizwa kwa demokrasia na misukosuko ya kisiasa nchini Srilanka kama inavyotokea Tanzania leo ilipelekea utalii wa nchi hiyo kushuka kwa kasi ya asilimia 43 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na hivyo kuanguka kabisa kwa uchumi wa nchi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuliambia Bunge lako tukufu hasara iliyopatikana kutokana na matukio yaliyotokea nyakati za uchaguzi na kama yameathiri idadi ya Watalii walioingia nchini baada ya uchaguzi na hata mpaka sasa.



#### 4. UTARATIBU WA KUTOA ZABUNI KATIKA KUUZA UTALII NCHINI NJE YA NCHI

**Mheshimiwa Spika**, Mara nyingi kumekuwa na changamoto kubwa katika utaratibu wa utoaji zabuni katika shughuli mbalimbali za serikali. Hii inapelekea kazi nyingi kushindwa kufanyika ipasavyo, kutumia fedha nyingi kuliko kusudio, au kushindwa kufikia malengo tuliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kwamba katika Mwaka wa fedha 2013/2014 Bodi ya Utalii nchini ilitoa zabuni ya kufanya matangazo ya utalii kwa timu ya Sunderland Association Football Club na Seattle Sounders F.C Mwaka 2014

**Mheshimiwa Spika**, Zabuni zilizotolewa ni namba PA/036/2013-14/NC/05 ya Sunderland yenye thamani ya shilingi za Kitanzania 1, 252,500,000 na zabuni namba PA/036/2013-14/NC/06 ya Seattle Sounders yenye thamani ya Shilingi 1,593,000,000.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa majibu mbele ya Bunge lako kwa maswali yafuatayo:

- I. Je, serikali ilitumia utaratibu gani katika kutoa zabuni hiyo?
- II. Je, kulikuwa na ushindani katika utangazwaji wa zabuni hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma(Public Procurement Act)
- III. Je, kufanyika kwa matangazo ya Utalii kwa kutumia timu hizo ilikuwa kwenye Mpango wa Bodi ya Utalii (TTB) ? Na kama kutolewa kwa zabuni hiyo haikuwa kwenye mpango wa bodi Je, bajeti hiyo ya kugharamia zabuni hiyo ilitoka wapi?

#### 5. NANI MNUFAIKA WA RASILIMALI NA VIVUTIO VYA TANZANIA? JE, NI WATANZANIA AU MAJIRANI WA TANZANIA?

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na utangazaji wa vivutio vya utalii bado kuna shida kubwa katika kulinda, kuthamini na kutangaza fahari zetu. Hivi karibuni katika mitandao mbalimbali ya kijamii ilisambaa video moja ikionyesha binti wa Kenya akitangaza kuwa Mali Kale ya Olduvai Gorge(Oldupai) iko nchini Kenya. Pamoja na hayo kuna ujumbe wa aina mbalimbali ukionyesha kuwa Mlima Kilimanjaro unaonekana vizuri ukiwa Nchini Kenya kuliko Tanzania. Hata baadhi ya ndege za Shirika la Kenya zinatangaza mlima Kilimanjaro kuwa uko nchini Kenya. Mfano, baadhi ya ndege za Shirika la Kenya (Kenya Airways

maarufu kama KQ, zimeandikwa katika mbawa zake **“The home of Mount Kilimanjaro”** huku zikitumia alama ya Mlima Kilimanjaro”.Jambo hili limesababisha watalii wengi kupita nchini Kenya ili waweze kuuona mlima huo na hivyo kwa namna moja au nyingine inapunguza idadi ya watalii kuja kutembelea mbuga zetu, mali kale au hata Milima tuliyonayo. Hata kama uhalisia ni kuwa Mlima huo hauko nchini Kenya lakini ni mali halali ya Watanzania basi ni lazima kuhakikisha mtu yoyote anayetumia alama ya Mlima huu kujitangaza kibiashara ahakikishe anaruhusiwa na serikali ya Tanzania kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Inashangaza serikali imebaki kutoa makanusho badala ya mkakati madhubuti wa kutangaza zaidi vivutio vyetu hivi na kuhakikisha umiliki wake unatunufaisha ipasavyo.katika hali kama hiyo unakuta tayari taifa linakuwa limeshapata hasara.

**Mheshimiwa Spika**, Kukosekana kwa mkakati madhubuti (Strategic plan) wa kutangaza rasilimali na vivutio vyetu kunasababisha nchi nyingine kunufaika zaidi. Kuwepo kwa ubinafsi, uzembe uliokithiri unaofanywa na watu wachache na kutowatumia Watanzania wenzetu walio nje ya nchi vizuri katika kutangaza na kuuza fahari ya nchi yetu kunasababisha vivutio vyetu kutotangazwa ipasavyo. Hivyo ni lazima sasa serikali kutoa fursa kwa taasisi au watu wenye uwezo ili waweze kutangaza vivutio na rasilimali zetu kinkakati zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi inaitaka serikali hususani Wizara ya Maliasili na Utalii na Mamlaka nyingine chini ya Wizara hii kuhakikisha zinaitekeleza kazi zake kwa ufanisi ikiwa ni kutangaza kwa nguvu zaidi vivutio na rasilimali zetu. Ni vyema sasa Mheshimiwa Rais afanye ziara yenye tija ya kuwahamasisha Watanzania walio nje ya nchi kuweza kuwekeza hapa nchini hii ni kwa uzito wa nafasi yake na kuonyesha kuwathamini na kuwajali kaka na dada zetu walio nje ya nchi. Mwaka 2014 Rais Kenyatta wa Kenya alifanya ziara ya namna hii katika nchi za Ulaya ambapo alitoa hamasa kubwa kwa Wakenya kuwekeza nyumbani.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hayo Kambi Rasmi inataka kujua ni hatua gani zitakazochukuliwa na serikali endapo Taifa lolote litabainika kuwa 'linapoka' umaarufu wetu au kutumia rasilimali zetu pasipo makubaliano ?

## **6. VIUMBE HAI NA WANYAMA PORI**

### **6.1 VYURA WA KIHANSI**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni moja ya nchi iliyo na vivutio vya kipekee zaidi duniani. Vyura wa kihansi wajulikanao kitaalamu kama (Nectophrynoidea

apserginis) ni vyura pekee duniani wanaozaa na pia huwa wananyonyesha vitoto vyao tofauti na amphibia wengine. Vyura hawa wanaopatikana katika maporomoko ya milima ya Udizungwa, wanaishi katika maji yanayotiririka kwa kasi na yenye mvuke mwingi unaosababishwa na nguvu ya maji.

**Mheshimiwa Spika**, Vyura hawa wanatoweka kwa kasi kubwa sana kunakosababishwa na uharibifu mkubwa wa mazingira na kufanya miradi mbalimbali ya kibinadamu bila kuchukua **tahadhari** za utunzaji wa mazingira. Vyura hawa wangeliveza kuliingizia taifa pato kubwa sana kwa upekee wao, na vilevile kutengeneza ajira kwa vijana endapo wangehifadhiwa vizuri kama kivutio cha kipekee kwenye utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo mwaka 2009, tafiti zilionyesha vyura hao wanatoweka na hivyo serikali iliamua kuwasafirisha na kuwapeleka Chuo Kikuu cha Colorado nchini Marekani ili kutengenezewa mazingira bandia ya kuwazalisha. Kwa taarifa zisizo rasmi serikali ilikwisha warudisha baadhi ya vyura hawa kwa awamu ya kwanza ila bado inafanya utaratibu wa kuwarejesha wengine hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Ni wazi kuwa kwa kupeleka vyura hao nje ya nchi tumepoteza mamilioni ya fedha ambazo zingetumika kutoa elimu kwa jamii, kuboresha mazingira na hata kutengeneza mazingira mbadala kwa vyura hawa kuzaliana hapa hapa nchini. Serikali imekuwa dhaifu katika kuwatumia wataalamu wetu na hivyo kulisababishia taifa hasara kubwa ya kulazimika kuwapeleka viumbe hawa nje ya nchi bila kujali ni kwa namna gani upekee wa viumbe hawa utaathiriwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali ituambie inafanya mkakati gani wa kuwanusuru vyura hawa wa kipekee kabisa duniani ambao wako mbioni kutoweka ?Vilevile, ituambie kwamba vyura ambao walisalia nchini Marekani wote wamerudishwa?Je, imefanya tathimini kwa vyura hao kuhakikisha kuwa huko kubadilishiwa mazingira hakujawaletea vyura hao athari zozote ?

## 6.2. BIASHARA YA NYARA (TROPHY DEALERS LICENCE-TDL)

**Mheshimiwa Spika**, biashara ya viumbe hai hapa nchini biashara inayoongozwa na sheria Namba 5 ya Wanyamapori ya mwaka 2009, Sehemu ya Kumi, kifungu cha 80(1). Leseni ambayo inatolewa kwa mujibu wa kifungu hiki inatolewa kila mwanzo wa mwaka na leseni. Biashara hii ya usafirishaji wa viumbe hai kwa sehemu kubwa inahusisha; ngedere,nyani, vyura, mijusi, konokono, ndege, kenge, nyoka na wadudu wengine watambao. Biashara hii imegawanyika katika madaraja 21 kwa kulingana na aina ya kiumbe husika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupatiwa leseni mhusika hutakiwa kulipia ada kwa ajili ya viumbe husika serikalini na hulazimika kuingia mikataba ya kibiashara ndani na nje ya nchi na wengine inawalazimu kwenda katika taasisi za fedha kukopa fedha za kufanyia kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imeanza kwa kutoa utangulizi huo ili kueleweka vyema na kwamba pale inapotokea kwamba Serikali imekamata viumbe au wanyama waliopo katika orodha ya leseni sio kwamba kuna kuwa na rushwa bali ni Serikali kutafuta nani hasa wa kumrushia mzigo pale mambo yanapoonekana kutokwenda vyema.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilisitisha biashara hii tarehe 17 March, 2016 ikiwa ni miezi miwili na nusu baada ya msimu wa biashara hiyo kuanza rasmi tarehe 1 Jan.2016 bila ya kuwashirikisha wadau wa sekta hii na bila sababu za maana. Hii inaweza kuitwa kuwa ni hujuma kwani tayari wafanyabiashara walikamata viumbe hao kwa ajili ya kuvisafirisha nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa leseni zao, maduhuli ya serikali ni asilimia 10 ya thamani halisi ya mauzo ya viumbe hai nje ya nchi. Takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2008-2010 maduhuli yatokanayo na biashara ya hii ya Nyara ilikuwa ni shilingi 408,724,551/-, takwimu za maduhuli kwa sasa zitakuwa zimepanda kutokana na wadau kuongezeka katika biashara hii, kumbukumbu za Wizara zinaonesha kuwa kuna makampuni 214 nchi nzima yanayojihusisha na biashara ya nyara.

**Mheshimiwa Spika**, tukumbuke kuwa biashara hii inaongozwa na Mgawo (QUOTA) unaopangwa na wataalam mbalimbali wa Idara ya wanyamapori kwa kuzingatia matumizi endelevu (sustainable utilization) kwa kila kiumbe husika.

**Mheshimiwa Spika**, mbali ya mapato ambayo serikali inapata bado pia ajira zinazotolewa na wafanyabiashara kwa wananchi wanapopatikana viumbe hao. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe Waziri kuruhusu wafanyabiashara ambao tayari wanamikataba ya kusafirisha na tayari wana mzigo wa kusafirisha nje waruhusiwe, kwa kusitisha barua ya tarehe 19/05/2016 yenye kumb. Na. HD.28/563/01/83 iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.

**Mheshimiwa Spika**, kusitisha kwa biashara ambayo tayari wahusika wamekatia leseni na biashara ni ya kipindi kifupi ni hasara kubwa sana kwa wahusika kwani tayari mitaji yao iko rehani na tukumbuke kwamba katika biashara kupata soko ni kazi ya miaka kadhaa na kupoteza soko hilo ni kitu cha dakika kadhaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa chombo

wezeshi kwa wafanyabiashara badala ya kuwa chombo filisi kwa wafanyabiashara.

## **7. UJANGILI NCHINI MFUPA MGUMU KWA SERIKALI YA CHAMA CHA MAPINDUZI**

**Mheshimiwa Spika**, bado suala la ujangili nchini limekuwa ni tishio kwa wanyama na hata binadamu wanaofanya shughuli halali ndani ya hifadhi. Ujangili nchini umeiletea Taifa sifa mbaya Kimataifa. Vipo vyombo mbalimbali vya habari duniani vimekuwa vikitangaza uwindwaji haramu, utoroshwaji wa wanyama pori wakiwa hai, na mauaji ya wanyama pori hasa tembo yanayoendelea kutokea nchini. Vilevile, makampuni binafsi ya utalii, watu binafsi na hata mashirika walishirika katika harakati za kupaza sauti kuhakikisha kuwa tembo wetu wanalindwa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika ripoti ya utafiti kuhusu ujangili wa meno ya tembo uliofanywa na Benki ya dunia (WB), Shirika la Umoja wa Mataifa Kupambana na Madawa ya Kulevywa na Ujangili (UNODC) na Shirika la Polisi la Kimataifa (Interpol) ulibaini asilimia themanini na tano (85%) ya meno ya tembo yaliyokamatwa maeneo mbalimbali duniani yalitokea Tanzania. Mnamo mwezi Julai 2006 kilo 2,500 za meno ya tembo yenye vinasaba kutoka Tanzania yalikamatwa nchini Taiwan katika mji wa Kaohsiung, mwezi machi mwaka 2009 nchini Filipino katika mji wa Manila zilikamatwa kilo 3,300, na kilo nyingi zaidi takribani 6043 zilikamatwa mwezi Desemba 2012 katika mji wa Port Klang, Malaysia.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Bunge la Kumi(10) aliyekuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Wizara ya Mali Asili na Utalii katika hotuba yake ya mapato na matumizi ya wizara hiyo 2013/2014, alizungumzia suala la Ujangili kwa kina na hata kutaja jina la wakala wa meli iliyokamatwa ikielekea Hong Kong ikiwa imebeba shehena ya meno ya tembo kutoka Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutoa ufafanuzi kuhusu suala hilo aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii wakati huo alikiri kuwepo kwa tatizo hili kubwa la ujangili, na usafirishaji wa meno ya tembo kwenye meli iliyoitwa Delmas Nakadha chini ya mmiliki Bus Herman Ledley. Waziri huyo wa Maliasili na Utalii alikiri kukamatwa kwa watuhumiwa na kufunguliwa mashtaka. Japokuwa mpaka leo hatukuwahi kusikia mrejesho wowote katika Bunge hili tukufu au kupata taarifa yoyote endelevu juu ya kesi ile au kujua endapo watuhumiwa walishinda kesi, waliachiwa kinyemela au bado kesi inaendelea kwa kuwa kesi hizi za ujangili zimechukua na tabia ya kuchukua muda mrefu sana.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hii yenye falsafa ya kutumbua majipu ni lazima sasa ijielekeze katika kuwatumbua wale wote wanaohusika katika kukwamisha

kesi hizi ili zisimalizike kwa wakati. Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ituambie mbele ya Bunge lako ni nini kinaendelea katika kesi hizi na kwa nini kesi za ujangili zimekuwa zikichukua muda mrefu kumalizika?

## **8. UNYANYASAJI UNAOFANYWA NA SERIKALI KWA WANANCHI WANAOISHI JIRANI NA HIFADHI**

**Mheshimiwa Spika, bado** kumekuwepo na tatizo sugu la migogoro kati ya misitu ya hifadhi na wananchi wanaoishi vijiji jirani na hifadhi. Wananchi hao wamekuwa wakipatwa na madhila ikiwa ni pamoja na kufyekewa mazao yao, kupigwa na askari wa hifadhi, kufukuzwa katika nyumba zao, kubakwa na kutozwa faini zisizo za kimsingi na baadhi ya askari wa hifadhi wasio waaminifu. Mfano, wananchi wa kijiji cha Nyamikoma kata ya Kyanyari Butiama na wale wa hifadhi ya Kyanyari ambao wanashindwa kufanya shughuli zozote za kimaendeleo kutokana na hifadhi za misitu kuweka mipaka ndani ya makazi ya wanakijiji hao. Aidha katika kitongoji cha Kangamburi kuna kisima cha maji salama ya kunywa kunadaiwa kuwa kipo ndani ya hifadhi hiyo ya msitu.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa zilizopo ni kwamba Serikali imetoa tangazo kuwa wananchi hao wanatakiwa kuwa wamehama eneo hilo mpaka tarehe 9/6/2016 ambapo mazao yao bado yako mashambani na hayajakuwa tayari kwa ajili ya kuvunwa. Jambo baya zaidi ni kuwa serikali haijatoa eneo mbadala kwa ajili ya wanakijiji hao ili waweze kuanza makazi mapya.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Vipo vijiji vingi nchini ambavyo vimepimwa na vina hati lakini bado wanavijiji wanaoishi maeneo hayo wananyanyaswa sana na watendaji wa hifadhi. Iweje, serikali itengeneze miundo mbinu katika vijiji hivyo zikiwemo shule, miundombinu ya maji, barabara, umeme lakini iwafukuze kwa hoja kuwa vijiji hivyo vipo ndani ya hifadhi?

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada za Wabunge wengi kuzungumzia migogoro hii bado serikali inasua sua katika kutafutia ufumbuzi migogoro hii. Haijaonesha nia ya dhati katika kutafuta suluhu ya kudumu. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe Waziri aingilie kati suala la migogoro wa kijiji cha Nyamikoma, na na kile cha hifadhi ya Kyanyari kwa kuwa wananchi hao wameishi hapo miaka mingi sana. Serikali ihakikishe inatafuta suluhu ya kudumu kwenye migogoro kati ya wananchi wanaoishi vijiji jirani na hifadhi. Pia serikali iwachukulie hatua za kinidhamu askari wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma kwa kudhalilisha utu wa wananchi wetu.

### **8.1 OPERATION TOKOMEZA**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taarifa ya Serikali, vitendo vya ujangili vinavyofanyika nchini vimegawanyika katika makundi mawili yafuatayo:-

**i. Ujangili wa Kujikimu (*subsistence poaching*)**

Aina hii ya ujangili inahusisha watu wenye kipato kidogo na hulenga zaidi katika kujipatia kitoweo na fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji mengine. Ujangili wa aina hii huathiri zaidi wanyama wanaoliwa na si Tembo.

**ii. Ujangili wa Biashara (*commercial poaching*)**

Aina hii ya ujangili inahusisha zaidi watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha na hulenga kupata nyara zenye thamani kubwa. Wanyama wanaoathiriwa zaidi na aina hii ya ujangili ni pamoja na Tembo, Faru, Simba na Chui.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kulitambua hilo tarehe 04 Oktoba 2013 ilizindua Operation Maalum ya kupambana na ujangili huo ili kuzuia vitendo hivyo ndani nan je ya hifadhi za Taifa, katika Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu. Pia kuwatambua mapema majangili na kujua nyendo zao ndani na nje ya maeneo ya hifadhi kwa kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wahusika wakuu wa nyara hizo za Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, badala ya Operation hiyo kufanyakazi kwa mujibu wa hadidu rejea tajwa, ni dhahiri hadi sasa wahusika wakubwa wa ujangili wa Biashara bado wapo na wanaendelea na biashara hizo. Waathirika wakubwa ambao kwa mujibu wa kamati maalum ya Uchunguzi ya Bunge hili hadi sasa bado hawajalipwa fidia kama ilivyoelekezwa. Je fidia kwa waathirika zitalipwa lini?

**Mheshimiwa Spika**, Rais wa awamu ya nne aliunda Tume maalum iliyoongozwa na Mhe Jaji Msumi ya kushughulikia suala hilo, lakini kwa bahati mbaya taarifa ya Tume hiyo hadi sasa imeishia kwenye makabati ya Ikulu na Watanzania hawakupata nafsi ya kuelewa nini Jaji Msumi aliona na kushauri, aidha hakuna hatua zozote za fidia zimechukuliwa kwa waathirika wa Operation hiyo ambao wengi walipoteza mifugo yao, walichomewa nyumba zao, walibakwa, walidhalilishwa na wengine walipoteza ndugu na jamaa zao na wengine wamekuwa walemavu.

**Mheshimiwa Spika**, ni muda mwafaka sasa Kambi Rasmi kutaka kuelewa ni majangili wangapi baada ya Operation hiyo kumalizika mali zao zimekamatwa na tayari kesi zao ziko mahakamani au tayari wamefungwa?

**Mheshimiwa Spika**, katika kuweka kumbukumbu sawa naomba kunukuu sehemu ya taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na mazingira ya mwaka 2015/16;



**Mheshimiwa Spika**, taarifa hiyo imewapa masuala makubwa wananchi kwa kuwa Ripoti ya Kamati ya Bunge iliyochunguza sakata hilo haikuwatia hatiani mawaziri hao bali waliwajibika kwa makosa yaliyofanywa na maafisa waliokuwa wanawasimamia. Watanzania wanajiuliza, Ripoti inasema nini kuhusu wananchi waliouliwa, wananchi walioteswa, walioporwa mifugo yao na ambao mifugo yao ilipigwa risasi? Ni busara kwa Serikali kuweka hadharani Ripoti hiyo ya Tume ya Kimahakama ili watanzania waweze uamini kama haki imetendeka kwa wote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa suala la kuchelewa kutoa hukumu na wakati mwingine ushahidi wa kesi za ujangili kuharibiwa ni changamoto kubwa katika mapori ya akiba na Hifadhi za Taifa, Kamati inatoa rai kwa vyombo vya Serikali kama vile Jeshi la Polisi na Mahakama kushirikiana na Idara ya wanyamapori kuhakikisha watuhumiwa wa kesi za ujangili wanashtakiwa kwa kupewa adhabu kali kwa mujibu wa Sheria. Kamati haipendi kuamini kuwa kesi hizi zinahujumiwa kutokana na askari polisi na mahakimu wachache kujihusisha na vitendo vya rushwa”.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliahidi kuwa wananchi hao watalipwa fidia lakini mpaka leo imekaa kimya. Kitendo cha kukaa kimya maana yake ni kwamba haijajali madhila wananchi wake waliyoyapata. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili kuwa ina mpango gani wa kuwalipa wananchi hawa fidia?

## 9. KAMPUNI YA GREEN MILES SAFARIS LIMITED

**Mheshimiwa Spika**, Katika hotuba ya Maliasili na Utalii iliyowasilishwa Bungeni na aliyekuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani mnamo Mwezi May 2014, alilieleza Bunge hili kuhusu uwindaji haramu usiozingatia Sheria na taratibu uliokuwa ukifanywa na kampuni ya uwindaji ya Green Miles Safaris Limited.

**Mheshimiwa Spika**, katika ripoti hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilielezea kwa kina namna kampuni hii ya Green Miles Safaris Limited ilivyokuwa imekiuka Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2009, kifungu cha 19(1), 24(2), (42),(47) (a),b(1),(56), 64(2), 65(1)a (i),(iv) na (v) ,na Sera ya Manyama Pori ya Mwaka 2007. Na, hivyo kupelekea Mhe Waziri aliyekuwepo wakati huo kuwanyang'anya Leseni ya kufanya biashara ya uwindaji hapa nchini. Ushahidi wa uharifu huo wa uvunjifu wa sheria ulitolewa na wahusika walikubaliana nao.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangaa, ni kwanini Mheshimiwa Waziri wa sasa kwa barua yake ya tarehe 9 may,2016 yenye Kumb. Na.SEC.315/563/01C/7 inaonekana kuwa inaipatia tena Kampuni hiyo kitalu cha uwindaji wakati tayari ilikwisha pokonywa leseni kwa kuwa ilivunja sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kwa barua hiyo hiyo inaonesha kuwa Waziri anaizuia kufanya uwindaji kampuni ya Wengert Windrose Safaris Ltd kuacha shughuli zake za uwindaji katika kitalu cha **Lake Natron Game Controlled Area (East) Hunting**. Hoja hapa ni je Kampuni hii iliingiaje na kufanya shughuli zake katika kitalu hicho? Na je, Kampuni ya **Green Miles** ilikuwa inafanyia wapi shughuli zake hadi kampuni nyingine ikawa inafanyia shughuli za uwindaji katika kitalu hicho?

## 10. MALI KALE

### 10.1 DINOSARI KUTOKA TANZANIA (DINOSAUR FROM TANZANIA)

**Mheshimiwa Spika**, Kabla ya vita kuu ya kwanza ya dunia mabaki ya mjusi mkubwa ajulikanae kama dinosari yalipatikana eneo la Tendaguru mkoani Lindi mwenye urefu wa mita za mraba takribani 22. Mabaki ya mjusi huyo yalichukuliwa na serikali ya Ujerumani kwenda mjini Berlin mwaka 1918 hadi 1919 kutoka kijiji cha Mipingo mkoa wa Lindi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa ripoti ya DW ya Januari 2016 inaonyesha kuwa watalii takribani 542,000 kwa mwaka 2015 walitembelea makumbusho ya mabaki ya mifupa ya mjusi huyu mkubwa zaidi duniani ukilinganisha na idadi ya 463,000 ya watalii waliotembea makumbusho hiyo mwaka 2014. Hii inaonyesha idadi ya watalii hao inaongezeka mwaka hadi mwaka kulingana na umuhimu wa kihistoria wa mijusi wa aina hii.

**Mheshimiwa Spika**, tukirejea katika kumbumbuku za mabunge yaliyopita suala la mjusi huyu lilijadiliwa na aliyekuwa Waziri wa Mali asili na Utalii Mheshimiwa Shamsa Mwangunga .Alieleza mbele ya Bunge hili kuwa serikali inafanya tathimini kujua faida na hasara za kumleta mjusi huyo nchini ikiwemo gharama za kumsafirisha na kujenga jengo la ghorofa tatu kwa ajili ya kumuhifadhi au namna ya kuzungumza na serikali ya Ujerumani ili wabaki na mjusi huyo na kisha nchi hizi zigawane mapato. Mh.Bernard Membe akiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa waliahidi kulifuatilia suala hili na kuhakikisha kuwa mjusi huyu atarudishwa nchini kwa msaada wa serikali ya Ethiopia yenye wataalamu na uzoefu uliofanikisha kurudisha nguzo za kihistoria nchini humo. Mpaka leo bado mjusi huyu hajarudishwa nchini kama Waziri huyu alivyoahidi na serikali ya Ujerumani inaendelea kufaidi. Kambi rasmi ya upinzani inataka kujua ni kwanini serikali ya CCM inachukulia mzaha chanzo hichi kikuu cha mapato ambacho kingeweza kusaidia bajeti za wizara zaidi ya moja.Ambapo mpaka sasa kila mtalii mmoja anayekwenda kumuona Mjusi huyo analipia kiasi cha Euro 20 mpaka Euro 25.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hayo hakuna mtaala wowote kuanzia shule za msingi mpaka sekondari ambao unatoa fursa kwa watoto wetu kuweza kujifunza historia ya mjusi huyu mkubwa zaidi duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa majibu ya kina ni kwa nini mpaka leo mjusi huyu hajarudishwa nchini na ni nini mpango wa serikali kuhakikisha kuwa mjusi huyu anarejeshwa nchini?

## 11. IDARA YA MISITU NA NYUKI

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha 2016/2017 idara hii na tasisi zake imetengewa jumla ya shilingi 70, 760, 767,000/- katika utekelezaji wa shughuli zote ndani ya Idara hii. Katika kiwango hicho cha fedha kilichotengwa kwenye mchanganuo hakuna fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kujenga vituo vya kudhibiti moto jirani na hifadhi ya misitu ili kukabiliana na mioto inayojitokeza mara kwa mara kwa sababu ya shughuli za kurina asali au ajali za moto zinazoweza kujitokeza katika hifadhi za misitu.

**Mheshimiwa Spika**, serikali chini ya Wizara hii haina budi kulichukua jambo hili kwa umuhimu wake kutokana na kuwepo kwa matukio ya mioto katika misitu mingi ya hifadhi nchini. Tunaharibu mazingira na kupoteza mamilioni ya hekari kwa kuwa tu vituo vya zima moto viko maeneo ya mbali na mara nyingi maeneo ya mijini.

## 12. MAKADIRIO YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**, Katika bajet ya Mwaka 2015/2016 Wizara ilitenga Bajeti ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo jumla ya shilingi **7,709,150,000** .Kati ya fedha hizo shilingi **5,709,150,000** ni fedha za nje na Shilingi **2,000,000,000** ni fedha za ndani. Katika ripoti ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya 2015/2016 Wizara ilipokea shilingi **1,000,000,000** mpaka Mwezi Machi 2016, zikiwa ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji Wizara ilipokea fedha za ndani kiasi gani na ilitumia kiasi gani? Je, kwa nini katika ripoti hii haikutajwa? Hali hii ya kukwepa kwepa kuonyesha matumizi sahihi ya fedha zote ambazo Wizara imekuwa ikipokea ndio haswa chanzo cha ufiadini katika wizara mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuja na majibu ya kutosheleza ni kwa nini fedha hizi za ndani hazikuonyeshwa zimetolewa kiasi gani na zimetumika kiasi gani? Serikali ituambie ni kwa nini imeendelea kukusanya fedha kidogo tofauti kabisa na mapato ambayo sekta

hii ingeweza kuchangia pato la taifa kutokana na wingi wa rasilimali zilizo chini ya wizara hii?

### 12.1. UJENZI WA JENGO LA UTALII PHASE 11

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2015/2016 serikali iliidhinishiwa jumla ya shilingi **1,000,000,000/-** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo hili. Serikali ya Marekani imekamilisha ujenzi wa Upande mmoja na Serikali ya Tanzania ilitakiwa kumalizia upande wa pili.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka ninapoongea sasa hivi fedha hizi hazijatolewa. Hivi serikali inawezaje kunufaika na jengo hilo endapo bado ujenzi huo unasuasua. Hii ni fedheha kubwa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasaidiwa lakini imeshindwa hata kumuonyesha yule anayesaidia kuwa inasaidika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuliambia Bunge hili ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa jengo hili linajengwa na kukamilika kwa wakati ili kuondoa tabia ya serikali kuacha viporo ambavyo kimsingi vinaisababishia serikali hasara kubwa.

### 13. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema hapo awali, ili taifa linufaike na utalii pamoja na maliasili za nchi yetu ni lazima Serikali iwekeze vya kutosha katika sekta hizo. Nilidokeza hapo awali kwamba ni aibu kwa taifa hili ambalo linasifiwa duniani kuwa na maliasili zenye thamani kubwa pamoja na vivutio vya utalii vilivyotia fora duniani kuendelea kuzama katika lindi la umasikini.

**Mheshimiwa Spika**, unapona kuna kitendawili (paradox) kati ya utajiri tulionao na kuongezeka kwa umasikini, ujue lipo tatizo la msingi linalohitaji kutatuliwa. Na tatizo hilo si jingine bali ni ukosefu wa mfumo wa uongozi ambao umeshindwa kutumia fursa za kiuchumi tulizonazo kuondoa umasikini ili kuifikia ndoto ya taifa – ndoto ya kuondokana na umasikini.

**Mheshimiwa Spika**, ni aibu kwa Serikali hii inayojigamba “hapa kazi tu” wakati nchi haina usafiri wa ndege wa uhakika (No reliable air transport). Katika hali kama hiyo, ni vigumu sana kunufaika na sekta ya utalii kutokana na ukosefu wa usafiri wa ndege wa uhakika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapata tabu kuelewa kama kweli Serikali hii ina nia ya dhati ya kupata mapato katika sekta ya utalii. Nasema hivi kwa sababu, Serikali haiko mstari wa mbele katika kutangaza utalii wa nchi yetu. Kutokana na ombwe hilo, nchi jirani kama Kenya inatumia vivutio

vya Tanzania kutangaza utalii wake. Hii ina maana kwamba kama Tanzania ingekuwa imeshatangaza vivutio vyake kwa utoshelevu na dunia ikajua kwamba Mlima Kilimanjaro mathalani uko Tanzania, Kenya isingeweza tena kuutumia mlima huo kutangaza utalii wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kufanya mzaha na maliasili ya nchi yetu. Miaka 55 ya umasikini chini ya utawala wa CCM inatosha. Kizazi cha taifa hili kinataka kunufaika na rasilimali za nchi hii na kuondokana na umasikini. Kwa sababu hiyo, tunaitaka Serikali kulieleza bunge hili, ina mpango mkakati gani wa uwekezaji katika maliasili na utalii wa nchi yetu utakaoliwezesha taifa kupata mapato endelevu na hivyo kulivusha taifa kuelekea uchumi wa kati kama Mpango wa Maendeleo wa Taifa unavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**Esther Nicholas Matiko (Mb)**

**WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

24 Mei, 2016

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa orodha ya wachangiaji kwa vyama vyote vyenye uwakilishi hapa ndani. Tutaanza na Mheshimiwa Catherine Magige atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko ajiandae. Mheshimiwa Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu katika uchumi wa nchi yetu. Naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi la Taifa (*TANAPA*) ni miongoni mwa mashirika ya umma yanayotuingizia pesa nyingi sana katika nchi yetu. Utalii katika nchi yetu unachangia 18% ya *GDP* ya Taifa. Jambo la ajabu na la kusikitisha sana, miaka zaidi ya mitatu *TANAPA* haina Bodi ya Wakurugenzi. Maamuzi muhimu yamekuwa yakitolewa na viongozi wa Wizara akiwemo Waziri na Makatibu Wakuu walioondoka na hata wa sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka kadhaa kulitokea mvutano juu ya ada zinazotakiwa kulipwa na wenye mahoteli maarufu kama *concession fee*, walishtakiana wakapelekana Mahakama Kuu na *TANAPA* walishinda kesi ile lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea kwa sababu hakuna Bodi ambayo ndiyo ilitakiwa wapange jinsi gani ada hizi zitatozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunapoteza mapato mengi sana kutokana na kukosa hizi fee za kwenye mahoteli. Kwa mwaka TANAPA inapoteza shilingi bilioni 10 kwa kukosa fees hizi. Shilingi bilioni 10 siyo pesa ndogo, ni pesa nyingi sana. Tunaona Rais wetu anavyohangaika kutafuta pesa, anabana matumizi, shilingi bilioni 10 hizi zingeweza kupeleka maji Arusha, Karatu, Longido, Ngorongoro na zingeweza kusaidia watoto wa maskini wakakaa kwenye madawati. Sijui ni kwa nini mpaka sasa hivi pesa hizi hazijaanza kukusanywa na ni kwa nini Bodi ya TANAPA mpaka sasa hivi haijaundwa. Waziri atakapokuja ku-wind up naomba aniambie ni lini Bodi ya TANAPA itaundwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA Ndugu Allan Kijazi kwa sababu amekuwa akimsaidia Rais kusaidia maskini. Tumeona juzi wamemkabidhi Mheshimiwa Makamu wa Rais shilingi bilioni moja kwa ajili ya madawati kwa mikoa 16, tunamshukuru sana kwa hilo. Nimeona nikitaja TANAPA bila kumtaja Ndugu Allan Kijazi nitakuwa sijaitendea haki hotuba yangu, nampongeza sana, naomba aendelee hivyo hivyo kum-support Rais wetu kuwa sasa ni kazi tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba moja kwa moja niende katika suala zima la ujangili. Ujangili umeshamiri sana, wanyamapori wamekuwa wakiuawa, tembo wapo hatarini kutoweka licha ya Serikali pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama kufanya jitihada za kutatua tatizo hili. Majangili wana silaha kali sana hasa katika mapori yetu kama Ugala, Loliondo na mapori mengine mengi. Mbaya zaidi sheria haziruhusu walinzi wa makampuni ya vitalu vya uwindaji na YWMA kutumia silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona sasa hivi ni wakati muafaka wa kuleta sheria ili walinzi wa haya makampuni waruhusiwe kutumia silaha kwenye hifadhi zetu ili washirikiane na walinzi wa wanyamapori na wa TANAPA, majangili wamekuwa wakitamba sana kwenye hifadhi zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba iwekwe adhabu kali sana kwa ajii ya majangili siyo kuwa watozwe fine tu hapana, majangili wana pesa nyingi, fine kwao ni kitu kidogo. Tumeona Serikali ya Kenya wameweka sheria atakayekutwa kwenye hifadhi bila kibali anapigwa risasi sisi hata kama hatuwezi kufanya hivyo, lakini ni wakati muafaka wa Serikali kuleta sheria hapa Bungeni ikiwezekana majangili wafungwe kifungo cha maisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inasemekana kuwa baadhi ya Wabunge ni majangili, wamekuwa wanajihusisha na biashara hii ya ujangili.

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeeh. (Makofi)

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Nina imani hakuna ambaye yupo juu ya sheria. Hata gazeti la Jamhuri la leo limeandika Mbunge jangili. Huyo Mbunge jangili ni nani, ni Munde Tambwe, Catherine Magiga au Ally Keissy, tunataka tufahamu. Vyombo vya usalama, vyombo vya sheria vipo wafuatiliwe ijulikane Mbunge jangili ni nani. Hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria na akikutwa kiongozi ambaye ni jangili kama Mbunge jangili ,naomba mfano uanze kuoneshwa kwake. Siyo tunalaumu tu watu wengine wakati majangili tuko nao humu humu ndani, tunataka kuwafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi majuzi gazeti ya Jamhuri liliandika makala ikaonesha jinsi vibanda vinavyokusanya mapato ya watalii kwenye mapori ya Loliondo na Longido, vibanda vile vilikuwa vinasikitisha sana, ni vibanda vya miti tu. Kweli watalii wanatuletea dola wanakuta watu wamekaa kwenye vile vibanda wanapokea mapato tuko *serious* na utalii wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Wizara haihusiki zinazohusika ni Halmashauri ya Longido na ya Monduli lakini mtalii anapokuja hazitambui zile Halmashauri bali Wizara ya Maliasili, naomba tuwe *serious* kwa hili. Tunataka kupokea dola za watalii, tunapokea kwenye vibanda, vibanda vya ajabu, ni aibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja naomba nielekeze mchango wangu katika misitu. Misitu inamalizwa, biashara za mkaa zimeshamiri sababu kubwa wakisema bei ya gesi au nishati mbadala ni kubwa. Naomba suala hili la mkaa ingawa kwa Wizara ni suala mtambuka lakini bado kuna ukweli misitu yetu ambayo iko chini ya Maliasili watu wanakata mikaa wanaimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilianganalie sana suala hili la kukata misitu na iwachukulie hatua ambao wanauza mikaa, maana wanakata miti bila vibali na sasa hivi tumeona magari yanasafirisha mkaa usiku kwenye ma-container. Naweza nikatolea mfano pale kwa Msuguli kuna watu wanakaa pale kwa ajili ya kukagua hizi lumbesa za mazao sasa huoni kama ni wakati muafaka watu wa misitu nao wakawepo pale kwa ajili ya kuhakikisha kuwa miti yetu haikatwi ovyo na kukwepa kodi kupitia misitu? Tunaomba sana Serikali ianganalie suala hili zima la mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa watu wanaongelea kuhusu ndege, mimi akinamama wa Arusha hawaniulizi kuhusu ndege, wanauliza kuhusu maji na mitaji. Kwa hiyo, naomba tujielekeze sana kuona haya masuala ambayo ni muhimu kwa ajili ya wananchi wetu, siyo tunajiangalia sisi tu maana wale wapiga kura kule hata ndege hawapandi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba TANAPA iendelee kuwasaidia vijana na akinamama kwa kuwapa mitaji. Kuna akinamama na vijana wengi ambao



wanafanya biashara ya utalii hasa katika Mkoa wangu wa Arusha iwasaidie kuwapa semina wapate elimu ya ujasiriamali ili waweze kutumia vizuri fursa hii ya utalii. Vilevile wawatafutie masoko, kuna akinamama wanauza shanga na vinyago kwa watalii watusaidie akinamama hao wapate soko ili waweze kujitosheleza na mahitaji yao mbalimbali kama ya kusomesha watoto wao na waweze kufanya biashara za kiutalii na wanufaike na utalii wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ila naomba tu Waziri atakaponijibu aniambie ni lini ataunda Bodi ya TANAPA, la sivyo nitatoa shilingi. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatiwa na Mheshimiwa Doto Biteko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa namna ya pekee naomba niwape hongera nyingi sana Waziri na Naibu Waziri na timu nzima ya wenzetu wa Wizara ya Maliasili. Naomba pia niwape hongera za dhati kabisa Mhifadhi Mkuu na Wahifadhi wa Gombe na *Mahale National Parks* kule Kigoma, wanafanya kazi nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema ninachotaka kusema, mimi hii Kampuni ya *Green Miles* naifahamu, nilikuwa kwenye Tume ya Wanyamapori. Kama haya yanayosemwa na Kambi ya Upinzani ni ya kweli, basi lipo tatizo kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo kampuni ya *Green Miles* tulii-*disqualify* nikiwa kwenye Tume kwa sababu ilikosa sifa. Nafikiri ni mambo ambayo Wizara mnaweza mkakaa na wenzenu mkayafanyia kazi vizuri kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri. Moja ya *disqualification* yao waliidanganya Tume kipindi kile na kwa kweli tukawa-*disqualify*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara na wataalam wenu mkae chini ikibidi mwende kule kwenye eneo lenyewe muweze kujiridhisha na hali halisi iliyopo pale. Maana yake nakumbuka Waziri wa Maliasili aliyepita hiyo kampuni aliinyang'anya leseni kwa kukosa sifa. Sasa nasema haya mambo yako ndani ya Wizara, mnaweza mkaangalia namna ya kufanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya ikolojia ya Kigosi Moyowosi. Hii ikolojia Kigosi Moyowosi inaanzia Mkoa wa Shinyanga eneo la Bukombe inakuja Kibondo inakwenda Kasulu mpaka Uvinza. Naomba niseme eneo hili limevamiwa na mifugo wengi sana na kusema ukweli linatishia uhai wa Mto Malagarasi na siyo Mto Malagarasi tu inatishia hata chepechepe (*wet land area*) ya Mto Malagarasi na hakika inatishia uwepo wa Ziwa Tanganyika. Nadhani ni jambo muhimu sana Serikali ikae na kuangalia namna njema na

nzuri ya kuwaondoa hawa wafugaji na kuwatafutia maeneo mengine ya kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme siyo jambo jema sana Mheshimiwa Waziri mkaanza kuwa na utamaduni wa kuua ng'ombe kwa risasi, hilo jambo linatufedhehesha sana kwa kweli. Kama nchi kunakuwa na makosa yamefanyika basi nchi hii ni ya kiistaarabu yatatuliwe kistaarabu. Wafugaji hawa waelekezwe, waondoshwe kwenye hifadhi, wasiharibu mazingira yetu, lakini kitendo cha kuua ng'ombe, kupiga risasi ng'ombe kinaturudisha kwenye ujima kwa kweli siyo ustaarabu wa leo. Naomba hilo jambo lizingatiwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ikolojia hiyo hiyo ya Moyowosi kuna msitu mashuhuri sana unaitwa Msitu wa Makere Kusini maarufu kama Pori la Kagera Nkanda. Hilo pori lilikuwa *gazetted* mwaka 1954, Septemba, nina hakika Wabunge wengi mlikuwa hamjazaliwa kwa sababu hata mimi mwenyewe nilikuwa sijazaliwa. Eneo hilo lilikuwa halina watu kipindi hicho lakini sasa hivi limejaa watu na kuna misugvano mikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia hotuba ya Waziri inazungumzia juu ya usimamizi wa misitu na Wakala kufanya mapitio, ukurasa wa 59 wa hotuba yake. Katika hilo eneo la Kagera Nkanda lenye wanavijiji wengi kuna migongano ya wakulima na hawa wenzetu wa *TFS*. Naomba mipaka ile ya mwaka 1954 iweze kuhuishwa hawa wakulima wapate maeneo yao ya kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nimuarifu Profesa kwamba ikolojia ile haitishiwi na kilimo cha wananchi wale wa vijiji vya Wilaya ya Kasulu bali ikolojia ile inatishiwa na mifugo mingi toka nchi jirani na mifugo mingi inayoingia katika eneo lile bila utaratibu. Tafadhali sana, kama alivyobainisha ukurasa wa 59 wa hotuba yake, naomba mipaka ile ihuishwe vizuri, tena wametumia neno zuri soroveya. Tunaomba usoroveya huo mkaurudie upya ili yale maeneo ambayo wananchi wameyalima kwa muda mrefu waendeleo kuyatumia bila kuwasumbua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wenzetu wa *TFS* wamekuwa ni walajji rushwa, wanasumbua watu wetu na kusema kweli hakuna tija hata kidogo. Mheshimiwa Waziri naomba hilo alizingatie na nimeshazungumza naye. Wananchi wetu wa vijiji vinavyozunguka pori lile wamekuwa wakilima pale kwa miaka 20 iliyopita na tumewazuia sisi kama Halmashauri wasikate miti wanalima kilimo rafiki. Kwa hiyo, ni muhimu sana Profesa akatoa maelekezo hawa watu wa *TFS* wasiwasumbue waendeleo kujikimu kupata maisha yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Mheshimiwa Waziri ningeomba Sheria ya Misitu Na.14 itazamwe upya kwani imepitwa na wakati.

Nchi hii ina watu wengi sasa, kabla watu hawakuwa wengi kiasi hiki. Ni vyema sheria hii ingeangaliwa na kusema kweli yale maeneo ambayo yamekosa sifa, yako maeneo Profesa yamekosa sifa kwa mfano mapori ya akiba na *open area* wapewe wananchi wakiwemo wafugaji tupunguze migogoro hii ambayo kama Taifa inatufedhehesha kwa kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja mdogo, kwa mfano eneo la wazi la Wembere lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 10,000 limepoteza sifa, hakuna mnyama tena, wananchi wanakatakata mikaa mle lakini hawa watu wa maliasili wanazuia watu kufanya shughuli zao. Maeneo kama hayo mngeyahuisha tukapunguza migogoro hii ya wakulima na wafugaji ili watu wafanye shughuli zao kwa sababu yale maeneo hayana sifa tena ya uhifadhi na yako mengi tu mkifanya tathmini mtagundua hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie ni kuhusu Sekta ya Utalii. Ukisoma hotuba ya Waziri ukurasa wa 81 unazungumza Wizara na *World Bank* kuandaa mpango mkakati wa kuendeleza utalii, ni jambo jema, lakini hawajaeleza *time frame* ya huo mpango mkakati wao. Ukurasa wa 89 umezungumzia kuainisha vivutio vya utalii nchini na wametaja Mikoa ya Mwanza, Mara, Kigoma, Geita na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Wizara, nilidhani kuanza kubainisha vivutio vya utalii pamoja na vivutio vya utamaduni ingekuwa ni *input* kwenye mpango mkakati wa Wizara. Kipi kinaanza, bila shaka unaanza mpango mkakati kabla ya kuzungumzia habari ya vivutio na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 81 na 89 wa hotuba ya Wizara, naomba wautazame upya ili kuleta maana zaidi kwamba lazima uanze na mpango mkakati halafu vivutio vya utalii katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Mara na kadhalika pamoja na *culture tourism* ziwe ni *input* kwenye mpango mkakati wenu. Bila shaka kama mnafanya kazi hiyo na *World Bank* ingekuwa jambo la busara sana basi mpango mkakati huo uwe na *time frame* na mtueleze katika mpango mkakati huo mmeandaa kufanya mambo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri baada ya mpango mkakati kukamilika, basi tu kwa mahusiano mema na Wabunge wenzake, Waziri atuletee mpango mkakati huo tuone ili tuweze kuwasadia baadhi ya mambo ambayo tunafikiri yanafaa kuwemo katika mkakati huo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda niliseme kwa ujumla wake kwa Mheshimiwa Waziri, ni kutangaza utalii.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo hasa Kagera Nkanda, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, halafu Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Wizara hii. Kabla sijafanya hivyo nimshukuru sana Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kusimama tena hapa na kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyoanza walionitangulia naomba nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Maliasili na Utalii kwanza kwa kutuletea hotuba hii nzuri, *detailed* na imegusa kila sekta kwenye Wizara yake. Naomba vilevile niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati inayosimamia Wizara hii nao kwa hotuba yao nzuri ambayo imetoa maoni na ushauri ambayo kwa kweli yanatusaidia sisi tunaochangia kuweza kujua maeneo gani yatafanyiwa kazi na Kamati iliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumemwona Mheshimiwa Waziri anavyohangaika na kupambana na ujangili nchini. Waziri na Wizara imeonyesha nguvu yake yote kwenye jambo hili. Nataka niwatie moyo kupitia mchango wangu huu kwamba kazi wanayoifanya ni kwa faida ya nchi, waendeleo mbele na wasivunjike moyo. Tumeona wale majangili wote waliotungua ndege wamekwishakamatwa. Juzi niliona video moja kwenye mitandao ya kijamii maaskari wetu wamekamata majangili haya yaliyokuwa yanafanya kazi ya kuua wanyama wetu. Naomba niwatie moyo na kuwaombea kwa Mungu waendeleo bila shaka wanyama hawa ni kwa faida ya nchi yetu na vizazi vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bukombe asilimia 40 ya ardhi ya Bukombe ambayo ni kilometa za mraba 8,055.59 ni hifadhi. Wananchi wanaoishi Bukombe wana maingiliano ya karibu na hifadhi ya Kigosi Moyowosi lakini mahusiano ya Kigosi Moyowosi hayajawahi kuwapatia faida na hapa nataka niseme kwa uchungu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walio wengi wa Wilaya ya Bukombe wana majonzi makubwa na hifadhi hii. Nimesimama hapa kumwomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama na kuhitimisha aje na majibu ambayo yatawapa tumaini watu wa Bukombe juu ya mahusiano mabaya ya Wahifadhi na wananchi wa Wilaya ya Bukombe. Nenda Ngara, nenda Biharamulo, njoo Bukombe, pita Mbogwe, nenda Kahama, nenda Ushetu kwa jirani yangu Kwandikwa kila Mbunge aliyemo humu ambaye anawakilisha maeneo haya

hana habari njema ya kuelezea juu ya mahusiano ya Maliasili pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako manyanyaso makubwa ambayo yamefanyika ukiambiwa hapa unaweza ukatokwa na machozi. Leo nataka niyazungumze haya na niseme hadharani ikiwa sitapata majibu, watu wa Bukombe watanishangaa kuunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, Kitongoji cha Idoselo kilichoko kwenye Kijiji cha Nampalahala, watu wa Maliasili wameingia hapo, wamechoma moto nyumba za wananchi 40, kijiji ambacho kina GN ya Serikali kwa maana hiyo kimetambuliwa na Serikali! Katika kijiji hicho tumefanya uandikishaji wa BVR, kampeni tumepiga kule, walishachagua Mwenyekiti wa Kijiji, kilishasajiliwa, kina GN ya Serikali, watu wametoka nyumbani wamekula chai wameshiba vizuri, wana magari na mafuta ya Serikali, wana kiberiti na bunduki, wanaenda kuchoma nyumba za wananchi ambao hawana uwezo wa kujitetea, wamepiga na wameharibu mazao ya watu, watu hao wapo wanaendelea kutamba na kusema kwamba mtatufanya nini. Jambo hili lisipopata majibu leo namwambia Mheshimiwa Waziri hapa hapa nakufa na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wananchi wale ambao wamelima mashamba yao, mazao yao yamekua yamefikia mahali fulani wanatumaini kwamba baada ya miezi fulani tunakwenda kuvuna tulishe familia zetu, tusomeshe watoto wetu, ananyanyuka mtu mmoja tu au wawili kwa sababu wana nembo ya Serikali kwa maana ya Maliasili wanakwenda kuchoma nyumba zao na baadaye wanatamba kwenye vyombo vya habari tumechoma vibanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie ikiwa wao wana maghorofa, hivyo vibanda vya wananchi wao ni maghorofa yao. Ikiwa wao wanakula vizuri hayo waliyosema ni *vi-plot* wao ndiyo mashamba yao ambayo yanalisha familia zao. Lazima nipate majibu kwenye Bunge hili, lazima wananchi wa Bukombe wafutwe machozi kwa jambo la ukaidi, kwa jambo hili kubwa lililofanyika Wilaya ya Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bukombe pamoja na mambo haya, kuna manyanyaso makubwa yamefanyika. Wako wananchi wamevunjwa miguu, wako wananchi wamevunjwa mikono, wako wananchi wamefanywa kuwa walemavu wa kudumu, walikuwa wanalima kwa ajili ya familia zao, leo watu hawa hawawezi kufanya hivyo kwa sababu wamekuwa walemavu, aliyefanya ni nani? Baadhi ya Askari wasio waaminifu wa Maliasili wamewaumiza watu hawa. Nataka majibu wananchi hawa mnawafanyia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imepiga risasi ng'ombe za wananchi, nataka majibu ni kwa nini. Ng'ombe waliopigwa risasi ni wa Ndugu Masanja Njalikila, ng'ombe sitini (60); Ndugu Hamisi Ngimbagu, ng'ombe wanane (8); Ndugu Manzagata Mang'ombe, ng'ombe mmoja (1); Ndugu Fikiri Masesa, ng'ombe wawili (2); Ndugu Sikujua Majaliwa, ng'ombe kumi na nane (18); Ndugu Blashi Ng'wanadotto, ng'ombe arobaini na tatu (43); Ndugu Juma Masong'we, ng'ombe kumi na mbili (12); Ndugu Mussa Seni, ng'ombe wawili (2); Ndugu Serikali Andrea, ng'ombe wawili (2); Ndugu Juma Langa, ng'ombe kumi na nane (18) na Ndugu John Mashamba, ng'ombe wawili (2); jumla ng'ombe 215. Ndugu Jofrey Omboko punda wake wane (4) wamepigwa risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa leo nataka majibu hatma ya watu hawa inapatikanaje. Kama inabidi nisimame kwenye Bunge hili nilie machozi kwa ajili ya wana Bukombe nitafanya hivyo, lakini watu wangu wapate majibu. Haiwezekani niwepo Mbunge hapa nimekaa kwenye kiti hiki cha kuzunguka, wananchi wangu wana mateso na nijione Mbunge mwenye furaha, hilo sitafanya. Naomba nipatiwe majibu, vinginevyo sitaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine limetokea na hili ni la kisheria na naunga mkono usimamiaji na utii wa sheria. Iko tabia ya watu kupewa adhabu ya kutaifishwa mifugo yao. Leo ninavyosimama hapa jumla ya ng'ombe 603 za wananchi wa Bukombe wametaifishwa, wamechukuliwa kuanzia siku ile ni mali ya Serikali. Nataka niseme kwenye kundi la wale waliopelekwa Mahakamani wenye ng'ombe walikuwa watano (5), watatu (3) walikubali kutoa fedha, wakapelekwa Mahakamani wakadanganywa kwamba wakiwa huko watachiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme fedha zao wamekula na ng'ombe zao zimetiafushwa lakini wako wawili (2) waliokataa kutoa fedha kujumuishwa tu kwenye mashtaka yale wakati wanadai ng'ombe wao Maliasili wamekataa kuwaweka. Wamekwenda kuhukumiwa wale ng'ombe kama ng'ombe wasiokuwa na mwenyewe. Watu hawa wamekwenda Polisi, wameripoti Maliasili wakawaambia tunaomba mtufanyie jambo moja mtuingize kwenye mashtaka na sisi tushtakiwe wamekataa kuwapeleka wanasema hawa ng'ombe hawana mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji huu una-*turnish image* ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Unyanyasaji huu hauwezi kumfanya Mbunge wa Bukombe afurahie Wizara ya Maliasili na utalii. *By the way* kwenye Sheria zao za Maliasili na Utalii sisi tunaopakana na hifadhi tunapaswa kupata asilimia 25% ya mapato yale. Toka nimekuwa Bukombe pale sijawahi kuona hata shilingi moja inapelekwa Bukombe. Naomba na hiyo hela Mheshimiwa Waziri na yenyewe aniambie naipataje kwenye Halmashauri yetu?



*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimwa Doto, ahsante sana.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na naomba niseme ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kulipongeza Shirika la Hifadhi la TANAPA na Ngorongoro kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhifadhi rasilimali hapa Tanzania. Imekuwa ni kawaida pale ambapo Serikali inashindwa kuhifadhi maeneo mbalimbali kimbilio lake ni shirika lake ambalo linawapelekea na kwa kiasi kikubwa kwa kweli wameonekana wanajitahidi sana kulinda rasilimali zetu na vituo vyetu hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo tetesi kwamba Serikali inataka kuhodhi mashirika haya, kuyarudisha mikononi mwake kwa hili napinga kwa asilimia zote. Kama ni kweli kwamba ziko taarifa Serikali inataka kuhodhi mashirika haya irudishe kwenye mikono yake, wawe wanaendesha wao ni uhakika kabisa kwamba tunakwenda kuua uhifadhi hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika mengi hapa nchini yalikufa kwa sababu Serikali imeshindwa kuyasimamia. Yale machache ambayo iliamua kuyapa *full authority* yajiendeshe yenyewe ndiyo bado yapo. Leo TANAPA na Ngorongoro wanajiendesha wenyewe kwa asilimia 100 na bado wanapeleka ruzuku Serikalini na ni mashirika pekee ambayo Serikali haiweki ruzuku hata senti moja. Leo kama wanataka kuyarudisha ndani ya mikono yao tunakwenda kuua uhifadhi hapa nchini. Naomba kama mpango huo upo ufe kabisa haufai kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana pekee TANAPA imetoa shilingi bilioni 10 kama ruzuku Serikalini na bado inajiendesha. Tumekuwa tunalia kilio hapa kwamba Serikali ijenge angalau miundombinu ya kwenda kwenye vivutio, barabara kutoka Iringa kwenda Ruaha kwa miaka 10 Serikali imeshindwa kujenga, leo tunanyang'anya mashirika haya mamlaka ya kujisimamia tunakwenda kuua uhifadhi. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa nimeona tunayo mapori ya akiba zaidi ya 28, tunayo mapori tengefu zaidi ya 42, tunazo hizi hifadhi za TANAPA 16. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri haya mapori ya akiba 28 na mapori tengefu 42, mengi yapo taabani na mengine hayapo, yapo kwenye vitabu kwenye *ground* hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapori haya yana hali mbaya, tumekuwa tunalia hapa, mapori haya mengine yamevamiwa miaka 35 iliyopita huko nyuma na wamejenga ndani ya hifadhi vijiji, hospitali na barabara. Tumekuwa tunalia hapa mapori haya yalivamiwa miaka mingi iliyopita Serikali haikuchukua hatua, wamesajili vijiji kisheria, wanapeleka huduma, leo Mheshimiwa Waziri anatuambia tuna mapori ya akiba 28, yako kwenye hali mbaya, mengine hayapo katika *ground*, yapo kwenye karatasi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora peke yake tuna vijiji zaidi ya 50 ndani ya hifadhi vina vyeti vya usajili na kila kitu kipo mfano shule na hospitali. Ninayo taarifa hapa kamili ya Kiserikali, Mkoa wa Tabora wenyewe vijiji zaidi ya 50, Wilaya ya Kaliua peke yake tuna vijiji 21 vimesajiliwa kisheria ndani ya hifadhi. Wananchi hawa wamekaa kwa hofu miaka mingi, Serikali tunaambia hapa miaka 10, lakini hakuna hatua inayochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea hatua ya leo Mheshimiwa Waziri angekuja na mpango kamili namna gani watu hawa wanashughulikiwa ili waache kuishi kwa hofu, waache kunyanyaswa, wanauliwa mifugo yao, wanaharibiwa mashamba yao, ni shida, ni matatizo makubwa. Watu wa hifadhi wanachokifanya kwa watu ambao wamesajiliwa kisheria siyo halali ndani ya nchi ambayo tunaishi kwa kufuata Katiba na sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu naomba nitaje tu kwa ufupi vijiji ambavyo vimeathirika na suala hili. Tuna Vijiji vya Ukumbi Kakonko, Lumbe, Usinga, Ukumbi Siganga, Kombe, Kashishi, Uyowa, Seleli, Nyasa, Mwendakulima, Sasu, Kiwakonko, Nsimbo, Mpanda Mlowoka, Mwahalaja, Chemkeni, Kanoge, Ulanga, Mwendakulima, vijiji 21 miaka yote watu wanaishi kwa hofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hapa atueleze nini hatma ya watu hawa na nini hatma ya shule ambazo zimejengwa kule? Hatuwezi kuacha wananchi waendeleo kuishi kwa hofu miaka yote, wanashindwa kufanya shughuli za maendeleo, lakini Serikali ipo tu imetulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la TFS. Tulianzisha Wakala wa Misititu (TFS) kwa maana ya kuokoa rasilimali ya misititu inayopotea na ndiyo lengo letu kama Watanzania, Wizara na Wabunge. Watu wa TFS wamekuwa ndiyo chanzo kikubwa cha kuangamiza misititu kuliko tulivyokuwa

mwanzoni. Leo watu wa *TFS* hawana mpango wowote makini wa kuja kuokoa misitu, wao wanakaa wanasubiri wachukue mbao, wagonge muhuri mbao isafirishwe. Serikali imeweka utaratibu, imefunga kabisa kutoa magogo kwenye miti ya asili pamoja na mbao kutoka kwenye misitu ya asili. Kwa nini Serikali inaweka malengo kwenye *TFS*? Kwa nini Maafisa Misitu wanapewa malengo ya makusanyo? Leo misitu yetu inateketea kwa kasi kubwa ya ajabu kuliko ilivyokuwa *TFS* haipo. Labda hawakupewa malengo, labda Serikali haikuwa na mipango, labda hawajaambiwa wanatakiwa wafanye nini. Hili ni tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *chain saws* zilizopo ndani ya maeneo ya misitu ya asili nyingi ni za watu wa *TFS*. Wao ndiyo wananunua *chain saws* wanawapa watu wao wanaenda kuweka kule kwenye misitu, kwa hiyo, hakuna tunachokifanya. Naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa kuhitimisha atuambie nini hasa kazi na wajibu wa *TFS*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFS* walikuja Kaliua, wamekuja kufyeka mahindi ya wananchi kwenye Jimbo langu, tena leo naomba njaa ikija, muwe wa kwanza kuja kuwalisha chakula wananchi wa Kaliua. Mahindi yalishafikia karibu kuzaa, wanakuja wanaweka *beacon* ndani ya nyumba za watu. Nimeongea nao kwenye simu hamfanyi kazi kwa weledi? Hamna mpango shirikishi, Wilaya haijui, Mbunge hajui, Mkurugenzi hajui, wanakuja wenyewe wanakwenda kufyeka mahindi ya watu, hawana weledi wa kufanya kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atujibu nini kazi ya *TFS*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikija hapa itujibu, kuna Tume ya Kimahakama iliundwa na Mheshimiwa Rais wa awamu iliyopita, kutokana na ripoti ya Operesheni Tokomeza kwenda kuangalia madhara makubwa waliyopata wananchi nchi nzima, leo ni mwaka wa tatu iko wapi ripoti ile? Iko wapi? Wananchi wanateseka, watu waliuawa, watoto wananyanyasika, mifugo iliteketea, operesheni tokomeza ilikuwa ya kutokomeza watu. Tunaitaka ripoti ya Mheshimiwa Rais hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako liagize tupate ripoti ya Tume ya Kimahakama ya Mheshimiwa Rais ili tuweze kuangalia namna gani ya kuwasaidia wale watu waliopata madhara makubwa sana na wengine walipoteza maisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni tozo kwenye hoteli za kitalii ambazo ziko ndani ya hifadhi. Kwa miaka mingi tumekuwa tunazungumzia suala hili la tozo. Tozo zinazotozwa sasa hivi na *TANAPA* ni za miaka 10 iliyopita wakati vitanda vikiwa vinatozwa dola 50 - 100, leo kitanda kimoja dola 300 - 500, tozo ni zile zile huu ni wizi, haiwezekani! Kwa nini *concession fee* iwe ya miaka 10 iliyopita? Leo maisha yamepanda, gharama zimepanda, vitu vyote vimepanda

Serikali imenyamaza kimya kuna nini hapa? Naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie, Mahakama imeshatoa *rulings* wale wafanyabiashara walishindwa kwa nini hatuletewi tozo nyingine zinazoendana na hali ya sasa?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa muda uliobaki hakuna Mbunge atakayeweza kuchangia kwa sababu ni mfupi lakini nilete kwenu matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni Wabunge watakaochangia mchana, nitawasoma majina wote kwa pamoja lakini Mwenyekiti ataangalia nani ataanza. Nao ni Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Boniphace Getere, Mheshimiwa Mohamed Mchengera, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Ester Mahawe, Mheshimiwa Injini Atashasta Nditiye, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

Wengine ni Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Risala Kabongo, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa James Millya, Mheshimiwa Gibson Meiseyeki, Mheshimiwa Joseph Haule. Halafu Mheshimiwa Yussuf Salim, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa James Mbatia. Hao ndiyo watakuwa wachangiaji wetu wa mchana.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa asubuhi kuna wageni hawakuweza kupata nafasi ya kuingia, nitawatangaza kwenu sasa hivi na ni wageni wa Mheshimiwa Esther Matiko. Tunaye Ndugu Yasinta Mgaya, Ndugu Magret Matiko, Ndugu Kisanta Matiko, Ndugu Nyangi Namwita, hawa ni wadogo zake Mheshimiwa Esther Matiko. Karibuni sana wadogo zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi leo jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 Jioni)*

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeambiwa Mheshimiwa Chumi atachelewa, tuendeleo na Mheshimiwa Mwilima na Mheshimiwa Kingu ajiandae.

**MHE. HASNA S.K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu, niwashukuru pia na wapiga kura wangu wa Jimbo la Kigoma Kusini kwa dua na maombi yao yaliyowezesha kesi iliyokuwa na mvuto mkubwa zaidi ya miezi sita hatimaye tarehe 17 Mahakama imeweza kutupilia mbali shauri la Ndugu David Kafulila. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nijikite kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Kwenye Wilaya yangu ya Uvinza tuna matatizo katika baadhi ya maeneo kwa mfano kwenye Kata ya Uvinza kuna Kitongoji cha Tandala. Kile kitongoji kimesajiliwa kwa mujibu wa sheria na wananchi wanaishi pale, lakini tatizo kubwa ambalo liko pale wananchi hawawezi kufanya shughuli yoyote ya maendeleo kwa sababu wanaambiwa pale ni eneo la hifadhi. Sasa unajiuliza inakuwaje eneo la hifadhi ambalo wananchi wanaishi zaidi ya miaka 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye hotuba yake ameonesha kwamba kwenye Halmashauri za Wilaya ana hekta karibu milioni 3.1, lakini kuna maeneo mengine yapo tayari yanakaliwa na wakaazi, tungeomba maeneo kama hayo yaweze kuachiwa na hatimaye yatumiwe na wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hicho Kitongoji cha Tandala hawana shule, wanasoma kwenye kibanda. Nimeweza kuwasaidia vitabu, nimewasaidia vifaa mbalimbali vya kujifundishia, kuna mzee mmoja amejitolea pale kufundisha watoto, watoto hawawezi kutembea kutoka pale mpaka kwenye Kijiji cha Chakuru kwenda kutafuta elimu. Kwa hiyo, ningepomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hapa hoja yake, basi aweze kuangalia maeneo kama hayo, Wizara iweze kuachia tuendeleo na masuala ya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo vilevile tatizo kama hilo kwenye Kata ya Nguruka, Kitongoji cha Nyangabo. Tunalo eneo la hifadhi linaitwa Rukunda Kachambi, nimeenda kutembelea pale, unakuta nyumba ya mkaazi hii hapa na GN iko nyuma ya choo. Wananchi wamebanwa kabisa, hawawezi kulima

na hawawezi kufanya shughuli zozote za maendeleo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri washirikiane na Wizara ya TAMISEMI kama ikiwezekana zile GN zisogezwe ili wananchi wapate maeneo ya kulima na kufanya shughuli zao za kimaendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Kata ya Itebula tuna eneo linaitwa Ipuguru. Eneo la Ipuguru ni hifadhi lakini kwa bahati nzuri hakuna wanyama wowote mle kwa zaidi ya miaka 20. Sasa kwenye maeneo kama hayo tungeomba basi hata wakulima waruhusiwe, lakini hata wafugaji pia waruhusiwe kutumia maeneo hayo. Wafugaji wamekuwa wanahangaika, wanaingiza mifugo yao kwenye mashamba, wanaingiza mifugo yao kwenye maeneo mbalimbali kwa sababu hakuna maeneo halisi ya kuchungia mifugo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuna eneo la Kurora, nadhani Mheshimiwa Waziri analifahamu. Hili eneo lilitengwa kwa ajili ya matumizi bora ya ufugaji, lakini kwa bahati mbaya wakulima wamevamia na kusababisha wafugaji watoe mifugo yao na ianze kuhangaika kwenye mashamba. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha ajaribu kuangalia kwenye Wizara yake kuna maeneo mengi yanaitwa kama hifadhi lakini kwa bahati mbaya wananchi wameshavamia na vijiji vimeshasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikia Mheshimiwa Magdalena Sakaya hapa anazungumza kwamba Tabora wana zaidi ya vijiji 50 vimesajiliwa kisheria ndani ya hifadhi. Tatizo hilo Mheshimiwa Waziri na sisi pia tunalo. Kwa mfano, sisi tuna ile Hifadhi ya Mahale ambayo ipo kwenye Kijiji cha Kalilani lakini Waziri anafahamu kuna mgogoro wa zaidi ya miaka 20 baina ya wananchi wa Kalilani na watu wa hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mgogoro unapelekea mpaka watu wa hifadhi hata zile shughuli za kijamii za kuwachangia wananchi wa Kijiji cha Kalilani wanakuwa hawatekelezi na badala yake wanakwenda kusaidia vijiji vingine ambavyo havipakani na ile Hifadhi ya Mahale. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili, ni mgogoro ambao uko ofisini kwa Mheshimiwa Waziri akiuliza ataambiwa. Katibu Mkuu wa CCM, Ndugu Kinana alipokuja tulimwambia na tulimkabidhi *documents* zote kwamba mgogoro baina ya wananchi wa Kijiji cha Kalilani na watu wa Hifadhi ya Mahale, tunaomba Mheshimiwa Waziri auangalie ili utatuliwe waweze kukaa kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba pia nitoe shukrani kwa watu wa TANAPA kwa sababu sisi kwenye ile Hifadhi ya Mahale watalii wanapokuja wanatumia usafiri wa boti kwa sababu barabara hakuna. Tunazo

kilometa kama 30 ambazo mtu hawezi kupita kwa gari na tuna mito kama mitatu ambayo inahitajika ijengewe madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watu wa TANAPA kwenye bajeti hii ya 2016/2017, wameweza kututengea shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kutengeneza barabara ile na tulipitisha kwenye kikao chetu cha barabara cha Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, nimeona pia nitoe shukrani zangu za dhati maana wangeweza kupeleka sehemu nyingine, lakini wameona waje kusaidia ili watalii nao waweze kupita bila tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia Mheshimiwa Waziri aangalie sana kama inawezekana kuboresha zile *speed boat* za Mahale kwa sababu kwenye Ziwa Tanganyika tuna kitu kinaitwa Rukuga, ni upepo mkali sana, unapokuwa mkali hata meli ya Liemba haiwezi kupita. Hata kama sikuangalia kwenye bajeti kama wametenga namna yoyote ya kuboresha usafiri maeneo yale, naomba waone umuhimu wa kuwaongezea watu wa Mahale *speed boat* nyingine kwa ajili ya kubeba watalii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 32. Asubuhi mdogo wangu Mheshimiwa Doto alichangia kuhusiana na masuala ya unyanyasaji wa wafugaji kwenye hifadhi. Mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Mbogwe ilizaliwa kutoka Bukombe, Mkoa mpya wa Geita. Matatizo hayo kwenye Hifadhi ya Kigosi wakati yametokea kwenye ile Operesheni Tokomeza, nilikuwa Mkuu wa Wilaya pale. Kwa kweli kabisa alichosema mdogo wangu ni kweli, unyanyasaji ni mkubwa sana. Wanapowakamata, hawawakamati tu kwamba wafuate sheria, sheria imewekwa kwamba watu wanapokamatwa wameingiza mifugo kwenye hifadhi wachukuliwe hatua gani. Wale maaskari badala ya kufanya hivyo wanawa-harass wale wananchi na wanawapiga risasi ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwamba tuko hapa leo kuipitisha bajeti ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii, tunatambua fika kwamba Mheshimiwa Waziri ndiyo kwanza amepewa dhamana kwenye hii Wizara na hii ndiyo bajeti yake ya kwanza. Kwa hiyo, badala ya kumshambulia au kum-*attack* moja kwa moja tumpe ushauri ili aweze kupokea, aangalie upungufu uliojitokeza kwenye Wizara yake siku za nyuma na aweze kuyafanyia kazi. Huu ndiyo ushauri ambao napenda kuutoa. Namfahamu Mheshimiwa Maghembe, najua ni mchapakazi na msikivu, yote haya tunayoyasema hapa atayasikia, atayapokea na atayafanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleee tu kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na nimwambie kwamba aangalie sana sekta ya wanyama pori. Wale maaskari wanaolinda hifadhi hizi wamekuwa ni shida kubwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niombe Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kuna mambo mengine wawasiliane pia na Waziri wa Kilimo. Kwa mfano, haya matatizo ya mifugo kuvamia hifadhi na wakati Uvinza tunazo *ranch* za Serikali kama tatu lakini zile *ranch* inaonekana siku za nyuma walipewa watu ambao hawako tayari kuzitumia na badala yake wanazikodisha kwa pesa nyingi. Kwa hiyo, kwenye matatizo kama haya wakae chini Wizara na Wizara, kwa mfano Wizara ya TAMISEMI na Wizara hii waone matatizo hayo ya GN ambazo zimeingia mpaka kwa wananchi walikojenga waweze kusogeza ili kutatua migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kingu hayupo tunaendelea na Mheshimiwa Chegeni ajiandae Mheshimiwa Yussuf Salim.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kusema kwamba naunga mkono hotuba hii ya bajeti. Mheshimiwa Profesa Maghembe anahitaji apate fedha akafanye kazi. Pamoja na yote hayo, kuna changamoto nyingi sana ambazo ningeomba leo Mheshimiwa Waziri anisikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo sasa hivi ni tatizo la wafugaji na hifadhi za akiba au mapori ya akiba yanayomilikiwa na TANAPA. Tunapoangalia sasa hivi tunaona kwa udogo wake lakini naona kuna mfukuto mkubwa sana unaweza kujitokeza na ukaleta matatizo ya kijamii katika nchi yetu. Leo hii mfugaji hathaminiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana wafugaji wanapoingiza mifugo kwenye pori, ni kinyume cha sheria tunafahamu, lakini kwa sababu mazingira jinsi yalivyo hatujaweza kujenga utaratibu mzuri na mahusiano mazuri kati ya wafugaji, wakulima na hifadhi zetu za Taifa. Tunajua kwamba sheria inakataza na Mheshimiwa anasimamia kwenye sheria, lakini bado kuna tatizo kubwa kwamba ni namna gani tuweke matumizi bora ya ardhi ili mfugaji huyu naye aone kwamba anathaminiwa na anapewa nafasi katika nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mahali katika nchi hii unaweza ukapuuza wafugaji, haiwezekani! Lazima wapewe nafasi yao na lazima waoneshwe ufugaji bora na wa kisasa au ufugaji ambao ni endelevu. Leo hii ardhi haiongezeki lakini watu wanaongezeka na mifugo inaongezeka. Mara nyingi tusipokuwa wabunifu na naomba Mheshimiwa Waziri anapokuwa anahitimisha hotuba yake hii hebu atuambie katika Wizara yake amejipanga



vipi kuweka mkakati kuona kwamba, hawa wafugaji wanapewa stahiki yao, wanaelimishwa, wanasaidiwa namna ya kufuga vizuri lakini pia waboreshe mazao ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haiwezi kutokea hivi hivi kama Serikali haiweki mkakati madhubuti. Kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri amesema lakini hajagusia namna gani anaweza kumsaidia mfugaji. Ameangalia zaidi sheria za kulinda hifadhi za Taifa, tunapenda ziwepo lakini bado kuna umuhimu wa kumsaidia mfugaji ili naye aweze kuona ubora na faida ya kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili lipo katika maeneo ya Kijeleshi. Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyokuja katika ziara ya Mkoa wa Simiyu alikuta matatizo katika Wilaya za Busega, Bariadi, Itilima na Meatu. Ina maana ukanda mzima wote wa Simiyu una mgogoro mkubwa sana na tusipotafuta ufumbuzi wa haraka ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu baadhi ya askari wa wanyamapori si waadilifu na si waaminifu kwani wanawatesa wafugaji hawa, wanatesa mifugo hii. Mheshimiwa Waziri alitoa tamko wakati nauliza swali hapa Bungeni alisaidia mifugo 6,000 iliyokuwa imefungiwa porini kwa siku tatu na wanaomba rushwa, wanaomba hela na wakipewa hela hazifiki zinapotakiwa kwenda, hazikatiwi risiti yoyote ile. Namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na watu wake hili suala likemee kwa nguvu zote na naomba tupate ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hiyo haitoshi suala hili ni mtambuka, lazima Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Ardhi, Waziri wa Kilimo, Chakula na Mifugo na Waziri wa Maliasili washiriki kikamilifu. Tusipopata *solution* itatupa shida sana huko tunapoelekea. Leo wafugaji wanagombana na wakulima, wanagombana na hifadhi, tutafika wapi? Namwomba sana Mheshimiwa Waziri tusaidie katika hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu suala zima la kudorora kwa sekta ya utalii. Tunajua uchumi wa dunia umebadilika sana, lakini napenda kuona Mheshimiwa Waziri anakuja na mkakati. Biashara ya utalii inazidi kudorora lakini ukiangalia biashara ya utalii imekuwa ikiingiza mapato makubwa sana katika nchi hii. Leo hii mahoteli hayana watu, hayana biashara, migahawa haina biashara, watalii hawaji na bado hizi gharama zingine za kuendesha utalii ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri hebu ajaribu kutusaidia kuja na *package* namna gani ya kuweza kufufua suala zima la utalii katika nchi yetu. Tusione kwamba watalii wanakuja tunafurahia, lakini tuone wanakuja na kutuma fedha ili ibaki hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala zima la geti ya Ndabaga ambayo ndiyo kielelezo na kioo cha *Western Corridor* upande wa Serengeti, lakini ukifika pale lile geti hali-reflect kwamba unaingia kwenye hifadhi kubwa ya Serengeti, limechakaa, liko hovyoo hovyoo, halina ukarabati wowote ule. Naomba haya mapokezi yaweze kuboreshwa ili kusudi hata mtalii anapokuja aone kwamba nimeingia kwenye kioo cha hifadhi kubwa hapa duniani, naomba Waziri alizingatie hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kumgusia Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA, nikamwambia tujitahidi kuboresha kwa sababu wanasema *reception counts before somebody enters into the house*, kwa maana kwamba mapokezi ya nyumba, unapofika pale mbele ya uso wa nyumba ndiyo kielelezo kwamba nyumba yako iko vipi kwa ndani. Naomba sana hilo tuweze kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ni suala zima la Hifadhi ya Sayaka, ni pori la akiba la zamani. Mheshimiwa Kiswaga aliwahi kuuliza hapa swali, ile hifadhi haipo, hakuna miti, hakuna nini, huwezi kusema ni hifadhi, wananchi wanalima, mazao yanakatwa eti ni hifadhi. Naomba jamani unyanyasaji wa namna hii tuachane nao. Namwomba Mheshimiwa Waziri atume watu wake waende kwenye hifadhi ya Sayaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Sayaka iko katika Wilaya tatu za Magu, Bariadi na Busega. Kwa upande wa Busega kuna Kata za Nyaruhande na Badugu na upande wa Magu Kata ya Sayaka. Naomba tuangalie kwa ukaribu kama tunadhani ile ardhi haina maana tena ni bora tukajaribu kuacha sehemu za vyanzo vya maji ili wakulima waweze kufanya kilimo cha kujikimu, watu wapate chakula. Leo watu wanalia wana njaa na mnasema kuna hifadhi ambayo imezuiwa wakati haipo. Kwa hiyo, naomba sana hili suala liweze kuangaliwa vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ni suala la tembo waharibifu. Sisi watu wa Busega na sasa hivi nimepata message nyingi wanalia kwamba tembo wanavamia, wanakula mazao yao na kuharibu mashamba yao na hakuna fidia yoyote ile. Naomba Mheshimiwa Waziri tutafute mkakati mbadala wa kujaribu kuzuia wanyama hawa ambao wanakuja kushambulia binadamu pamoja na mazao yao, matokeo yake wananchi wanalima sana lakini siku ya siku wanakosa faida, hawawezi kuvuna. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la hii Operesheni Tokomeza. Kuna watu walinyanga'anywa silaha zao wakati wa zoezi hili, silaha zao za jadi na silaha zingine ambazo walikuwa wamezisajili hazijarudishwa mpaka leo. Hivi Mheshimiwa Waziri nini dhana nzima ya kuwasaidia wananchi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Waziri anapohitimisha hotuba yake atuambie ni nini hatma ya watu hawa ambao silaha zao zilichukuliwa wakati wa zoezi hili la Operesheni Tokomeza. Kwanza tujue silaha hizi ziko wapi na zinafanya nini na je, watarudishiwa? Ni vema haya yote Mheshimiwa Waziri akayaweka vizuri na nilishazungumza naye anayafahamu, ili kusudi hawa wananchi waweze kupatiwa haki yao bila kuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine utalii lazima tuendeleo kuu-*embrace* vizuri. Leo hii Watanzania unafika *airport*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf Salim, ajiandae Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni ya leo kusimama hapa. Jioni ya leo nataka kumshauri tu Mheshimiwa Waziri na kuishauri Serikali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri awe makini, atulie *bardan wasalaman, laa takhaf wa laa tahzan*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hadithi ndogo wakati nasoma miaka ya 70, darasa la tatu kulikuwa na kitabu kidogo cha Kiswahili maarufu tukikiita Haji na Selele, kilikuwa na hadithi nyingi ndogondogo. Sasa tukisoma tukimaliza mwisho wake tunaulizwa hiyo hadithi imekufunza nini? Moja kati ya hadithi iliyokuwemo ni ile ya mtu aliyekuwa na kuku wake kila siku akitaga yai moja la dhahabu. Siku hiyo akaamua kumchinja ili apate mayai mengi ya dhahabu matokeo yake akakosa yote. Hadithi hii inatufunza nini? Tamaa nyingi mbaya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na-*declare interest* kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Wizara hii, lakini pia nimeshawahi kutumikia Idara ya Misitu na Utalii, kwa hiyo nazungumza kitu ambacho kinaelea katika kichwa changu, nakifahamu. Binafsi wakati nilipoteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati hii na nikakutana na viongozi wa Wizara nilieleza waziwazi baada ya taarifa kwamba sifurahishwi na *TFS* na nikawa na mashaka nayo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika zaidi baada ya kupata semina na ile hofu yangu ikathibitishwa na mtaalam aliyebobea katika masuala ya misitu kwa utafiti wake alioufanya kwa muda wa miaka mitatu juu ya *TFS*. Nakushauri nini Mheshimiwa Waziri? Kwa sababu ameyakuta haya lakini kwa sasa yeye ndiye mwenye dhamana na Wizara hii, kwa hiyo, mwaka huu namshauri tu ila mwakani nitambadilikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFS* ni nzuri katika ukusanyaji wa kodi lakini namwomba Mheshimiwa Waziri alinganishe sasa tunachokipata na athari tunayoipata, vinalingana? Misitu ya asili inapotea na itazidi kupotea na kwa mujibu wa mtaalam baada ya miaka 10 Tanzania hii itakuwa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwakumbushe wale wanaokumbuka mwishoni mwa miaka ya 80, kazi kubwa tuliyoipata Watanzania na dunia kwa suala la HASHI na HADO kwa Mikoa ya Dodoma na Shinyanga ilivyokumbwa na janga la ukame, kazi iliyofanyika ndani na nje ya nchi. Binafsi nilifika Dodoma hapa kwa ajili ya kupanda miti kutokana na hali iliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri aichambue *TFS*, aone udhaifu wake. Udhaifu wa *TFS* ni menejimenti, ni lazima ahakikishe kwamba anabadilisha, wanakusanya vizuri, wanapanda vizuri, lakini katika misitu ya asili suala la kuelekeza nguvu tu kwamba wakusanye kodi wanatumaliza misitu kitu ambacho kitakuja kuwa ni hatari kubwa kwa Taifa hili. Badala ya rehema hii misitu itakuja kuwa nakama kwetu, Mheshimiwa Waziri namshauri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo hatuwezi kuwa na misitu endelevu, hatuwezi kuwa na misitu yenye tija, hatuwezi kuwa na misitu ambayo itatuletea faida sisi na kizazi chetu kama hatuna wataalam katika fani hiyo ya misitu. Leo nchi hii ina Chuo kimoja tu cha Misitu Olmotonyi, lakini Serikali imekitelekeza. Chuo kile kimekuwa kama yatima, hakina ruzuku yoyote kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kile chuo kiangaliwe, kipewe ruzuku, kisimamiwe, kismeshe wataalam wengi zaidi ili warudi katika misitu yetu ambayo iko chini ya Wizara, Halmashauri na Vijiji ili iwe ni misitu endelevu kwa faida yetu na faida ya kizazi kijacho. Huo ndiyo ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa siku ya leo katika upande wa misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye utalii. Amezungumza na kutoa ufafanuzi mkubwa juu ya nia yake ya kutoka kwenye watalii milioni moja na zaidi kwenda milioni tatu. Ni wazo zuri, tunaliunga mkono kwa sababu tunafahamu ongezeko la watalii litaleta faida gani kwenye nchi yetu, lakini

lazima tujue tunataka aina gani ya watalii katika nchi yetu? Kwanza iwe ni kwa ajili ya kukuza mila na desturi zetu lakini wawe ni watalii wenye faida siyo watalii vishuka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, ili kupata watalii wazuri lakini kuwa na wawekezaji wazuri katika sekta ya utalii na kuondoa tofauti baina ya watalii, wawekezaji na jamii inayozunguka hivi vituo vya kitalii lazima kuwa na *triangle* ambayo itahusisha *investors*, Serikali na *community*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutakapokuwa na *triangle* hiyo na wakawa pamoja na kujua mwekezaji anahitaji nini, Serikali inahitaji nini na jamii inahitaji nini, mkawa mnasimama katika kitu kimoja, mwekezaji akija hapa katika muda mfupi atakuwa amepata idhini ya kuwekeza lakini pia itakuwa uwekezaji huo una faida kwa sababu kila mmoja atakuwa anajua majukumu yake na yamepangwa yapo. Kwa hiyo, hilo namshauri Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi mtalii anachohitaji ni huduma. Inasikitisha unapokwenda katika hoteli zetu au katika vivutio vyetu vya kitalii kwa zile huduma zinazopatikana pale. Mtalii hahitaji jengo zuri ambalo labda lina ma-AC na kadhalika, anachohitaji hata kama ni kibanda cha nyasi lakini kiko katika kiwango gani? Je, tumeviweka katika viwango vile ambavyo wao wanavifurahia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli watalii wanafurahia sana *tradition* yetu lakini je, watendaji wetu ambao wanafanya kazi hiyo, wanafanya kazi wakiwa na uweledi huo? Ndiyo maana katika Kamati nikakikamata sana Chuo kile cha Utalii, je, mnafundisha kulingana na mahitaji tunayoyahitaji ndani ya nchi yetu? Kwa hiyo, chuo kile kitoe wataalam ambao watakuwa ni wale wanaohitajika kulingana na mazingira yetu na matakwa yetu na lengo letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana mwaka mmoja wa kuondoa yale yote mabaya ambayo leo tunamwambia ambayo ameyakuta na mwakani hapa atakapokuja katika bajeti tuje tuone *improvement*. Kama ipo mimi tutakuwa pamoja, kama haipo Mheshimiwa Waziri kwa kweli mimi nitakuwa adui namba moja katika hili. Kwa sababu ninayoyazungumza nayazungumza nikiwa nayajua na najua kuna nini. Leo nazungumza tu hapa vizuri lakini siku nyingine nikiamua kuzungumza vibaya atakuja kuelewa kwamba kweli hiki kitu ninachokizungumza nakifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunataka kile chuo kinachotoa vijana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lucy Owenya wajiandae Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba na Mheshimiwa Rose Tweve.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kipekee naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na nikiwa kama mdau wa utalii na Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii niweze kuchangia yangu machache. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii unachangia 17.5% kwenye pato la Taifa, lakini tunaweza tukafanya vizuri zaidi kama tutakuwa na mikakati ya kutosha kwanza kwa kuutangaza vya kutosha na pili kuhakikisha kwamba tunagundua utalii mpya. Nimefurahi Mheshimiwa Waziri amesema atatangaza sehemu za utalii Mwanza na kila mahali, lakini naomba nimshauri tu hata hapa Dodoma kuna utalii mzuri tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama naweza nikashauri kuna mawe mpaka Singida. Dodoma tunaweza tukatangaza utalii wa *Stone Mountain* kama ilivyo *Table Mountain South Africa*, watu wanaenda kwenye *Table Mountain* wanatembelea mashamba ya zabibu. Kwa hiyo, wanaweza wakapita hapa kama *destination* ya *a day tour*, wakifika hapa watatembelea hiyo *Stone Mountain*, watatembelea zabibu, wanaweza wakatembelea Chuo Kikuu na *attraction* ya Bunge as well. Kwa hiyo, watu wa Dodoma nao wanaweza wakapata mapato kutokana na utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaweza tukawa na watalii *throughout the year* kuanzia Januari mpaka Disemba lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri wajaribu kuwa na *rates* za *peak season* na *low season*. Kwenye hoteli tayari tuna *peak* na *low season* na wakati huu mwezi Machi mpaka wa Julai pia *airlines* zina *low season*. Kwa hiyo, ningeshauri Wizara muangalie ni namna gani mnaweza mkapunguza ile *park fee* ili tuweze kuendana na utalii kama nchi nyingine zinavyofanya; kunakuwa na *low season* na *high season*. Kwa hiyo, ningeshauri wafanye hivyo ili tuweze kuongeza watalii zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzania Tourist Board* imetengewa *4.1 billion*. Kwenye hii *4.1 billion* wametoa *1.4* kwa ajili ya mishahara, ina maana wanabaki na *2.6 billion*. Mheshimiwa Waziri amesema wataenda kutangaza *CNN*, *BBC* na matangazo mengine wataweka kwenye majarida na kadhalika. Hata hivyo, kwenye Hotuba ya Upinzani wamesema mwaka 2013/2014, walifanya maonesho kule Sunderland - UK na wanadaiwa karibu shilingi bilioni tano. Sasa



sielewi kama hii 2.6 billion inaenda kulipa deni au lile deni linalipwa na nani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia vifungu vyote vya randama ya Maliasili na Utalii sijaona hili deni wanalipaje. Mheshimiwa Waziri hebu alete bajeti ambayo ina uhalisia, watakuja kumtumbua hapa, watasema hafanyi kazi lakini pesa hapewi. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri aandikie bajeti yenye uhalisia, aseme madeni ni haya na anahitaji pesa kiasi hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumzie kidogo Mlima Kilimanjaro. National Parks zimeingiza shilingi bilioni 185, out of shilingi 185, Kilimanjaro National Park imeingiza shilingi bilioni 60, hizi ni fedha nyingi sana. Najua KINAPA wanajaribu kujenga madarasa na kadhalika lakini bado Halmashauri zinazouzunguka Mlima Kilimanjaro hazifaidiki na mapato yanayotokana na Mlima Kilimanjaro. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye migodi wanapata 0.3% ya pesa zinazotokana na mgodi, kwa nini isifanyike hivyo kwa Kilimanjaro? Shilingi bilioni 60 ukitoa 0.3% ni hela nyingi sana ambazo zingepewa Halmashauri wakaweza kufanya maendeleo yao wenyewe, wakatengeneza zahanati na madarasa. Mheshimiwa Waziri hata Mwanga ipo katika hizi Halmashauri ambazo zinafaidika na mapato ya Mlima Kilimanjaro, kwa hiyo, nategemea atalichukulia hili on a serious note. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mlima Kilimanjaro ni lazima Wizara ishirikiane na Wizara ya Mazingira, Mlima Kilimanjaro unaharibika. Wamejaribu kukusanya takataka kutoka Mlima Kilimanjaro lakini bado hazijakwisha. Kwa sababu wataalam wako hapa kule Mti Mkubwa kupitia Lemosho na kule Barafu, vyoo viko vitatu na vya shimo ambapo ma-porter, ma-guide na wageni, zaidi ya watu 300 wanatumia vyoo hivyo. Tumekuwa tukiongea hapa ndani ya Bunge hili kuna vyoo ambavyo vilitoka Ujerumani kwa ajili ya majaribio sijui mpaka sasa hivi vyoo vile vimeishia wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kujumuisha atueleze vile vyoo mpaka sasa hivi vimeishia wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo linaenda sambamba na maji. Barafu, Mweka na Millenium Towers, hakuna maji. Kwa nini sasa KINAPA wasichukue maji kutoka Karanga waka-pump yakaja pale juu ili watalii waweze kuyatumia badala ya sasa hivi wanaenda kuzoa maji mbali na kuyaleta pale. Sasa hivi kule crater watu wana camp crater lakini Mheshimiwa Waziri crater hamna choo, watu wanalala kule halafu ndiyo wanapanda juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watalii wanakuja zaidi ya mara 10 wanakuta mambo ni yaleyale business as usual. Kwa hiyo, naomba waangalie ni jinsi gani wataweza kutengeneza kule crater kuwe pasafi, ni pachafu sana.



Kwa hiyo, waangalie ni jinsi gani wataweza kutengeneza kule juu ili hawa *tour leaders* wanaorudi waweze kutuletea watalii kwa wingi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *Southern Circuit*. *Southern Circuit* tunashindwa kuiuza kwa sababu miundombinu si mizuri. Tumekuwa tukizungumza mara nyingi, sasa Wizara hii na Wizara ya Miundombinu iangalie ni jinsi gani inaweza kutengeneza miundombinu ya kwenda *Southern Circuit*. Wawekezaji wanakuja wanataka wakajenge hoteli lakini wageni watafikaje huko, hoteli ni ghali sana. Kuna ndege moja inayoenda huko inaitwa *Coastal Air* lakini *price* yake ni sawa na mtu anayetoka hapa kwenda *Europe*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazungu wengi wanaokuja Tanzania wana-*save for years*. Unakuta mtu ame-*save almost five, six years* ili aweze kuja Tanzania. Tukumbuke wageni wengi wanakuja kwa *credit card*, akifika hapa anajaribu kuangalia ni kwa jinsi gani anaweza ku-*save* aizungukie Tanzania yetu ilivyo nzuri lakini unakuta mara nyingi wanaishia kwenye *Nothern Circuit* kwa sababu ni *cheaper*, kuna hoteli nyingi lakini wanashindwa kwenda *Southern Circuit* kwa sababu ni *too expensive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali muangalie ni kwa jinsi gani mnaweza kushirikiana na Wizara ya Miundombinu ili muweze kutengeneza hizo barabara ili wawekezaji waweze kuja kujenga hoteli kule na tuweze kuiuza kama tunavyoiuza *Nothern Circuit*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo huyu mjusi aliyeko huko Ujerumani. Kambi ya Upinzani imezungumza vizuri sana, ni fedha nyingi zinazopatikana kule Ujerumani. *Euro 25* kwa watu 550 unaongelea karibu shilingi bilioni nne, sasa hivi sisi hatuhitaji hizo shilingi bilioni nne kweli?

Mheshimiwa mwenyekiti, ni kwa nini sasa msifanye *arrangement* aidha na sisi tupate *percent* yetu kama ikishindikana msafirisheni basi yule mjusi. Akiwekwa kwenye meli akawekwa pale Dar-es-Salaam ina maana watalii watakuja Dar-es-Salaam badala ya kwenda Ujerumani na sisi tutafaidika. Kuna vipesa vidogovidogo tunahangaikanavyo kwa ajili ya zahanati na kadhalika si vitapatikana pale! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nategemea sasa Mheshimiwa Waziri anavyokuja kutujibu atatueleza ana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba yule *dinosaur* wanamsafirisha aje hapa. Katika Bunge hili yule mama wa Lindi mpaka tukamuita mama mjusi humu ndani, alikuwa anamzungumzia kweli lakini hakuna kilichofanyika mpaka leo. Ni mategemeo yangu sasa kwa wakati huu Mheshimiwa Waziri atakuja na majibu atueleze ana mikakati gani ya kuhakikisha mjusi yule anarudi Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisikitisha, mpaka sasa hivi hatuna Bodi ya TANAPA. Naomba Waziri anapokuja kujumuisha hapa hebu atueleze ni kitu gani au ni kwa nini wanashindwa kuunda Bodi ya TANAPA? Vitu vingi sana haviendi, tunalalamika hapa bila Bodi hawawezi kwenda kufanya chochote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aje atueleze ni lini ataunda Bodi ya TANAPA...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dua William Nkurua ajiandae Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mheshimiwa Tweve ni kesho, ataingia Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuongea katika Bunge lako Tukufu. Daima nitaendelea kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Nanyumbu kwa maamuzi yao ya busara yaliyosababisha mimi kuwa Mbunge wao na hatimaye ndiye mwakilishi wao katika jengo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuzaliwa nchi hii ya Tanzania, ninamshukuru sana Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni nchi ambayo Mungu aliipendelea na bado natafiti kwa nini tumependelewa hivi sijapata jibu. Nchi hii ina vivutio vikubwa duniani, sisi ni miongoni mwa watu tunaomiliki Mlima Kilimanjaro, unasifiwa kwamba ni wa pili duniani au wa kwanza Afrika, upo Tanzania lakini Tanzania hii ndio nchi ya pili duniani kuwa na vivutio vingi sana, lakini pamoja na hayo yote tukiacha mambo mengine kama *Tanzanite* na mambo mengine ambayo Tanzania anamiliki peke yake, dunia nzima anayo Tanzania peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa kwa kweli lazima tukiri hatujajipanga vizuri kutumia vitu hivi ambavyo Mungu ametupatia. Pamoja na hayo ambayo yanatajwa Wizara hii ndio ambayo kama tungeitumia vizuri, wataalam wetu wangejipanga vizuri ni Wizara ambayo ingeweza kupatia nchi hii fedha nyingi ambazo malalamiko mbalimbali ya barabara, hospitali na mambo mengine, tungeweza kutumia Wizara hii kutafuta hizo fedha na hatimaye Watanzania wakanufaika na huduma mbalimbali katika ukusanyaji wa fedha kupita Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukizungumza ukweli bado hatujakaa vizuri. Sasa kama walivyotangulia wengine kwamba Mheshimiwa Maghembe ndiyo ameanza kubeba huu mzigo, lakini hapa tutazungumza mapungufu mengi ambayo tumeona yamejitokeza kule nyuma. Mimi ni miongoni mwa watu wanaosema tunakushauri, tutakuangalia baadaye, lakini tunakushauri na

utusikilize vizuri, kwa sababu kama hutatuelewa sisi nafikiri na sisi hatutakuelewa mbele ya safari, itatulazimu tuwe hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanza kushauri Wizara hii katika eneo la kutengeneza Watanzania kupenda mazingira hasa ya hifadhi na mbuga za wanyama. Wizara yako ina jukumu kubwa la kuwafanya watu wapende mbuga za wanyama, wapende hifadhi. Watapenda baada ya kuona matunda mazuri yanayotokana na hilo. Binadamu ameumbwa kupenda mazuri na kuchukua mabaya, ukimfanyia jambo zuri mwanadamu anafurahi, ukimfanyia vibaya anakasirika ndio binadamu wa kawaida, na Watanzania wengi wako hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu wote ambao wamezunguka hifadhi kwa kweli wao wanajiona wako katika eneo la balaa sana. Kwa sababu mateso wanayopata wale ambao wamezunguka hifadhi ni makubwa mno utafikiri Serikali haipo. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu na Nanyumbu tuna hifadhi tunaita Lukwika – Lumesule. Hifadhi ile kila siku inakuwa yaani mipaka tunayoifahamu sisi inaongezeka. Wananchi wamepanda mazao yao lakini unashangaa unaambiwa hifadhi sasa inafika hapa. Sasa wananchi *automatically* wanaichukua hifadhi hata kama utawaambia kitu gani wanaichukua kwa sababu hifadhi inaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akitembelea kwenye Jimbo langu kwenye Kata ya Lumesule, Kata ya Napacho kwenye vijiji vya Napacho vyenyewe, Kijiji cha Mitonga na kwa ujumla ile Kata vijiji vyake wao wamezunguka hifadhi, lakini hifadhi imekwenda kukata mikoroshu na kuwaambia kwamba ninyi mpo ndani ya hifadhi. Wananchi wale wanaichukua hifadhi na wanaona kwamba kuwa karibu na hifadhi ni kero. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, hakikisha kwamba mgogoro huu ambao upo kwenye Kata ya Napacho unaondolewa ili wananchi wapende hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Kata ya Mkonona, kijiji cha Marumba na vitongoji vyake vya Namunda na Namaromba, kijiji kimesajiliwa, kina shule ya msingi, kina zahanati, kina barabara, kijiji kipo tangu Uhuru, leo wanaambiwa wapo ndani ya hifadhi. Sasa kama Serikali watu hawa imewapa miundombinu hii wamekaa hapo, watu wamehamia pale wamejenga majumba yao wanaambiwa leo wapo ndani ya hifadhi, wananchi hao wanaishi kwa mashaka. Tunawafanya watu wajisikie vibaya ndani ya nchi yao, unategemea wananchi watapenda hifadhi? Nakuomba sana Waziri, mimi nina matumaini makubwa unaweza kubadilisha hii hali. Twendeni tuwaache hawa watu waishi katika nchi yao vizuri, kama tulizubaa sisi Serikali tukawaachia watu wakae mudu mrefu ni kosa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama tuna uwezo tutume watu wakatahimini pale walipwe fedha waondoke kama tuna uwezo, kwa sababu wananchi wako pale hawakuambiwa chochote, wamepewa Hati, kupewa Hati maana yake ni sehemu sahihi na salama kuishi. Leo unawaambiwa iko ndani ya hifadhi, huu ni unyanyasaji, kwa hiyo lazima tutengeneze mazingira rafiki na wanachi. Hilo Mheshimiwa Waziri ni eneo la kwanza ambalo nimetaka nishauri na naomba tulizingatie.

Mheshimiwa Menyekiti, eneo la pili tuwe na utaratibu mzuri wa kutoa ahadi zinazotekelezeka. Kwa mfano Wilaya ya Nanyumbu kwenye Kata hii ya Napacho kipindi hiki tarehe 8/08/2011 alitembelea Waziri wa Maliasili na Utalii kipindi hicho Mheshimiwa Ezekiel Maige. Alikwenda kijiji cha Chimika na Masuguru, alikuta pale wananchi wana shida kubwa ya maji, na shida aliyoiona kipindi kile mwenyewe akaahidi kutoa shilingi milioni sita Chimika na kutoa shilingi milioni sita Masuguru ili Halmashauri iongeze fedha nyingine wananchi wale wapatiwe maji kwa sababu na wao wamezunguka hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea Mpaka leo fedha hiyo haijalipwa, Halmashauri imeandika barua nyingi hazina majibu. Sasa wananchi unapowaambia kuwa karibu na hifadhi kuna manufaa ya kuweza kupatia miradi mbalimbali na kutatua kero hawaoni. Yote haya yanasababisha wananchi wachukie hifadhi.

Ninaamini uongozi mpya wa Mheshimiwa Profesa Maghembe tutaondoa tatizo hili na hatimaye wananchi wataona faida ya kuzunguka hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuchangia eneo la utoaji wa adhabu kali kwa watu ambao wanapatikana katika maeneo ya hifadhi. Kwanza na mimi nataka niwe mmojawapo ninayekiri kwamba sipendi watu waingilie maeneo ya hifadhi, maeneo haya tumeyatunza kwa ajili yetu sisi na vizazi vinavyokuja ili Watanzania baadaye waweze kurithi huu utajiri ambao Tanzania tunao. Lakini wale watu ambao wamepata haya matatizo wameingia kule na wakaweza kushikwa wakadhibitiwa basi wapelekwe kwenye vyombo vya sheria wakapate hukumu stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea wananchi wanapigwa afadhali nyoka, yaani nyoka huyu mnayemfahamu ananafuu anavyopigwa kuliko anayeshikwa kule. Lakini siku zote Serikali inatangaza kwamba tuwaambie wananchi wasichukue sheria mkononi, wale wanaopigwa njiani, barabarani? Mtu anashikwa ndani ya hifadhi analetwa mpaka kijijini anapigwa anaburuzwa, hii sio sheria mkononi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi napowakemea wananchi jamani acheni tabia, mkimkamata mwizi msimpige, mpelekeni mahakama. Wanauliza

Maliasili wakitukamata sisi mbona wanatupiga hovy mbona hawatupeleki mahakamani? Unajibu kitu gani hapo? Mheshimiwa Waziri, una uwezo wa kuthibiti hili ondoa, askari wetu wasitumie sheria mkononi, tunajenga tabia mbaya kwa Watanzania na wao watatumia sheria mkononi, tusiwalaumu kama sisi wenyewe tunawafundisha hii tabia.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri hii mizigo ambayo imeikuta jaribu kuiondoa na nina uhakika utakuwa na uwezo wa kuiondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho nilitaka nijielekeze katika kuiomba Serikali kutotumia nguvu za ziada hasa kwa maeneo mengine ambayo inatia aibu. Wilaya yangu sio ya ufugaji, kwa hiyo tatizo langu tu kidogo lipo la migogoro ya wafugaji wachache waliokuja kwenye Wilaya yangu hasa kwenye Kata ya Masuguru, lakini maeneo mengi Waheshimiwa Wabunge wamelalamika humu kwamba askari wanapiga risasi ng'ombe. Hii inaleta aibu kwa nchi yetu....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Dkt. Tizeba ajiandae Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, ajiandaye Mheshimiwa Mendrad Kigola.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nitachangia katika maeneo mawili, nitachangia kuhusu sera ya uhifadhi na baadaye nitachangia katika migogoro ya wafugaji na Serikali.

Mheshimiwa Menyekiti, sera ya uhifadhi shirikishi ni sera nzuri sana. Ukiisoma utaona ni kwa namna gani sera ile inavyozingatia maslahi ya wananchi katika uhifadhi wa maliasili za aina zote. Lakini kuna tatizo kubwa sana katika utekelezaji wa hii sera, kwa sababu sheria na kanuni zilizotungwa kuhusiana na hii sera hazitoi nafuu yoyote kwa wananchi, zimeegemea upande mmoja na nitatoa mifano kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, uhifadhi shirikishi wa misitu, utakuta msitu wa Serikali au shamba la miti liko eneo fulani. Wananchi kwa mujibu wa sheria wanalazimika kushiriki katika kuhakikisha kwamba shamba lile la Serikali haliungui moto, halihujumiwi, haliibiwi, halifanywi nini kadhalika na kadhalika. Lakini inapofika muda wa kunufaika na hilo shamba hao wananchi waliokuwa wakiambiwa hayo yote hawaonekani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo nilikuwa namuuliza hapa Mheshimiwa Kigola wa Mufindi, kwamba hivi huko Mufindi ndugu yangu wananchi wa vijiji vyako shule zao madawati yamo? Jibu hapana!

Mnafaidikaje? Ananiambia kuna baadhi ya vijiji wanapata pata kingao kidogo hakitoshi hata kuezeka nyumba tano, kumi za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa nimuombe sana Waziri, nilimsikia juzi Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa huko Kusini, nilisikia vyombo vya habari sasa sijui kama ni kweli na nitaomba sana athibitisha hili jambo kwamba sasa Wizara imeelekeza ugawaji wa *quater* zile za kuvuna katika mashamba haya ya Serikali ushirikishe pia vijiji vililo katika maeneo hayo, yaani ya Serikali za Vijiji zilizo katika maeneo hayo. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri katika ku-*close* hotuba yako mtupe basi huo uhakika tusije kutoka hapa tunaamini tuliyasikia kwenye vyombo vya habari kumbe si hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili uko kwangu inasikitisha sana, Msitu wa Buhindi uko pale, unaomba Mbunge au Halmashauri mpate mgao wa miti ili muondoe tatizo la madawati, mnapewa *cubic meter* 100. *Cubic meter* 100 hizo Mheshimiwa Waziri hatupati bure tunapewa kama mfanyabiashara wa mbao, tunaambiwa na zenyewe tuzilipie. Sasa muanze kupitisha mchango kwa wananchi ili kulipia *cubic meter* 100 kwenye shamba la umma. Haya mambo yako chini ya uwezo wa Mheshimiwa Waziri, hayahitaji sheria, ayafute tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale ndio wanaoutunza ule msitu, sasa iweje tena ikifika wakati wa kuvuna wanaambiwa walipie fedha ili kupata miti kadhaa pale kwa ajili ya kujengea darasa la umma, kujengea zahanati ya umma, kujengea nyumba ya mwalimu ya umma? Nikuombe sana, lakini pia msemaji mmoja amewasifia *TFS* kwa kukusanya sana mapato, nadhani yuko kule bwana kwanye kambi ile kule. Nakubaliana naye kabisa wenzetu wale wanajua kweli kukusanya, lakini sasa wanakusanyaje? Swali la pili hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita kwa mfano katika hifadhi za Serikali hizi ambazo kulikuwa na wananchi wanafanya shughuli zao mbalimbali, kwa ruhusa ya *TFS* watu hawa walikuwa wanatozwa kiasi kidogo tu cha kuwa kule ndani shilingi 64,000 kwa mwaka. Hawa watu walioko kule wanaganga njaa hakuna matajiri kule. Baadaye ghafla imetungwa kanuni nina hakika sio wewe Mheshimiwa Maghembe, atakuwa aliyekutangulia. Imetungwa kanuni watu hawa wanatakiwa walipie shilingi 74,000 kwa *square meter* moja. Sasa fikiria huyu mtu, mvuvi, na hili nadhani Mheshimiwa Mwigulu unafahamu tulishakuambia, mvuvi anazo kodi zingine 13 tofauti, lakini hata makazi tu kwenye eneo anakofanyia kazi anaambiwa alipe shilingi 74,000 kwa *square meter* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvuvi wa dagaa anahitaji eneo la kuanikia dagaa. Sasa lile linapigiwa na lenyewe hesabu, *square meter* moja shilingi 74,000 mtu kama ana *square meter* 20 shilingi milioni moja sijui kiasi gani uko. Watu wanatozwa mpaka shilingi milioni tano, wale maskini wale wanaambiwa



walipe shilingi milioni tano hutaki toka, Sasa haya mambo siyo mazuri sana na nimemuomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli liko ndani ya uwezo wako, hili unaweza kulifuta mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hili la migogoro ya wafugaji na Serikali, mimi nasema mgogoro wa wafugaji na Serikali na si mgogoro wa wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri Serikali yote iko hapa, hivi tafsiri ya ufugaji wa kisasa kwa leo ni ipi? Maana tunaambiwa kuchunga ni vibaya kwa hiyo, wafugaji wapunguze mifugo yao kwa sababu wanachunga. Lakini yule anayegawiwa ranchi pale Kitengule au wapi, huyo anaonekana na mfugaji mzuri kwa sababu amekatiwa kipande cha ardhi na mifugo yake iko mle ndani. *Be it* 300, 1,000 kwa sababu ina kipande cha ardhi amegawiwa huyu ni mfugaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule ambaye hajagawiwa kipande rasmi na Serikali ni mchungaji, ni mtu mbaya, apunguze mifugo yake. Niombe sana tupate kwanza tafsiri ya ufugaji uliokuwa mzuri, ni ule wa ng'ombe ndani ya banda unakata manyasi unaweka au namna gani. Lakini tatizo langu sio tu hapo, tatizo ni sera yenyewe ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya mifugo haikwenda mbali ikaitazama mifugo hii wakati wa majanga, sisi binadamu tumejiwekea kinga kwenye mazao kwa sababu tunakula sisi, kwamba ikitokea jua likawaka sana wananchi wakaacha kuvuna kwa vile ni binadamu basi tulianzisha *NRFA* na kadhalika. Utaratibu upo ulionyooka wa kuhakikisha watu hawafi njaa, mbona hatuweki utaratibu wa mifugo kuhakikisha haifi njaa? Mifugo si tunaihitaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu ya muda Mheshimiwa Waziri, haitoshi hapa mimi nikaelezea mimi ninachokifikiria chote, nitakuomba tu kabla ya kesho jioni tafuta muda hata wa dakika 20 tuzungumze niseme ninachokifikiria kuhusu hili jambo. Tunaweza kabisa katika Awamu hii ya Tano tukaweka nyuma suala la migogoro ya Serikali na wafugaji kwa sababu uwezekano huo upo na Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kumaliza tatizo la hivi, wako wengine wameshafanya na hawana habari tena na migogoro ya hifadhi na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakuandama tu, Maghembe na migogoro ya wafugaji, si lako hili ni mtambuka mno. Linahitaji ushirikishwaji wa Serikali nzima ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linakwisha kabisa na miaka ijayo wananchi waendeleo kufanya ufugaji usiokuwa na shida na kilimo kisichokuwa na shida; kwa sababu *issue* inayosumbua wafugaji ni pale mifugo yao



inapokosa malisho basi. Mifugo kama ina malisho huwezi kumuona Msukuma anatoka Meatu anakwenda Sumbawanga...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar hayupo, Mheshimiwa Mendrad Kigola, ajiandae Mheshimiwa Boniphace Getere na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia na mimi katika hoja hii muhimu sana. Mimi leo sehemu kubwa itakuwa ni ushauri kwa sababu Waziri anayeanza sasa hivi ni mara ya kwanza kushika nafasi hii ya Wizara ya Maliasili. Ila nataka niseme tu, Wizara ya Maliasili ni Wizara ngumu sana kwa sababu inagusa maeneo mengi sana ambayo yanahusu maslahi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianza na masuala ya migogoro ya wananchi na Hifadhi. Kila kona Tanzania nzima kuna hifadhi ya misitu, na kule kwangu Mufindi kuna vijiji ambavyo viko ndani ya msitu lakini nataka niseme kwamba vile vijiji vilianza miaka mingi sana, miaka ya 1974, 1976, kwa hiyo misitu umekuta vijiji, kwa sababu ile misitu imepandwa mwaka wa 1977. Sasa namuomba Waziri, kuna vijiji vile ambavyo Mawaziri waliopita waliweza kutembelea vile vijiji na walihidi kwamba wataachiwa na waliunda Tume, Tume ikafanya mchakato kule, na bahati nzuri sana wakasema kwa sababu siku hizi ni ushirikishwaji pamoja na wananchi, basi yale maeneo watawaachia wananchi waendeleo kufuga na kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuomba kuna kijiji cha Kitasengwa pale, Kitasengwa ni kijiji ambacho kinapakana na msitu pale na wananchi waliacha maeneo makubwa kuwaachia Wizara ya Misitu wakabakiwa na maeneo madogo na yale maeneo madogo Wizara ya Misitu inataka kuwanyang'anya. Nakuomba Waziri yale maeneo madogo wawaachiwe wananchi wa Kitasengwa pale, na watu wa misitu wanaelewa na barua tulishaandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuna kijiji cha Ihomasa, Mheshimiwa Waziri Ezekiel Maige alienda, hata kipindi cha Mheshimiwa Balozi Kagasheki alienda pale, na walihidi kabisa kwamba yale maeneo wanayaachia wananchi. Lakini mpaka leo hawajayaachia wananchi wale, nakuomba Waziri, mimi Waziri Maghembe nakuamini sana. Kwa sababu na tume imeishaundwa noamba wananchi wa Ihomasa, wapewe lile eneo dogo waendeleo kuishi; kwa sababu wanashindwa kulima na tunasababisha njaa. Kuna kijiji kingine kiko pale Kilolo ambacho kinaunganika na Udumuka, na wenyewe wana tatizo linalolingana na Kijiji cha Kitasengwa. Ni maneo ambayo wananchi wanapata chakula pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na wenyewe waweze kuachiwa maeneo hayo. Kuna hifadhi nyingine iko kwenye Kijiji cha Iyegeya, Iyegeya ni kijiji kiko Luhunga pale. Kile kijiji kuna hifadhi kubwa sana imebaki tu, hakuna wanyama wala nini, wanaita hifadhi, sasa mimi huwa nashindwa kuelewa hifadhi inahifadhi nini kwa sababu pale hakuna msitu. Ni eneo pori tu wanasema hifadhi, wananchi hawana sehemu ya kulima wala kufanya nini, naomba wawaachie wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mawaziri wote waliopita walishafika kule na wakaahidi kwamba wataachiwa, naomba na wewe basi umalizie ufanye mkutano na wale watu. Kwanza mikutano tulishafanya sana, ni kutoa amri tu, siku moja waendeleo unakaa ofisini unaagiza Wizara yako, basi wananchi wanaweza kuachiwa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ningependa sana kuchangia ni kuhusu Jimbo la Mufindi Kusini ambapo wananchi walio wengi walihama kuachia maeneo Wizara ya Misisitu. Na walifanya vizuri siwezi kusema walifananyia vibaya, kwa sababu ule msitu sasa hivi ni Pato kubwa sana la Taifa. Na hatuwezi kusema Serikali inafanya biashara hapana, Serikali inatoa misaada, inatoa service kwa wananchi, na wananchi wale lazima wanufaike na misitu. Sasa cha ajabu inakuwa kinyume chake kwa nini? Tunashindwa kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mdogo tu, kijiji cha Nyololo ni kijiji kikubwa sana, kijiji cha Igowole ni kijiji kikubwa sana, ukienda Igowole mpaka kule Sawala, mpaka kule Kibawa, mpaka Mninga vijiji vyote hivi vilikuwa ndani msitu. Na waliachia Wizara kwamba wapande misitu, ili Taifa letu liweze kupata faida. Lakini cha ajabu sasa hivi vile vijiji vinavyozunguka ndani ya msitu havipati faida, kuna vitu vingine ni vidogo vidogo tu mimi nashangaa sana Wizara haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunategemea kwa mfano Mji ule Nyololo pale ukiangalia ng'ambo ya huku juu ni msitu mkubwa karibu kilometa 40, tumeachia Wizara, kijiji cha Nyololo hakina hata maji. Maji ambayo hata shilingi milioni 20 haiwezi ku-cost, kwa nini Wizara inashindwa kusaidia huduma za kijamii? Tunasema wawekezaji wasaidie huduma za kijamii kwenye vijiji vinavyohusika, lakini kijiji cha Nyololo hakina maji hakina barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata barabara tu Wizara ya Misisitu mna magreda pale, magreda tukienda pale mpaka uandike barua uomboteze ufanye nini, na wale watu ndio wanaolinda msitu. Watu watapataje moyo wa kulinda msitu wakati hawana hata barabara, hata maji tu mnashindwa. Mimi Mheshimiwa Waziri Maghembe namuamini sana, naomba vijiji vinavyozunguka misitu lazima vipate huduma za kijamii. Na tunaposema huduma za kijamii ni zipi, nataka nikuambie Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya huduma ya maji,

ukisaidia kujenga zahanati, ukasaidia kujenga kituo cha afya, wewe utakuwa umesaidia huduma za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wizara utasikia tunatoa mafunzo jinsi ya utunzaji wa misitu na kulinda moto. Hivi wewe unalinda moto wakati una afya mbaya na kituo cha afya hakijajengwa na kiko ndani ya msitu? Mheshimiwa Waziri mimi nakuomba sana, kwa mfano ukienda pale Mninga tuna kituo cha afya pale, kituo kile kimejengwa miaka mitano, mpaka sasa hivi hakijaisha. Unaenda pale utasikia Wizara ya Misitu eti wametoa labda mbao 100, mbao 200, kwa nini usitoe msitu tu useme umemaliza kituo cha afya tumemaliza kila kitu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mbunge nilienda pale nikatoa bati 200, mifuko ya simenti 100, Wizara inatoa mbao 20 au 10 hiyo haiwezi kukubalika kabisa hiyo. Mheshimiwa Waziri nataka nikuambie kitu kimoja, mwaka huu lazima tuone Wizara ya Misitu inatoa vitu vya kijamii vinaonekana. Kwa mfano, hapa nilikuwa nasoma hapa, mmesema mnategemea kukusanya shilingi bilioni sita, mwaka wa jana walikusanya shilingi bilioni nne, shilingi bilioni nne sisi wana Mufindi hatujafaidi. Sisi suala la madawati lilitakiwa liwe historia tu, hapa tunaanza kuongelea madawati sisi watu wa Mufindi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa juzi alisema anaitua Wabunge tuanze kuchangisha madawati, hatuchangii. Misitu ipo pale tuanze kuchangia kwa nini, lazima misitu ile ifanye kazi pale, hatuwezi kuwa tunasimamia kulinda misitu; halafu mnatubanabana sisi Wabunge na fedha ndogo ndogo hizi, wakati kuna shilingi bilioni sita iko hapa hiyo haiwezi kukubalika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka madawati pale yakamilike. Mwaka jana mimi niliomba nikasema katika shilingi bilioni nne, mtupatie hata shilingi bilioni moja tu Wilaya ya Mufindi tutakuwa tumemaliza madawati, matokeo yake wanaenda kutoa madawati 100. Hatuwezi kudanganywa kama watoto wadogo, tutalindaje misitu? Haya umesema hapa kuna masuala ya mradi wa nyuki. Nilisikia siku moja kuna kikundi fulani kimechonga mizinga, badala ya kuwagawia wananchi wanaoishi kwenye misitu kule, wakaanza kufanya biashara wakasema kila mzinga shilingi 60,000 sasa tena ni biashara imetoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajua mnawahamasisha ili wafuge nyuki, sasa utapeli tapeli huu unatoka wapi huu, hii inakuwa ni tatizo hatuwezi kuwa tuna matatizo tunayaona hivi na mwaka huu sisi tuko *smart*. Nadhani Wabunge wanaotoka Wilaya ya Mufindi watakuwa wakali sana kwa hili, hatuwezi tukawa tunahaibika na vitu vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunakuja kwenye ugawaji wa vibali. Ugawaji wa vibali unaenda kitapeli tapeli, mtu anafanya kama biashara ya kwake. Ie ni mali ya Serikali, ya wananchi wote, utakuta mtu mmoja anagawagawa vibali anagawa kwa wananchi anafanya biashara, kwa nini asishikwe apelekwe polisi ahukumiwe, mnamuangalia tu. Matokeo yake sisi Wabunge tunapata makashfa makubwa, sisi hatulali kule, mtu mwingine anakaa Dar es Salaam kule, amekusanya vibali analala usingizi, sisi kule tunalala tunalinda moto kule, mwenyewe anakuja kutapeli kule, hii haiwezi kukubalika hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri bajeti yake itapita, na kwa sababu ya mara ya kwanza tunamsamehe kwa leo, lakini ninayoyaongea haya, *next time* nikiona yametokea sitakubaliana kabisa. Watu wanaleta ujanja ujanja wa vibali, tumesema vibali mpeleke kwenye vijiji, vijiji vile ukisaidia Kijiji kimoja kibali kimoja tu wakajenga zahanati, kijiji kimoja utakuwa umesaidia watu zaidi ya 70, au zaidi hata 1000. Kijiji cha Mninga kiko ndani ya msitu hata zahanati miaka mitano hatujamaliza, kwa nini usiwape kibali pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani vitu vingine ni vitu rahisi rahisi tu, Serikali tutaanza kuilaumu kwa vitu vidogo sana. Hatuwezi kulaumu kwa vitu vidogo vya utekelezaji. Kwa kweli hii inaleta uchungu sana, kuna vitu vingine ni vitu vidogo vidogo lakini kwa ajili ya watu wachache wanatuletea gharama kubwa ya kuweza kuhutubia kila siku. Mwaka jana nakumbuka Waziri Mkuu alitutuma mimi na Waziri Nyalandu tukaenda Mufindi kule, Waziri Nyalandu alienda pale akafanya mkutano mzuri kwa wananchi, wananchi wakampigia makofi, kwenye utendaji ikawa zero kwa nini? Haiwezekani kabisa hii ndugu yangu, haiwezekani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Bunda, kwa kunipa nafasi ya kuja hapa Bungeni na mimi nijumuike na wenzangu katika kuwatetea Watanzania wenye matatizo mengi. Nianze kwa migogoro ya moja kwa moja, migogoro ya wafugaji na hifadhi za wanyama pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi hapa, lakini kwenye Jimbo langu la Bunda kuna eneo maarufu linaitwa Kawanga, na mimi niombe kwa kusema wazi tu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, ng'ombe ana laana, toka mmetunga Sharia hii ya wanyama pori ya kukamata ng'ombe mnamfanya kama nyara, mnamkamata porini hachungi na mnampiga risasi, Mawaziri zaidi ya tisa wamesha toka humu ndani;

ng'ombe ana laana. Kwa hiyo, yeyote anayeshughulika na ng'ombe vibaya ajue mambo yake yatakwenda vibaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu eneo la Kawanga. Eneo hili mwaka 1974 alikuja Mwalimu Nyerere pale kama kijiji cha ujamaa, akawashauri wananchi wa maeneo yale kwamba jamani acheni maeneo ya malisho. Wakavuka Mto Lubana wakaacha eneo la Kawanga, wakawa wamechimba malambo mawili makubwa ya Chifu Makongoro, wananywisha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994 ukaja ujanja ujanja eneo hili likachukuliwa kama *game reserve*, *Ikolongo Game Reserve* na *Grumeti Game Reserve*, pori la akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza huwa najiuliza hivi pori la akiba maana yake ni nini? Mwalimu alisema hivi vitu vya akiba viwepo pale ambapo wananchi wana shida wapewe nafasi.

Sasa inavyoonekana mapori ya akiba yote ni ya wanyama pori, ikija kwa binadamu nongwa. Leo ikitokea *operation* ya kuzuia tembo asiende kwenye mashamba ya watu na *operation* ya kwenda kuzuia ng'ombe wasiende porini, *operation* ya ng'ombe inachukua nafasi. Kwa sababu ng'ombe wanakuwa na faida ukiwatoa kwenye *operation* unawakamata unawatoza, wanatoa hongo na mnawauza sijui hela za ng'ombe zinazouzwa zinaenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Kawanga wakahama watu, mkalifanya Pori la Grumeti, malambo mawili yako upande ule, mpaka wetu ni mto, na mto ule maana yake ng'ombe akivuka tu, amekamatwa ndivyo mpaka ulivyo. Lakini kutoka kwenye mpaka wa Mto Rubana kwenda kwenye watu, unatembea nusu kilometa kwenda pale mbele, ndiyo *buffer zone* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi najiuliza kama wananchi wa maeneo yale tembo wanakula mazao yao, ngo'mbe hawavuki kwenye Mto Rubana, malambo yao mmechukua na hamkufidia halafu mnasemaje tuna mahusiano mabaya na ninyi? Profesa Maghembe mimi naomba nikuambie hivi, pengine kule Mwangi ninyi Ubunge wenu wakati fulani akisema fulani mnapata. Sisi Ubunge wetu ni wa kazi, kuna maeneo mengine Ubunge akisema mkubwa fulani watu wanapewa, lakini sisi Ubunge wetu mpaka utoe jasho ndipo upate. Sasa naomba uje Kawanga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina ugonvi na wewe, na mimi nikuambie wazi wala huna ugonvi na Wabunge, tatizo lako ni kwamba una-*attack* ng'ombe, kwa nini una- *attack* ng'ombe sisi tunaolea ng'ombe. Mimi mke wangu ametoka ng'ombe namuita Nyabulembo, sasa wewe una-*attack* ng'ombe mara kwa mara kwa nini? Tunataka ng'ombe kweli watoke porini

sawa, lakini watoke kwa mpango maalum. Hivi kwa nini majangili wamewashinda porini mnang'ang'ana na ng'ombe? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa kwenye ripoti ya wapinzani hapa, anasema kwamba ujangili ni mfupa uliowashinda CCM. Na kila siku asubuhi, hata leo asubuhi nimesikia, kwamba kiongozi mmoja mhifadhi wa wanyama pori sijui amekamatwa na pembe za ndovu. Sasa kwa nini msishughulike na hawa mnashughulika na ng'ombe? Profesa achana na mambo ya ng'ombe watakulaani hapa. Naomba uje Kawanga uangalie mpaka ulivyo ni mbovu. Lakini ndugu zangu Wabunge tunaotoka kwenye maeneo ya wafugaji, naomba niwaambie wazi, hizi kanuni na sheria za wanyama pori zitaua watu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zitaua humu ndani, sheria hii imeandika ng'ombe ni kama nyara, akikamatwa anapelekwa mahakamani, akionekana ameingia porini auzwe. Ng'ombe wa Usukumani, ng'ombe wa Jimbo la Bunda, ng'ombe wa Tarime na maeneo mengine ana tofauti gani na ng'ombe wa Ngorongoro? Ng'ombe wa Ngorongoro anachunga na wanyama, kwani ile sheria ya Ngorongoro imekuwa ni sheria ya Mungu haibadiliki? Sheria ya Ngorongoro ambayo ng'ombe wanachunga na wanyama haibadiliki imekuwa ni sheria ya Mungu? *It's too rigid* haiwezi kubadilika. Tuone maeneo mengine ambayo yanahitaji uhitaji wa Ngorongoro wapelekewe hiyo sheria. Profesa nakuomba uje Bunda, uangalie eneo la Kawanga tuone ni namna gani tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo. Nakupongeza kwa maana ya kwamba msimu mdogo uliopita umenisaidia sana, tembo kidogo, watu wamevuna. Lakini ndugu zangu Wabunge na ndugu zangu Watanzania, mnyama tembo, mama mmoja tulienda kwenye mkutano akatuuliza hivi, hivi hao tembo hawana uzazi wa mpango? (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana kama wamezidi tuwafanyie uzazi wa mpango, tembo siku hizi wanakwenda kwenye maghala, wanaangusha maghala wanakula mazao. Maeneo ya Bunda, Unyari, Kiumbu, Mariwanda na kwa Mheshimiwa Ester Bulaya pale Bukore na Mihale wanakula mazao asubuhi na mchana na Profesa upo. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipiga kelele hapa mnasema tumekuwa wabaya, watu hawa wanaozunguka wanyama pori hawa, mazao yao yanaliwa fidia haipo. Tunadai fidia zaidi ya milioni 400 hamjalipa kutoka mwaka 2012 mpaka leo, na wanakula mazao kila siku na magari mnayo, watu mnao, mkiambiwa mnasema kwamba Halmashauri ndiyo ilinde wale wanyama. Halmashauri ina askari pori mmoja na gari bovu halipo na Halmashauri hazina



own source. Halmashauri hazina hela unawaambia walinde tembo watalinda saa ngapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mbaya zaidi Halmashauri alinde tembo, asipolinda tembo anakula mazao, wakila mazao mnalipa nyie hivi kwa nini mpo hasara sasa? Kwa hiyo nilikuwa nafikiri kwamba ni vizuri ukaangalia. Lakini mambo mengine niseme mapambano ya kuzuia ujangili yaendeleo kuwepo, kuimalisha misitu yetu muendeleo kuimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze kidogo juu ya TFS. Hao TFS ulionao nikushukuru kwanza umewashughulikia, ni jipu. Haiwezekani kwenye makusanyo yao, kila mwaka asilimia 100, asilimia 200, asilimia 150 uliona wapi? Yaani kila makusanyo ya TFS asilimia 100, asilimia 250, asilimia 300 uliona wapi? Angalieni makusanyo yao asilimia walizokusanya kila mwaka, asilimia 120, asilimia 110, asilimia 116 kila mwaka, wao makadirio yao yanakuwaje mpaka wapate hizo asilimia? Kwa hiyo, mliangalie hili nalo hao watu inawezekana wakawa jipu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ya shilingi milioni 400 watu wa Bunda unawalipa lini? Hii fidia sijaona kwenye bajeti yako. Profesa ukija hapa uniambie kwamba hii kitu unalipa lini. Lakini naomba kuanzia leo na kwenda muda unaokwisha, kwa muda wa mwezi mmoja na nusu naomba mtusaidie kupata magari ili watu wale wapate mavuno yao. Wamebakiza mwezi mmoja tu, tembo leo wanaenda usiku na mchana na kama hamuwezi, Profesa ngoja nikuambie, Marekani ni wanjanja sana lakini wanaishi na Mexico. Waliona haiwezekani kuishi na Mexico maskini na wao wakiwa matajiri, ikabidi wawafadhili wao wapate hela. Hamuwezi mkafanya wananchi wanaozunguka maeneo ya pori, mkasema eti mtakuwa marafiki wakati ninyi mnawanyonya haiwekani, lazima muwafadhili ili waweze kuishi na wanyama vizuri. Na ninyi niwaambie huku Serikalini... (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Riziki, ajiandae Mheshimiwa Risala.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Mimi ni-declare interest kwamba ni mdau wa maliasili. Kwanza nimezaliwa Selous, lakini ya pili ni Mwenyekiti wa Kupambana na Ujangili, say no to poaching. Bahati nzuri Kamati yangu tulizunguka Tanzania nzima, tukaona mazingira ambayo tumeyaona lakini nataka na mimi nitoe kama ushauri kama utaweza kusikilizwa, lakini tuangalie suala la uhifadhi na environment ya Tanzania.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata bahati kuhudhuria mikutano mbalimbali ya *climate change*. Tanzania sasa hivi tunakwenda kwenye *gold*, tumetoka katika *green* tunakwenda kwenye *gold*, maana yake Tanzania inakwenda kwenye jangwa. Sasa tujiulize tunaangalia maslahi ya nchi au tunaangalia maslahi binafsi ya kwamba mimi niwe Mbunge, ili fujo ya nchi kuingia katika *disaster* ya kuwa katika *gold* na hali ya nchi kuwa katika ukame. Wabunge sisi tujiulize na tujipe nafasi ninachokizungumza nchi yangu inakwenda wapi? Tunakwenda katika jangwa! Tulikuwa na Profesa mmoja akatuambia mnaiona Tanzania? Tanzania inakwenda katika jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nchi za Uarabuni wanapanda miti na kuhakikisha wanautoa udongo India, kuhakikisha Arabuni kama Dubai inakuwa katika *green* na mvua wanapata sasa hivi. Lakini Tanzania mito mingi mikubwa sasa hivi inakauka na inapotea kabisa. Nataka nimshukuru na niwapongeze watu wa Ngorongoro, niwapongeze watu wa TANAPA na Wamasai waliopo ndani ya Ngorongoro, wale ni wahifadhi wazuri na wanasimamia ndiyo maana mpaka leo *Ngorongoro Conservation* inaonekana kama *Ngorongoro Conservation*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana TANAPA na uhifadhi wake, na kutoa tozo kubwa kwa ajili ya Serikali mwaka huu wametoa shilingi bilioni 10. Niko katika kamati ya uwekezaji, mashirika ambayo yameweza kujitegemea ni Ngorongoro, TANAPA, *National Housing* na TRA basi, mashirika mengine yote yako katika hali ya kufa. Sasa tujiulize tunataka uhifadhi au tunataka tuhakikishe uhifadhi hamna, mvua hamna tutaishije Tanzania hii? Hata mito haitakuwepo. Leo wewe ni mfugaji unaingia ndani ya Pori la Serengeti kuna simba, kuna tembo mgongoni una bunduki, nipe tafsiri yake ni nini hapo? Sielewi kabisa hiyo picha inayoniambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pili tuhakikishe haya mapori ni michoro ambayo ilikuwepo tangu enzi ya mkoloni, walijua tuwaweke maeneo ya uhifadhi hawa Waafrika watamaliza misitu yote watahakikisha hifadhi hakuna hata mvua itakuwa haipatikani. Na ndiyo maana kuna *demarcation* kuna, kuna ma-beacon ambayo yameweka mle ndani kuhakikisha hizi alama zinaendelea kudumu lakini kwa uhifadhi waliamua kuhakikisha wamewagawia, mwisho tunajiuliza je, tugawe hifadhi zote watu wachukue wamalize wafugaji halafu hii nchi ikae katika ukame? (Makofi)

Nataka nitoe tafsiri ya hili, wafugaji walipelekwa Mkoa wa Lindi walitoka Ihefu, Ihefu ilikauka kabisa TANESCO hata mvua ilikuwa hamna, maji hamna nchi ikaingia katika giza. Lile giza limepelekwa Lindi, shamba la bibi Lindi nenda leo Selous hakuna simba, nenda leo Selous hakuna ndovu wamehakikisha wafugaji wameingia mpaka ndani ya Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujiulize tunaangalia maslahi ya nchi au tunaangalia mimi nichaguliwe kuwa Mbunge halafu baadaye niendeleo kuwa Mbunge nchi iingie katika *disaster* haikubaliki. Ninakuomba Waziri mwenye dhamana toa semina Wabunge wajitambua kama uhifadhi ni kitu kizuri ndani ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwaka 2008 nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Maliasili Mwenyekiti wangu alikuwa Job Ndugai. Ni wewe ndiwe uliyeanzisha CNN, ndipo Tanzania ikaanza kukua katika utalii. Ni wewe ndiye ulileta *fixed rate* watu wakaambiwa ni lazima watu wenye mahoteli walipe baada ya kuona wewe unataka kuupaisha uchumi na wao kazi yao ni kuuhujumu uchumi walikuondoa kwa kuhakikisha uchumi ulio ndani ya maliasili unaporomoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuombea kwa Mwenyezi Mungu akulinde, akupe afya njema uiongoze nchi kama anavyoiongoza Waziri wa Ardhi na wewe nataka nikupe fimbo hiyo ufanye kazi hiyo, kazi kwa kwenda mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimezaliwa Selous, nimezaliwa Selous mimi ni Mngindo kwa asili ninatoka ndani ya Liwale. Selous ndiyo mbuga kubwa ya kwanza katika Afrika na ninaweza kusema ni duniani haijatangazwa, kuna *corridor* kubwa ya tembo ambao wanatoka Mozambique wanakuja Tanzania wakiingia Tanzania wanaingia Namtumbo, wanaingia Masasi, wanaingia Nachingwea, wanaingia Liwale, wanaingia Kilwa wanakwenda mpaka Mahenge wanavuka wanakwenda mpaka Tarangire. (Makofi)

Sasa ushoroba huu wanafaidika nini na watu wa Kusini? Ninaomba madawati yaliyopangwa ya TANAPA yawapeleke watu wa Lindi, Mtwara na Ruvuma wafaidike nayo. Huyu sungura asigawiwe kwa upande mmoja, hii siyo haki. Tulidai haki ya gesi mkasema gesi ni ya Watanzania kwa nini madawati mnagawa kwa mafungu? Nataka nihakikishiwe, Mheshimiwa Waziri pamoja na kukupenda sana kama haujapeleka *allocation* Lindi sitakubaliana, kama hujapeleka *allocation* Ruvuma sijakubaliana na wewe na kama hujapeleka *allocation* Mtwara kwa kweli sikubaliani nawe na ninaomba sheria hii irudishwe hapa tuifute ili angalau Tanzania nzima wafaidike. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi unaongoza kuwa na rasilimali kubwa, tumepiga kelele ya mjusi ambaye yuko Ujerumani kila mwaka wanapata dola bilioni tatu Tanzania hata senti tano hatuipati. Hapa wanatufanyia dhihaka mjusi, mjusi, lakini ni haki ya mjusi. Maeneo yale tupate shule, tupate barabara lakini mpaka leo watu wa Ujerumani wanafaidika na yule mjusi, sisi tunapata nini? Nataka Mheshimiwa Waziri wa dhamana aniambie tozo linalopatikana kutokana na yule mjusi linakwenda Mipingo Tendeguru, sisi

tusibakie kama boga linasuka mikeka wenye tunalala chini, hatukubali kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa iko katika urithi wa dunia na katika urithi wa dunia Kilwa ni namba 21 duniani hata hizo Ngorongoro, TANAPA ziko nyuma lakini kwa vile iko Kusini mpaka leo imeachwa katika urithi wa dunia. Hautuzwi, hakuna mapato, hakuna kinachoangaliwa kule Kilwa zaidi ya tumepaacha hakuna ndege zinazokwenda kule, watu wanakwenda kinyemela nyemela hakuna mapato yanayopatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la utalii. Mtalii akija Tanzania anakuja na package, anaingia TANAPA, anaingia Ngorongoro, anakwenda Zanzibar. Masikitiko yangu makubwa Zanzibar hakieleweki hela zinakwenda wapi? Imefikia mahali kuwa tozo zinazopatikana Zanzibar ni hela za watu wajanja, inafikia kujiuliza Zanzibar kuna nini? Utalii wa Sychelles umewafanya mkawa matajiri, Zanzibar watu wanaendela kuwa maskini kwa vile hawasimamii rasilimali yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Zanzibar wameshindwa kusimamia utalii tupo tayari kusimamia utalii wa Zanzibar na utaruka. Kama huku TANAPA wanaweza kukusanya shilingi bilioni 100, Ngorongoro shilingi bilioni mia moja na Zanzibar iko wapi hela ya utalii aibu kubwa sana. Ifike mahali ujiulize kuna fanyika nini mpaka Zanzibar ikaonekana hata utalii wa maana, pesa inayongia kama concession fee Zanzibar hakuna? Kule kuna ujanja na ulaji ambao hauna mwenyewe na kazi yao kutoa vitenge, wakiwapa vitenge wamemalizika tuuangelie utalii wa Zanzibar kwa jicho la huruma watu hawa waweze kusaidiwa. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Au apewe Maalim Self.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Na wampe Maalim Self afanye kazi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Risala, ajiandae Mheshimiwa Mbatia, halafu Mheshimiwa Mohamed Mchengera.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ambayo inachangia Pato kubwa la Taifa. Kwanza kabisa nipende kuipongeza hotuba nzuri ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu mimi nitajikita kwenye suala zima la utalii. Tunapozungumzia utalii nitazungumzia mambo matatu muhimu ili tuwe na utalii endelevu. Ili tuwe na utalii endelevu tunahitaji vivutio vya utalii, ili tuwe na utalii endelevu tunahitaji namna ya kufikia vivutio hivyo,

tunahitaji malazi ya kuwalaza wageni wetu wanapofika kwenye vivutio vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala la vivutio vya utalii. Nchi yetu ya Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na vivutio vyenye ubora wa hali ya juu ukilinganisha baada ya nchi ya Brazil. Lakini cha kusikitisha sana pamoja na kwamba Wizara hii inachangia asilimia kubwa kwenye Pato la Taifa, kwa mfano nikiangalia asilimia 17.5 inachangia Pato la Taifa kupitia Utalii, lakini asilimia 4.8 inatoka kwenye misitu, asilimia 25 ya Pato la Taifa kupitia fedha za kigeni zinatoka kwenye suala zima la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nashangaa sana tunaona kitakwimu mapato haya ni makubwa lakini ukilinganisha na vivutio tulivyonavyo bado tunahitaji kuwekeza nguvu kubwa sana kwenye suala la kuboresha utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vivutio tulivyonavyo bado tunapata mapato kidogo sana, lakini tunapata watalii wachache sana ambao wanatembelea vivutio vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imejaa mambo mengi imejaa mipango mingi; lakini niseme ukweli tusiporekebisha changamoto za miundombinu, hasa miundombinu ya barabara bado suala la utalii tutakuwa tunaimba kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu na barabara ni changamoto kubwa hasa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mikoa ya Magharibi na Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Ukitaka kuwekeza katika Mikoa ya Kusini, Mikoa ya Magharibi na Mikoa ya Kanda ya Ziwa utakumbana na suala zima la changamoto ya barabara. Gharama zinakuwa ni kubwa sana kwa wageni wetu wanaotembelea hifadhi zetu na maeneo yetu ya utalii hii ni kwa sababu ya changamoto za barabara. Wawekezaji wengi wanashindwa kuwekeza katika sekta ya utalii ni kwa sababu ya changamoto ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia changamoto nyingine kubwa ni ya viwanja vya ndege. Tuna viwanja vya ndege vya kimataifa vya Kilimanjaro, Dar es Salaam, lakini sasa tuna uwanja wa ndege wa Songwe. Uwanja wa ndege wa Songwe ambao tunategemea ndio utakuza utalii wa Kusini hauwezi kufanya kazi peke yake usiposhirikiana na viwanja vidogo kwa mfano kiwanja a Iringa, kiwanja cha Katavi ambacho a ndege zinazokwenda kwenye hifadhi ile ya Katavi zinaweza kutua kule; hatuwezi kukuza utalii wa mikoa hii kama hatuwezi kuimarisha hivi viwanja vya ndege. Nikisema hapa leo gharama ya kutoka Dar es Salaam mpaka kwenye hifadhi ya Ruaha na kurudi ni karibu dola 700, (shilingi 1,400,000). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni mtalii gani au mwekezaji gani anaweza kuwekeza kwenye utalii kwa gharama zote hizi? Ni mtalii gani wa ndani ambaye anaweza akatoka mfano Mkoa wa Iringa kwenda Hifadhi ya Ruaha kwa kulipa 800,000 kwa usafiri wa gari? Tutakuwa tunaimba utalii wa ndani, tutakuwa tunaimba uwekezaji lakini hatutoweza kuwekeza kama miundombinu hii haitafanyiwa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la malazi. Suala la malazi ni changamoto kubwa, niwapongeze wawekezaji wa Mkoa wa Arusha ambao wao wameweza kuwekeza zaidi pia kwenye masuala ya hoteli. Hoteli nyingi zilizopo katika Mkoa wa Arusha zina hadhi za hoteli ya kitalii. Lakini hoteli hizi zinazidiwa wakati wa *high season* watalii wanalazimika kwenda kulala nchi jirani, wanalala Nairobi ni kwa sababu hoteli hizi hazitoshi, lakini pia hoteli zetu zilizojengwa kwenye mikoa yetu ya Nyanda za Juu Kusini mfano Mikoa ya Iringa, Mbeya, Mikoa ya Magharibi, Mikoa ya Kanda ya Ziwa bado ni changamoto kubwa kwa wageni wanaotembelea maeneo hayo. Kwanza huduma zinazotolewa kwenye hoteli zile ni huduma duni ambazo haziendani na hadhi ya huduma ambazo wageni wetu wanatarajia. (Makofi)

Vilevile ningependa kutoa ushauri kwa Serikali, watoe masharti nafuu kwa wawekezaji hawa mnaotaka kuwekeza katika sekta ya utalii, kuwekeza kwenye *tour operators*. Kwa mfano mwekezaji anataka kuwekeza Kusini unatofautishaje mwekezaji wa Kusini na mwekezaji wa Kaskazini, kwanza mwekezaji wa Kusini ana changamoto ambazo nimezitaja, vivutio vile viko mbalimbali, barabara ni mbovu, lakini pia mwekezaji huyu hajavutiwa. Wizara haijampa mwekezaji huyu ya yeye kuwekeza katika mikoa hii ya Kusini. Kwa mfano ukiwekeza katika suala zima la utalii, la *tour operator* unatakiwa kulipa dola 2,000 na sijui kwa nini ni dola kwa Mtanzania mimi nilitegemea labda watalipa *Tanzania shillings* lakini analipa dola, dola 2000 kuwekeza *tour operator*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu *tour operator* anahitaji kulipa TRA, anahitaji kulipa SUMATRA malipo yamekuwa ni mengi. Lakini huyu *tour operator* nitamtofautishaje na *tour operator* anayekuja kuwekeza Kusini? Wanaokuja kuwekeza Kusini, Mikoa ya Magharibi na Mikoa ya Kanda ya Ziwa wapunguziwe angalau ifike hata dola 1000 ili waweze kuvutiwa kuja kuwekeza katika mikoa ile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiboresha maeneo haya ya uwekezaji, mahoteli yetu, *tour operator*, tunaweza pia tukatoa ajira nyingi sana kwa wazawa ambao wengi wamemaliza vyuo. Kwa mfano Chuo cha Taifa cha Utalii kimetoa wanafunzi wengi wa *certificate* pamoja na *diploma* tangu mwaka 2006, lakini wanafunzi hawa hawajaajiriwa, hawana ajira hata kwenye Wizara.

Kwa hiyo, ningependa pia Waziri anapokuja kuhitimisha hapa atuambie pia ni ajira ngapi zimetoka kwa wanafunzi hawa waliomaliza katika chuo hiki kama ilivyo Mweka na Pasiansi?. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kuongelea suala pia la Maafisa Utalii katika mikoa yetu. Ninaomba Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na TAMISEMI iangalie namna ambavyo itaweza kuajiri Maafisa Utalii kwenye mikoa yetu, wilaya zetu, lakini pia kwenye halmashauri. Hii itasaidia sana kuibua vivutio mbalimbali vilivyoko kwenye mikoa yetu kwa kushirikiana na wataalam. Vilevile itasaidia kuondoa umaskini kwa wananchi wanaozunguka katika maeneo yanayozunguka hifadhi zetu au maeneo yetu ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanaoishi kwenye maeneo hayo wamekuwa ni maskini kwa sababu hawana namna ya kutumia vile vituo vyao bila miongozo ya hawa maafisa utalii. Ukiangalia suala zima la utalii wa kitamaduni, utalii huu sasa hivi umepotea hauthaminiwi, lakini ukiangalia nchi nyingi zimekuwa zikitumia utalii wa kitamaduni kuweza kunufaisha wananchi wanaozunguka karibu na maeneo ya hifadhi, wamekuwa wakitumia tamaduni zao, wamekuwa wakitumia taaluma zao kwa mfano wengine wamekuwa ni wachoraji na wameweza kufaidika sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siungi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbatia, ajiandae Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango kwenye hoja hii iliyoko mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri inaonesha kwamba Wizara yake au sekta ya utalii inaingiza asilimia 25 ya fedha zote za kigeni katika Taifa hili, kwa hivyo ni sekta nyeji. GDP - Pato la Taifa katika utalii, na hii ni zaidi ya miaka mitatu iliyopita tunataka atupe takwimu za sasa, ni asilimia 17.5, ya leo ikoje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tanzania ni ya pili kwa vivutio vya utalii duniani baada ya Brazil. Tumekaa na sekta ya utalii wakati Mheshimiwa Chenge akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tukafanya michanganuo mingi na tukatoa ushauri kwa Serikali namna bora ya kuweza kuweka mazingira mazuri na rafiki na yenye kuvutia ili tuweze tukaingia kwenye ushindani hasa wa soko la utalii duniani. Ukizungumzia Serengeti, ina kilometa za mraba zaidi ya



14,000 tukishindana na Masai Mara ambayo ina kilometa za mraba 1,400, ukizungumzia Mlima Kilimanjaro, ukizungumzia Ukanda wa Bahari ya Hindi kilometa 1,424, unataja vingi tu lakini Tanzania inashika nafasi ya 110 kati ya nchi 133 kwenye mazingira rafiki na mapato katika sekta ya utalii, huu ni uendawazimu, yaani kwenye mtu mwenye akili nzuri unaona kabisa hatuko serious. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka na wewe Mwenyekiti tulikuwa pamoja kwenye Kamati ya *Chenge One* kuhusu sekta ya utalii wakati tunatafuta vyanzo vipya vya mapato. Leo hii kulikoni sekta hii, nimesoma hotuba ya Waziri, TANAPA mchango wake kwenye maendeleo ya jamii ni *one billion*, wakati ukiangalia kwa mfano Mlima Kilimanjaro peke yake mapato yake ni zaidi ya bilioni 60 kwa mwaka ambayo ni asilimia 34 ya mapato yote ya sekta ya utalii. Lakini ukiangalia mazingira yanayozunguka Mlima Kilimanjaro, likiwepo Jimbo la Vunjo, hali ya vijiji ambavyo viko karibu na mlima huo hali yake ni hoi bin taabani. (Makofi)

Leo hii Mbunge unaambiwa uchangie kujenga shule, changia madawati, changia huduma sijui za nini hii haiwezekani wakati vivutio tunavyo, fedha zipo. Hii ni Serikali naamini ni endelevu ya chama hicho hicho. Serikali iliyopita Waziri mwenye dhamana alikubali kwenye Bunge hili kwamba angalau asilimia 25 ya mapato yanayotokana na hifadhi hizi yaweze kuhudumia maeneo ambayo yako karibu na hifadhi hizi, ambapo ukiwa karibu na waridi unanukia waridi. Sasa leo hii ukiangalia maeneo haya yako hoi bin taabani lakini mapato haya je, leo hii Wizara yake inaendeleza ile sera ambayo ndiyo nilikuwa nataka iwe endelevu katika kuhakikisha tunapata mapato au laa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri inajichanganya, ukisoma ukurasa wa 87 unasema mwaka 2014 walipata bilioni nne kutokana na kodi ya vitanda kwa watalii ambayo ni dola moja na nusu kwa kila kitanda kwa usiku. Ukisoma ukurasa wa 127 mwaka 2014 watalii waliolala watalii hotelini ni 1054 na wastani wa kukaa hotelini siku kumi, ukizidisha unapata zaidi ya shilingi bilioni 31 na sio bilioni nne ambazo zimeandikwa hapa na ni takwimu zinazotoka hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu Wizara hii ili iweze ikawa ni endelevu lazima kuwe na mazingira rafiki kwa wawekezaji hasa wazawa kwenye sekta ya utalii. Ukiangalia kodi ambazo Serikali inatoza kwenye sekta ya utalii na hasa *tour operators* ni zaidi ya 40. Tumeimba, tumeimba, tumeimba! Ajira zinazotolewa vijana kwa mfano kule Marangu kule ambao wanaelekea Mlima Kilimanjaro hawa *ma-tour guiders* hali ya maisha waliyonayo ambayo ni hoi bin taabani hakuna sera ya kuweza kuwalinda vijana hao. Kama sekta ya utalii umesema *indirectly* inatoa ajira zaidi ya milioni moja, je wale ambao wanazalisha katika sekta hii hali yao inakuwa ya namna gani?



Mheshimiwa Mwenyekiti, ada hizi, tozo hizi, leseni hizi ambazo wewe unamkamua ng'ombe tu huna namna bora ya kuweza kumlisha huyo ng'ombe ili aweze kutoa maziwa zaidi; angalia utalii wa Kusini ulinganishe na utalii wa Kaskazini na kama huu utalii wa Kaskazini unazalisha zaidi unasaidiaje utalii wa Kusini ili kweli kama sisi ni wa pili kwa vivutio vya utalii tuweze tukafaidika na rasilimali hii badala ya danadana ambazo tunapiga kila siku hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia viwanja vya ndege kwa mfano cha Musoma kiko kwenye hali gani? Angalia kiwanja cha ndege cha Iringa kiko kwenye hali gani? Angalia viwanja vya ndege vya kusini kwa mfano Masasi pale ile *air strip* iko kwenye hali ya namna gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu Serikali iangalie upya tozo na ada na leseni katika sekta hii ili kujenga mazingira rafiki na endelevu, na hizi fedha zinazotokana na tozo zirudi sasa kwenye sekta yenyewe na hasa kujenga miundombinu ambayo itakuwa ni rafiki na tuweze tukazalisha zaidi. La sivyo huwezi ukakamua tu wakati hutengenezi hali ya ulinzi na usalama kwenye mbuga zetu na kwenye mazingira ya utalii; hali ya miundombinu ya vyoo na hali ya maji, hali ya barabara na hali yote ya mazingira ambayo ni rafiki katika sekta ya utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa wanyapori. Vitalu zaidi ya 50 vimerudishwa. Mwaka 2008/2009 Serikali ilikuwa inapata zaidi ya dola milioni 20 kwa mwaka kutokana na uwindaji. Leo hii mazingira yamekuwa tofauti kwenye soko la ushindani, mwaka jana Serikali imepata dola milioni nne tu kutoka dola milioni 20 miaka minane iliyopita. Sasa hapa tunaenda mbele tunarudi nyuma? Na hapa kwenye ukurasa wa 36 tunawapongeza TANAPA, ndio wanafanya kazi vizuri, Mlima Kilimanjaro uhifadhi umekuwa wa kwanza kivutio katika Bara la Afrika lakini je, mazingira yale yanatuweka kwenye mazingira gani ambayo leo tunaweza tukasema kweli Tanzania au wanaozunguka mazingira hayo ni rafiki na ni endelevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe kupitia kwako kwenda kwa Serikali kwamba waangalie tena, narudi tena, kodi hizi, tozo hizi na ukiangalia wawekezaji wazawa kwenye sekta ya wanyama pori ambao ndo tungewasaidia zaidi ya asilimia 90 wameondoka wamefilisika, jjulize kwa nini? Kwanini hamkai nao? Kwanini hamzungumzi? Kwa nini hatujengi mazingira rafiki? Huwezi ukakaa mahali ukajifungia, watu wachache wanafanya maamuzi kwa wale wawekezaji ambao ndio wangesaidia taifa letu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Tanzania yetu hii tuna haki nayo sote kwa pamoja. Mawazo mazuri ni mawazo mazuri tu hata kama yangekuwa yametoka kwa shetani. Ukisoma taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuna mawazo lukuki ambayo yataisaidia sana Serikali. Ukisoma taarifa ya kamati

hasa ukurasa wa 12 na 13 ni mawazo mazuri kweli kweli lakini mbona tunarudia kauli zile zile miaka nenda rudi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nishauri kwamba yafaa Mheshimiwa Waziri afanye semina na Wabunge wote, Wabunge wampe mbinu mpya, mawazo mazuri, fikra mpya za kisasa za kuhakikisha Wizara hii miaka mitano ijayo tunatoka hapa tulipo kwenye asilimia 17 ya DGP twende hata asilimia 30 mpaka asilimia 50 tuendane na kigezo cha sisi kuwa wa pili kwa vivutio vya utalii duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mwenyezi Mungu akubariki. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, ajiandae Mheshimiwa Alex Gashanza, Mheshimiwa Paulo Issaay na Mheshimiwa Esther Mahawe.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema alienijalia afya njema kusimama ndani ya hili Bunge lako hili Tukufu. Lakini pia nimtakie pole bibi yangu Nyankulu kutoka kule Mtanange, leo hii anapambana na vita ya kansa, namuombea apone haraka ili aendelee kuniombea.

Tatu niseme tu kwamba niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa namna ya kipekee kabisa kuniomba leo hii nibaki ndani ya Bunge kwa sababu siku ya leo ni siku ambayo Mwenge umefika katika Jimbo langu la Rufiji. Kwa kutambua kwamba Jimbo la Rufiji linabeba asilimia 50 ya Hifadhi ya Taifa letu, wakaniambia nibaki kwa ajili ya kuzungumza mambo ya msingi kabisa kwa ajili ya ustawi wa taifa letu hili la Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hii ni nchi yetu sote, nianze kwa kusisitiza kwamba nchi hii ni yetu sote. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kumteua Brigedia Jenerali Gaudencia Milanzi. Tunatambua uteuzi wake una changamoto nyingi kwamba anapaswa kufanya kazi, kupambana na majangili ili ni kufuta aibu kubwa iliyotokea mwezi Januari ya kuuwawa kwa rubani wa ndege Bwana Roger Gower. Hakika jina la *pilot* huyu litakumbukwa katika nchi yetu na litaandikwa katika historia kwani alikuwa ni miongoni mwa wapambanaji wanaosaidia kupambana na ujangili katika nchi yetu hii ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia kwa undani sana taarifa za kwenye mitandao lakini pia nimefuatilia kwa umakini uwasilishwaji wa hoja mbalimbali ndani ya Bunge lako hili Tukufu. Pia nina fahamu zipo taarifa za wadau

mbalimbali kutumiwa ili kujaribu kukwamisha bajeti ya Wizara hii; wadau mbalimbali wakiwemo na wanasiasa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango mbalimbali iliyowasilishwa katika Bunge lako hili Tukufu imejikita kwa watu wengi kuzungumzia haki za wafugaji lakini wamesahau kwamba wakulima tunao na wana haki zao za msingi na wanachangia asilimia 25 ya Pato la Taifa la nchi yetu hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere aliwahi kutukumbusha kuhusiana suala hili la kubagua au kubaguana, kuanza kuwabagua watu fulani kuwaona watu fulani wao ni muhimu kuliko watu wengine. Lakini naomba nisisitize Ibara ya 13(4) ambayo inafafanua kuhusu haki ya kutobagua watu au kundi fulani. Wakulima wamebaguliwa sana ndani ya hili Bunge lako Tukufu. Ninaomba niseme wakati wa uwasilishwaji wa Wizara ya Kilimo tuliona wafugaji wengi walifika hapa Dodoma, lakini pia wakati wa uwasilishwaji wa Wizara hii wafugaji wengi pia wapo ndani ya Dodoma hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu Ibara ya 13(5) ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayofafanua mambo kadhaa na *emphasis is mine* na nisisitize hili:- “Katika kutimiza haja ya haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia utaiifa wao, kabila, pahali wanapotoka, maono yao ya kisiasa, rangi, dini, jinsia au hali yao ya maisha kwa namna ambayo watendewe wao ili waweze kupewa fursa au faida katika nchi hii.” Ibara hii inasisitiza haki ya kutobagua watu fulani. Naomba msisitizo huu Waheshimiwa Wabunge wauchukue ili tunapokuwepo hapa tujadili haki za msingi za wananchi wetu wote wa Tanzania bila kubagua huyu ni mfugaji au huyu ni mkulima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vurugu hizi kati ya wakulima na wafugaji nizungumze kidogo, hazikuanza zamani sana sisi kule Rufiji tulizoea kuamka unakutana na mpunga; lakini leo hii mifugo imeingia, lakini silaumu kilichotumika ni Ibara ya 14 ya Katiba yetu ambayo inaruhusu Mtanzania kuishi popote. Ibara hii ya 14 ilitumia baada ya Waziri Mkuu Fredrick Sumaye pamoja Lowassa kuendeleza mchakato huu wa kuhakikisha kwamba mifugo inasambaa ndani ya nchi yetu. Si tatizo baya kwa sababu huu ni utekelezaji wa Ibara hii ya 14. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa nikumbushie Ibara hii ya 14 ambayo inakwenda sambamba na ukumbushwaji wa sheria mbalimbali. Ninaamini Wabunge wengi wanasahau kwamba tunazo sheria nyingi ambazo zinatuongoza katika nchi yetu hii, na iwapo tutawashauri wananchi wetu kufuata sheria hizi hakutakuwepo na mgogoro wowote kati ya wakulima na wafugaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushie Sheria ya Matumizi ya Ardhi Namba 6 ya mwaka 2007 ambayo inatoa mchakato mzima wa namna gani ardhi itatumika na wapi wakulima waweze kufanya kilimo chao na wafugaji waweze kufuga wapi mifugo yao. Pia tunayo Sheria ya Mpango wa Vijiji sheria ya mwaka 1999 lakini pia tunao Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Mpango huu ni wa mwaka 2013 mpaka 2033. Tunayo sheria ya kuhifadhi maliasili pamoja na miongozo mbalimbali ya viongozi isiyokinzana na Katiba. Tunayo Ibara ya 26 ya katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatusisitiza wananchi wetu kufuata sheria. Tatizo hapa ni wananchi kutotaka kufuata sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe tu kwamba sheria hizi zilitungwa na Bunge hili, kama tunaona sheria hizi ni mbovu ni jukumu la Bunge letu...

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Ni jukumu la Bunge letu hili Tukufu kubadilisha sheria hizi.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya kaa chini.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Katika kubadilisha sheria hizi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya kaa chini.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Ibara ya 26 inazungumza wazi sina sababu ya kuisistiza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nirudi kwenye hoja zangu za msingi, hoja ambazo wa Rufiji wamenituma nije niwawakilishe hapa. Nianze kuzungumzia kodi ya kitanda. Niende haraka haraka, kodi hii ya kitanda ambayo ilitoka shilingi 8,000 kwenda shilingi 120,000 kodi hii iliundwa ili kuwakandamiza Warufiji. Mimi nikuombe kodi hii ambayo hata kama Mrufiji umelalia kitanda miaka 30 unawajibika kukilipia kodi iwapo unatoka nacho Rufiji unakwenda Wilaya zinazofuata Kibiti na maeneo mengine.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mwenyekiti taarifa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe kodi hii...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche nakuomba ukae, nakuomba ukae, nakuomba ukae

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kuiondoa kodi hii ambayo ni kodi kandamizi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche nakuomba ukae, unabishana na kiti?

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Kwa wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji. Nitaomba taarifa kuhusiana na kuondolewa kwa kodi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unabishana na kiti? Hebu kaa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 30(3) ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inanipa mamlaka mimi kupitia iwapo sheria au miongozo ya Serikali inakinzana na Katiba, mimi kama Mbunge na mwanasheria nguli nitakuwa na uwezo wa kufungua kesi ya Kikatiba ilikuweza kuomba Mahakama kutoa tafsiri fasaha ya kuondoa kodi hii ya kitanda ambayo ni kandamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa mbele ya Bunge lako hili Tukufu, baada tu ya kumaliza Bunge hili iwapo Waziri hataifuta kodi hii nitafungua kesi ya Kikatiba kwa sababu kodi hii ni kandamizi na ikinzana na Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona hiyo nisiizungumzie kiundani zaidi lakini nirudi kwenye kodi ya mkaa. Kodi hii ya mkaa imekuwa ikiongezeka siku hadi siku. Niliwahi kufanya tafiti kuhusiana na kodi ya *excise duty*, kodi hizi ambazo zinakuwa zinatolewa na Serikali ili ku-*discourage consumption*. Kuongezeka kwa kodi ya mkaa kunasababisha ongezeko kubwa la maisha kwa wananchi wetu wa Jimbo la Rufiji ambao wanategemea biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende mbele, nikimbie haraka haraka kidogo, naomba nizungumzie kuhusiana na pesa ya upandaji wa miti. Wananchi wangu wamekuwa wakichangia wanapokuwa wanalipa kodi ya mkaa wanachangia kiasi cha shilingi 830 kwa gunia kwa ajili ya kupanda miti. Naomba nipate taarifa kutoka kwa Waziri miti ambayo imeshawahi kupandwa na watu wa *TFS* ili kuweza kujiridhisha kwamba miti hiikweli inapandwa na pesa hii inatumika inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka kutokana na muda nizungumzie suala la migogoro...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza na ajiandae Mheshimiwa Zacharia Issaay. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haya lete miongozo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Na mimi naomba nitoe mchango wangu mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niamze kwa masikitiko katika Wizara hii. Kama ambavyo wenzangu wameongea kama pato la Wizara hii ni shilingi bilioni moja, na sisi Watanzania tunapigwa bakora, wananchi wanaenda kwenye msitu wanapigwa bakora, ifike mahali tuone basi kile kinachopatikana kina tija kiasi gani. Ninaomba sheria ya Wizara hii iwekwe mbele ya Bunge hili tuiptie upya yote tuangalie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingi za Wizara hii zimekuwa kandamizi na hii inaipelekea jamii yetu kupata matatizo mara nyingi hasa wale wanaokaa na kukutana na mazingira yale ya hifadhi. Kwa hiyo, naomba sheria itazamwe upya mbele ya Bunge hili ili tuone jinsi ambavyo inaenda na wakati wa sasa na pia ni sheria yenye manufaa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ninaomba basi pia tutazame, muone jinsi ambavyo fidia inayotolewa ni ya ajabu sana. Mwaka jana kabla ya mwezi Oktoba tembo walitoka Msitu wa Marang wakaenda mpaka kwenye Wilaya yangu ndani ya Jimbo langu wakaua watu watatu hadi mazishi hakuna mtu wa TANAPA aliyekuja. Kama anaweza kutoka tembo mpaka kilometa 40 au 30 akamuua mtu na bado sisi tunakaa huku tunazungumza mjadala wa bajeti ya Wizara hii tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaelekea pabaya, inaonesha tembo ndio wana thamani kuliko binadamu. Na mimi nikuombe wewe na Serikali kwa ujumla jinsi ambavyo tunapata madhara makubwa ya tembo hawa wanaotoka msitu wa Marang katika Jimbo langu na wanakula mazao ya watu mashambani huku wanaua wananchi, hakuna hatua inayochukuliwa tulipowaita TANAPA hawakuja mpaka siku ya tatu, hatimaye tembo wanaua watu watatu kwa siku tofauti. Tuangalie sana upana wa jambo hili, kama ambavyo wananchi wanapata madhara na pia fidia hakuna hatushiriki kwenye mazishi, tunapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kabisa tutazame jinsi ambavyo sheria ipo nyuma ya wakati, sheria ipo nyuma ya maisha ya wanadamu wetu na haiwatendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa kawaida akiingia msituni katika misitu ya Marang huko Jimboni kwangu, Waziri afahamu hili, mtu wa kawaida akipita kwenye msitu au akakutwa kwenye msitu hana kitu chochote anapigwa na askari; sisi bado tunaanza kupiga meza tunafurahia Wizara hii. Kama ni hiyo shilingi bilioni moja iondolewe kwenye bajeti upatikanaji wa huduma upungue kupitia fedha hizo ambazo mnatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika sana kama askari alieenda shule aliyepata taaluma anaanza kumpiga badala ya kumpeleka mbele ya sheria tunakwenda wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamsikitikia sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo watu wake wamekuwa wa ajabu. Tuliendesha *operation* tokomeza ikazalisha mambo ya ajabu sana na Watanzania wengi wakafa bado Bunge halijaanza kutazama jambo hili leo bado askari wanapiga wananchi wetu. Ninamuomba Waziri, nilimuomba mara nyingi afanye ziara kwenye Jimbo langu awasikilize wananchi, aje na karatasi nyeupe wananchi waandike mambo waliyofanyiwa na kama Rais anatumbua atumbue kuanzia kwa Waziri mpaka kwa watendaji wengine wote. Nimekasirika sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, wananchi wangu wamedhurika na pia kama ambavyo tukio linatokea Waziri ni mzito kufika, watendaji ni wazito kufika, hatimaye wananchi wanawekwa njia panda. Mimi siko tayari kuungana na hii Wizara, nipo kinyume kabisa. Nimtake Waziri apange ziara na apange ratiba ya vikao vya ujirani mwema kote Tanzania kwenye mazingira ambayo kuna hifadhi hizi ili kila mara kwa kila robo tuone wananchi wamefanyiwa nini. Hifadhi hizi zilikuwepo kabla TANAPA hawajaja, jamii walilinda, walihifadhi ndiyo maana hifadhi ziko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika sana; mimi ni wa CCM habari ya CCM hapa hakuna, hapa tuzungumze uchafu. Bila ziara, askari wanatoka kwenye msitu wanaenda kukamata wananchi, wanawapiga wananchi bado mnasema eti tunafanya vizuri, hakuna. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; vikao vya ujirani mwema vimeachwa kwa sababu matendo yao hayafanani na hali halisi ya Watanzania na haki za binadamu. Nimekasirishwa sana, kijiji cha Tawi nilikotoka mimi tembo wameuwa watu wawili kilometa 50; kama hatuwezi kuwarudisha tembo msituni tuna sababu gani sasa ya kupiga makofi eti kushabikia hii Wizara? Halafu mtu wa Mbulu anafuata fidia Dar es Salaam; aliwe shamba fidia Dar es salaam, fidia yenyewe shilingi laki moja. Anakwenda tena anakufa mtu fidia sijui shilingi laki tano Dar es Salaam; hivi kutoka Mbulu kwenda Dar es Salaam na kuishi kwenye gesti na hoteli na nini ni shilingi ngapi?



*(Hapa kuna Mheshimiwa Mbunge alimsemesha Mzungumzaji)*

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Tulia wewe, shuwaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shilingi ngapi zinapotea? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa TANAPA kwenye misiba inayotokana na wanyama iwekwe kwenye sheria, migogoro itatuliwe haraka; migogoro inaaachwa mpaka wananchi na TANAPA wanaingia uadui, tunapata uadui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa madini msitu wa Marang. TANAPA wanachimba madini kwenye msitu, mwananchi akiingia anakamatwa na anauawa. Kama Usalama wa Taifa wapo, wale watu watatu waliokufa kule Magara fanyeni uchunguzi walikufa kwa ajili ya nini. Wananchi wanasema walikufa kwa sababu walikwenda kuiba madini, Kaizer akienda kuiba madini ndipo anauawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri afanye ziara, aende msitu wa Marang, Jimbo la Mbulu, aende Yaeda Chini. Yaeda Chini usiku hutatoka, majangiri ni bunduki zinatembea utafikiri hii ni nchi ya vita. Habari ya u-CCM mnayoleiteta hapa ni ya kazi gani kama mambo ni ya hovy hovy? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitaka Serikali hii ijiangalie upya!, Serikali hii ijiangalie upya. Kama watu wanauawa kwa ajili ya kwenda kuchimba madini na TANAPA wanachimba; ninakutaka Waziri, nenda kwenye msitu wa Marang ukachukue hatua ya wale wanaochimba msitu wa Marang na wa Manyara, watoke wale TANAPA na wao wasichimbe, hawana sababu ya kuchimba pale. Mali zinazokamatwa zinakuwa miradi ya watu. Mali inakamatwa, mbao inakamatwa inauzwa, ni miradi ya watu, mnasema tunapata shilingi bilioni moja ya kazi gani? Shilingi bilioni moja itatufikisha wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana, na ninaitaka Serikali; kazi ya Bunge ni kuibana Serikali, na wewe Waziri tunaanza na wewe. Tuanze na wewe na wewe uwabane walio chini yako. Mtu yeyote wa CCM achukue hatua juu yangu kama anaweza. Kama ni namna hii... *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nani alikuja kwenye kampeni wakati tunafanya kampeni? Kila mmoja alitetea kiti chake ndiyo maana tuko huku. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ahsante, waambie!

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kura zangu zilipungua kule Daudi, Gehandu, Marang kwa ajili ya mtindo huu huu wa kuleana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ahsante, ahsante! Ahsante muda wako umekwisha, ahsante sana! Ahsante! Nakuomba ukae chini. Nakuomba ukae chini. Nakuomba Mheshimiwa ukae chini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge kadhaa walipiga makofi na kushangilia)*

**MWENYEKITI:** Nakuomba ukae chini. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, halafu Ajiandae Mheshimiwa Mahawe, ajianda Mheshimiwa Engineer Nditiye.

*(Hapa Mheshimiwa Zacharia P. Issaay aliyemaliza muda wake aliendelea kuongea)*

**MWENYEKITI:** Hapana, samahani, umeshamaliza muda wako.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mahawe! Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, ajiandae Mheshimiwa Nditiye, ajiandae Mheshimiwa Kikwete.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba dakika zangu kumi, kila nikichangia ninapewa dakika mbili, dakika tano wakati wengine wametumia dakika kumi; naomba unitendee haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpe tu pole Mbunge wangu Mheshimiwab Issaay, inatia hasira wakati mwingine lakini pole sana kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema, ni kweli kwamba sekta ya utalii inatoa mchango wa asilimia 25 ya pato la fedha za nje katika nchi yetu, lakini ni kweli wakati mwingine inakuwa inaumiza baada ya kuona kwamba uharibifu mkubwa unafanywa na wanyama... Wabunge naomba tusikilizane.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa!

**MBUNGE FULANI:** Endelea mwanangu.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana...

**MWENYEKITI:** *Order please*, naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu mkubwa unafanywa na wanyama, lakini badala yake fidia ama kifuta jasho kinachotolewa ni kweli kwamba ni kidogo sana. Hii ndiyo inayopelekea kwa kweli watu kupata shida wakati wa kampeni za uchaguzi baada ya kuona kwamba hawatendewi haki. Inafika mahali labda wanyama wanaonekana wa thamani kuliko mwanadamu. Ni kweli kwamba hili linapaswa kuangaliwa kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme kwa upande wa Wilaya ya Babati Vijijini, wanyama walifanya uharibifu na Mheshimiwa Jitu Soni kwa zaidi ya miaka mitano amekuwa akifuatilia kifuta jasho cha wananchi husika, lakini katika pesa ambazo zinafikia zaidi ya shilingi milioni 100 ameambulia kupata shilingi milioni 12, tunaomba Wizara hii sasa iweze kuangalia namna gani hawa wananchi walioathirika wanaweza kupata fidia hiyo japo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe shukrani za dhati kwa TANAPA kwa kuweza kufungua geti la Sangaiwe pamoja na geti la Mamire ili kuweza kuruhusu wananchi kufanya biashara zao ndogo ndogo. Niombe Wizara iweze kutusaidi kukusanya hiyo 0.3 levy ili kwamba mapato haya yaweze kuwa ya msaada kuliko inavyofanyika sasa, maana hoteli zinazozunguka hifadhi hizo zimekataa kata kata kulipa tozo hizo za 0.3 percent.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo naomba pia niseme miaka michache iliyopoita wakati wa *Operation Tokomeza* mama mmoja kule katika Kata ya Galapo, Mkoani Manyara aliauwa, ikaundwa Tume ya Kijaji mpaka sasa hatujapata jibu lolote kuhusu mauaji yale. Tunaomba Wizara itusaidie kujua nini kiliendelea kuhusu mauaji yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na zaidi sana naomba ni-*declare interest* kwamba mimi pia ni mdau wa utalii. Kuna utitiri mkubwa wa kodi zisizopungua 15 katika uwekezaji huu wa utalii. Haiwezekani wananchi wetu wakalifikia goli la kuondokana na umaskini wakati kodi ni nyingi kupita kiasi. Mheshimiwa Mchengelwa ametoka kuzungumza habari ya *night bed levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni nini maana ya mtalii. Inawezekana mtu akitoka Arusha kwenda Dar es Salaam kwenda kumuuguza mgonjwa wake Muhimbili na akawa analala kwenye hoteli pale Dar es Salaam anaweza akawa anaitwa mtalii. Tatizo ni kwamba kodi hii haiko-*fair*. Kama ni *Mount Meru Hotel* inalipa *one point...*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaomba utulivu ndani ya ukumbi.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hii ya *night bed levy* kwa kweli imekuwa kikwazo kwa wafanyabiashara wadogo. Unakuta mtu hoteli yake anauza vyumba kwa shilingi 30,000 au 50,000 analipa *the same amount* na mtu ambaye ana hoteli ya kitalii, au *let us say* hoteli ya *Mount Meru* ama hoteli nyingine kubwa za nyota nne au nyota tano. Sasa usawa uko wapi? Hili litazamwe na Wizara hii, Mheshimiwa Maghembe tunaomba ulitupie jicho, *night bed levy* imekuwa kikwazo kwa wafanyabiashara wadogo kama wale wenye *guest houses* wanatozwa kodi kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo niseme pia *TALA license* imekuwa ni kilio cha muda mrefu. Hapo Kenya wanatoza dola 300 kwa *TALA license*, lakini pia wanatoza kwa gari hawatozi kwa kampuni. Huku kwetu una gari moja, tano, mbili, mia tano unatozwa dola 2,000 kwa nini? Hili kimekuwa kilio kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulipia *TALA license* unalipa *land rent*, unalipa *tax* zote 15, huyu mtu anapataje faida? Anawezaje kutusaidia kuongeza ajira kwa vijana wetu? Nilisema tena watu wengi wameweka magari yao nyumbani, wameshindwa kufanya biashara ya utalii kwa ajili ya utitiri wa kodi. Ifanyike *review* kwenye kodi hizi ili utalii wetu uweze kuleta tija katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu, inawezekana sana kuhakikisha kwamba pia na misitu yetu inatusaidia. Ukienda nchi za watu watoto wanagombana na wazazi wao kubadilisha *ipad*, *laptop* mpya, *smart phones*, sisi tunajadili habari ya dawati wakati misitu iko hapo. *TFS* wanakusanya zaidi ya shilingi bilioni 50, ni ukataji wa miti tu unaendelea, hakuna miti inayorudishwa kupandwa. Tutakwenda hivi mpaka lini? Mtoto kukaa kwenye dawati Tanzania inakuwa ni *privilege*, kweli? Tutaondoka lini huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiri kwamba tunaweza kurekebisha hali hii, kama tuna sera mbovu basi tuziangalie tena, tuzirekebishe ili kwamba yote yanayoendelea katika nchi hii yawe ni kwa maslahi ya Mtanzania maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme haraka haraka juu ya Mlima Hanang. Mlima ule ni wa tatu kwa urefu hapa Tanzania, lakini kuna uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea katika Mlima Hanang. Tunaomba ikiwezekana mlima huu ukabidhiwe kwa *TANAPA* ili waweze kuulinda maana uharibifu unaofanyika pale ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisiendeleo sana, niwaachie na wenzangu wengine dakika chache zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nditiye, ajiandae Mheshimiwa Ridhiwani na ajiandae Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba unisaidie niweze kutumia dakika zilizobaki za Mheshimiwa Ester Mahawe halafu na za kwangu niendeleo kuzitumia. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwanza na suala zima la uhifadhi wa misitu yetu. Mimi wakati mwingine huwa nashangaa sana. Sijabahatika wala sikufanikiwa kuwa mmoja wa waongejaji wa jazba sana; ndivyo nilivyombwa, halafu sioni ubaya. Lakini ninajaribu kuona namna ya kuwashawishi na kuwashauri Wabunge wenzangu, sisi ni viongozi, kuna mambo mengi sana yanaudhi, wala haina siri, lakini ukishakuwa kiongozi lazima uwe na kifua cha kuweza kumeza mambo mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si swali la kujuliza sana, ni kitu cha kawaida kabisa kwamba hakuna hata mmoja wetu hapa ambaye hajui umuhimu wa kutunza misitu yetu. Ni jambo lililo wazi kabisa kwamba mifugo ina faida kubwa sana kwa nchi yetu, lakini nakuhakikishia, mifugo haiwezi kuwepo kama tutaruhusu hii misitu yetu inayotuletea mvua ili misitu ichipuke na wanyama wapate mahala pa kulishwa, kama itateketea. Nchi itakuwa jangwa kama tukiruhusu mifugo iingie kwenye hifadhi na kuanza kulisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanaotoka mikoa ya wafugaji wanajaribu kujenga hoja tu kwamba ng'ombe hawana tofauti na nyati. Hebu wajaribu kufuatilia vizuri, wana tofauti kubwa sana na nyati. Miaka 30 iliyopita kwenye miaka ya 1980 Shinyanga ilivyo leo haikuwa hivyo na mifugo ilikuwepo na hakukuwa na *contradiction* yoyote na misitu nayo ilikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba sana, Waheshimiwa Wabunge tuone ukweli, nchi yetu itageuka kuwa jangwa na hii mifugo tunayoitetea leo haitakuwa salama wala haitakuwa hai kama nchi yetu itakuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache siasa, tuwaambie wananchi wetu ukweli. Kwenye kampeni watu wote tumezungumza mambo mengi, lakini sasa turudi tuwaambie ukweli kwamba tukiruhusu sasa mifugo ikaenda kulisha kwenye misitu yetu nchi itakuwa jangwa, kwa hiyo, hata hiyo mifugo nayo itakufa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko ninakotoka Wilayani kwangu Kibondo ukihesabu mifugo ya wananchi wa Wilaya ya Kibondo, naomba nisizungumze kama mbaguzi, haizidi 60,000, lakini kwenye Pori la Moyowosi tuna ng'ombe zaidi ya 300,000, kila siku ni ugomvi, kisingizio ni kwamba wanakwenda kunywa maji Mto Malagarasi, sasa hivi kina cha Mto Malagarasi kimeshuka, nchi inakwenda kuwa jangwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia kuhusu suala la wanyamapori na uhifadhi na nitaongelea Pori la Moyowosi au Kigosi. Suala la ujangili linaendelea kutetemeshwa sana nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kibondo kuna ofisi kubwa sana ya Moyowosi, nilifanikiwa kwenda kutembelea pale, nikaongea na wafanyakazi kama mwanakamati wa Kamati ya Maliasili na Utalii. Nilipata changamoto zao nyingi sana, Mheshimiwa Waziri naomba uzishike. Pale kwenye ile ofisi wana magari matatu mazuri kabisa, lakini OC haifiki, matokeo yake wanaweza wakasikia bunduki ya kuua mnyama imelia *somewhere* lakini mafuta ni mpaka waombe kwa wale waliomiliki vitalu, hiyo ni aibu. Naomba sana hilo Serikali ilitilie umuhimu na iwasaidie sana wale wahifadhi waweze kufanya kazi zao bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nitakwenda kwenye sekta ya utalii. Si siri ndiyo sekta ambayo inaingiza fedha nyingi sana za kigeni kwa Taifa letu. Ina-contribute 25 percent ya fedha za kigeni katika uchumi wa nchi yetu, lakini sekta hii bado haijapewa kipaumbele cha kutosha, tunaomba sana Serikali sasa igeuze macho, iangalie sekta ya utalii. Tukiwa kama nchi ya pili kwa vivutio vingi vya utalii baada ya Brazil hatustahili kuwa hapa tulipo. Tunatamani nchi yetu i-contribute hata 50 percent ya Pato la Taifa kupitia utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo litawezekana tu kama tutawezesha Bodi ya Utalii kufanya matangazo stahiki. Bodi ya Utalii ya Tanzania kwenye bajeti iliyopita haikufikia hata Shilingi bilioni tatu ilizopewa kwa ajili ya kufanya matangozo ya utalii. Matokeo yake Bodi ya Utalii ya nchi jirani ya Kenya ilipewa zaidi ya bilioni 50 kufanya matangazo ya utalii kwa ajili ya nchi ya Kenya, ambayo unaweza ukaenda kwenye mbuga mojawapo ya kwao ukazunguka kilometa sita ukaona swali mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na matangazo wanayoyafanya watalii wengi wanashuka Kenya, wanadanganywa danganywa, uongo uongo weanakuja kuangalia wanyama kwetu halafu wanarudi Kenya wanaingiza pesa nyingi sana Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sishangai sana kuona kwamba hata Mlima Kilimanjaro, Kenya ndio wanaoutangaza zaidi kuliko Tanzania, hiyo ni aibu.

Ninaomba sana Bodi ya Utalii iwezeshe, ipangiwe fungu kubwa la pesa ili iweze kutangaza utalii wetu na nchi iweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mali kale. Nilipata mshituko mkubwa sana, kama miezi miwili iliyopita nilipomuona binti mmoja wa Kikenya akiitangazia dunia kwamba Olduvai Gorge iko Kenya na kwamba sasa dunia iende ikaangalie unyayo wa mtu wa kale kabisa duniani ambao unapatikana Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Serikali ilichukua jukumu la kukemea na wale wakakanusha. Lakini kusema kweli tayari *damage* iliyofanyika kwa yale maelezo ya yule binti ni kubwa sana hayawezi kukanushwa tu kirahisi rahisi kama vile na ikaweza kuleta *impact* kwa uchumi wetu wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali ichukue juhudi za makusudi za kuhakikisha vivutio vyetu vinatangazwa na *TANAPA*, *TTB* pamoja na Ngorongoro. Bila kufanya hivyo wenzetu wataendelea kuchukua *advantage* ya sisi kukaa kimya na tutaendelea kupata shida ya kutopata mapato stahiki kutokana na vivutio ambavyo Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa *TDL*. Ninazo taarifa kama Mwenyekiti wa Kamati ni-*declare interest* kwamba kuna *three percent* ya *gross* ambayo inatakiwa iende kuimarisha Chuo Cha Utalii, iimarishe *TTB* na shughuli za ku-*promote* utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mashaka kama hiyo pesa kweli inafika, naomba sana hili lifuailiwe ili *TTB* ipate nguvu, lakini na Chuo chetu cha Utalii ambacho kwa hapa Afrika ya Mashariki ni chuo cha kipekee sana kiweze kupata *facilities* za kuwafanya vijana wetu waweze kujifunza utalii, na ajira nyingi kwenye hoteli zetu zichukuliwe na Watanzania badala ya kuchukuliwa na watu kutoka nchi jirani zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nizungumzie Chuo cha Misitu cha Olumotonyi. Wakati tunafanya ziara ya kamati tulizungukia chuo kile, kila hali mbaya sana. Tunaiomba sana Serikali, ukitaka kupata faida lazima uwekeze. Huwezi kutegemea kuvuna kama hujalima na kupanda. Kinachoonekana sasa hivi Serikali inataka ivune mahala ambapo haikupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Misitu ni chuo muhimu sana kwa maendeleo ya Tanzania, ni chuo cha kipekee kwa Afrika Mashariki na Kati kinachofundisha watu uhifadhi wa misitu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana kipewe kipaumbele, kiwezeshe fedha, kiongezewe bajeti ili kiweze kutufundishia vijana wetu tuweze kupata tija kutokana na chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Msigwa, akitoka Msigwa anakuja Mheshimiwa Ridhiwani, akitoka Ridhiwani Mheshimiwa James Millya akitoka James Millya atafuata Mheshimiwa Keissy.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mimi nianze na Wizara kama ambavyo mchangiaji Mheshimiwa Lucy Owenya amesema, ili tupandishe uchumi wa *Southern circuit* lazima tufungue milango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana Bunge lililopita tumezungumzia sana kuhusiana na uwanja wa Nduli Iringa pamoja na barabara inayotoka Iringa Mjini kwenda *National Park*. Ningeomba Wizara kama inawezekana hebu tushirikiane basi hata na *TANAPA* tutengeneze ile barabara kusudi tuweze kuzalisha pesa nyingi zinazotokana na hifadhi ambayo ni kubwa ya pili hapa Afrika, ningeomba hilo mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninataka nizungumzie kuhusu wanyama waliotoroshwa, hiki ni kiporo. Kwa bahati mbaya Wabunge huwa tunasahau tulikotoka, hiki ni kiporo. Bunge lililopita tumezungumza sana juu ya ujangili, lakini kuna wanyama waliokuwa wametoroshwa uwanja wa *KIA*. Bunge lililopita tulitoa azimio, AG wewe ni shahidi hapa tulikubaliana wote kwamba lazima ufanyike uchunguzi ni akina nani walitorosha wale wanyama, sasa hivi hakuna kesi, mwanzoni mlikuwa mnasingizia kuna kesi mahakamani, sasa hivi hakuna kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliingiaje ndege ya kijeshi? Jeshi lilionaje hapa? Usalama wa Taifa ulionaje? Hayo mambo bado hayajatolewa majibu. Serikali ya Qatar, nilibahatika kwenda Qatar walisema wamezoea kuchukua wanyama kwa *style* hiyo. Tulitoa Azimio kwenye *Hansard* inaonyesha Bunge lililopita. Ninaomba Waziri haya mambo hayawezi kulala kiporo kama tunataka tukomeshe ujangili, maana yake Serikali hii imesema inafukuwa makaburi, tuendeleo kufukuwa makaburi hayo ni nani alihusika kutorosha hawa wanyama kuwapeleka Qatar, lazima turudishe na Bunge liliazimia. Naomba AG utasaidia Wizara hii namna gani tulifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni hili suala ambalo Kambi ya Upinzani imezungumzia kuhusu Kampuni ya *Green Miles*. Kampuni ya *Green Miles*, amezungumza Mheshimiwa Mbunge Mzee wangu hapa, mimi nilikuwa miongoni mwa Kamati ya Wabunge wanne, tuliokuwa tunachunguza utoroshaji wa wanyama. Tulipochunguza kampuni ya *Green Miles*, kama alivyosema haikupewa vitalu vya uwindaji kwa sababu ilikuwa haina sifa. Kamati ya ushauri ilimshauri Waziri kwamba hii kampuni haina sifa, imesema uongo, lakini haihifadhi kwa sababu kwenye kuwinda kunahitaji uhifadhi, kwa bahati mbaya au vinginevyo mambo yalivyokwenda hii kampuni ikapewa. Ilivyopewa tukayashuhudia yale ambayo walivunja kanuni za uwindaji na kulikuwa na *infringement* zaidi ya 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Julai niliweka CD hapa kuonesha jinsi ambavyo wanawinda vibaya! Hawa watu hawana sifa za uhifadhi na Waziri aliyepita aliamua kuifutia leseni ya uwindaji kwa sababu wanawinda vibaya, suala hili lilivuta hisia za Kimataifa katika masuala ya uwindaji, suala hili lilivuta hisia za Watanzania vituo karibu vyote vya televisheni vilionesha jinsi ambavyo hawa watu wanawinda vibaya wanyama, hawana sifa ya kuwinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza Mheshimiwa Waziri umetoa barua tena. Hapa Mheshimiwa Maghembe, kwenye masuala ya uhifadhi niko na wewe, sikubaliani kwamba ng'ombe waende kila mahali, lakini kwenye suala hili sikubaliani na wewe. Kwa sababu tunakubali kuwa uwindaji ni pamoja na uhifadhi, *hunting is about conservation*. Mwindaji yoyote ambae hawezi ku-*conserve nature* hatustahili katika nchi yetu! Sasa inawezekanaje hawa watu ambao hawana sifa, kuna *infringement* zaidi ya kumi na ngapi? Lakini Waziri aliyekutangulia alifuta, kulikuwa na makosa sita aliyaona. Walikuwa wanawinda ngedere hawaruhusiwi kuwinda ngedere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa chini ya miaka 16 anawinda, sheria inakataa, walikuwa wanatumia bunduki ambazo zinaziba sauti, sheria inakataa, wewe mwenyewe unajua kwenye sheria ya mwaka 2009 na *regulations* za mwaka 2010. Hawa watu wamevunja sheria, leo wanarudi wanarudi kwa mlango gani? Ninaomba Waziri utuambie hawa watu ambao hawana sifa za kuwinda wamerudije tena kwenye maeneo hayo? Tutakuwa tunaleta mchezo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge hebu tuwe *consistance* kama tunataka tufanye uhifadhi. Wale waliokuja kuchukuwa wanyama wetu, watu walipiga kelele sana Bunge lililopita wakasema tunataka hata mifupa irudi. Nani alichukuwa hao wanyama? Hiyo ndege ya Qatar iliingiaje? Tulizungumza hapa kwamba mpaka na Ikulu ilikuwa inahusika, hatujapata majibu ya kutosha. Lakini hawa ambao walizuiwa

wanarudi tena kwa mlango wa nyuma wamerudije? Naomba Mheshimiwa Waziri haya mambo utupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuna Mbunge, asubuhi amezungumza kwamba mpaka kwenye magazeti wanaandika kwamba kuna Wabunge wengine ni majangili. Hii ni kashfa kwa Bunge, hatuwezi kukaa kimya. Hili Bunge tumeambiwa kuna wala rushwa, Bunge hili wengine wanapiga mtindi, Bunge hili tena tunaambiwa kuna majangili. Tutakuwa na chombo cha umma kipi ambacho haya mambo kama hatuwezi kuyasemea? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu kama kweli imeandikwa *Jambo Mills* gari yake hii hapa, kama ni kweli lazima tupate majibu na kwa bahati mbaya labda yeye hayupo na inasemekana, taarifa zinasemekana mpaka na gari lingine la *Jambo Mills* lilikamatwa na pembe za ndovu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile halitoshi, huyu mtu kuna leseni moja ya madini na yeye anahusika. Haya madini yako kwenye kitalu kule Meatu ambacho kuchimba madini hairusiwi kwenye hifadhi Waziri unajua Huyu mtu sijui amepataje kulikuwa hakuna EIA? Amepata, wanatumia wafugaji kuwaingiza eneo la uwindaji kwa kisingizio kwamba hawana malisho ili waweke *pressure* kusudi wakachimbe madini mpaka wamepata hiki kibali.

Nimshukuru Mkuu wa Mkoa alizuia hiki kibali na nimuombe Waziri wa Madini alifuatilie hili suala, ni nani alitoa kibali hiki, watu waingie kwenye hifadhi, sheria yetu inakataa kwamba wasiingie kwenye hifadhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu kama kweli haya mambo yanafanyika na yeye anahusika, Bunge lijisafishe, tujue kuna tatizo gani kama ni ya uongo asafishike, lakini vyombo vya habari vimeandika, vyombo vya habari vimetoa, anahusika, wanasema kuna Mbunge anahusika wamemtaja kwenye magazeti, ukienda kwenye mitandao na yeye hajakanusha. Lakini kuna wakati walivyokamatwa hawa watu waliachiwa, wakatoa fedha kidogo tu wakati wengine wanasota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanasafirisha tumbili, umewaweka ndani sasa hivi wanasota, lakini hawa watu wanatembea, inaoneka waliokamatwa wana nasaba na huyu mtu alyetajwa hapa, lakini wametoa faini wakaachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama wanaonekana hapa hawakuchukuliwa hatua zozote, lakini wengine wamesafirisha tumbili tu wale tena wana haki, wale walikuwa wanasafirisha tumbili vizuri hawana makosa, akina Mzee Mlokozi wale wanalala tu kule ndani. Hawa wanatembea

barabarani na wanatumia kisingizio, nikuombe hata hili suala la Toya Mheshimiwa Waziri hebu liangalie kwa upana wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa bahati nzuri miaka yote mitano nimekuwa kwenye hilo eneo kidogo naelewa, watu wa Toya muwaangalie kwa jicho la karibu sana. Manyanyaso wanayoyapata na taabu wanayoipata kwa kweli haiwahusu. Tunajaribu kuwarudisha nyuma hawa ambao ni Watanzania wazawa, wanafanya biashara zao, tunawa-drag chini bila sababu. Niombe Watanzania wenzangu *the fact* sisi ni Wabunge hapa, tupo kwa ajili ya maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemu mmoja unasema: *'it is not economical to go to bed early and save all the candles if the result is twins* (siyo jambo la kiuchumi kwenda kulala mapema ukatunza mishumaa yote kama matokeo yake yatakuwa ni mapacha). Kama tutadhani ni uchumi kupeleka ng'ombe kila mahali kusiwe na mipaka, tusidhani litakuwa jambo la kiuchumi, baadaye tutapata hasara ya Taifa hili, ni lazima tu-save nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni ya wafugaji, nchi hii ni ya wakulima, nchi hii ni ya wafanyakazi, nchi hii ni ya viwanda, kwa hiyo, lazima tutenge maeneo. Ndiyo maana China walivyooona nchi ni ndogo wakaweka sheria ya kuzaa mtoto mmoja. Kwa hiyo, hatuwezi tukasema ng'ombe wawe kila mahali, hatuwezi kusema ufugaji uwe kila mahali, tukabaliane wote kama viongozi, tutenge maeneo maalum. Mheshimiwa Waziri, kuna asilimia 10 nchi hii ya ufugaji wa ng'ombe, ambao ng'ombe tulionao milioni 25, wakiwekwa vizuri tunaweza tukawatunza. Lakini hatuwezi kukubali kutumia mifugo tukaharibu uhifadhi, tukaharibu utalii ambao unatuletea fedha za kigeni asilimia 25 na GDP ya asilimia 17. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, badala ya kugombana hapa na wananchi wametuita hapa kama viongozi, kama watu wenye busara, badala ya kugombana hapa kuwa na mawazo madogo ya kuwaza Jimbo lako hebu tuwe na *national interest*, tukae wote kwa pamoja tukubaliane. Hii nchi ni yetu sote, tukubaliane mifugo ikae wapi, samaki wakae wapi, ng'ombe wake wapi? Mheshimiwa Waziri tukiruhusu jazba zitutawale hapa tutaishia kugombana. Kama wananchi huko wakituona, mfugaji anagombana na mkulima, mkulima anagombana na mfugaji, huko nje tutaanzisha vita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha wa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kikwete, ajiandae Mheshimiwa Millya na pia a jiandae Mheshiwa Keissy.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba nzuri ya Waziri wetu wa Maliasili na Utalii, ambayo hakika kwangu imetoa fumbo au imetoa jibu la mambo ambayo nilikuwa nahitaji kuyasikia. Mheshimiwa Waziri kwanza nikupongeze na kukuunga mkono katika hotuba yako hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote naomba kumwambia ndugu yangu Msigwa nimemsikia hapa amezungumza juu ya jambo la *Green Miles*. Ninachokifahamu Mheshimiwa Msigwa, hukumu imeshatolewa juu ya kesi ile ya *Green Miles*. Bahati mbaya sana hawa ambao wewe unaowasema ni dhaifu, hawana sifa, mahakama imeamua kuwapa kitalu. Mheshimiwa Waziri atakuja kuyazungumza vizuri, lakini nilitaka nitoe taarifa hii mapema ili upate kuifahamu halafu Mheshimiwa Waziri aje kututhibitishia kama niliyoyasikia mimi ndivyo yalivyo au yana walakini katika lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, niungane na ndugu yangu Mheshimiwa Msigwa aliposema kwamba nchi hii ni ya kwetu wote na tunapaswa kuzungumzia *interest* za nchi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tanzania, mwezi Oktoba mwaka jana, walichagua Chama cha Mapinduzi, tuzungumzie maslahi ya nchi hii. Huo ndiyo wajibu wetu wa kwanza kama Wabunge tunaotokea ndani ya Chama cha Mapinduzi, kuzungumza juu ya *interest* za nchi yetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Msigwa anachofanya ni kutukumbusha juu ya wajibu yetu na sisi tunakushukuru kwa sababu ndiyo wajibu wetu kuendelea kukumbushana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa kipindi kirefu sana imekuwa katika migogoro mikubwa ya wakulima na wafugaji, pamoja na hilo migogoro ya uhifadhi na vijiji vyetu nayo imekuwa ni moja ya donda ndugu. Mimi nimewahi kuzungumza katika Bunge lililokwisha, Bunge la Kumi juu ya matatizo makubwa yaliyopo baina ya watu wa kijiji cha Matipwili, Gongo, Mkange, Manda na Hifadhi ya Saadani. Ziko hatua ambazo zilikwishafanyika kipindi kile cha Mheshimiwa Nyalandu, alikwenda kule akakutana na Wananchi wale, wakafanya mikutano, lakini Mheshimiwa Waziri Maghembe, ambaye hii ndiyo bajeti yako ya kwanza ninaamini kwamba kuna vitu unabidi uvisikie kutoka kwetu Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba yale waliyokubaliana Mheshimiwa Nyalandu na wananchi wangu, mpaka sasa hivi imeendelea kuwa ni kizunguzungu na hakuna majibu sahihi yaliyokwishapatikana. Kwa hiyo, ninachokuomba Mheshimiwa Waziri, unapokuja kujumuisha au kuhitimisha hotuba yako, ni vema jambo hili pia nalo ukalizungumza ili wananchi wangu wa vijiji vilivyotajwa, waweze kusikia kauli yako wewe Waziri mpya wa Wizara hii,

ukitoa majibu yaliyo sahihi na jinsi gani tunaweza kukamilisha mchakato ambao ulianzishwa na wenzako waliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nimewasikia watu wengi wakizungumza juu ya matatizo ya ng'ombe katika hifadhi zetu. Mheshimiwa Waziri, nataka nikwambie mimi ninayo Hifadhi ya Wamimbiki, na yoyote yule anayetaka kusimamia hapa kutetea ng'ombe wakae ndani ya hifadhi huyo ni adui wangu wa kwanza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwambieni ndugu zangu, haiwezi kugeuzwa nchi yetu ikawa yote ni sehemu ya kuchunga ng'ombe, haiwezekani, lazima tuweke mipaka na lazima tu- *identify* maeneo ambayo ng'ombe wanatakiwa kwenda kuchungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Halmashauri ya Chalinze, wananchi wa Tanzania, wananchi wa Bagamoyo, kwa kipindi kikubwa sana wamekuwa wanategemea sana Hifadhi ya Wamimbiki kwa ajili ya kupata fedha za kigeni, lakini pia kwa shughuli za kitalii zilizokuwa zinafanyika katika maeneo yale. Sisi wengine Wamimbiki tunatembea na mguu kuingia kule. Tumekuwa tunashuhudia wanyama wakati tuko wadogo, leo hii Mheshimiwa Waziri, wanyama wale hawapo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu hata hatuelewi wametokea wapi, wamekaa ndani ya hifadhi ya Wamimbiki, baya zaidi ambalo linafanyika hatulipendi, inakatwa miti, watu wanatengeneza makazi ndani yake, na matokeo yake ni kwamba miezi mitatu iliyopita ndugu zangu tumeshuhudia tembo katika Mji wa Chalinze - Bwiringu. Tumeshuhudia tembo katika Mji wa Chalinze, kwa nini wamekwenda Chalinze, ni kwa sababu hawana njia zingine za kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupeni taarifa kwa sababu sisi wengine kule Chalinze ni kwetu, hatujaenda kutafuta vyeo. Tembo wanapotoka Mozambique, wanakuja kupitia kwa Selous na wakifika maeneo ya Mikumi wanagawanyika katika makundi mawili, lipo kundi ambalo linakwenda Kaskazini mpaka Hifadhi ya Manyara na liko kundi ambalo linakwenda Mashariki mwa Tanzania, ambalo linakwenda mpaka Hifadhi ya Saadani. Kinachoshangaza, kwa shughuli zinazofanyika pale, na shughuli ambazo zinaonekana kwamba Wizara haichukulii kimkakati jambo hili, wale tembo sasa hawana sehemu ya kwenda. Matokeo yake tembo hawa wanatafuta njia nyingine za kufika Saadani, ndiyo matokeo yake wanafika kwenye nyumba za watu na inakuwa ni taabu katika maisha yetu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo liko *serious*, hatutakiwi kulifanyia mchezo, kama ambavyo leo hii wako baadhi ya wenzetu kwa mfano, Biharamulo kule, imefika sehemu kwamba wanaomba lile pori sasa ligawanywe ili watu wapate kuhifadhi ng'ombe, badala ya kufanya shughuli za hifadhi asilia. Kama ambavyo leo hii mbuga ya Serengeti inataka nayo kupotea kwa kuwa ng'ombe wamejaa wengi au kule katika pori la Kigosi na pori tengefu la Loliondo. Mheshimiwa jambo hilo kwa Halmashauri ya Chalinze hatuko tayari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima leo hii, utuambie ni mkakati gani ambao kama Wizara mnao na mmejipangaje kuhakikisha kwamba mnaondoa mifugo hiyo katika eneo lile ili sasa mambo mazuri ya uhifadhi wa hizi asili uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, Mheshimiwa Waziri tunalo tatizo lingine pia katika *Uzigua forest*; *Uzigua forest* imekuwa ni kilio cha muda mrefu na mwisho wa siku hapa mzee tunaweza tukageuzwa majina yetu yakawa ni *Uzigua forest* hapa, Mheshimiwa Waziri hili nalo naomba ulitolee jibu. Wananchi wamekuwa wanauliza juu ya mipaka ya hiyo *Uzigua forest*, lakini hifadhi yetu hii imeendelea kukua, inaonekana tofauti na ambavyo hifadhi nyingine zinaendelea kuwepo. Lakini majibu yamekuwa ni yale yale kwamba tutakuja halafu hatuna jibu la moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mheshimiwa Waziri, na hili jambo nafikiri ni jambo la Serikali yote ilisikie. Kumekuwa na tatizo moja la *ECO-Energy*. *ECO-Energy* walipewa maeneo na vijiji vyetu, lakini cha kushangaza zaidi baada ya kutangaza juzi kwamba mradi ule hautokuwepo, kipande cha hifadhi ambacho kilikuwa katika miliki ya vijiji vyetu vile, hifadhi ile kinarudishwa katika eneo la *TANAPA*, Saadani.

Mheshimiwa Waziri naomba tu nikupe angalizo, wananchi wangu wa Halmashauri ya Chalinze, walitoa maeneo yale kwa ajili ya kupata faida nayo. Faida yao kubwa ilikuwa kwamba *ECO-Energy* walime miwa, lakini wao wawe ni *outgrowers*. Leo hii maeneo yao yale meamua Serikalini kuyachukuwa na kuyafanya yawe sehemu ya *TANAPA*. Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie, katika jambo hili hatutokubalina na mimi nitakamata shilingi yako kama hakutakuwa na jibu ambalo linatuambia kwamba ardhi hii itarudishwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Serikali mnaweza mkaamua lolote, lakini katika jambo hili la ardhi ya wanavijiji wangu, kama hatujafika na sisi kulalamika, kama alivyolalamika juzi Mheshimiwa Mbowe pale na ardhi ile ya Kilimanjaro, ningomba jambo hili mlitolee majibu mazuri zaidi.



Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya Operesheni Tokomeza, wenzangu wamezungumza kwamba ardhi ile ya Operesheni Tokomeza imechukua bunduki za watu, imechukua magobole ya wazee wangu pale katika vijiji vyetu vinavyozunguka hifadhi zetu, lakini baada ya kumalizika operesheni ile hatuoni silaha zile zikirudishwa kwa wananchi wale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, uje kutoa jibu katika jambo hili. Mwenzako Mheshimiwa Nyalandu hapa alikuwa kila siku anatumbia kwamba itatoka kesho mpaka anaondoka hakuna jambo lolote. Nataka wewe katika Serikali hii, uje kutuambia inakuwaje juu ya yale mambo ambayo tulikuwa tunaongea kila siku juu ya silaha hizi za jadi walizokuwa wanatumia wazee wangu pamoja na magobole na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nieleze pia kama walivyosema wenzangu juu ya jazba zilizotawala humu ndani!

Waheshimiwa Wabunge, hatupaswi kuwa na jazba! kazi yetu Wabunge ni kushauri, tutumie nafasi hiyo kushauri. Maana leo hii tunaposikia kauli kwamba hii CCM gani, mimi nikiwa kama Mjumbe wa NEC, naomba ni- *declare interest*, nakwazika...(Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Millya, ajiandae Mheshimiwa Keissy, ajiandae Mheshimiwa Chumi.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze masikitiko yangu makubwa kwamba wafugaji wanapambana na nini? Wanapambana na dola nyingi dhidi ya uhai wa watu. Wizara hii ni Wizara pekee yenye dola nyingi kweli ambazo *interesting group*, zingine ambazo ziko nje ya nchi zina-*interest*, na mimi hapa imebidi nitoe kidogo leo elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumeanza utalii nchini mwetu? Mwaka 1892 alikuja Muaustralia mmoja anaitwa Oscar Bowman, mwaka 1913 akaja mwingine anaitwa Stewart Edward White mzungu wa Kiingereza, akaja mwingine anaitwa Bernard Dimezec pamoja na mtoto wake anaitwa Michael wakaandika kitabu kimoja kinachoitwa *Serengeti shall never die*. Baada ya wazungu hawa kuandika vizuri kitabu hicho, Waingereza, mwaka 1959 wakaamua kuwaondoa wafugaji wa Kimasai Serengeti, wakasema wala hawafai. Tumewatunzia mazingira hayo kwa damu na jasho letu tukiwapa na ng'ombe wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe takwimu nyingine, kwa nini kuna migogoro ya wafugaji na wakulima nchi hii! Serengeti zimeondoka *square kilometers* 14,750 kutoka kwa wafugaji, Mkomazi - *square kilometers* 3,500 za wafugaji, Ngorongoro zimeondoka *square kilometers* 8,300 za wafugaji, Tarangire National Park zimeondoka *square kilometers* 2,850 za wafugaji, watu hawa mnawapeleka wapi! *It's a calculated genocide*, mnataka maisha yetu yasiwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo aliyekuwa Waziri Mkuu wa nchi hii, Edward Moringe Sokoine, kati ya mwaka 1948 na 1958 ndipo wakati alikuwa anamaliza shule ya msingi na sekondari. Mikataba hii inaingiwa, mnaondoa maeneo haya makubwa kutoka kwa watu wetu. *Where were there any informed consent?* Naongea hivi, kuna wafugaji wako Zambia wanasuka watu nywele, kuna wafugaji wako Dar es Salaam wamekuwa walinzi, Serikali mnawaonaje, tunaanza kuwa watu wabaya kwenye nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnatupiga, tumewahifadhia mazingira haya yote tukiamini kwamba tunatunza maisha yetu. *I declare interest*, siamini kwamba utalii ni mbaya, lakini utalii mbaya unaoumiza maisha yetu ni utalii usiokubalika na nitakuwa wa mwisho kukubali utalii wa namna hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanauliza maswali mengi, wanasema mifugo inaharibu mazingira, mmoja amezungumza hapa, hivi ni ng'ombe gani anayeua tembo, ni ng'ombe gani anayeua simba. Lakini geuzeni swali upande wa pili, watu wanaotegemea mifugo, karibu watu milioni mbili nchi hii, geuzeni usemi kwamba hawa mifugo wamekufa, *its their livelihood*, leo Serikali ianze kuwalisha hawa, mnaongelea *17 percent* ya GDP ya nchi. Je, mkianza kuwalisha watu hawa kwa sababu hawana mifugo, hawana maisha, itakuwa ni mbaya sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikitika kwenye kauli ya Mheshimiwa Waziri juzi na bahati mbaya wafugaji wa Kimasai wamekupigia kura kwa takribani miaka 15 kule Same. Unasema mifugo haifai, mifugo inaumwa, wanyama wasisafirishwe. Sasa nina maswali mawili; maana yake ni kwamba hawafai kuliwa na kwamba maisha ya watu ni ya bei rahisi kuliko pesa? Swali la pili, je, tuambiwe kwamba ni kauli ya Serikali kwamba wale wote wanaotegemea nyama nchi hii na wale wanaosafirisha kwenda Mataifa mengine wasisafirishe nyama kwa sababu wanaumwa, itoke kauli ya Serikali? Mheshimiwa Waziri amenisikitisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kuna WMAs, tunachoomba wafugaji wa Kilindi, Mheshimiwa Msigwa ameongea hapa milioni 25, ndugu yangu naomba upate hili, tuna ng'ombe milioni 25, hatutaki kuongezewa eneo, mipaka ambayo iliwekwa kabla sisi hatujawa na akili ya

kisheria na ndiyo maana unaona Wamasai wengi, Mheshimiwa Ole-Nasha, wengine wote wanasoma sheria kwa sababu ya uonevu mkubwa. Sisi hatuli wanyamapori hao, hatuli simba, hatuli swala, tunawatunzia, lakini basi *let it be fair*, na ninyi msituumize. Kimotorok mnatufukuza, Emoret mnatufukua, Same mnatufukuza, Kilosa mnatufukuza, Bukombe mnatumiza, Hanang' nina picha hapa, maskini wa Mungu mfugaji anatoka Katavi ameumizwa, kuna PF3 hapa. Mnatuumiza, mmetufanya watumwa kwenye nchi yetu. Naomba Serikali mkae chini mtufikirie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba utalii ni kitu kizuri, lakini Waheshimiwa Wabunge iwe *fair*. Naomba Sheria za WMA zilianzishwa na jamii, Kifungu kile cha 12 kilichoanzisha sheria hiyo badilisheni. Tunapata hela zetu, Simanjiro tumekataa WMA, lakini Kiteto na Longido wanafanya WMA. Mheshimiwa Waziri, hela zinachelewa sana, tunaomba mtume hizi hela mapema. Lakini kile Kifungu cha 51 cha sheria hiyo, ongezeni *percentage*, imekuwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeumia sana, Wamasai hawajasoma nchi hii, sheria za nchi hii hazijaangalia bado watu hawa. Kule Afrika Kusini wakati wa ukombozi, mwaka 1994 wakasema tuletteni *an affirmative action*. Tunacholilia hapa, wengine tumesoma siyo kwa sababu ya sera za CCM, ni bahati za makanisa na bahati za wengine wazungu tu. Mmetusahau muda mrefu, mnatuumiza muda mrefu, naombeni mfikirie kwamba Bunge hili lianze kutenda haki kwa ajili ya watu hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, fikirieni mifugo, *its not about business, it is a livelihood*. Mimi nisipokuwa na ng'ombe siangalii kuhusu hela. Lakini lingine ni lile linahusiana na Mheshimiwa Lowassa na Mheshimiwa Sumaye, Wakili mwenzangu ameongea, ninasikitika sana, watu hawa wanasahau *records*. Mwaka 2006 Lowassa akiwa Waziri Mkuu wa CCM alifukuza mifugo lhefu, hapakuwa hata siku moja na tamko la Kiserikali kutoka kwa Lowassa na Sumaye kutapanya mifugo yote nchi hii, msipotoshe umma. Nimuombe Wakili mwenzangu anapoanza kusimama aongee na *authority*, tunatetea utu, hatutetei biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, Mungu awabariki sana. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa huku ikiwa ng'ombe mnapiga makofi, ikiwa mazingira mnapiga makofi, sasa sijui. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Keissy, ajiandae Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu. (Makofi)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi katika kuongelea Wizara hii muhimu sana katika nchi yetu. Bila Wizara hii kuwepo vyanzo vya maji vyote vingekauka, kama Wizara hii haikuwepo hakuna miti katika nchi hii, ingekuwa jangwa. Kusema kweli lazima tufuate sheria. Leo kuna maziwa kwenye bahari, *Lake Tanganyika, Lake Nyasa, Lake Rukwa, Lake Victoria* na mwambao wa bahari, lakini nyavu haramu zinakamatwa zinachomwa hatusikii kelele. Kwa sababu wanakwenda kinyume na sheria. Watu wanaojenga kwenye *road reserve* wanavunjiwa maghorofa yao, hatusikii kelele. Lakini kelele ng'ombe anapoingia kwenye *Game Reserve* au *National Park* tunasikia kelele, kwa nini tusikie kelele? Tufuate sheria, kila kitu kina mpaka wake, haiwezekani mimi leo niingie kwenye nyumba ya mtu bila hodi. Ie ni sheria, ni nyumba zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungu na ubaya wao, lakini tangu enzi za zamani walikuwa wanaita mashamba ya bibi, ilikuwa mwiko hata kuchuma jani. Leo tunakwenda kuchoma pori, tunafanya tunavyotaka na kila kitu, lazima tufuate sheria ndugu zangu. Morogoro tulikuwa tunaita Morogoro maji yanatiririka, leo Morogoro maji yako wapi?

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri, kabla ya Bunge kuisha nipe magari kwenda kwenye doria kule *Lwafi Game Reserve* na Rukwa, kupambana na waingiza mifugo mle ndani, wanatuharibia mbuga zetu. Nilizungumza na Mheshimiwa Nyalandu hapa akiwa Waziri, alikuwa tayari kunipa gari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaingiza ng'ombe kule, tuna mbuga kule, *game reseve* ya kilometa 6,800 lakini hakuna gari, majangili wanaua tembo hovyoyote, leo hata mavi ya tembo hatuyaoni. Wanachoma pori hovyoyote, ng'ombe wamekuwa ndiyo nyati badala ya nyati mle ndani, hatuwezi kukubali, sheria zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kugeuza jangwa ndugu zangu, nchi itakwenda wapi? Tutapata wapi maji ya kunywa! Bora mimi *Lake Tanganyika* inaweza ikawa na maji mengi, ninyi mtakwenda wapi, Dodoma itakwenda wapi? Acheni kuwa na jazba, fugeni ng'ombe kama Denmark, Denmark wana ng'ombe chache lakini wanauza maziwa nchi nzima. Leo mnafuga ng'ombe, ng'ombe moja ana kilo 70 unasema una ng'ombe! Hatuwezi kukubali kuharibu mazingira kwa ajili ya wafugaji, hatutakubali! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu ni asilimia 75, wewe umezungumza wafugaji milioni mbili na wakulima wako wangapi nchi hii? Leo hawana sehemu ya kulima, watakosa maji wakulima wetu, tutapata wapi chakula tukikosa mvua, hatuna uwezo wa kumwagilia nchi nzima, kwa hiyo, ndugu zangu lazima tufuate sheria. *Game reserves* zipo kwa sheria *national parks* zipo kwa sheria na mfugaji yupo kwa sheria na mkulima yupo kwa sheria, hatukubali mkulima kwenda kulima kwenye *game reserve* wala mfugaji kwenda kwenye *reserves*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoma nyavu hapa kila siku mnasikia, wavuvi haramu kule Ziwa Tanganyika. Mimi mwenyewe shahidi, nilishaenda kushuhudia wanachoma nyavu za milioni saba, milioni nane, Mwanza wanachoma nyavu, Bukoba wanachoma nyavu, Pangani wanachoma nyavu, huku kote wanachoma nyavu, hatusikii kelele, kwa sababu wanavunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba zote zinavunjwa, juzi wamevunja nyumba Dar es Salaam kwenye njia za maji, nani anapiga kelele hapa, kwa sababu wamejenga kinyume na sheria.

Wewe unaingiza ng'ombe wako kwa nguvu zako utegemee pesa zako na wakulima wetu wanapata shida, wanakwenda kuhonga Mahakimu, hakuna kesi ya mkulima ilishida, mimi nina ushahidi. Hakuna kesi ya mkulima na mfugaji imekwenda mahakamani mkulima akashinda, hakuna! Hatuwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwangu kule kuna ng'ombe 200,000 wakati tulikuwa na ng'ombe labda 200 au 300. Wafipa ng'ombe wao ni wa kulimia. Mfipa kabisa mfugaji ng'ombe 50, leo kuna ng'ombe 200,000. Na mimi nimeshazungumza, walipe kodi. Hatuwezi kuwaachia namna hii walipe kodi, wana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi inalalamika haina hela MCC imetufinya misaada, wakati kuna mahali wanasema wana ng'ombe wengi, hawalipi kodi hawa. Vyanzo vingi vya hela hapa mnaviacha, ndiyo maana wanakuja kutambukatambuka hapa. Sisi hatukuona siku ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi mkulima hapa nje, Wizara hii tumeona wafugaji wamejazana hapa. Ndugu zangu tukiachia watachungu ng'ombe mpaka Ikulu. Hatuwezi, twende kwa sheria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kule kwangu kuna matatizo, mamba ndiyo wametuzidia. Watu wangu waliumwa na mamba, tumepiga kelele walipwe hiyo fidia maana yake huwezi kulipa maiti aliyekufa, thamani yake ni kubwa sana. Lakini sheria inasema mtu akiliwa na mamba, akiliwa na tembo, alipwe. Kwa hiyo nafuata taratibu, nina watu wangu kule wameliwa na mamba *Lake Tanganyika*, walipwe fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, lazima tuheshimu sheria nchi hii. Ni kama wewe una nyumba yako mimi nikuingilie mle ndani, ninywe chai bila idhini yako, ninywe maji bila idhini yako utanipeleka Polisi. Ni kama *Katavi Game Reserve*, *Luafi Game Reserve*, hizi zote zina sheria na sheria zimetungwa hapa Bungeni na nyingine tangu Mkoloni ametunga sheria hizi, tukiachia hivi wenyewe ndugu zangu ni mwaka mmoja hakuna mnyama nchi hii, kuna watu wanachukua *national parks* ndugu zangu, ajabu kabisa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila *national park*, bila *game reserve* ndugu zangu mvua hakuna, vyanzo vya maji vitakwisha. Mnaweza ninyi, mna hela Wabunge mnanunua maji ya chupa, watu wetu hawana hela ya kununua maji. Hatuna hela ya kununua maji, ni haya maji ya mvua ndiyo yanakwenda ardhini tunachimba visima. Leo miaka mitatu ikiwa hakuna maji hapa, mvua hakuna, tutakufa na ng'ombe wenu watakufa na mbuzi watakufa na kondoo watakufa na nguruwe vilevile, mtabaki na nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nawaambia ndugu zangu, hakuna kwenda kinyume cha sheria, sheria ni msumeno, mtu yeyote anavamia ni kama vile wavuvi wanavua haramu, lazima wakamatwe wachomewe nyavu zao ili samaki waendeleo kuishi. Samaki watakwisha, kwa hiyo tunaomba sheria itekelezwe. Hatuwezi kubembelezana, hatuwezi kutishana humu ndani, hakuna kumtishia mtu humu ndani. Mheshimiwa Maghembe amekuta sheria ipo. Nawapongeza TANAPA kwa kutupa madawati, kafanyeni kazi. Serikali yetu ina meno ya tembo yamejazana, msifanye kama Kenya. Uzeni, tupate pesa tununue magari na silaha kupambana na majangili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupambane na haya majangili kwa hali yoyote. Vijana wetu hawa ma-*game rangers* wakienda mule ndani wanapambana kwa bunduki na yale majangali, akimuwahi anamuua. Kwa hiyo na ninyi wafanyakazi wa Serikali ma-*game rangers*, mtu unamkuta *game reserves*, *national parks*, mpige risasi afe! Kwa sababu ukimuachia atakuua wewe. Kaenda kufanya nini mule ndani, kwa idhini ya nani! Kaenda mfano, *Katavi National Park*, kufanya nini mle ndani kama siyo jangili, nani kampa idhini? Ni kumtandika risasi tu maana yake ukichelewa kumpiga risasi anakupiga wewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni watu wabaya, tumewakamata Namanyere na bunduki nakuambia Mheshimiwa Maghembe, lakini wanaachiwa polisi. Nimekuletea ushahidi, wamekamatwa majangili na nyama ya tembo kilo 200 imepakiwa ndani ya gari linaitwa Noah, lakini siku mbili tatu wanaachiwa. Wanakamatwa na bunduki, siku mbili tatu wanaachiwa mpaka vijana wa TANAPA wanachoka! Kesi zao zinaishia hovyoyovyoyo tu. Nimekuletea sijapata majibu mpaka leo, nina wiki ya tatu, kwa ushahidi kabisa kwamba majangili wamekamatwa kule Nkasi lakini wanaachiwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Rais Magufuli anasema, unamkamata mtu *red-handed* na jino la tembo, unamkamata na bunduki, na nyama ya tembo, unampeleka mahakamani anashinda kesi, *red-handed!* Hapa kuna nini, rushwa kubwa, siyo ndogo. Hawa dawa yao ni kule wanapokamatwa maana yake ukimpeleka mahakamani anakushinda, ni kumtandika risasi mambo yaishe huko huko mbugani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuchezeza, kuharibu mapori yetu kwa ajili ya faida ya ninyi kizazi cha leo, kumbukeni kizazi kinachokuja. Je, miaka ya nyuma wangukuwa wanaharibu kama mnavyoharibu ninyi mikaa, kuni, ng'ombe mle ndani, tungeishi hapa? Kumbukeni na ninyi bado mnaendelea kusihhi nchi hii. Mwenyezi Mungu kawaambia dunia karibu miaka miwili iishe? Mna ahadi ya Mwenyezi Mungu dunia karibu iishe? Kwa hiyo, kuna vizazi na vizazi vinavyokuja na hii ni mali yetu wote, lazima tuitunze na tufuate sheria, sheria ni msumeno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na pole sana nimekusumbua sana kuku-*remind* kwa sababu ilikuwa nichangie asubuhi na nilifunga safari kutoka Jimboni kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii kwa sababu wiki iliyopita alifanya ziara na alifika kwenye Jimbo letu ambako kuna msitu mkubwa wa *Sao Hill*. Waheshimiwa Wabunge, huu ni msitu mkubwa katika Afrika Mashariki na Kati. Pia nipende kupongeza *TANAPA* kwa kutoa madawati, naamini na kule Mafinga yatafika. Lakini pia napenda kupongeza uongozi wa shamba la misitu ya *Sao Hill* kwa jinsi ambavyo tunashirikiana vizuri katika shughuli mbalimbali za kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, sasa nijielekeze kuchangia. Kuna msemu kaa karibu na waridi na wewe uweze kunukia kama waridi. Sasa kule Mafinga bahati mbaya sana na Wilaya ya Mufindi kwa ujumla, tuko karibu na waridi ambao ni msitu wa *Sao Hill* lakini hatunukii kama waridi, kama alivyosema Mheshimiwa Kigola, tuko kwenye msitu lakini watoto wanakaa chini, sijui ni laana ya namna gani.

Kwanza ningependa kuzungumzia kuhusu vibali. Kuna mgao wa namna tofauti katika kutoa vibali, lakini utoaji wa vibali umegubikwa na ujanja ujanja usiokuwa na mfano. Niseme kabisa mwanzoni, kama sitapata maelezo mazuri wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha nitakusudia kutoa shilingi. Katika suala la vibali, kwanza kabisa kweli msitu huu ni wa Kitaifa lazima unufaishe Watanzania wote, lakini kama nilivyosema, kama unakaa karibu na waridi lazima unukie



kama waridi. Msitu huu lazima kwanza uanze kuwanufaisha wale waliozungukwa na msitu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi babu yangu alikuwa *Sub Chief* wakati wa ukoloni. Sisi watu wa Mufindi, watu wa Mafinga tumetoa maeneo, tumepanda miti...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya ukumbi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa maeneo, tumepanda miti, lakini pia sisi ndiyo tunaolinda ule msitu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali, ninaomba Wizara katika mgawao wa vibali kwenye shamba la msitu wa *Sao Hill* lazima watu wanaozunguka msitu wapate, lazima wavunaji wadogo wadogo watizamwe, vijiji vitizamwe, makundi maalum hata *under privilege* kama vile akina mama wajane wapate, vikundi vya walemavu wasioona, walemavu wa ngozi, wasiosikia wapate vibali kupitia jumuiya zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu namuomba Mheshimiwa Waziri na timu yake tunataka *by name and by location* tujue watu wa kule wangapi wamepata vibali? Hatutaki kukaa karibu na waridi tusinukie kama waridi. Leo hii tuko karibu na waridi lakini wanaonukia waridi wako Tanga, wako Mwanza wako Zanzibar. Wakati huu Mheshimiwa Waziri hatuwezi kukubaliana hata kidogo kwenye suala la vibali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na suala la vibali ukienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, wachimbaji wadogo wanapewa ruzuku na Serikali. Mwaka jana Serikali imewapa ruzuku wachimbaji wadogo kiasi cha bilioni saba *point something*, mwaka huu wametengewa *billion six point something*. Je, kwa nini tusiwatengee pia ruzuku wavunaji wadogo ili waweze kununua mashine za kisasa. Kwa sababu zile mashine walizonazo tunazoita *ding dong* tunazotaka kuzipiga vita uwezo wake ni mdogo kiasi kwamba katika gogo *the recovery percentage* ni *only 25*, asilimia 75 inakuwa ni *waste product*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ije na utaratibu tutoe ruzuku kwa wavunaji wadogo waweze kununua mashine za kisasa ili kusudi hata wakivuna msitu basi tuweze kupata mazao yenye tija na siyo mabaki mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo la vibali kuna suala la MPM zamani tukiita SPM (Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo). Kiwanda cha karatasi kinapewa *cubic meter* laki mbili kwa mwaka, lakini cha kusikitisha MPM wanauziwa nusu ya bei wavunaji wetu wanauziwa *cubic* mita moja shiligi 28,000, MPM shilingo 14,000 lakini *worse enough* hawa MPM wamepewa kiwanda wazalishe karatasi, wanachofanya wanazalisha *at a certain stage*

wanasafirisha *raw material* inaenda Kenya zinazalishwa karatasi tunaletewa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, hata watu walioajiriwa pale kuna *foreigners* wako pale, wengine kazi yao wengine ni kuhesabu magogo kazi ambayo hata mtu ambaye ameishia darasa la pili anaweza kuifanya. Ninaomba Mheshimiwa Waziri na AG ningepomba upitie mkataba wa MPM kwa nini wao wanunue nusu bei, halafu watu wetu tununue kwa bei kubwa lakini pia tusinufaike na kiwanda hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda unakimbia ningependa pia kuzungumzia sekta ya utalii, tunakiri kwamba hii ndiyo sekta ambayo inaingiza mapato ya fedha za kigeni kwa wingi. Je, *Tanzania Tourist Board (TTB)* ambao wanawajibu wa kufanya *promotion* wameachwa kama watoto yatima, ukienda leo hii Kenya bajeti ya *promotion* na *advertisement* ni zaidi ya dola milioni 85, Uganda hapa ambao tunaona siyo washindani wetu wanatenga milioni nane *USD*, Rwanda milioni 11, sisi *TTB* tunaitengea chini ya milioni mbili, je, tutaweza kutangaza? Tunabaki tu kusema sisi ni wa pili kwa vivutio inatusaidia nini kuwa wa pili kama hatunufaiki na tutanufaika vipi kama hatuwekezi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tourism Development Levy (TDL)* kulingana na sheria Ngorongoro na *TANAPA* wanatakiwa wawape *TTB* asilimia tatu kuchangia katika masuala ya *promotion*, lakini fedha zile zinaenda kwanza Wizarani zinaingia kwenye mambo mengine. Miaka mitatu, minne kabla ya sheria hii *TTB* walikuwa wanapewa 1.5 na *TANAPA* 0.5 na Ngorongoro ilitusaidia tukatangaza mpaka kwenye *premier league*, hivi leo hii tungekuwa tukiitangaza kwenye *Leicester City* unadhani tungekuwa tumenyanyua utalii kwa kiasi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba tunaposema utalii unachangia tuwekeze pia katika kuhakikisha kwamba tunajitangaza ipasavyo. Haiwezekani leo hii eti tumewatengea *TTB* wafanye ziara za maonyesho ziara tano unataka uvutie utalii! Haiwezekani hata kidogo tukatoka. Hata suala la vitanda kwamba ni 1.5 *US dollar* mimi nashauri tu-charge kwa asilimia kwa sababu mtu anayelaza kwa shilingi 30,000 unam-charge 1.5 *USD*, anayechajisha laki vivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Balozi Adadi, ajiandae Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ni muhimu sana kwa sababu suala la Maliasili na Utalii ni kitu kimoja ambacho ni muhimu na kinachangia pato kubwa kwenye uchumi wa Taifa asilimia 17.3 siyo mchezo. Sasa kuna mambo mengi ambayo yapo ndani ya Wizara hii lakini mimi ningependa kujikita kwenye mambo ya hifadhi na pili kwenye suala la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo hifadhi nyingi sana lakini kuna hifadhi nyingine ambazo zimesahauliwa, kuna hifadhi ya misitu ya Amani kwa mfano, ni hifadhi kubwa ambayo ina hekta karibu 47,000 na ina mambo chungu nzima ndani yake. Kuna vitu ambavyo viko ndani ya msitu huo ambavyo havipatikani ulimwengu huu. Kuna vipepeo ndani ya msitu huo ambavyo huwezi kuvipata dunia yote hii, kuna kima weupe ambao wako mle, kuna nyoka wa ajabu ambayo mimi nilipata nafasi ya kuyaona pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yapo ndani ya msitu huo na ambayo naona kama Wizara hii haikuyaona kama ni muhimu na ndiyo maana msitu wa Amani imechangiwa kidogo sana kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukiangalia kwenye *page 54, page 61, 62 na 63* ni kama imeguswa tu *by the way*. Lakini kuna mambo muhimu ambayo yapo huko kwenye msitu wa Amani ni msitu mkubwa na msitu ambao una mambo mengi sana kuna ua ambalo liko pale huwezi kulipata dunia nzima, kule Amani wanaliita Dungulushi. Hili ni ua ambalo lina harufu ambalo likichanganya na mambo ambayo yako kule Amani mambo ya hiliki, mambo ya karufuu sasa ile mandhari yake ambayo unaipata kule ni kitu tofauti sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maofisa wa Mheshimiwa Waziri wamesahau kitu kama hicho kwamba Amani kuna vitu ambavyo ni muhimu, Amani kuna vitu ambavyo ni vya msingi na ingetakiwa waweke umuhimu sana kwenye hifadhi hiyo ya misitu. Pamoja na msitu huu kuwa na hekta 47,000, lakini pia umezungukwa na misitu mingine midogo midogo karibu sita ambayo ipo pembeni yake. Kuna misitu midogo kwa mfano msitu wa Derema, Lunguza, Tongwe Kwani, Nilo, Kambai, Manga, Mlinga yote ni misitu ambayo inazunguka pale Amani na kuufanya ule msitu uwe mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mtafiti mmoja na mtalii mmoja ambaye alitembea hifadhi nyingi hapa duniani na alipofika pale Amani alishangaa sana namna ambavyo hatuupi ule msitu wa Amani. Aliulinganisha msitu wa Amani na Kisiwa kimoja kiko kule Amerika ya Kusini Ecuador, hicho kisiwa kinaitwa Galapagos muangalie kwenye ramani mtakiona. Kuna vitu ambavyo vina vutia zaidi sasa alipoangalia msitu wa Amani akaona msitu ulivyo jaa, ulivyo nona, akasema huu ni msitu kwa ulimwengu na hifadhi ambayo

nimewahi kutembea huu unaweza kuwa wa pili duniani. Sasa hii ni kitu muhimu sana ambacho Mheshimiwa Waziri inabidi uangalie na uone umuhimu wa msitu huu ambao una kila aina ya vitu, viumbe mbalimbali ambavyo viko pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu huu pamoja na kuwa ni wa asili kuna malalamiko ambayo wananchi wa Derema wako 1,128, ambao wamehamishwa kutoka kwenye ule msitu na kwamba tunaenda kuwapa maeneo mengine na wale wananchi fedha ambazo wamelipwa ni ndogo sana. Wananchi hawa wamezunguka wamekwenda Ikulu karibu sijui mara ngapi? Wamekwenda hapo Wizarani kwako Mheshimiwa Waziri sijui mara ngapi? Na mimi tu nilipokuwa Mbunge hii ni barua yangu ya tatu kukuandikia kwamba hawa wananchi 1,128 kwa nini wamepunjwa wamepewa hela kidogo mimea yao ambayo ilikuwa ndani ya hifadhi kama hiliki, karafuu ilikuwa ni mingi, lakini hela ambayo wamepewa wamekadiriwa ni kidogo sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *last week* nimepokea barua kutoka Wizarani kwako inasema kwamba kufuatana na sheria hao walitakiwa walipwe sijui kila mche shilingi hizi, jamani, kila sheria *general rules* ina *exception* zake, kwa hiyo *exception* ambayo unaweza kuipa kutokana na umuhimu wa huo msitu mmeamua kuwahamisha hao watu jamani wapeni haki zao. Nitakuja kukuona Mheshimiwa Waziri, lakini ni muhimu sana uangalie namna gani mtaweza kuwapa hawa wananchi ambao wamelalamika, wamehangaika, wamekwenda kila ofisi wamekuja Dar es Salaam sijui mara ngapi kudai hizo haki zao lakini hawasikilizwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo tulisema kwamba hawa tunawahamishia kwenye shamba moja la Kibaranga pale ambalo shamba hilo ni haya ambayo yamerudishwa hati, lakini shamba la Kibaranga bado halijarudishwa hati na Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi simuoni hapa lakini nilishamlalamikia kwamba tunasubiri hati inyang'anywe ya shamba hilo tuweze kuwakabidhi hao wananchi wa Derema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema kwamba kuna mambo mengine ambayo amesahau, kuna Pango la Amboni kule karibu na Muheza, Tanga pale. Sasa lile pango badala ya kuwa utalii limekuwa ni maficho ya magaidi, magaidi wako mle kila siku askari wanakwenda mle, kila siku wanawatoa, sasa sijui limesahauliwa kwamba siyo eneo moja la utalii au ni namna gani? Ninaomba Mheshimiwa Waziri suala hilo pia liangaliwe na hilo pango pia lipewe kipaumbele kwa sababu ni kitu kimoja muhimu sana. Kuna vitu ambavyo viko vya kihistoria kwenye vitu kama hivyo ambavyo tunatakiwa kuviangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Amani pamoja na kuwa na kutengeneza mbao za mitiki ni sehemu moja ambayo tunatengeneza mbao za mitiki, tuna mashamba makubwa sana ya mitiki pale. Mjerumani alitengeneza reli mpaka inafika Amani kwa ajili ya kuichukua mitiki, lakini hiyo reli imekufa na ndiyo maana nilikuwa napiga kelele kwamba ni muhimu tupate barabara ya lami ya kutoka Amani kilometa 40 mpaka Muheza. Kuna mambo chungu nzima ambayo yako pale ambayo yangeweza kuwa *facilitated* na huo mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalie suala la utalii kwa haraka haraka, utalii kama unavyoonekana kwa kweli haulingani, watalii ambao wanakuja hapa nchini hawalingani na vivutio ambavyo tunavyo. Tuna mbuga karibu zaidi ya 15 acha hizo hifadhi ambazo tunazo kubwa kabisa hapa ulimwenguni, nasikitika sana kusema kwamba utalii tunaingiza watalii milioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Victoria falls* pale Zimbabwe wao *Victoria Fall alone* na wanaingiza watalii milioni mbili na nusu wanaingia pale kwa mwaka, tuna kila aina, jamani nafikiri Mheshimiwa Waziri inabidi uangalie namna gani ambavyo tunaweza kufanya au kuwafanya watalii waingie nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua njia moja ni hiyo kwamba hatuna ndege na ninashukuru sana kwa bajeti hii kuweka ndege. Watalii wengi wanapenda *direct flight* akitoka Ulaya moja kwa moja anatua hapa, kwa hiyo naamini kwamba hizo ndege ambazo zimepatikana mtazitumia vizuri na mtazipanga vizuri ili ziweze kutuletea watalii wengi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mlima Kilimanjaro, ni muhimu sana mimi nilipata bahati ya kupanda Mlima Kilimanjaro mwaka juzi, mwezi Disemba. Ningefurahi sana mnetengeneza programu ya Waheshimiwa Wabunge wapande mlima huu ili waone huko njiani kukoje, lakini njiani hakulingani na hali halisi iliyopo huko Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vibanda ambavyo viko hapo Horombo, vingine vipo pale Kibo, watu wanalala kwa shida. Mheshimiwa Mbunge mmoja alizungumzia mambo ya vyoo, mimi nilipandia njia ya Marangu naomba viangaliwe. Vile vi-*hut* vimejengwa miaka sijui mingapi iliyopita, ukienda pale *Kibo hut* kuna vibanda ambavyo vimejengwa sijui lini? Sasa hii sijui kwa sababu labda viongozi hawapandi ule mlima na kuona matatizo ambayo yako mle, lakini ni vizuri wakayatatua....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shabani Shekilindi ajiandae Mheshimiwa Gibson Meiseyeki na Mheshimiwa Kakoso ajiandae.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya na nguvu kuweza kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Naomba nimpongeze Waziri Maghembe na timu yake kwani hotuba yake ina vina, imegusa, lakini nimuombe isiwe ya maandishi tu iwe ya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite moja kwa moja katika kuchangia juu ya upandaji wa miti. Miaka ya nyuma misitu iliungua baadhi ya maeneo katika nchi hii, hususani Lushoto, mpaka sasa hivi maeneo yale bado ni mapori hayajapandwa miti. Niishauri Serikali yangu sikivu iandae mikakati kwa ajili ya kupanda miti katika maeneo yale kuanzia Korogwe, Lushoto mpaka kushuka maeneo ya Same kule ni jangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na kupanda miti iwasaidie pia wakulima mmoja mmoja wa miti waweze kupanda kwenye mashamba yao, kwani ukitaja Lushoto ndiyo kuna wahifadhi, watunzaji wa mazingira wakubwa sana. Leo hii maeneo yale ambayo ni vichaka yanatia aibu. Naiomba Serikali yangu tukufu ipange fungu kwa ajili ya kupanda miti katika milima ile ya Lushoto, pia iwasaidie wakulima hawa mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie moja kwa moja kwenye mgao na uvunaji. Tunashukuru tumepakana na misitu ya Shume, Mazumbai, Baga, Gare, lakini misitu ile bado haisaidii wananchi. Katika mgao wanaangalia wale watu ambao wana uwezo na kila mwaka watu wanaopewa mgawo ni wale wale. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu na nimuombe Waziri Maghembe kipindi hiki ahakikishe kwamba mgao ule au fuatilie waliopata ni wangapi na ni wa aina gani? Mimi kama Mbunge wao wamenituma baada ya kulalamika kilio hiki kwa muda mrefu sana. Mgao huu pia au uvunaji huu haujazingatia watu wanaochakata viwandani, kwa mtu mmoja mmoja na kwa vikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvunaji kwa mtu mmoja mmoja. Misitu ya Serikali hii watu wanapeleka kuchakata kwenye viwanda, viwanda viko mbali sana na miti ile. Kuna sehemu wanaita Makanya, Ngwelo, Gare, Ubiri, Lushoto, Mbwei, Malibwi na Kilole, maeneo haya yako mbali sana na viwanda. Kitu cha ajabu na cha kushangaza watu hawa wameweka sheria moja kwa ajili ya kuvuna kwa vikundi au kwa ajili ya kuvuna na *chainsaw*, wamekataza kuvuna kwa *chainsaw* wavune kwa shoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wakulima wangu wale wa miti sasa waruhusiwe kuvuna kwa *chainsaw* kwani ukitoa mti kutoka Makanya au mtu wa Makanya akivuna mti hawezi kupeleka moja kwa moja mpaka kiwandani, lakini Mheshimiwa Maghembe watu hawa anawakataza anasema kila mtu avune kwa shoka kitu ambacho ni kigumu, ndiyo maana nikasema



ameangalia upande mmoja tu kwa ile misitu ya Serikali lakini hajaangalia kwa mtu mmoja mmoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Maghembe, atakaposimama ku-*wind up* basi aangalie vitu hivi. Ahakikishe kwamba watu wangu awaruhusu sasa wavune kwa *chainsaw*. Kwa sababu mtu yule hawezi kukata mti wake kule mpaka akapeleka kiwandani, itakuwa ni shida. Tunawaomba hata mbaao za madawati wanashindwa kuvuna wanasema kwamba tumekatazwa kuvuna kwa *chainsaw*. Kwa hiyo, hili ningeomba baada ya kusimama Mheshimiwa Maghembe basi alitolee ufafanuzi, ili watu wangu waweze kuvuna kwa *chainsaw*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mheshimiwa Maghembe alitembelea Jimboni kwangu kule Lushoto, alikuta changamoto, pamoja na kwamba sikuwa na taarifa za ujio wake kama angenipa taarifa, basi ningemwambia hali halisi ilivyo, yeye alienda moja kwa moja mpaka ofisini kwa wataalam wake tu, na alipofika kule alichukua maneno ya wataalam akayaacha ya wananchi. Ninamshauri siku nyingine akienda atafute na Wabunge, hii siyo kwa Waziri Maghembe tu, Waziri yeyote atakayeenda *site* basi atafute Wabunge kwa sababu Wabunge ndiyo wanajua changamoto zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Lushoto inapakana na msitu, ninamuomba Mheshimiwa Maghembe kuna akina mama kule wanatafuta kuni msituni wanakamatwa, shoka zao zinachukuliwa zinaenda kuhifadhiwa ofisini, mapanga na kila kitu, watu wale ni walindaji wakubwa wa misitu. Nashukuru Mheshimiwa Maghembe alienda pale akawaambia kina mama wale basi waendeleo kutafuta kuni na waende na mapanga na mashoko, lakini wasije wakatafuta mti ambao ni mbichi. Kwa hiyo, nimuombe atakaposimama basi aliongelee hilo suala hapa ili liingie kwenye *Hansard* na watu wangu waweze kupata nguvu kwa ajili ya kutafuta kuni msituni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri wa Maliasili na Utalii, ashirikiane na Waziri wa Viwanda, kuna Kiwanda cha *Ceiling Board* pale Mkumbara; kiwanda kile kinakufa, hakina tatizo lolote, kina *skyline* inatoa magogo kutoka Shume kushuka chini. Lakini kwa sasa hivi kinakufa, na kinakufa bila sababu yoyote, ningemuomba sasa Mheshimiwa Waziri Maghembe na Mheshimiwa Mwijage wafike pale *Mkumbara Ceiling Board*, waone kiwanda kile jinsi kinavyonyanyasika, na watu wa pale jinsi wanavyonyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa pale hata kulipa bili ya umeme wameshindwa, sambamba na hayo naamini kabisa Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Maghembe watakapofika Mkumbara basi moja kwa moja wataenda mpaka kwenye Kiwanda cha Chai Mponde, naamini Mheshimiwa



Mwijage kama kweli ana hofu ya Mungu atatoa sauti yake na kufungua viwanda vile, wananchi wa kule wananyanyasika, hata kulipia karo ya shule wanashindwa, hata mlo ni mmoja kwa sababu ya chai yao kiwanda hakijafunguliwa wanashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Mwijage, nitamwekea hata mafuta aende *Mkumbara Ceiling Board* kwa sababu itakuwa ni ziara yake hiyo basi aende mpaka Mponde pale aone wakulima wa chai wanavyonyanyasika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gibson Meiseyeki, na Mheshimiwa Kakoso ajiandae.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kabla sijachangia nikiri kwamba mimi ni mfanyabiashara wa utalii kwa takribani miaka 12 sasa kwa hiyo ni *field* yangu ya *experience*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachangia kwa masikitiko kwa kiasi fulani, wengi wamezungumza hapa kila mmoja anafahamu ni kwa kiasi gani nchi yetu ni nzuri, iko kwenye *at least top ten* za dunia, lakini tumekaa hapa tunashangilia, wakati fulani Wabunge huku walipiga makofi kwamba tumefikia watalii milioni moja. Watalii milioni moja ni wachache mno, sana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama *South Africa* ambayo tuko *equally beautiful I would say*. Wanakwenda sasa hivi watalii milioni 12 kwa mwaka, Misri wako milioni 15, wakati ule kabla hawajagombana sijui sasa hivi iko ngapi. Nchi kama Thailand nazungumzia nchi ambazo hazina uchumi mkubwa kama sisi, wana watalii milioni 25 kwa mwaka, Indonesia, Singapore milioni 15; Tanzania watalii milioni moja tunashangilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa umefika tufanye jitihada za maksudi kuhakikisha kwamba tunanyanyua kiwango hiki cha watalii wanaokuja Tanzania, kiukweli kama sasa hivi wanakuja milioni moja tu wanachangia asilimia 17 ya *GDP* yetu wangepika milioni tano ingekuwaje, kwa mfano? Ingekuwa ni zaidi ya nusu ya *GDP*; kwa maana hiyo ingeweza ku-*observe shock* zote hizi za matatizo ya ajira kwenye Taifa letu, ningekuwa nina mamlaka ningeweza kusema kwamba Serikali yenu hii ya sasa angalau ingechukua vitu vitatu *comprehensively*. Ingechukua viwanda vya Mheshimiwa Mwijage kama anavyokuja navyo vizuri; amejipambanua vizuri Mheshimiwa Mwijage kwenye viwanda, mchukue Mheshimiwa Mwigulu kwenye kilimo, mifugo na uvuvi, ukaweka na utalii hapo tunaweza kuchukua watu wengi ambao hawana ajira

katika Taifa letu tukawa-*absorb* kwenye maeneo haya. Hivyo, ningeshauri tu kwamba tuangalie ni sababu zipi zinapelekea Taifa letu kukosa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu nilionao mimi, nimekwenda kwenye *trade fair* za kutosha na watu wa Mheshimiwa Maghembe wa *TTB* nimekwenda nao na nina masikitiko makubwa sana kusema kwamba watu wetu wa *TTB* wanakwenda kwenye *trade fair* kupumzika, hawaendi kufanya kazi ukilinganisha na mataifa mengine ambayo tunayakuta kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata nilivyosikia mmewanyang'anya sijui fungu mmelipeleka wapi niliona ni sawa tu, kwa sababu wenzetu wale wanakwenda kupumzika hawaendi kutafuta biashara, mara nyingi nimekwenda nao kwenye masoko mbalimbali nje ya nchi. Kwa hiyo, niseme kwamba tuangalie tena ni maeneo gani ambayo mojawapo ni kwamba Tanzania ni *destination* ambayo ni *very expensive*, ni ghali mno kuja Tanzania ukilinganisha na kwenda maeneo mengine ambayo naona watu wanaweza wakawa wanavutika kwenda kutalii maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tu-*review* tena hizi sababu ambazo zinasababisha tuwe ghali. Kwa mfano, *airport* zetu wanasema *handling fees* ni mojawapo inayosababisha tiketi ziwe ghali kwa watalii wanapotaka kuja Tanzania. *If that is the case* na kwamba kweli tunataka ku-*promote* utalii Tanzania tufike hiyo namba ya watalii ambayo mmeiweka *target* kwa sasa hivi ambayo ni milioni tatu ambayo naiona ni wachache, tuangalie hivi sababu vidogo vidogo, *handling fees*, *airport departure taxes* zile mnazi-*regulate* vipi ili kupunguza gharama ya mtu kuja Tanzania, maana yake mtalii anapokuja tusizungumzie ile *package* tu ambayo anailipa kuja kufanya utalii, lakini zungumzia pia na fedha anazokuja nazo mfukoni nyingi ambazo Watanzania wengi huko mitaani wanazisubiri kuuza bidhaa zao, vitu mbalimbali ambavyo wazungu wanavinunua. Tena wanavinunua kwa kusema *mzungu price*, *tourist price*, siyo kama wengine. Sisi tunakunywa soda shilingi 600, shilingi 700; mzungu anakunywa kwa shilingi 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakifika milioni tano ina maana kutakuwa na dola nyingi ambazo tutazi-*retain* hapa, ambazo zimekuja *indirect*. Kwa hiyo, tuangalie mapato ambayo ni *indirect*, mtalii anaweza kutuletea. Kwa hiyo, tujaribu kuwa-*entertain* waje kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine vitu vingine vinavyosababisha tukose watalii wa kutosha, kuna hizi *issue* za viza, tusishindane na Uingereza, Ufaransa sijui na ninyi mnapokwenda kutembea nje mnalipa viza kubwa. Muingereza aki-*charge* laki mbili kwenda Uingereza, tusishindane nao kwa sababu wale wanapokea watalii karibu milioni 50 kwa mwaka, sisi watalii 1000! Kwa hiyo, tuangalie namna gani tunawa-*entertain* kupunguza mzigo ili hawa watu waje

wakishafika hapa ndiyo tutajua jinsi ya ku-*deal* nao, mnafahamu pia kwamba mtalii anapofika hapa anachukua *precautions* nyingi sana.

Mheshimiwa Waziri, nisikitike kwamba *figures* ambazo umetupa hapa za watalii waliokuja mwaka jana siyo sahihi. Utalii mwaka 2014/2015, ume-*drop* kwa zaidi ya asilimia 50 mzee. Ugonjwa wa Ebola ilitu-*affect* sana na tumepunguza wafanyakazi sana kwenye makampuni yetu huko Arusha. Niseme tu kwamba ukitaka kufanya uhakiki vizuri wa hili jambo kesho kutwa *week end* inayokuja kuna *Karibu Fair*, nenda pale utawakuta wadau wa utalii, wahoji, waulize biashara ilikuwa vipi bila kujali ninyi mmekusanya kiasi gani, kwa sababu kuna mbinu nyingi za ninyi kukusanya mapato, kwa hiyo, utalii uli-*drop* sana, toka Ebola ilivyozuka, tulipoingia kwenye uchaguzi pia watalii wanatabia ya kutotembelea nchi, lakini ninyi rekodi zenu zinasema ni *80 percent*, siamini kama hiyo ni sahihi na tukafanye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungu wanapokuja, *sorry* kule Arusha tumezoea kusema wazungu, badala ya kusema watalii. Watalii wanapokuja wanameza dawa za malaria, lakini pia kwa baadhi ya nchi wanapofika *airport* wengine kama hawajadungwa sindano, wanandungwa sindano ya *yellow fever*, pale panatokea kizungumkuti kikubwa sana unajua siyo kila mmoja anapenda kudungwa sindano, wakija pale maafisa walioko pale wengine hata kwa yale mataifa ambayo hayatakiwi kudunga hizo sindano wanakamatwa wanakuwa *harassed*, wakati mwingine hongo zinatembea wanaingia bila kudungwa hizo sindano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme kwamba tufanye *overhaul* ya *marketing strategies* zetu tukafanye kazi. Ningeshauri kwamba yale mataifa ambayo ni makubwa yanaleta utalii kama Ujerumani, Uingereza, Canada, USA nimesema, Japan tuseme na China; kwanini tusifungue ofisi kule na tukawapa watu kazi na wapewe *target* ya kuhakikisha kwamba wanaleta wageni Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina ni watu ambao wana uchumi mzuri sana sasa hivi lakini kiukweli tumeshindwa kuwa-*reach* kwenye soko lile. Pamoja na kwamba kweli tunataka kujilinda wenyewe hapa ndani kwenye suala la utalii wawekezaji kutoka nje ni muhimu sana. Kuna matatizo ya lugha na *connection*, tukisema kwamba sisi wamatumbi hapa ndiyo tuifanye tu peke yetu hatutafikia hiyo *target*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo *Immigration* waangalie namna gani tuna *collaborate* na hawa watu wanaotoka nje, maana hawa ndiyo wana *access* na masoko ya kule kwao. Tuwarahisishie utaratibu wa kuingia hapa na wao watakapoleta wageni wakifika hapa kwetu na sisi tutapona hapo. Lakini tukisema tufanye wawekezaji wa ndani na nini? Kumchukua mzungu kutoka

Russia kumleta hapa siyo kazi rahisi tuwaachie wenyewe ambao wana *interest* ya kuwekeza kwetu, tuwawekee mazingira mazuri, na yawekwe rahisi kama Rwanda wanavyo fanya, Tanzania tumekuwa na *bureaucracy* kubwa sana, ningeshauri kwamba tuangalie hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *Airlines*, pamoja na kwamba mnakwenda kununua ndege zenu ambazo ni chache kwa kweli na ningeshauri pia kwamba tununue na zile ndege ndogo kama hizi za *Precision Air - HR* kwa ajili ya kuweza kuhudumia viwanja vyetu vidogo vidogo hapa ndani, kulikoni kuwaachia *private sectors* ambao *flight charges* zao ni ghali sana. Kutoka tu Arusha kwenda na kurudi Serengeti shilingi 800,000. Kwa hiyo, tuwe na ndege za Serikali au ambazo tunaweza tukawa na ubia ili tuweze ku-*regulate price* za *fares*. Tuweze kutoa wageni Arusha kuwapeleka Ruaha, Katavi na maeneo mengine kama Mikumi, kufanya hivyo sasa hivi ni tatizo, mgeni akileta *enquiring* kwenye makampuni yetu anataka kwenda Kusini na sisi tuko Kaskazini huwa hatufanyi hiyo biashara, kwa sababu ya jinsi ya kufika kule gharama ni kubwa sana na pengine kwa sababu ya uchache wao tunakuwa hatuna *contacts*. Kwa hiyo, tuboreshe maeneo hayo ili tuweze kutanua huu uwigo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *airlines* za kimataifa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nianze mchango wangu kwa kuchangia juu ya Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi hii ipo Mkoa wa Katavi, ni hifadhi kubwa sana, lakini bahati mbaya sana Wizara husika haijaitangaza. Ili tuweze kutangaza utalii ni vema tukaelekeza mawazo kwa maeneo yote ya nchi yetu. Ukanda wa Kusini utalii haujatangazwa ndiyo maana Mbuga ya Ruaha, Mbuga ya Katavi, Mahale hazifanyikazi vizuri kwa sababu Serikali yenyewe imeweka mipaka; utalii unaotangazwa katika nchi yetu zaidi unatangazwa kwa Mikoa ya Kanda ya Kaskazini. Ninaiomba Serikali ielekeze nguvu kutangaza na maeneo mengine ili zile fursa wapate kuzitembelea, tuna imani watalii watakuwa wengi pindi watakapokuwa wamebadilisha na maeneo mengine wakaenda kuangalia fursa zilizopo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia suala la Hifadhi ya Katavi kwa sababu Mbuga ya Katavi inayo uwezo wa kuunganisha watalii wa kutoka Katavi na wakaenda Mbunga ya Mahale ambayo iko Mkoa wa Kigoma ambao ni jirani, wanaweza wakitoka Mkoa wa Iringa katika Hifadhi ya Ruaha

wakaja Mbuga ya Katavi na baadaye watalii hao wakaenda Mahale, wanaweza wakapata maeneo mengi ya kuangalia utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mbuga ile ya Katavi tunaiomba Serikali iangalie uhifadhi wa hifadhi hiyo ya Katavi kwa sababu upo uwezekano hifadhi hii ikatoweka kwa sababu hakuna miundombinu mizuri. Ninaishauri Serikali tunao Mto wa Katuma ambao unaifanya Hifadhi ya Katavi iwepo, itunze na ihakikishe inaandaa mazingira mazuri ya kuhifadhi ili kuwe na utaratibu wa kuvuna maji, kuna maeneo wakati fulani inapofika kipindi cha mwezi wa Oktoba hifadhi hii huwa inakauka, hakuna maji na wanyama kama boko na mamba huwa wanakufa kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye hifadhi ya wanyama ya Katavi, bado wafanyakazi wanaofanyakazi kwenye hifadhi hii wanashida kubwa sana ikiwa ni pamoja na vitendea kazi hawana, ninaiomba Serikali kupitia Wizara husika iwapelekee vitendea kazi ili waweze kupambana na majangili wanaoenda kwenye mbuga hii sambamba na hifadhi ya Msitu wa Luwavi ambao ni jirani na kwa Mheshimiwa Keissy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la migogoro kati ya vijiji ambavyo vinazungukwa na WMA. Kumekuwa na tatizo kubwa sana kati ya vijiji vya Kabage, Kungwi, Sibwesa, Kasekese, Kaseganyama na Kapalamsenga. Vijiji hivi kila mara wananchi wanasumbuliwa wanachomewa nyumba na Serikali kwa sababu wao wana migogoro na WMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, WMA ni ardhi ambayo wanavijiji walikubaliana, lakini bado wananchi hakuna walichonufaika na mpango mzima wa WMA. Ninaiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri, fanya ziara Mkoa wa Katavi utembelee kwenye vijiji hivyo, uje utatue tatizo la WMA ambayo inawalazimisha wananchi hawana faida nayo, ukitatua huu mgogoro utakuwa umesaidia sana wananchi kwenye maeneo hayo. Ni vizuri tukaangalia pande zote mbili, mimi naamini uhifadhi tunauhitaji sana kwa sababu unalinda mazingira na unawafanya wananchi waneemeke na fursa zilizoko. Yale maeneo ambayo yamekuwa na migogoro ni vizuri Serikali mkawa karibu ili mkawatendea haki wale wananchi, tutoe dhana ile ambayo ipo ya kila siku kusikiliza hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninapenda kuzungumzia ni hifadhi ya misitu. Mkoa wangu wa Katavi una hifadhi mkubwa sana ya misitu na tuna eneo la Hifadhi la Msitu wa Tongwe, ambapo kumekuwa na uvunaji holela wa magogo yanayochukuliwa na wasimamizi wakubwa sana ni TFS ambao wanasimamia misitu kwenye nchi yetu kwa ujumla. Ninaiomba Serikali tunahitaji sasa maeneo ambayo kunavunwa hiyo misitu, kuwe na kitu ambacho kinawanufaisha wananchi kwenye maeneo husika, vipo vijiji ambavyo vimepakana na hiyo misitu, wanatunza lakini hawanufaiki, unafika mahala hata

watoto wanaosoma kwenye shule, hawapati madawati kwenye maeneo hayo. Ni vema Serikali ikaja na mpango wa kuangalia maeneo ambayo yanawanufaisha wananchi na wanatunza ile misitu kuwe na mrejesho ambao utawafanya wawe na nguvu ya kuhifadhi hiyo misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia sana eneo lingine wakati ule wa Operesheni Tokomezwa. Wananchi hasa wakulima walinyang'anywa silaha ambazo zinawasaidia kufukuza wanyama waharibifu. Serikali ije na majibu kwa sababu wananchi hawa wanaolima, wanyama waharibifu wanakwenda kuharibu mazao yao na silaha zote walishazibeba. Tunaomba Serikali iwarudishie wananchi hawa....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Wizara hii ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi ni moja tu katika Wizara hii. Najaribu kukumbuka kwamba katika Maziwa madogo madogo katika Afrika, Ziwa Rukwa ndiyo Ziwa pakee kwa nchi ya Tanzania ambalo limetengwa kwa ajili ya kufuga mamba. Mamba ni wengi kweli na hata sasa hivi ninavyoongea samaki hakuna Ziwa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wa vijiji vya Some, Manda, Udinde, Rukwa, Maleza, Mbangala wanategemea samaki, lakini wanapoenda kuvua samaki hakuna samaki na wamedumaa. Nilikuwa nawasiliana na Mheshimiwa Mwigulu alipokuwa kwenye Wizara yake hapa nikamwambia jamani hebu tengeni fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kuona kwa nini samaki hakuna Ziwa Rukwa. Katika hali ya kawaida samaki hawapo kwa sababu ya mamba ni wengi sana. Serikali inavuna mamba kidogo kwa mwaka vibali vya mamba 60 kwa mwaka wakati mamba wanazaliana sana kwa kila mwaka. Mheshimiwa Waziri, hebu jaribu kuliangalia hilo jamani wenzenu tunakufa kwa mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mimi kule Jimboni kwangu, Jimbo la Songwe malaria au magonjwa mengine haya hatuyajui sana, lakini mamba ndiyo kilio kikubwa kwa wananchi wa Jimbo la Songwe.

**MBUNGE FULANI:** Kuleni mamba!

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa Mheshimiwa Malocha kule Jimbo la Kwela ni vilio vya mamba, vijiji ambavyo



vimezunguka Ziwa Rukwa hata kwenye Jimbo la Mheshimiwa Silinde vilio ni mamba. Sasa wenzenu tunakufa kwa mamba Serikali inakuja hapa inasema eti huwa inawafidia watu wanaoliwa na mamba! Hebu niambieni mlishawahi kumfidia nani ambaye ameliwa na mamba?

Naomba kesho Mheshimiwa Waziri uniambie ulishawahi kumfidia mwananchi gani katika Ziwa Rukwa ambaye ameliwa na mamba ama labda mamba amemkamata hata mkono, sijawahi kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayesema hapa ndiyo muhanga wa mamba namba moja, baba yangu Mzee Augustino amekamatwa na mamba ni marehemu na mimi ndiyo nimemrithi, sijawahi kuona kwamba kuna pole ya Serikali, sasa siyo kuja kudanganya hapa kwamba huwa mnawafidia watu. Kesho nitashika shilingi uniambie fedha za baba yangu zipo wapi, hakuna! Huyu ni baba yangu, lakini mdogo wangu amekamatwa na mamba hakuna fidia, mama yangu aliyenizaa mimi amekamatwa na mamba hakuna fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muhanga namba moja ndiyo maana nasema nachangia kwa uchungu au labda nitoe machozi hapa. Mimi ni yatima kwa sababu ya mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena mimi ni yatima kwa sababu ya mamba! Mamba ni adui yangu namba moja. Sasa kama mamba ni adui kwa sababu yupo kwenye maji siwezi kumkamata, adui yangu mwingine ni Mheshimiwa Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa sababu ya mamba.

Naomba kesho uniambie fedha za baba yangu na mama yangu kwa ajili ya kunifidia mimi, kunipa pole ya mamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimefanya *research* toka mwaka 1990 mpaka leo wananchi wangu 128 wameuliwa na mamba. Wengine wananchi hawaendi kuvua samaki wanakwenda kuoga, wanakwenda kufua nguo na kadhalika wanajeruhiwa miguu, mikono, ni mamba. Nenda hospitali ya Mwambani pale Mkwajuni majeruhi ni kwa ajili ya mamba, sasa Serikali ipo wapi? Jamani tuoneeni huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi lete watu wafanye utafiti, samaki wapo wapi Ziwa Rukwa mbona mmelitelekeza Ziwa Rukwa, hakuna namna nyingine yoyote ukisikia bajeti hapa zinakwenda *Lake Tanganyika*, zinakwenda *Lake Victoria*, zinakwenda *Lake Nyasa*, utafiti wa bahari, jamani Ziwa Rukwa kwetu ndiyo uchumi wetu ukiacha kilimo! Hebu njooni muangalie wenzenu tunakufa jamani, kama nilivyosema mimi nimeathirika sana naomba niache tu, naweza nikaanza kulia hapa. *(Makofi)*



**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na mchangiaji wetu wa mwisho ameacha kuzungumza, pole sana Mheshimiwa Mulugo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina majibu ya miongozo kutoka kwa Spika. Mwongozo wa Spika kuhusu suala lililolombewa Mwongozo na Mheshimiwa Cecilia Paresso Mbunge kuhusu kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 17 Mei, 2016 katika Kikao cha 21 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge alisimama na kuomba Mwongozo wa Spika akitumia Kanuni 68(7). Katika kujenga hoja yake alitumia Kanuni ya 64(1)(a),(f) na (g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 ambaye alisema kuwa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge, aliwasema watu vibaya, alitumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha wengine. Alitumia maneno kwamba kuna mlevi mmoja aliyechangia humu ndani lakini pia alisema upande wa Upinzani ni debe tupu ni sawa na wake wenza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kutoa Mwongozo wangu naomba nitoe ufafanuzi ufuatao wa Kikanuni kuhusu maombi ya Mwongozo wa Spika na kuhusu utaratibu. Narejea ufafanuzi wa Kiti uliotolewa tarehe 02 Mei, 2016 katika mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge, kuhusu kauli iliyokuwa imetolewa na Mheshimiwa Dkt. Possi Abdallah, Mbunge - Naibu Waziri wa Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu. Nanukuu sehemu ya uamuzi huo kama ifuatavyo:-

"Mara nyingi suala la kuomba mwongozo linachanganywa na maombi yanayohusu kuhusu utaratibu, inaonekana Mheshimiwa Mbunge alikusudia kuomba Kuhusu Utaratibu chini ya Kanuni ya 64(2), ambayo ni mahususi kwa Mbunge anayeamini kuwa Mbunge mwingine amekiuka masharti ya Kanuni ya 64(1). Kanuni ya 64(2) inamtaka Mbunge kusimama mahali pale na kusubiri ruhusa ya Spika ili azungumze na kisha atasema kuhusu utaratibu na kisha kueleza masharti yaliyovunjwa chini ya Kanuni ya 64(2) na baada ya hapo Mheshimiwa Spika atatoa maelekezo."

Kikubwa kinachotakiwa chini ya Kanuni ya 64(2) ni kuwa Mbunge aseme Kuhusu Utaratibu na kwamba Mbunge atakayeomba utaratibu atoe ombi lake wakati huo huo kabla ya Mbunge anayeaminiwa kukiuka masharti ya fasili ya kwanza ya Kanuni ya 64 kumaliza kutoa maelezo yake. Maombi ya Mwongozo na Kuhusu Utaratibu ni masuala ya Kikanuni na mara nyingi Waheshimiwa

Wabunge tunayachanganya. Utaratibu unatakiwa kufuatwa ni tofauti katika masuala hayo.

Waheshimishiwa Wabunge, ili kuzingatia masharti ya Mwongozo au kuhusu utatibu inafaa Waheshimiwa Wabunge tuzisome vizuri Kanuni ili tuzingatie na kurahisisha matumizi sahihi ya kanuni zetu. Kiti kinazidi kusesitiza kuwa matumizi sahihi ya Kanuni hizi yazingatiwe maombi ya Mwongozo wa Spika na Kuhusu Utaratibu yaletwe chini ya Kanuni zinazohusika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima kaa kimya.

Pamoja na ufafanuzi huo Kiti kwa kutumia mamlaka iliyopewa chini ya Kanuni na kwa kuzingatia Kanuni ya 65(1) naelekeza kuwa maneno aliyotamka Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge yafutwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge na kwa kuwa ilikuwa ni lugha ya kuudhi. Huu ni Mwongozo wangu umetolewa leo.

Waheshimiwa Wabunge, nina Mwongozo mwingine, Mwongozo wa Spika kuhusu suala lililolombewa Mwongozo na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge kuhusu kauli za kichochezi zilizotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika maoni yake, kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Alhamisi ya tarehe 05 Mei, 2016 katika Kikao cha 13 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge alisimama kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na kuomba Mwongozo wa Spika, kwa msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati anawasisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2016/2017 alitumia maneno makali kwamba Zanzibar ipo kwenye kutawaliwa na kwamba Serikali yetu inaongozwa kwa mujibu wa taratibu za kiimla. Pia alitumia kauli za kichochezi kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa hotuba yake.

Mheshimiwa Mchengerwa aliomba Mwongozo wa Spika kama maneno hayo makali na kauli za kichochezi zipo ndani ya taratibu za Bunge. Kama siyo vinginevyo anamtaka Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kufuta maneno yote ya kichochezi katika hotuba yake.

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya kujiuliza kutokana na Mwongozo huu ni kama kuna kauli za kichochezi katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kuwa hotuba

iliyowasilishwa na Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mbunge, ilikuwa imebeba maoni na fikra za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Utaratibu wa kuwepo Wasemeji Wakuu wa Kambi Rasmi za Upinzani Bungeni kuhusu Wizara zilizopo Serikali upo kikanuni, maoni ya wasemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hutolewa kwa kuzingatia Katiba, Kanuni na Sheria nyinginezo katika uendeshaji wa Bunge.

Ibara ya 18(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeweka misingi ya uhuru wa kutoa maoni, Ibara hii inafafanua kuwa kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake kwa namna atakavyoona inafaa.

Aidha, Ibara ya 100(1) ya Katiba imeliwezesha Bunge kuwa na uhuru wa mawazo na majadiliano. Kwa mujibu wa Ibara hiyo uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote. Ibara ya 100(1) ya Katiba inasomeka kama ifuatavyo; "Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali pengine nje ya Bunge."

Hata hivyo, uhuru wa mawazo au majadiliano katika Bunge siyo *absolute*, majadiliano katika Bunge yanaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Hivyo majadiliano yoyote Bungeni ambayo yanakwenda kinyume na Kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge yatazuiwa kwa mujibu wa Kanuni. Ndiyo maana kama kuna Mbunge yeyote atakiuka Kanuni za majadiliano zilizowekwa katika Sehemu ya Tano ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016, atashughulikiwa kwa utaratibu uliowekwa Kikanuni.

Katika kulinda Kanuni za majadiliano Bungeni, Kamati ya Kanuni za Bunge itakuwa na wajibu wa kushauri uzingatiaji wa Kanuni katika mijadala ndani ya Bunge. Kama hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingekuwa na matatizo au haikuzingatia Kanuni na taratibu za majadiliano Bungeni bila shaka Kamati ya Kanuni za Bunge ingeliona hili na kushauri ipasavyo.

Hivyo basi, kwa kuwa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge hakuainisha maeneo ya uchochezi katika hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo aliomba yafutwe na kwa kuwa Kamati ya Kanuni za Bunge haikushauri kuwa kuna uvunjaji wa kanuni katika hotuba, hivyo basi, Kiti hakitatoa uamuzi wa kufuta maneno yote katika hotuba husika. Huu ndiyo Mwongozo wa Kiti. (*Makofi*)

Mwongozo wa Spika kuhusu suala lililoombewa mwongozo na Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge kuhusu majibu yaliyotolewa na

Mheshimiwa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mbunge na Waziri wa Nishari na Madini.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Alhamisi ya tarehe 05 Mei, 2015 katika Kikao cha 13, Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge alisimama kwa ajili ya kuomba Mwongozo wa Spika akitumia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. Vilevile katika kujenga hoja yake alitumia Kanuni ya 46 kuomba Mwongozo huo kuhusu majibu ya Mheshimiwa Sospeter Muhongo, Mbunge na Waziri wa Nishati na Madini, aliyoyatoa Bungeni tarehe 04 Mei, 2016. Majibu hayo ya Mheshimiwa Muhongo aliyoyatoa wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge, lilitokana na swali lake la msingi Namba 97 kwa mujibu wa *Order Paper* ya siku hiyo.

Majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Muhongo Mbunge, Bungeni ni kama ifuatavyo nanukuu kama inavyosomeka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge: “Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimfahamisha Mbunge asivyovifahamu, kwanza Arusha ni kwamba pale KIA tumeweka *substation* kwa ajili ya umeme wa KIA na maeneo ya pale tu. Ukienda Mererani juzi katika wachimbaji kumiwa *Tanzanite*, wachimbaji tisa wanatumia umeme bila kulipa wanaiba umeme kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge naomba ukitaka umeme wa uhakika shughulika na wezi wa umeme wa Arusha, ahsante.”

Mheshimiwa Bilago, Mbunge alisema majibu hayo ya Waziri ni kwamba alimuomba Mheshimiwa Mbunge aende akalinde watu wanaoiba umeme ili maji yapatikane Arusha, hivyo akataka kupata Mwongozo kama Wabunge wamekuwa ndiyo walinzi wa wezi wa umeme. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Bilago Mbunge, majibu ya Mheshimiwa Waziri Muhongo yalikuwa ya kejeli. (*Makofi*)

Kwa kuzingatia Kanuni ya 46 aliyoirejea Mheshimiwa Mbunge alipokuwa anaomba Mwongozo swali la kujiuliza ni iwapo majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri hayajatimiza masharti ya Kanuni ya 46 kutoa majibu ya nyongeza. Kwa wepesi wa rejea na nukuu Kanuni ya 46 kama ifuatavyo: “Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kikamilifu kama alivyoulizwa, isipokuwa kwamba kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi. Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza, kabla ya muda wa kujibu swali hilo kufikiwa. Endapo Mbunge muuliza swali atamuomba Waziri ampatie nakala ya jibu la swali kabla ya muda wa kujibu swali hili haujafikiwa basi Waziri anaweza kumpa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu kama alivyoombwa. Waziri Mkuu au Waziri mwingine yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri.”

Nimeamua kuinukuu Kanuni hii kwa ukamilifu wake ili niweze kueleweka vema kwa kuwa wakati Mheshimiwa Waziri akitoa jibu hilo, alikuwa akitoa majibu kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge, alilokuwa ameliekeza kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji hivyo Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Muhongo Mbunge alitumia Kanuni ya 46(3).

Waheshimiwa Wabunge, inavyoonekana hapa kwa mujibu wa nukuu niliyoitoa hapo awali ya majibu ya Waziri maneno yaliyomsababisha Mheshimiwa Bilago kuomba Mwongozo huu ni maneno shughulika na wezi wa umeme wa Arusha.

Mheshimiwa Bilago ametafsiri maneno haya kwamba ni kuwafanya Wabunge kuwa walenzi wa wezi wa umeme, hata hivyo kwa kawaida kazi ya Mbunge anayoifanya hapa Bungeni ni ya uwakilishi wa wananchi ambayo mara nyingine tunawaomba kura tunapowahidi kushughulikia kero zinazowasumbua ambazo naamini mojawapo ya kero hizo ni maji na umeme.

Aidha, wananchi wote tukiwemo Wabunge tunao wajibu Kikatiba kushiriki katika shughuli za Serikali yetu ili kujenga nchi yetu. Naomba ninukuu Ibara ya 8 (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ifuatavyo Ibara ya 8(1); "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo (d) wananchi watahiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii."

Vilevile kama nilivyotoa majibu ya awali jana katika swali la ulinzi na usalama siyo tu wa miundombinu ya umeme lakini ulinzi na usalama wa kila kitu katika nchi hii ni jukumu la wananchi wote pamoja na Wabunge. Hii ni kwa mujibu pia wa Ibara ya 27 kifungu kidogo cha Katiba inayosema kama ifuatavyo; "Kila mtu ana wajibu wa kulinda mali asilia ya Jamhuri ya Muungano, mali ya mamlaka ya nchi na mali yoyote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi na pia kuheshimu mali ya mtu mwingine."

Kwa hiyo, kwa kuwa shughuli za Serikali zinajumuisha kupambana na wezi wa aina mbalimbali ikiwemo wanaoiba umeme, Kikatiba wananchi wote tunapaswa kushiriki katika shughuli hii ili tujenge nchi inayozingatia haki ya kijamii ikiwemo kupata huduma ya umeme.

Hivyo, maneno aliyotumia Mheshimiwa Waziri kwamba Mheshimiwa Mbunge ashughulike na wezi wa umeme alieleza suala ambalo tayari limewekwa katika Katiba yetu, huu ndiyo Mwongozo wangu. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kesho tutaendelea na Wizara hii na jioni Mungu akipenda tutaimaliza.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,  
Tarehe 25 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*